

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA NNE

Kikao cha Kumi na Moja – Tarehe 9 Februari, 2019

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Tunaendelea na Mkutano wetu wa Kumi na Nne, leo ni Kikao cha Kumi na Moja, Katibu.

NDG. STEPHEN N. KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

HATI ZILIZOWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU (K.n.y. WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII):-

Azimio la Bunge la Kuridhia Ubudilishaji Hadhi Mapori ya Akiba ya Biharamulo, Burigi, Kimisi, Ibanda na Rumanyika – Orugundu kuwa Hifadhi za Taifa.

MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII):-

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Ubudilishaji

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Hadhi Mapori ya Akiba ya Biharamulo, Burigi, Kimisi, Ibanda na Rumanyika – Orugundu kuwa Hifadhi za Taifa.

MHE. CECIL D. MWAMBE (K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA MALIASILI NA UTALII):-

Maoni ya Msemadi Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani juu ya Wizara ya Maliasili na Utalii kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Ubudilishaji Hadhi Mapori ya Akiba ya Biharamulo, Burigi, Kimisi, Ibanda na Rumanyika – Orugundu kuwa Hifadhi za Taifa.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:-

Maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali (Na.2) wa Mwaka 2019 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.2) Bill, 2019*].

MHE. MASHIMBA M. NDAKI (MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI):-

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali (Na.2) wa Mwaka 2019 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.2) Bill, 2019*].

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM (K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:-

Maoni ya Msemadi Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani juu ya Wizara ya Fedha na Mipango kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali (Na.2) wa Mwaka 2019 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.2) Bill, 2019*].

SPIKA: Ahsante sana. Katibu.

NDG. STEPHEN N. KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

HOJA ZA SERIKALI

Azimio la Bunge la Kuridhia Ubadilishaji Hadhi Mapori ya Akiba ya Biharamulo, Burigi, Kimisi, Ibanda na Rumanyika – Orugundu kuwa Hifadhi za Taifa

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU (K.n.y. WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII): Mheshimiwa Spika, naomba sasa kuweka Mezani Azimio la Bunge la Kuridhia Ubadilishaji wa Hadhi ya Mapori ya Akiba ya Biharamulo, Burigi, Kimisi, Ibanda na Rumanyika – Orugundu kuwa Hifadhi za Taifa, kama ifuatavyo:-

KWA KUWA, kifungu cha 3 cha Sheria ya Hifadhi ya Taifa, Sura ya 282 kinampa Rais kwa idhini ya Bunge kwa Tangazo la Rais litakalochapishwa katika Gazeti la Serikali, mamlaka ya kutangaza eneo la ardhi kuwa Hifadhi ya Taifa kwa madhumuni ya sheria hiyo;

KWA KUWA, Sera ya Wanyamapori ni kudumisha uhifadhi endelevu kwa kuanzisha na kuboresha maeneo yaliyohifadhiwa kwa madhumuni ya kulinda bioanuwai katika Hifadhi za Taifa, Mapori ya Akiba, Mapori Tengefu na maeneo ya wazi;

NA KWA KUWA, Pori la Akiba la Kimisi lillianzishwa kwa Tangazo la Serikali Na.116 la mwaka 2003 wakati Mapori ya Akiba ya Biharamulo, Burigi, Ibanda na Rumanyika – Orugundu yalianzishwa kuititia Tangazo la Serikali Na. 275 la mwaka 1974 ambapo imekusudiwa matangazo hayo yafutwe ili kubadilisha hadhi ya mapori hayo na kuwa Hifadhi za Taifa;

NA KWA KUWA, mchakato wa kisheria wa kupandisha hadhi Mapori ya Akiba ya Biharamulo, Burigi, Kimisi, Ibanda na Rumanyika – Orugundu kuwa Hifadhi za Taifa umekamilika

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

na mipaka yake kubainishwa kama inavyoonekana katika kiambatanisho cha Azimio hili;

NA KWA KUWA, katika kuyapandisha hadhi mapori hayo imeonekana ni muhimu kuyaunganisha Mapori ya Biharamulo, Burigi, na Kimisi;

NA KWA KUWA, kwa kuridhia Azimio hili Taifa litapata manufaa yafuatayo:-

(a) Kuimarisha uhifadhi wa maliasili, hususan wanyamapori, mimea na mazalia na makuzio ya samaki na viumbe wengine kwenye maji; na

(b) Kuongeza Pato la Taifa kwa msingi kuwa ubadilishaji wa hadhi wa Mapori haya ya Akiba kutasababisha hifadhi hizo kuwa vivutio vya utalii;

HIVYO BASI, kwa kuzingatia manufaa ya utangazaji wa hifadhi tajwa za Taifa, naomba sasa Bunge hili katika Mkutano huu wa Nne kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 3 cha Sheria ya Hifadhi ya Taifa, Sura Na. 284 liridhie Azimio la Ubadilishaji Hadhi Mapori ya Akiba ya Biharamulo, Burigi, Kimisi, Ibanda na Rumanyika – Orugundu kuwa Hifadhi za Taifa.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:
Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Jenista Mhagama. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, moja kwa moja nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii ili awasilishe taarifa ya Kamati kuhusiana na Azimio hili. Mheshimiwa Mwenyekiti, anakuja Mheshimiwa Mbunge wa Korogwe Vijijini, Mheshimiwa Mnzava karibu sana.

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII): Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 53(6)(b) ikisomwa pamoja na kifungu cha 6(6)(b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016; na kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu Azimio la Bunge la Kubadilisha Hadhi Mapori ya Akiba ya Biharamulo, Burigi, Kimisi, Ibanda na Rumanyika – Orugundu kuwa Hifadhi za Taifa kwa kueleza chimbuko na manufaa na maoni ya Kamati kuhusu uamuzi huu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, chimbuko la Azimio. Tarehe 16 hadi 18 Machi, 2018, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii ilifanya ziara katika Mapori ya Akiba ya Biharamulo, Burigi na Kimisi kwa lengo la kukagua Mradi wa Kuyajengea uwezo Mapori ya Akiba kupambana na ujangili. Katika ziara hiyo, Kamati ilijiona changamoto mbalimbali ikiwemo ubovu wa miundombinu ya barabara, uvamizi wa mapori uliotokana na uwepo wa wakimbizi kutoka Rwanda uliosababishwa na vita vya mauaji ya Kimbari ya mwaka 1994. Uwepo wa wakimbizi hao ulisababisha kuongezeka kwa shughuli za kibinadamu ikiwemo kilimo, ufugaji, uingizaji wa silaha za kivita uliochangia kuongezeka kwa ujangili.

Mheshimiwa Spika, changamoto hizo zinasababisha maeneo hayo muhimu yenye fursa kubwa za utalii kuharibiwa na kuwa na mchango mdogo kiuchumi. Baada ya kubaini changamoto hizo, Kamati iliishauri Serikali kuyapandisha hadhi mapori hayo kuwa Hifadhi za Taifa kwa kuainisha faida za hatua hiyo ambazo ni pamoja na kuimarisha ulinzi wa rasilimali hizo muhimu na kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia ushauri wa Kamati kuhusu kupandisha hadhi Mapori ya Akiba, Serikali imeleta hoja ambayo ni Azimio la Bunge. Nafurahi kulijulisha Bunge

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Iako Tukufu kuwa wewe uliamua kuileta hoja hiyo kwenye Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa mujibu wa Kanuni ya 53(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, kutokana na masharti ya Kanuni ya 53(4) ya Kanuni za Bunge, mapema jana, tarehe 8, Februari, 2019, Kamati ilifanyia kazi hoja hii muhimu iliyyotokana na ushauri wa Kamati. Kutokana na kazi hiyo, sasa nawasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni na ushauri kwa kuanza na manufaa ya uamuzi huu.

Mheshimiwa Spika, imeelezwa umuhimu wa kiekolojia wa mapori hayo ambayo yanapakana na maziwa, mito, misitu, vijito, maeneo oevu na vyanzo vyaa maji. Pia mapori hayo yana miinuko na vilima mbalimbali vinavyopendezesha mandhari ya mapori hayo. Uwepo wa aina mbalimbali za wanyamaporis wakiwemo kuro, viboko, tembo, pongo, ngiri, fisi, korongo, twiga, swalapala, nyamela, tumbili, mbega mwekundu, chatu, pundamilia, simba na nyani. Viumbe wengine ni samaki na nyoka na ndege wa aina mbalimbali. Vilevile, mapori hayo yanapitiwa na Mto Kagera na kuna Maziwa makubwa ambayo ni Victoria, Burigi na Ngoma, maziwa hayo ni kivutio muhimu cha utalii na chanzo cha maji kwa wanyamaporis na bioanuwai nyingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa Serikali kuyapandisha hadhi Mapori hayo ni mwendelezo wa jitihada za Serikali ambapo baada ya kuendesha operesheni ya kuondoa mifugo na wavamizi wengine, hali iliyo sababisha kuboresha mazingira na sasa wanyamaporis walikuwa wamekimbia wameanza kurejea kwa wingi. Kupandisha hadhi Mapori haya kuwa Hifadhi za Taifa sio tu kutaimarisha ulinzi bali pia kujenga mazingira bora kwa ajili ya kuendeleza utalii na kukuza pato la wananchi wanaoishi jirani na hifadhi hizo na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, aidha, kucheleva kupandishwa hadhi Mapori hayo kutazorotesha jitihada za Serikali kulinda

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

maliasili zetu. Uwepo wa Uwanja wa Ndege wa Chato na kupandishwa hadhi kwa mapori haya kuwa Hifadhi za Taifa kutachangia sana kufungua fursa za utalii katika Kanda ya Ziwa na hivyo kukuza kipato cha wananchi wanaopakana na hifadhi hizo kutohana na shughuli za utalii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kipekee, Kamati inapenda kumshukuru na kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na Serikali yake kwa kukubali ushauri wa Bunge hadi kuwasilisha Azimio la Bunge kwa ajili ya utekelezaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, maoni ya Kamati. Uamuzi wa kupandisha hadhi Mapori haya kuwa Hifadhi ya Taifa utaimarisha ulinzi. Hatua hii itajenga mazingira bora kwa ajili ya kuendeleza utalii na kukuza pato la Taifa. Kamati inalishawishi Bunge lako Tukufu kuitisha hoja hii.

Mheshimiwa Spika, ili kuepusha uwezekano wa hifadhi mpya kukabiliwa na migogoro, Kamati inaishauri Serikali kuhakiki mipaka husika na kuwashirikisha wananchi ili kuepuka kuwepo kwa migogoro kati ya hifadhi na wananchi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuwasilisha maoni ya Kamati. Kwa kipekee kabisa, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa ushirikiano walioutoa wakati wa kuchambua Azimio hili na hatimaye kuwasilisha maoni yake mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kumshukru Katibu wa Bunge, Ndugu Stephen Kagaigai; Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndugu Athuman Hussein; na Katibu wa Kamati, Ndugu Gerald Magili kwa kuratibu shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha na naunga mkono Azimio hili. (*Makofii*)

**MAONI YA KAMATI KUHUSU AZIMIO LA BUNGE LA KUBADILISHA
HADHI MAPORI YA AKIBA YABIHARAMULO BURIGI, KIMISI,
IBANDA NA RUMANYIKA - ORUGUNDU KUWA HIFADHI YA TAIFA
KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Kanuni ya 53(6)(b) ikisomwa pamoja na Kifungu cha 6(6)(b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu Azimio la Bunge la kubadilisha hadhi ya Mapori ya Akiba ya Biharamulo, Burigi, Kimisi, Ibanda na Rumanyika-Orugundu kuwa hifadhi za Taifa kwa kueleza chimbuko, manufaa na maoni ya Kamati kuhusu uamuzi wa Serikali.

2.0 CHIMBUKO LA AZIMIO

Mheshimiwa Spika, Tarehe 16 – 18 Machi, 2018, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii ilifanya ziara katika Mapori ya Akiba ya Biharamulo, Burigi na Kimisi kwa lengo la kukagua mradi wa kuyajengea uwezo Mapori ya Akiba kupambana na ujangili. Katika ziara hiyo Kamati ilijiona changamoto mbalimbali zikiwemo:-

- (i) Ubovu wa miundombinu ya barabara ambayo inasababisha sehemu kubwa ya Mapori kutofikika kwa urahisi na hivyo kufanya kazi ya ulinzi kuwa ngumu; na
- (ii) Uvamizi wa Mapori uliotokana na uwepo wa wakimbizi kutoka Rwanda uliosababishwa na vita vya mauaji ya Kimbari vya mwaka 1994.

Uwepo wa wakimbizi hao ulisababisha kuongezeka kwa shughuli za binadamu ikiwemo Kilimo, ufugaji, uingizaji wa silaha za kivita uliochangia kuongezeka kwa ujangili.

Mheshimiwa Spika, changamoto hizo zimesababisha maeneo hayo muhimu na yenye fursa kubwa za Utalii kuharibiwa na kuwa na mchango mdogo kiuchumi. **Mheshimiwa Spika**, baada ya kubaini changamoto hizo, Kamati iliishauri Serikali kuyapandisha hadhi Mapori hayo kuwa hifadhi za Taifa kwa kuainisha faida za hatua hiyo ambazo ni pamoja na kuimarisha ulinzi wa rasilimali hizo muhimu na kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia ushauri wa Kamati kuhusu kupandisha hadhi Mapori ya Akiba, serikali imeleta hoja ambayo ni Azimio la Bunge. Nafurahi kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa uliamua kuileta hoja hiyo kwenye Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa mujibu wa Kanuni ya 53(3) ya Kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Spika, kutokana na masharti ya Kanuni ya 53(4) ya Kanuni za Bunge, mapema jana tarehe 8 Februari, 2019, Kamati ilifanyia kazi hoja hii muhimu iliyotokana na ushauri wa Kamati. Kutokana na kazi hiyo, sasa nawasilisha mbele ya Bunge lako tukufu maoni na ushauri kwa kuanza na manufaa ya uamuzi.

3.0 MANUFAA

Mheshimiwa Spika, imeelezwa umuhimu wa kikolojia wa Mapori hayo ambayo yanapakana na Maziwa, mito, misitu, vijito, maeneo oevu na vyanzo vya maji. Pia, mapori hayo yana miinuko na vilima mbalimbali vinavyopendezesha mandhari ya mapori hayo. Uwepo wa aina mbalimbali za wanyamapori wakiwemo kuro, viboko, Tembo, Pongo, Ngiri, Fisi, Korongo, Twiga, Swalapala, Nyamela, Tumbili, Mbega mwekundu, Chatu, Pundamilia, Simba na Nyani. Viumbe wengine ni samaki, nyoka, na ndege wa aina

mbalimbali. Vile vile Mapori hayo yanapitiwa na mto Kagera na kuna maziwa makubwa ambayo ni Victoria (Biharamulo), Burigi (Burigi) na Ngoma. Maziwa hayo ni kivutio muhimu cha utalii na ni chanzo cha maji kwa wanyamapori na bioanuai nyingine.

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa Serikali wa kuyapandisha hadhi Mapori hayo ni mwendelezo wa jitihada za Serikali ambapo baada ya kuendesha operesheni ya kuondoa mifugo na wavamizi wengine hali iliyo sababisha kuboresha mazingira na sasa wanyamapori waliokuwa wamekimbia wameanza kurejea kwa wingi. Kupandisha hadhi Mapori haya kuwa Hifadhi za Taifa siyo tu kutaimarisha ulinzi bali pia kujenga mazingira bora kwa ajili ya kuendeleza utalii na kukuza pato la wananchi wanaoishi jirani na hifadhi hizo na Taifa kwa ujumla. Aidha kuchelewa kupandisha hadhi mapori hayo kutazorotesha jitihada za Serikali za kulinda Maliasili zetu.

Mheshimiwa Spika, uwepo wa Uwanja wa ndege wa Chato na kupandishwa hadhi kwa Mapori haya kuwa Hifadhi za Taifa kutachangia sana kufungua fursa za utalii katika Kanda ya Ziwa na hivyo kukuza kipato cha wananchi wanaopakana na hifadhi hizo kutokana na shughuli za utalii.

Mheshimiwa Spika, kipekee Kamati inapenda kumshukuru Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na Serikali yake kwa kukubali ushauri wa Bunge hadi kuwasilisha Azimio la Bunge kwa ajili ya utekelezaji.

4.0 MAONI YA KAMATI

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa kupandisha hadhi Mapori haya kuwa Hifadhi za Taifa utaimarisha ulinzi. Hatua hii itajenga mazingira bora kwa ajili ya kuendeleza utalii na kukuza pato la Taifa. Kamati inalishawishi Bunge lako tukufu kupitisha hoja hii.

Mheshimiwa Spika, ili kuepusha uwezekano wa hifadhi mpya kukabiliwa na migogoro, Kamati inashauri Serikali kuhakiki Mipaka husika kwa kuwashirikisha wananchi ili kuepuka kuwepo na migogoro ya mipaka.

5.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spka, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii kuwasilisha maoni ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, kwa kipekee kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa ushirikiano walioutoa wakati wa kuchambua Azimio hili na hatimaye kuwasilisha Maoni yake mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg.Stephen Kagaigai, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndg,Athman Hussein, Katibu wa Kamati Ndg.Gerald Magili kwa kuratibu shughuli za Kamati.

Mheshmiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono Azimio.



Mhe. Kemilembe J. Lwota, Mb
MAKAMU MWENYEKITI
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA
ARDHI, MALIASILI NA UTALII

9 FEBRUARI, 2019

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mnzava kwa kutupatia maoni ya Kamati kuhusu jambo lilopo mbele yetu.

Sasa nimuite Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Maliasili na Utalii ambaye atatoa maoni ya Upinzani kuhusu Azimio lililo mbele yetu. Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa, tafadhali karibu.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA – MSEMAMI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:
Mheshimiwa Spika, hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Azimio la Kuridhia Ubadilishwaji wa Hadhi ya Mapori ya Akiba ya Biharamulo, Burigi, Kimisi, Ibanda na Rumanyika – Orugundu kuwa Hifadhi za Taifa kwa mujibu wa Kanuni ya 86(6) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu, mwingu wa rehema na upendo kwa kuniweka hai na mwenye nguvu na kuweza kusimama hapa mbele ya hadhira hii ili kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani juu ya Azimio lililo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kufikisha kwa Watanzania wote salamu za Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani, Mheshimiwa Freeman Mboge na Mheshimiwa Esther Matiko ambao wapo Magereza Segerea kwa usemi unaosema: *"Patriotism is loyalty to the country always, loyalty to the Government when it deserves it"*. Kwa nukuu hiyo tafsiri isiyo rasmi ni kwamba: "Uzalendo ni utii kwa nchi yako wakati wote na utii kwa Serikali pale inapostahili". Kambi Rasmi ya Upinzani ina wajibu wa Kikatiba wa kuhoji matendo ya Serikali katika kutekeleza majukumu yake. Tutakuwa waitifu pale tu Serikali inapostahili na inapotimiza majukumu yake na kutupa sababu ya kuipenda nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa muktadha huo, ni wajibu wetu kuhakikisha Serikali haifanyi jambo lolote ambalo litaharibu Taifa letu. Tukumbuke kwamba Serikali huja na kuondoka lakini nchi inabaki palepale.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Sika, nchi yetu imekuwa ni miongoni mwa nchi zilizobahatika kuwa na vivutio vingi vya utalii katika Ukanda wa Afrika, hivyo kuwa ni nchi yenye fursa kubwa inayoweza kutumia sekta hii ya utalii katika kuinua uchumi wake. Sekta ya utalii ndiyo sekta inayoingiza fedha nyingi za kigeni na pia ina uwezo wa kutoa ajira nyingi za moja kwa moja na zile ambazo siyo ajira za moja kwa moja kama vile kupitia kwa kile kinachoitwa *multiplier effect* kwenye ajira zitokanazo na utalii.

Mheshimiwa Spika, katika hoja iliyo mbele yetu ya Serikali kuliomba Bunge Kuridhia Kupandishwa Hadhi kwa Mapori ya Akiba kuwa Hifadhi ya Taifa ikiwa na lengo la kupanua maeneo ambayo yanakuwa yanasisimamiwa na TANAPA na hivyo kuongeza maeneo ya utalii hapa nchini. Takwimu zinaonesha Tanzania ina eneo la kilometra za mraba 945,234, kati ya eneo hilo takribani robo, kilometra za mraba 236,808.1imeachwa kwa ajili ya matumizi ya wanyamapor, Hifadhi za Taifa na Mapori ya Akiba. Usimamizi wa maeneo ya wanyamapor unahusisha Hifadhi za Taifa 16 zinazosimamiwa na TANAPA, Mapori ya Akiba 28 na Mapori Tengefu 42 ambayo yanasisimamiwa na TAWA.

Mheshimiwa Spika, Mapori ya Akiba yanayotakiwa kupandishwa hadhi ya Biharamulo, Burigi, Kimisi, Ibanda na Rumanyika – Orugundu ni miongoni mwa mapori yanayosimamiwa na TAWA. Mapori hayo yana jumla ya kilometra za mraba 5,251, ambapo mapori matatu ya Burigi, Biharamulo na Kimisi yanazungukwa na Kata 18 zenye vijiji 48. Aidha, mapori ya Ibanda na Rumanyika yanazungukukwa na Kata 12 zenye Viji 24. Kwa ujumla ni kuwa, eneo ambalo linapandishwa hadhi lina jumla ya Kata 30 na Viji 72.

Mheshimiwa Spika, tukumbuke kuwa maeneo haya ni maeneo ya wafugaji wengi sana. Hivyo basi, ni ukweli kuwa maeneo haya mara nyingi yanakuwa na migogoro baina yao na Serikali katika kutafuta maeno ya malisho kwa mifugo yao.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, upandishwaji wa hadhi wa mapori siyo jambo la kutoa kauli tu au kuletwa kwa Sheria Bungeni na kuitipisha, bali ni jambo linaloendana na uwekezaji wa kutosha katika maeneo husika ili maeneo hayo yaweze kuwa na hadhi ya kuwavutia watu kutembelea maeneo hayo. Uwekezaji katika maeneo husika ni miuondombinu kama barabara, mawasiliano ya uhakika na mahoteli kwenye maeneo husika na pia kuwa na aina mbalimbali za bidhaa za kiutalii ambazo zitawenza kuweka soko ili kuwavutia watalii.

Mheshimiwa Spika, Serikali inasema kuwa uridhiwaji wa azimio hili ni kuwa Taifa litapata manufaa yafuatayo:-

La kwanza, kuimarisha uhifadhi wa maliasili hususan wanyamapori, mimea, mazalia na makuzio ya samaki pamoja na viumbe vingine kwenye maji;

Pili, kuongeza pato la Taifa kwa msingi kuwa ubadilishaji hadhi wa mapori hayo ya akiba kutasababisha hifadhi hizo kuwa vivutio vya utalii.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kwanza ni kweli, lakini kwa kuwa maeneo husika yanapandishwa hadhi yapo chini ya TAWA na hivyo uhifadhi bado upo pale pale. Hivyo kupandishwa kwa hadhi kwa maeneo hayo kuwa hifadhi badala ya mapori ya akiba ni kuongeza matumizi kwenye maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kuongeza pato la Taifa siyo jambo la kutoa kauli, bali pato litaongezeka kutohana na uwekezaji utakaofanyika katika eneo husika. Ili kupata fedha, inabidi tutumie fedha. Hivyo, tuna mashaka makubwa kama kweli azima iliyokusudiwa itafikiwa au itakuwa ni mzigo tu kwa hifadhi nyingine.

Mheshimiwa Spika, takwimu za TANAPA zinaonesha kuwa kati hifadhi 16 zilizo chini yake ni hifadhi tano tu ndizo zinajidesha kwa faida, hivyo kuweza kuendesha hifadhi nyingine 11 zilizobaki. Hii inatoka na ukweli kwamba uwekezaji

unaofanywa kwenye hifadhi zetu hauzifanyi hifadhi zetu kuwa shindani na hifadhi za jirani zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna hoja za misingi ambazo tungependa tupatiwe majibu na Serikali, kwamba miaka yote Serikali imekuwa ikijitahidi kujenga miundombinu ili kuufanya Ukanda wa Kusini na Nyanda za Juu Kusini kuwa kituo cha utalii. Ndiyo mojawapo ya sababu ya kuhakikisha uwanja wa ndege wa Iringa na Songwe; vilivyojengwa na kukarabatiwa, ingawa bado havijafikia kiwango kinachotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais Magufuli wakati wa Sherehe ya Mei Mosi mwaka 2018 Mkoani Iringa alisema, Serikali imelenga kuimarisha utalii Kanda ya Kusini. Aliongeza na kusema kuwa wananchi walizoea kufanya utalii maeneo ya Kaskazini, wakati Ruaha ni Mbuga kubwa yenye vivutuo bora, lakini haikutembelewa na watalii kwa kuwa miundombinu haijaboreshwa. Ni kwa nini tuache ambapo tayari kunafahamika na kuanza kuwekeza sehemu ambayo itahitaji nguvu nyingi sana za uwekazaji hadi kuanza uzalishaji?

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Ukanda wa Kusini ndiyo uliokuwa katika mipango ya Serikali kuufanya kuwa kituo kingine cha Utalii baada ya Ukanda wa Kaskazini (*Tourist Destination*). Sasa hii haraka inayoletwa hapa kupandisha Mapori hayo ya Akiba kuwa hifadhi kwa minajili ya kuufanya Ukanda wa Ziwa Magharibi kuwa kivutio cha utalii, wakati ukweli ni kwamba uwekezaji bado ni mdogo ukilinganisha na uwekezaji ambao tayari umefanywa kwa Ukanda wa Kusini, haraka hiyo inatoka wapi?

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani tunaona hili ni sawa na kufukuza sungura wawili kwa wakati mmoja jambo ambalo linaweza kupeleka kukosa sungura wote wawili. Kuna msemo unaosema, "*you can not chase two rabbits at the same time.*"

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa inaonesha kumekuwa na mtafaruku wa matumizi ya maeneo husika baina ya wafugaji na wakulima kwa miaka kadha ambapo wananchi

wengi wamepoteza mifugo yao na wengine wako Magereza, kwa kushindwa kulipa faini, Serikali zote za *CCM* zilizopita zilishalionta tatizo hilo na ziliwu katika mchakato wa kuachia baadhi ya mapori kati ya hayo yanayopandishwa hadhi kuwa ni kwa matumizi ya wananchi: Je, mchakato huo umefikia wapi?

Mheshimiwa Spika, imetulazimu kuhoji jambo hilo kutokana na ukweli kwamba Kata 30 na Vijiji 72 vinavyozunguka eneo husika na ukweli kwamba idadi ya watu inaongezeka kwa kasi kubwa wakati ambapo ardhi kwa ajili ya shughuli za kibinadamu inabaki kuwa ile ile. Hili ni jambo la hatari sana kwa wanyamapori kupewa umuhimu mkubwa kuliko wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tayari maandalizi yameshakamilika ili kutimiza azima ya Serikali ya kuyapandisha hadhi mapori hayo tajwa, tunaomba Watanzania wajulishwe: Je, wananchi wanaozunguka mapori husika, wanapangiwa mkakati ili waweze kuendesha maisha yao ya kila siku bila kuwepo na uvunjifu wa amani na ukiukwaji wa haki za msingi kama ambavyo imetoa pale mifugo yao na wao wenyewe wavyodhalilishwa katika operesheni kadhaa zilizoendeshwa na Serikali?

Mheshimiwa Spika, mwisho, tunafahamu umuhimu wa hifadhi katika nchi yetu kama ambavyo tumejaribu kueleza hapo awali. Jambo la msingi ni kuwa badala ya kufanya uhifadhi wa wanyamapori na bioanuwai ni vyema pia tukahakikisha kuwa wananchi nao wanakuwa na amani katika miyo yao ili waweze kushiriki katika uhifadhi huo na uhifadhi uwe na maana kwao.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba hadi sasa kuna mikopo imeshatolea na Taasisi za Kimaifa ili kuhakikisha *Southern Circuit* inakuwa ni kitovu kingine cha utalii sambamba na kile cha Kaskazini. Tumeshindwa kuona mkakati huo kama unatekelezeka kwa vitendo zaidi ya kuwa kwenye makaratasi tu: Je, tatizo ni nini?

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa tulizonazo, Kambi Rasmi ya Upinzani, *World Bank* wanasita kutoa pesa kwa ajili ya kuimarisha utalii Kusini, yaani *REGROW* kwa kile kinachodaiwa Serikali kukiuka makubaliano ya awali. Kama tulivyohoji hapo awali kuhusu baadhi ya mapori katika hayo yanayopandishwa hadhi kukakibidhiwa kwa wananchi ili yatumike kwa shughuli zao za kiuchumi kwa minajili ya kuondoa migogoro baina ya Serikali na wananchi hawa ambao sehemu kubwa ni wafugaji, suala hilo liliishia wapi?

Mheshimiwa Spika, kauli ya majuzi ya Mheshimiwa Rais, kuhusu kuwaacha wananchi wanaozunguka maeneo ya hifadhi, kama walikuwa wanafanya shughuli zao za kutafuta riziki, kuendelea kufanya hivyo na wasisumbuliwe: Je, jambo hili kwa njia moja ama nyingine si zinakinzana na kauli hiyo ya Mheshimiwa Rais?

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

**HOTUBA YA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU
AZIMIO LA KURIDHIA UBADILISHAJI HADHI MAPORI YA AKIBA
YA BIHARAMULO, BURIGI, KIMISI, IBANDA NA RUMANYIKA-
ORUGUNDU KUWA HIFADHI ZA TAIFA KAMA
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

(Kwa mujibu wa Kanuni ya 86(6) ya Kanuni za Bunge la
Toleo la Januari, 2016)

1. UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema na Upendo kwa kiniweka hai na mwenye nguvu na kjuweza kusimama hapa mbele ya hadhira hii ili kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani juu ya AZIMIO liliilo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kufikisha kwa watanzani wote salama za Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani pamoja na Mheshimiwa Esther Matiko ambao wako

Magereza Segerea kwa usemi unaosema kwamba; “**Patriotism is loyalty to the country ALWAYS, Loyalty to the Government when it deserves it”**

Mheshimiwa Spika, kwa nukuu hiyo tafsiri isiyo rasmi “*Uzalendo ni Utii kwa nchi yako wakati wote na Utii kwa Serikali pale inapostahili*” Kambi Rasmi ya Upinzani ina wajibu wa Kikatiba wa kuhoji matendo ya Serikali katika kutekeleza majukumu yake. Tutakuwa watifu pale tu Serikali inapostahili na inapotimiza majukumu yake na kutupa sababu ya kuipenda nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Kwa muktadha huo ni wajibu wetu kuhakikisha Serikali haifanyi jambo lolote ambalo litariharibu taifa ietu. Tukumbuke kwamba Serikali huja na kuondoka lakini nchi liko pale pale.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imekuwa ni miongoni mwa nchi zilizobahatika kuwa na vivutio vingi vya utalii katika ukanda wa Afrika hivyo kuwa ni nchi yenye fursa kubwa inayoweza kutumia sekta hii ya utalii katika kuinua uchumi wake. Sekta ya Utalii ndiyo sekta inayoingiza fedha nyingi za kigeni na pia inauwezo wa kutoa ajira nyingi za moja kwa moja na zile ambazo sio ajira za moja kwa moja kama vile kupitia kwa kile kinachoitwa ***multiplier effect*** kwenye ajira zitokanazo na utalii.

Mheshimiwa Spika, katika hoja iliyo mbele yetu ya Serikali kuliomba Bunge kuridhia kupandishwa hadhi kwa mapori ya akiba kuwa hifadhi za Taifa, ikiwa na lengo la kupanua maeneo ambayo yatakuwa yanasmamiwa na TANAPA na hivyo kuongeza maeneo ya utalii hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha Tanzania inaeneo la kilometa za mraba 945,234. Kati ya eneo hilo takriban robo ya eneo hilo(236,308.8 sq.km) imeachwa kwa ajili ya matumizi ya wanyama pori. (Hifadhi za Taifa na Mapori ya Akiba). Usimamizi wa maeneo ya wanyamaporii unahuisha hifadhi za taifa 16 zinazosimamiwa na TANAPA, Mapori ya akiba 28, na Mapori tengefu 42 ambayo yanasmamiwa na TAWA.

Mheshimiwa Spika, Mapori ya akiba yanayotakiwa kupandishwa hadhi ya Biharamulo, Burigi,Kimisi,Ibanda na Rumanyika-Orugundu ni mionganini mwa mapori yanayosimamiwa na TAWA. Mapori hayo yanajumla ya kilometra za mraba 5251, ambapo mapori matatu ya Burigi, Biharamulo na Kimisi yanazungukwa na kata 18 zenye vijiji 48. Aidha, Mapori ya Ibanda na Rumanyika yanazungukwa na Kata 12 zenye vijiji 24. Kwa ujumla ni kuwa eneo ambalo linapandishwa hadi lina jumla ya kata 30 na vijiji 72.

Mheshimiwa Spika, tukumbuke kuwa maeneo haya ni maeneo ya wafugaji wengi sana, hivyo basi ni ukweli kuwa maeneo haya mara nyingi ynakuwa na mgogoro baina yao na Serikali katika kutafuta maeneo ya malisho kwa mifugo yao.

Mheshimiwa Spika, Upandishwaji wa hadi wa mapori sio jambo la kutoa kauli tu au kuletwala kwa sheria Bungeni na kuipitisha, bali ni jambo linaloendana na uwekezaji wa kutosha katika maeneo husika ili maeneo hayo yawe na hadhi ya kuwavutia watu kutembelea maeneo hayo. Uwekezaji katika maeneo husika ni miundombinu kama barabara, mawasiliano ya uhakika na mahotel kwenye maeneo husika na pia na kuwa na aina mbalimbali ya bidhaa za kiutalii ambazo zitawezwa kuwekwa sokono ili kuwavutia watalii

2. MAUDHUI YA AZIMIO

Mheshimiwa Spika, Serikali inasema kuwa uridhiwaji wa azimio hili, ni kuwa Taifa litapata manufaa yafuatayo;

- i. Kuimarisha uhifadhi wa maliasili hususan wanyamapori, mimea na mazalia na makuzio ya samaki na viumbe wengine wa kwenye maji; na
- ii. Kuongeza pato la Taifa kwa msingi kuwa ubadilishaji hadhi wa mapori hayo ya akiba kutasababisha hifadhi hizo kuwa vivutio vya Utalii.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kwanza ni kweli lakini kwa kuwa maeno husika yanayopandishwa hadhi yapo chini ya TAWA na hivyo uhifadhi bado upo pale pale, hivyo kupandishwa

kwa hadhi kwa maeneo hayo kuwa hifadhi badala ya mapori ya akiba ni kuongeza matumizi kwenye maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kuongeza pato la taifa, sio jambo la kutoa kauli bali pato linaongezeka kutokana na uwekezaji utakaofanyika katika eneo husika. Ili kupata fedha inabidi utumie fedha, hivyo tuna mashaka makubwa kama kweli azma iliyokusudiwa itafikiwa au itakuwa ni mzigo tu kwa hifadhi zingine.

Mheshimiwa Spika, takwimu za Tanapa zinaonesha kuwa kati ya hifadhi 16 zilizo chini yake ni hifadhi 5 tu ndizo zinajiendoesha kwa faida na hivyo kuweza kuziendesha hifadhi zingine 11 zillizobakia. Hii inatokana na ukweli kwamba uwekezaji unaofanywa kwenye hifadhi zetu hauzifanyi hifadhi zetu kuwa shindani na hifadhi za jirani zetu.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja za msingi ambazo tungependa tupatiwe majibu na Serikali, kwamba miaka yote Serikali imekuwa ikijitahidi kujenga miundombinu ili kuufanya ukanda wa kusini na nyanda za juu kusini kuwa kituo cha utalii na ndio mojawapo ya sababu ya kuhakikisha uwanja wa ndege wa Iringa na Songwe uvilivyojengwa na kukarabatiwa ingawa bado havijafikiwa kiwango kinachotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais Magufuli wakati wa Sherehe ya Mei Mosi mwaka 2018 mkoani Iringa alisema Serikali imelenga kuimarisha utalii Kanda ya Kusini. Aliongeza na kusema kuwa wananchi walizoea kufanya utalii maeneo ya Kaskazini wakati Ruaha ni mbuga kubwa yenye vivutio bora lakini haikutembelewa na watalii kwa kuwa miundombinu haijaboreshwa. Ni kwanini tuache ambapo tayari kuna fahamika na kuanza kuwekeza sehemu ambayo haitahitaji nguvu nydingi sana ya uwekezaji hadi kuanza uzalishaji?

Mheshimiwa Spika, ni ukweli kwamba ukanda wa kusini ndio uliokuwa katika mipango ya Serikali kuufanya kuwa kituo kingine cha utalii baada ya Ukanda wa Kaskazini (Tourist destination), sasa hii haraka inayoletwa hapa kupandisha mapori hayo ya akiba kuwa hifadhi kwa minajili ya kuufanya

ukanda wa ziwa MAGHARIBI kuwa kivutio cha Utalii wakati ukweli ni kwamba uwekezaji bado ni mdogo kulinganisha na uwekezaji ambao tayari umefanyika kwa ukanda wa kusini haraka hiyo inatoka wapi? Kambi Rasmi ya Upinzani tunaona hii sawa na kufukuza sungura wawili kwa wakati mmoja jambo ambalo linaweza kupelekea kukosa sungura wote wawili. Kuna msemo usemao "**You cannot chase to Rabbits at the same time**"

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa inaonyesha kumekuwa na mtafaruku wa matumizi ya maeneo husika baina ya wafugaji na wakulima kwa miaka kadhaa ambapo wananchi wengi wamepoteza mifugo yao na wengine wako magerezani kwa kushindwa kulipa faini. Serikali zote za CCM zilizopita zilikwishalionna tatizo hilo na zilikuwa katika mchakato wa kuachia baadhi ya mapori kati ya hayo yanayopandishwa hadhi kuwa ni kwa matumizi ya wananchi. Je, mchakato huo umefikia wapi?

Mheshimiwa Spika, imetulazimu kuhoji jambo hilo kutokana na ukweli kwamba kata 30 na vijiji 72 vinavyozunguka eneo husika na ukweli kwamba idadi ya watu inaongezeka kwa kasi kubwa wakati ambapo ardhi kwa ajili ya shughuli za kibinadamu inabaki kuwa ni ileile, hili ni jambo la hatari sana kwa wanayamapori kupewa umuhimu mkubwa kuliko wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tayari maandalizi yameisha kamilika ili kutimiza azma ya Serikali ya kuyapandisha hadhi mapori hayo tajwa, tunaomba watanzania wajulishwe, je wananchi wanaozunguka mapori husika wanapangiwa mkakati gani ili waweze kuendesha maisha yao ya kila siku bila ya uwepo wa uvunjifu wa amani na ukiukwaji wa haki zao za msingi kama ambavyo imetokea pale mifugo yao na wao wenyewe walivyodhalilishwa katika operesheni kadhaa zilizoendeshwa na Serikali?

3. HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, tunafahamu umuhimu wa uhifadhi katika nchi yetu, kama ambavyo tumejaribu kueleza hapo awali,

lakini ni jambo la msingi kuwa badala ya kufanya uhifadhi wa wanyapori na bioanuwai ni vyema pia tukahakikisha kuwa wananchi nao wanakuwa na amani katika miyo yao ili waweze kushiriki katika uhifadhi huo na uhifadhi uwe na maana kwao.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli kwamba hadi sasa kuna mikopo imeshatolewa na taasisi za kimataifa ili kuhakikisha *Southern circuit* inakuwa ni kitovu kingine cha utalii sambamba na kile cha kaskazini. Lakini tumeshindwa kuona mkakati huo kama unatekelezeka kwa vitendo zaidi ya kuwa kwenye makaratasi tu. Je tatizo nini? Na kwa taarifa tulizonazo Kambi ya Upinzani World Bank wanasita kutoa pesa kwa ajili ya kuimarisha utalii Kusini (Regrow) kwa kile kinachodaiwa Serikali kukiuka makubaliano ya awali.

Mheshimiwa Spika, kama tullivyojoji hapo awali kuhusu baadhi ya mapori kati ya hayo yanayopandishwa hadhi kukabidhiwa kwa wananchi ili yatumike kwa shughuli zao za kiuchumi kwa minajili ya kuondoa migongano baina ya Serikali na wananchi hao ambao sehemu kubwa ni wafugaji, suala hilo liliishia wapi?

Mheshimiwa Spika, kauli ya majuzi ya Mheshimiwa Rais kuhusu kuwaacha wananchi wanaozunguka maeneo ya hifadhi kama walikuwa wanafanya shughuli zao za kutafuta riziki kuendelea kufanya hivyo na wasisumbuliwe, je jambo hili kwa njia moja ama nyingine si linakinzana na kauli hiyo ya Mheshimiwa Rais?

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha.

.....
Peter Simon Msigwa, Mb
WAZIRI KIVULI-WIZARA YA MALIASILI NA UTALII
9/2/2019

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa, tunakushukuru sana. Sasa tunaelekea kwenye uchangiaji kama nitakavyoelekeza. Wakati natoa tangazo dogo, basi wajiandae wachangiaji kama ifuatavyo:-

Ataanza Mheshimiwa Risala Kabongo, atafuatiwa na Mheshimiwa Albert Obama na Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein atafuatia. Kabla yao, naomba niwatambulisse wageni walioko katika jukwaa la Spika. Ninao wageni kumi ambao ni kutoka chama cha Mapinduzi Mkoa wa Dodoma, wakiongozwa na Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM, Taifa, Ndugu Leila Burhan Ngozi na mume wake, Ndugu Ramadhan Kamala. Ahsante sana na karibuni sana.

Ndugu Leila Ngozi ndiye mlezi wa Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Dodoma, amefuatana na Henry Msunga ambaye ni Katibu mwenezi Mkoa. Ahsante. Asia Halamga ambaye ni Katibu wa Umoja wa Vijana wa Mkoa, Henry Kakurwa pia yumo; yuko Abushehe Hassan, Michael Masaga, Nyemo Ndagala, Katibu wa CCM wa Mkoa - Jamila Yussuf, yuko Ndugu Ramadhan na Ndugu Baraka.

Karibuni sana Bungeni mwone mambo yanavyoendelea na mtapata maelezo zaidi kutoka kwa Maofisa wetu wa Bunge. Kwa wageni wengine mliopo msiwe na wasiwasi, nitawatambulisha kadri muda unavyoenda. Sasa nimkaribishe Mheshimiwa Risala, atuanzishie dakika kumi. (*Makofi*)

MHE. RISALA S. KABONGO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika hii mada muhimu iliyoko mezani. Hoja ya kupandisha hadhi Mapori ya Akiba ya Biharamulo, Burigi, Kimisi, Ibanda na Rumanyika, Orugundi kuwa Hifadhi za Taifa ndiyo hoja ambayo tumekuwa kukijjadili muda mrefu katika Kamati yetu ya Maliasili na Utalii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikiri tu kuwa mimi ni Mjumbe wa Kamati hiyo na kwamba nichukue fursa hii kipekee kumpongeza sana, Mkurugenzi wa Hifadhi za Taifa TANAPA,

Ndugu Allan Kijazi pamoja na timu yake kwa kuendelea kusimamia maeneo ya Hifadhi za Taifa *TANAPA*, yenyé hifadhi 16, mapori ya akiba 28, mapori tengefu 42 yanayosimamiwa na *TAWA*. (*Makofí*)

Mheshimiwa Spika, Mapori ya Akiba yanayopandishwa hadhi ni mionganí mwa mapori 42 yanayosimamiwa na *TAWA*. Kumekuwepo na jitihada mbalimbali za kukabiliana na changamoto za ujangili wa mapori kwenye maeneo yanayopakana na mapori ya akiba. Maeneo mengine yanayokuwa na changamoto ni sehemu ya ujambazi ambao umekithiri maeneo ya mipakani. (*Makofí*)

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine ni uvuvi haramu ambao umekuwa ukikabili mapori haya na uingizaji wa silaha za kivita ambazo pia zimekuwa zikiingizwa kuitia kwenye mipaka ya mapori haya. Kumekuwa na malengo mbalimbali ambayo yamesababisha kupandisha mapori haya kuwa hifadhi za Taifa. Malengo hayo ni pamoja na kuimarisha uhifadhi wa maliasili kama tulivyoona kwenye Kamati yetu, hususaní pia wanyama pori, mimea adimu, mazalia ya samaki, viumbe wengine na ndege wa aina mbalimbali ikiwemo korongonyangu.

Mheshimiwa Spika, kuimarisha ulinzi wa mipaka yetu imekuwa ni hoja muhimu pia ya kufanya maporo haya kupandishwa hadhi. Sambamba na hilo ni kuimarisha mifumo ya kisheria ambayo itakwenda kusimamiwa na hifadhi za Taifa *TANAPA*. Vilevile kuongeza pato la Taifa kuitai shughuli za utalii ambazo zitakwenda kuendeshwa katika ukanda wa hifadhi za Magharibi. Kwa kuwa shughuli za kijamii hazitaruhusiwa kuendeshwa katika mapori haya wakati eneo hili linapandishwa kuwa Hifadhi za Taifa, napenda kushauri masuala yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hii inaweza kupelekea kuendelea kuwa na migogoro mingi ambayo imekuwa ikitokea katika maeneo mengine kama haya, wananchi wa maeneo haya ambao ni wafugaji kulingana na Sheria za Hifadhi hawataruhusiwa kuendelea kufanya shughuli za

kijamii kama kufuga, kuokota kumi na kuvua samaki. Hivyo, sambamba na kupandisha hifadhi hizi, mapori haya ningependa kushauri mambo yafuatayo ili Serikali iweze kuyatekeleza:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sasa hii ni fursa ya miji ya jirani kama Geita, Biharamulo, Bukoba na Ukerewe, napenda kushauri kuweko na mikakati ya kuendeleza miji hii. Hivyo, viwango vya utoaji huduma viwe vinakidhi mahitaji ya soko la utalii ili kuwezesha wananchi wanaopakana na Mikoa ile kuweza kufaidika na hili suala la upandishaji hadhi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, suala langu la pili ningependa kushauri Serikali ijenge mazingira kuiwezesha *TANAPA* kuyaendeleza mapori haya yatakayopandishwa hadhi. Suala la tatu, napenda kuishauri Serikali kusaidia miundombinu ya kufika hifadhi, iboreshwe. Suala la nne, naomba Serikali isaidie kuondokana na urasimu wa kutoa misamaha ya kodi kwa wafadhili wanaotoa pesa kusaidia maeneo hayo, hasa kwenye suala la miundombinu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia kushauri Serikali kuwe na bajeti ya kutosha kusaidia shughuli za uendeshaji kwa kuwa mpaka sasa kati ya Hifadhi 16 za Taifa ni hifadhi tano tu ambazo zinaijendesha zenyewe, hifadhi nyungine zote ni tegemezi. Kwa hiyo, kwa kuwa tunaenda kwenye kipindi cha bajeti, kuwe na bajeti ya kutosha kusaidia hifadhi hizi kuijendesha. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Serikali ione kuna haja sasa ya kufanya Wizara ya Maliasili na Utalii kuwa ni kipaumbele cha Taifa kwa kuwa Wizara hii sasa imekuwa ikichangia pato kubwa la Taifa na kwamba ni mionganini mwa Wizara zinazoingizia pato kubwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja hii ya kupandisha hifadhi hizi za Magharibi kuwa na hadhi ya *TANAPA* kwa kuwa kupandisha hadhi hifadhi hizi zitaisaidia sana wananchi wanaozunguka

maeneo haya ya Magharibi kuendelea kiuchumi, lakini pia kusaidia mipaka yetu ambayo inayozunguka nchi jirani. Vile vile, kama tulivoona, itasaidia ulinzi katika nchi yetu na kuzua migogoro mingi ambayo inatokana na nchi zinazozunguka katika hifadhi zetu.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Risala Kabongo. Kwa msiofahamu, Mheshimiwa Risala ni mtu ambaye anatokea kwenye masuala ya uhifadhi na utalii. Kwa hiyo, anafahamu anachokiongea. (*Makof*)

Mheshimiwa Albert Ntabaliba, nilikuwa nimekutaja.

MHE. ALBERT O. NTABALIBA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii, nami niweze kuunga mkono azimio hili la kupandisha haya mapori na kuwa hifadhi. Kilichonisukuma niweze kuunga mkono maazimio haya, sisi Mkoa wa Kigoma tumeathiriwa sana na hili pori lilitokuwa la Biharamulo. Hili pori la Biharamulo lilitokuwa linatufanya mabasi yanapopita pale ya abiria lazima uende na Askari wakiwa wanalinda. Ukiwa na gari lako la binafsi, uende na Askari wakulinde mpaka utakapofika maeneo ya Kibondo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa kulipandisha hadhi hili kuwa hifadhi, tuna uhakika kwamba mambo yataanza kuwa mazuri kwa sababu majambazi kutoka Burundi na Rwanda wamekuwa wakijificha mle. Kwa hiyo, ndiyo sababu iliyonifanya nivutike kuunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, siyo hivyo tu, hata haya mapori mengine tunazo faida nyingi za kiuchumi kwa sababu nazo zitakuwa ni sehemu ya utalii, lakini *tour guide* wetu watapata ajira na mahoteli yataweza kuwekwa pale kwenye baadhi ya maeneo na vile vile mapato utalii nayo yataongezeka. Faida nyingine, tutaendelea kutunza mazingira kwa sababu, kwa kuwa ni mapori watu wamekuwa wakienda kufanya shughuli mbalimbali za ufugaji, wanalima, wanakata miti, wanakata mkaa ndani ya yale mapori. Kwa hiyo, hifadhi

nzima inakuwa imeharibika. Kwa hiyo, sababu hizo zinasababisha tuweze kuunga mkono azimio hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kikubwa zaidi ni faida za kiuchumi tutakazozipata kwenye mapori haya. Mengine nashukuru kwamba kwa kuwa yanaenda *TANAPA* na tuna Mkurugenzi pale Kijazi yuko imara kuweza kuyasimamia, kwa hiyo, naye tunampa wito kwamba aweze kuyawekeza miundombinu ndani ya hifadhi ili nayo hadhi yake iweze kuwepo. Zaidi elimu iweze kutolewa kwa vijiji vinavyozunguka kwa sababu wengine walikuwa wanakidhi mahitaji yao mle. Kwa hiyo, elimu iweze kutolewa kwa vile vijiji vinayozunguka ili faida ya hifadhi hizi ziweze kuonekana.

Mheshimiwa Spika, sitaki kupoteza muda, naunga mkono maazimio haya. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Nilikuwa nimekutaja Mheshimiwa Yussuf, dakika tano, Mheshimiwa Magdalena Sakaya dakika tano.

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata dakika tano na bila kupoteza muda niunge mkono maamuzi haya ya Serikali, niipongeze Serikali, niipongeze Wizara kwa uamuzi huu.

Mheshimiwa Spika, katika mchango wangu kwa sababu ni mtaalam na mimi katika sekta ya Maliasili na Utalii basi nitatoa angalizo na ushauri zaidi na dakika tano ulizonipa ni kidogo lakini nitajaribu kuzitumia vizuri.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, naomba Serikali iiangalie hii *TANAPA* kwa macho mawili sasa kwa sababu tunaiongezea mzigo *TANAPA*, ni sawasawa na gari unaliongezea shehena ya mzigo, kwa hiyo ulaji wake wa mafuta, *tyresna break* utaongezeka zaidi. Kwa hiyo, *TANAPA* iangaliwe kwa macho mawili kwa sababu matumizi yake yatakuwa ni makubwa zaidi. Tukumbuke kwamba *TANAPA* ina hifadhi 16 na ni tano tu ndiyo zinazojitegemea zilizobakia zote zinategemea huku. Kwa hiyo, uwezo wa *TANAPA*

kurudisha kwenye Serikali utakuwa mdogo na lazima tuiangalie kwa macho mawili.

Mheshimiwa Spika, kitu cha pili ambacho naiomba Serikali hiki ikifanye kwa umakini mkubwa na kitapunguza gharama, ni ushirikishwaji wa wananchi katika zoezi hili. Ningependa hifadhi hii iwe ni hifadhi ya mfano sasa katika Taifa ili kuondoa yale malalamiko yote yaliyokuwepo katika hifadhi. Sitaki kuamini kwamba ushirikishwaji wa wananchi umekamilika au wameshirikishwa kikamilifu. Sijui *approach* iliyotumika, nimesoma kabrasha lote suaona, lakini niseme tu kwamba kama wananchi watashirikishwa kikamilifu na wakapewa *alternative* nyingine za maisha yao, wao ndiyo watakuwa walini wa kulinda hili.

Mheshimiwa Spika, nimeshamshauri Mheshimiwa Waziri mara nyingi, Zanzibar katika mapori tulikuwa na walini zaidi ya 30 sasa hivi kila pori linalindwa na walini watano kwa sababu wananchi wenyewe ndiyo wanaolinda maeneo yao, lakini wamepangiwa na wameshirikishwa. Sasa sijui *samplesmaana* yake nimesoma ameshirikisha Kamati za Ulinzi na Usalama, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya lakini hajataja kijiji hata kimoja ambacho ameshirikisha na ametumia *approach* gani kuwashirikishwa wananchi na kwa kiasi gani na wao wametoa maoni yao na kukubali, kwa sababu ni lazima itapishana, vijiji 48 kila kijiji kina mahitaji yake tofauti.

Mheshimiwa Spika, uthibitisho katika hilo ukisoma ukurasa wa 15 na ukurasa wa 17, kwenye fungu lile 314 na fungu 332 litakupa uthibitisho kwamba ushirikishwaji wa wananchi umekuwa mdogo wasingeweza kuvunja *beacons* ambazo zimebekwa. Kwa hiyo, waliwashirikisha katika kuonesha ile mipaka ya asili lakini hawajawashirikisha katika zoezi hili zima ambalo wanataka kulifanya nao watafaidika vipi na watakuwa na sehemu gani. Wananchi wakishirikishwa vizuri nasema tena kwamba ulinzi ambao *TANAPA* watapata kazi kubwa ya kulinda utakuwa umekatika kwa sababu wananchi wenyewe ndiyo watakaolinda wakijua watafaidika vipi katika hili. Katika hili pia suaona kama

ametaja WMS, je, katika vijiji hivi 48 vyote hakuna kijiji ambacho kina WMS ambayo ipo pale na imeshiriki vipi na imetoa maoni gani.

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa, uwekezaji wowote, baada ya sasa umeshawekeza kazi kubwa sana iliyopo na ya gharama kubwa ni *marketing*. Sasa Serikali pamoja na TANAPA sijui imejipanga vipi kwa sababu hiki ni kitu kipyä kinaanzishwa katika suala zima la *marketing*. *Marketing* ni gharama kubwa, inahitijî watu wenye weledi, watu ambaao wanaujua undani wa yale mapori na kilichomo mule ndani na namna gani wamejipanga kuitangaza hii ili sasa lile lilokusudiwa liweze kufikiwa. *Marketing* kwa maana mbili; *marketing* kwa maana ya wale wawekezaji watakaokuja kuwekeza pale, namna gani wame wahamasisha, warmewatengenezea miundombinu ya kuhamasika kuwekeza pale, lakini *marketing* na ya wageni ambaao sasa waje kutembelea pale.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya dakika tano, nakushukuru sana.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Magdalena Sakaya nilishakutaja dakika tano pia.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi uliyonipatia pia niweze kuchangia azimio ambalo liko mbele yetu. Niishukuru pia Serikali kwa kuweza kusikiliza ushauri wa Kamati na kuweza kupandisha mapori haya ya akiba kuweza kuwa chini ya TANAPA.

Mheshimiwa Spika, ni matarajio ya wananchi wa maeneo yale kwa sababu maeneo haya yalikuwa ni mapori kutokana na kwamba Serikali ilikuwa haiwekezi kwenye mapori haya ya akiba na yalikuwa ni mapori kiasi kwamba ndiyo maana Wabunge wanasema kwamba yalikuwa ni vichaka vya majambzi na vichaka vya wezi. Matarajio sasa ya wananchi wa maeneo yale kwamba baada ya mapori haya kupandishwa kuwa hifadhi za Taifa watanufaika kikamilifu sana na uwepo wa hifadhi hizi jirani yao.

Mheshimiwa Spika, naomba pia niipongeze *TANAPA* kwa kazi nzuri wanayoifanya chini ya Mkurugenzi wake Mkuu na Watumishi wote wanafanya kazi kubwa sana lakini kwa mazingira magumu sana. Tunapowaongeza majukumu, lazima pia tuangalie namna ya kuwawezesha wapate *finance* ya kutosha kuweza kuwekeza kwenye mapori hayo. Kama *TANAPA* hawatawekeza kwenye mapori haya yakaweza kuwanufaisha wananchi wa maeneo yale kiukweli itakuwa ngumu sana kwa mapori haya kuweza ku-success kwa sababu bado ujangili utaendelea katika maeneo yale kwa sababu hawataweza kufanya doria za kutosha.

Mheshimiwa Spika, pia *TANAPA* wana miradi ya *out reach*, wana miradi inaitwa miradi ya "ujirani mwema" ambapo wanawawezesha wananchi wa maeneo yanayowazunguka kuwajengea miundombinu mbalimbali ya elimu, ya afya na mambo mengine kiasi kwamba inawafanya wananchi wanaona sasa maeneo yale ni maeneo yao. Kwa hiyo kama *TANAPA* wasipowezeshwa waweze kutoa miradi ya ujirani mwema wananchi hawa hawataona umuhimu wa kuweza kuyatunza maeneo haya. Kwa hiyo naiomba sasa Serikali wakati wanaiongezea *TANAPA* mzigo wa majukumu ya kazi pia waangalie namna ya kuwawezesha ili waweze kufanyakazi hii kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, *TANAPA* pamoja na kufanya kazi yao vizuri, kutunza mapori 16 na sasa hivi wameongezewa mengine na wanaendelea kuongeezewa, lakini pia wanalipa kodi zote stahiki kwa Serikali. Naiomba Serikali, kwa kuwa tunaiongezea *TANAPA* majukumu, *TANAPA* iliambiwa kulipa 10 percent ya mapato yake yote kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali, kwa kuwa sasa tunaiongezea *TANAPA* majukumu mazito zaidi, tupungue ile asilimia inayokwenda kwenye Serikali Kuu ili sasa wabaki nayo kwa ajili ya kuwawezesha mapori haya ambayo tunawapa. Tuangalie Ruaha imeshindwa hata kutengeneza barabara vizuri kutokana na kwamba kipato chao ni kidogo.

Mheshimiwa Spika, mapori haya haya tuliyoyafanya kuwa chini ya *TANAPA*, sasa pia yanahitaji utangazaji, lakini

pia yanahitaji kuweza kuhakikisha kwamba miundombinu yake kule ndani inakuwa mizuri. Kwa hiyo pamoja na nia nzuri ya Serikali, kama mapori haya hayatawezeshwa, lakini pia wananchi wale waone faida zake kuhakikisha kwamba hakuna migogoro. Leo *TANAPA* kuweza kuondoa migogoro kwenye maeneo kama Mikumi, hakuna migogoro kabisa na maeneo mengi wametumia rasilimali kubwa, wamefanya kazi kubwa kwa hiyo migogoro ya ardhi, maeneo ya jirani yakiwa kila siku haiishi bado *TANAPA* watakuwa na mzigo mkubwa wa kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, naiomba sasa Serikali kwanza ifanye kazi kubwa kuhakikisha kwamba maeneo yale ambayo wananchi wale wamezunguka ihakikishe kwamba inasaidiana na *TANAPA* kuweza kuhakikisha kwamba wananchi wale wanakubali maamuzi yale yaliyofanywa na Serikali ili waweze kukubali kwamba maeneo yale yatakwenda kuwanufaisha lakini siyo kwa maneno, waone kwa vitendo kwenye maeneo yao. Waone hospitali zinajengwa, waone shule zinajengwa, waone vituo vya afya vinajengwa, waone miundombinu yao inawezeshwa ili wawe *part and parcel* ya maeneo haya ambayo yameweza kupandishwa hadhi kuweza kuwa hifadhi za Taifa.

Mheshimiwa Spika, naunga hoja hii mkono kwa malengo kwamba Serikali ihakikishe kwamba *TANAPA* inawezeshwa vya kutosha na hasa ile *10 percent* ya mapato makubwa kwenye Mfuko wa Serikali ipungue iwe *five percent* ili *percent* inayobaki iende kuwekeza kwenye mapori ambayo tunaipa *TANAPA* mzigo wa kuweza kuendesha.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Magdalena Sakaya. Sasa twende kwa Mdau mwenyewe, Mheshimiwa Christine Ishengoma, Dokta.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi. Kwanza kabisa

naunga mkono hoja ya azimio iliyopo ya kupandisha hadhi Mapori ya Akiba ya Biharamulo, Burigi, Kimisi, Ibanda na Rumanyika Urugundi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono kwa sababu mapori haya yalikuwa yanaleta matatizo ya wananchi hasa waliozunguka mapori haya. Wakati wanaposafiri lilikuwa ni tatizo kubwa kutokana na ujangili, kutokana na watu wanaobeba silaha yaani ilikuwa ni tatizo kweli. Kwa hiyo naamini kuwa hata vijiji vyote vilivyozunguka mapori haya watakuwa wamefurahi sana, watakuwa na amani, watakuwa kwa kweli wanaona vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, kupandisha haya mapori kuwa Hifadhi ya Taifa kutasaidia kuimarisha na kupandisha utalii kwenye nchi yetu kutokana na mapori haya, kutaimarisha na kupandisha kipato cha nchi pamoja na vijiji vinavyozunguka mapori haya na kutaleta amani kwa wananchi wanaozunguka mapori haya. Kwa kweli ni jambo zuri sana na pia kwa kutumia na kuwepo kiwanja cha Ndege cha Chato kitasaidia sana kuwapeleka Watalii wataokuwa wanakwenda kwenye mapori ya hifadhi hizi kwa sababu hizi Hifadhi za Biharamulo, Burigi, Rumanyika, Ibanda zote zinazunguka Kiwanja cha Ndege cha Chato. Pia kuwepo kwa maziwa ya Victoria, Burigi na Mto Ngono kutasaidia sana watalii na kukuza utalii wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nafurahi na sina mengi na naamini kuwa Wabunge wote wataunga mkono na wananchio wote kwa kukuza utalii wa Magharibi na yenyewe itakuwa nzuri sana kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono azimio hili. (*Makofî*)

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Peter Msigwa dakika 10.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi. Dhana nzima ya uhifadhi wa mazingira yaani *Flora* pamoja na *Fauna* wote kama

Watanzania tunapenda sana, lakini masuala kadhaa katika mambo ambayo nimeyazungumza muda uliopita ni lazima kama Taifa tuwe tumejiliza na kujihoji.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu imekuwa na mipango mingi sana na hasa Wizara hii, lakini kuna wakati mwininge mipango hii huwa haifiki mwisho. Kupandisha hadhi mapori ni jambo jema, lakini kabla hatujapandisha ni lazima tujihoji masuala ya msingi sana. Ni kweli kama wenzangu ambao tuko nao kwenye Kamati wamepongeza utendaji mzuri sana wa *TANAPA*, namna ya uhifadhi na kwa kweli *TANAPA* wanafanya kazi kubwa sana ya uhifadhi na kama Bunge tunapaswa tuendelee kuwaunga mkono, lakini bado nauliza swalii lile ambalo wenzangu wameuliza.

Mheshimiwa Spika, *TANAPA* tunazidi kuiongezea mzigo kwa sababu haya mapori yalkuwa *TAWA*, *TAWA* tumeipa mamlaka, sasa *TANAPA* ambayo ni hifadhi zake tano tu ambazo zinaendesha hifadhi zingine 11. Swali ambalo tunapaswa kujiliza kama Serikali na kama Taifa; pamoja na kwamba tunaongeza hizi hifadhi lakini lazima tuwe na mikakati ambayo itasababisha hifadhi hizi ziweze *ku-generate income*. Kama *TANAPA* ina hifadhi tano zinaendesha hifadhi 11 ni dhahiri kwamba mapato mengi ambayo yangeweza kuleta shughuli nyingine za kimaendeleo tunajikuta yanakwenda kuendeleza hifadhi zingine.

Mheshimiwa Spika, sasa niombe Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa ajaribu kutupa picha ni namna gani hizi hifadhi zingine ambazo hazija -*break even* kwa muda mrefu, ni nini mkakati za Wizara kwa hizi hifadhi zingine 11, *time limit* ni kwa kiwango gani hizi hifadhi zitaendelea kuwa tegemezi kwa hifadhi zingine au tutaendelea kuchukua kiwango kile kinachopatikana kwenye hifadhi zingine na kuendelea kutunzwa kwenye maeneo mengine. Hili ni jambo ambalo tunapaswa tuijilize kabla ya kwenda haraka haraka kufanya maamuzi tunayokwenda kuyafanya.

Mheshimiwa Spika, jambo kubwa ambalo tunapaswa tuijilize; kwenye Bunge la Bajeti Mheshimiwa Waziri alikuja

hana na tukapanga mipango mizuri sana ya kukuza utalii Kusini mwa Tanzania na mipango ilikuwa mizuri sana, Serikali ikaenda *World Bank* ikakopa pesa Dola bilioni 150 kuhakikisha maeneo ya Mikumi, Ruaha, Selou yote tunaiimarissha ili tukuze utalii upande wa Kusini. Ni maeneo machache tu, lakini kabla kabla hatuja-take off tumeanza tena maeneo mengine. Tunapenda Tanzania tuiunganishe yote kwa pamoja, lakini hatuvezi kufukuza sungura wawili kwa wakati mmoja. Waziri hajatoa maelezo ya kina ni kwa kiwango gani *REGROW* inaendelea mpaka sasa.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema tuna taarifa kwamba *World Bank* wame-pool out kwa sababu Serikali haiku consistency kwenye maamuzi yake. Wananchi wa Kusini wametutamanisha, wametupa imani, wakazi wangu wa Manispaa ya Iringa wallkuwa na matumaini makubwa kwamba tunakwenda kuinua utalii sasa, wakazi wa Mbeya, wakazi wa Mikumi, hata Selou waliaminisha Taifa hili. Nakuwa na wasiwasi isije ikawa kama wakati ule wa gesi watu waliimba hapa gesi, gesi, gesi, gesi ikaenda, baada ya muda ikapotea tena.

Mheshimiwa Spika, napata tabu kwamba inaonekana hata hii *REGROW* inaweza ikawa kiini macho. Nimwombe Mheshimiwa Waziri atupe maelezo ya kina ni kwa kiwango gani na kwa namna gani kuboresha *Southern Circuit*. Hitaathirika na mipango mingine sasa tunayokwenda tena upande mwingine kabla huku hatujamaliza. Serikali ya Chama cha Mapinduzi imekuwa ni bingwa sana wa kuanzisha miradi na kuachia njiani kama ambavyo wanataka kufanya sasa hivi. Uwanja wa Nduli kwa mfano pamoja na kuongeza runway lakini bado tunahitaji kuwa na jengo la wageni, la wasafiri hatujaimarissha, bado tunahitaji kuwa na barabara kutoka Iringa Mjini kwenda Ruaha *National Park*. Wajumbe wa Kamati wataniambia ni tabu kweli kweli kusafiri kutoka Iringa Mjini kilomita 104 kutoka Iringa Mjini kwenda Ruaha *National Park*, haya mambo hayajafanyika.

Mheshimiwa Spika, tulizungumza mradi huu ulikuwa ukatengeneze barabara nzuri za kwenda Selous kwenye mahotelini na hela tumeshapata. Tumeanza ku-service mkopo, lakini sasa ghafla tumeongeza mambo mengine ambayo wakati bado hatujaimarisha. Niseme siwezi kusema naunga au napinga, lakini kuna maswali mengi yanaleta ukakasi, kwa nini hili jambo lije kwa haraka na haya mapori tunayo?

Mheshimiwa Spika, jambo lingine; wenzangu wanasema itasaidia kupunguza migogoro. Wote hapa ni mashahidi zimetokea kampeni mbalimbali mara tokomeza, mara nyingi, kugombana na wananchi, wafugaji hasa wanapoingia kwenye hifadhi na tumekuwa tukii-*task* Serikali kwamba lazima itenye maeneo ya wafugaji na uhifadhi. Sasa leo watu wanasema kwa kuongezewa hifadhi tutapunguza migogoro, sasa hii migogoro mingine yote iliyoko kwenye hifadhi imetokana na nini? Kwa sababu wananchi huwa wana-*intrude* kwenye maeneo ya hifadhi. Sasa ni kwa kiwango gani Serikali imeweka utaratibu ambao hatutaingia kwenye matatizo kwa sababu hifadhi zote za nchi hii ukienda karibu zote kuna ugomvi katika wafugaji na wahifadhi, kuna watu wanavamia maeneo ya uhifadhi.

Mheshimiwa Spika, sasa tusije tukawa tunakuja hapa kwa haraka haraka, halafu baadae tena tukaingia kwenye shida ambayo kimsingi tusipofanya vizuri tunaingiza gharama kwa *TANAPA* yenyewe kuijendesha, kwa sababu kwanza itaanza kugombana tena na watu. Tunaifanya *TANAPA* iwe adui kwa wananchi kwa sababu hatujapanga mipango vizuri. Watu wakiona magari ya *TANAPA* wanawachukia, watu wakiona mavazi ya *TANAPA* wanawachukia kwa sababu wanaona kama wanaumiza, wakati tulitakiwa tuweke utaratibu mzuri wananchi waone faida ya uhifadhi huu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naomba Mheshimiwa Waziri lazima atuambie ni namna gani mpango huu hautaathiri mpango mzuri ambao umeanza upande wa Kusini. Kusini kuna maeneo, isiwe sifa tu kwamba Ruaha ni kubwa lakini uwekezaji mdogo. Naamini tukienda huku

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

*TANAPA*sasa, watahamisha pesa nyingi sana kuanza kubeba mzigo mkubwa huu wa Magharibi wakati Kusini hatuja-*take off*, hatuja-*take off* kwenye miundombinu, hatuja-*take off* kwenye mambo ya mahotelii, mambo ya *customer service*, mabo ya *customer care*, *hospitality* kwa ujumla iko chini, badala hizi pesa tungeweka kwenye vitu vya msingi ambavyo vingesababisha vitu vya juu vijichukulie vyenyewe, tunaongeza mzigo mkubwa.

Mheshimiwa Spika, nadhani kama Bunge kwa pamoja tungetafakari tusifanye haya mambo kishabiki, wote tunahitaji maendeleo, tunahitaji uhifadhi kama nilivyosema, siko kinyume na uhifadhi kabisa, lakini kama Taifa na kwa pamoja tunatakiwa haya masuala tuyaangalie wka upana, tuone yataleta tija gani. Kwa hiyo kwa ujumla, sikatai au siungi mkono ila nataka kwanza wote tutafakari kwa ujumla tuone ina tija gani hasa kwa kuzingatia *REGROW* naomba nipate majibu ya Mheshimiwa Waziri ili niweze kuwa *comfortable* kama mwakilishi wa Kusini. Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Peter Msigwa. Mheshimiwa Salma Kikwete dakika 10.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza kabisa, naomba niunge mkono Azimio la Bunge Kuridhia Ubadilishaji wa Hadhi Mapori ya Akiba ya Biharamulo, Burigi, Kimisi, Ibanda na Rumanyika-Orugundu kuwa Hifadhi za Taifa. Naunga mkono Azimio hili kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, katika mapori haya kwa kweli hali ya kiusalama kwa wananchi wakati wanatasafiri kutoka eneo moja hadi lingine ilikuwa si yenye mazingira rafiki. Watu wakisafiri ilikuwa ni lazima kuwe na wasindikizaji kwenye maeneo hayo. Kwa kuipandisha hadhi ina maana hali ya usalama itakuwa imeboreka zaidi na ni jambo zuri kwa maeneo yale na ni jambo zuri kwa wananchi wetu wa Taifa letu la Tanzania kwani kila mtu anahitaji usalama, anahitaji kuishi na anahitaji ulinzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika kwenye mapori haya ambayo yamepandishwa hadhi majirani zetu au watu wa maeneo mbalimbali waliweza kuyavamia na kuyamiliki kuwa ya kwao. Kwa muktadha huu sasa hivi hawataweza kuyavamia tena kwa sababu yako chini ya *TANAPA* watayaangalia katika mazingira bora zaidi. Sambamba na hilo, maeneo haya ni muhimu sana katika uchumi wa Taifa letu na maeneo yale yanayozunguka. Maeneo haya ni mazuri kiutalii kwa sababu ndani yake kuna maziwa, Uwanda wa Savana na vyanzo vya maji ambavyo ni muhimu sana katika mazingira ya kiutalii na wananchi ambao wapo katika maeneo yale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tukizungumzia Geita kama Geita kuna Uwanja wa Ndege mkubwa ambao unajengwa. Uwanja huu kwa maeneo haya kupandishwa hadhi hautakuwa tena uwanja ule ambao unaitwa *white sleeping giant* au *white sleeping elephant* matokeo yake watalii kutoka maeneo mbalimbali watautumia uwanja ule na utaweza kuleta tija kwa Taifa letu. Kwa hiyo, ni muhimu sana kwa maeneo haya kupandishwa hadhi ili kuweza kuleta mazingira bora na rafiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, siku za nyuma kuliwekwa maazimio ya maeneo ya Kusini kuwa ni maeneo ya kiutalii, wakati tunazungumzia maeneo haya tusiyaache yale maeneo ya Kusini kwa sababu Kusini kama Kusini iliachwa nyuma kwa muda mrefu. Kwa hiyo, nachoshauri ni lazima yale maeneo ya Kusini yapewe kipaumbele, wakati huku tunatoa kipaumbele na kule kutolewe kipaumbele kwani Tanzania ni moja na sote ni wamoja.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kurudia tena kuunga mkono hoja. Ahsanteni sana kwa kunisikiliza. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Salma Kikwete. Mnaofuata wachache nitawapa dakika tano ili tumalizie hapo, tuanze na Mheshimiwa Innocent Bilakwate atafuatiwa na Mheshimiwa Amina Mollel.

MHE. INNOCENT S. BILAKWATE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii muhimu. Kwanza naunga mkono asilimia 100 kwa sababu kupandisha hadhi mapori haya ni muhimu sana hasa kwa sisi tunaotoka Kagera. Tulikuwa tunapata wakati mgumu kupita kwenye mapori ya Biharamulo, hali ilikuwa mbaya lazima muwe na Polisi vinginevyo mlikuwa mnavamiwa. Baada ya kupandisha hadhi mapori haya tunaamini usalama utakuwepo na tutasafiri salama. Pia wale majangili ambaao walikuwa kwenye yale mapori tunaamini hawatakuwepo tena na usalama utakuwa mzuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono pia kwa sababu mapori mawili ya Ibanda na Rumanyika yako Kyerwa. Mapori haya ni muhimu na yana wanyama ambaao kwa kweli ni muhimu sana. Ninaamini Serikali baada ya kupandisha hadhi mapori haya sasa tutaenda kupata watalii na Serikali Inaenda kuongeza kipato tutakapokuwa tumeweka mazingira mazuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupandisha hadhi mapori haya tunatamani tuone wananchi wetu wanapata elimu ya kutosha ili wasiweze kuvamia tena mapori yale kwa sababu wengine walikuwa wanategemea kwenda kutafuta kuni na kadhalika. Kwa mfano, kule Kyerwa kwangu kuna miti inaitwa Emisambyia, ni miti muhimu sana na ni mirefu sana ikilindwa mazingira yetu yatakuwa mazuri. Nachoomba sana Serikali iendelee kutoa elimu ili wananchi wajue umuhimu wa kupandishwa hadhi mapori haya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine tunatamani waweke mazingira rafiki hata kwa watalii wanaokuja. Pawepo na barabara, mahotelii mazuri ili kuwavutia watalii kufika kwenye maeneo yale. Tunatamani hata wananchi ambaao wanazunguka maeneo haya waweze kunufaika. Wananchi waone shule zinajengwa kupitia mapori haya na miundombinu mingine mizuri inaimarishwa ili wananchi waendelee kuiunga mkono Serikali na kuyalinda mapori haya kwa sababu tunajua wananchi wengi ndio wamezunguka mapori haya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, mimi naiunga sana mkono Serikali kwa kupandisha hadhi mapori haya. Kule kwangu kuna Majimoto Mtagata, niwakaribishe sana Waheshimiwa Wabunge yale maji yanatoa moto na watu wengi wamekuwa wakienda pale wakiamini katika yale maji kupokea uponyaji. Tunawakaribisha sana Waheshimiwa Wabunge mfike Kyerwa, mjionee maajabu ya Mungu.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Amina Mollel dakika tano atafuatiwa na Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko dakika tano pia.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Awali ya yote, nailpongeza Serikali kwa umamuzi wake wa busara kwa kuleta Azimio hili katika kuyabadilisha Mapori haya ya Akiba ya Biharumulo, Burigi, Kimisi, Ibanda na Rumanyika pamoja na Orugundu kuwa sasa Hifadhi za Taifa. Kwa maana hiyo basi Hifadhi za Taifa zitaongezeka kutokana na upandishwaji wa mapori haya.

Mheshimiwa Spika, naomba nitaje faida zitakazopatikana kutokana na hifadhi hizi zilizoanzishwa. Kwanza kabisa, pato litakalopatikana litaongezeka katika pato la Taifa na vilevile ajira zitapatikana na hivyo vijana wanaoishi katika maeneo yale kwa namna moja au nyingine itawasaidia sana hasa katika zile kazi kwa mfano za kuongoza watalii na shughuli nyingine mahoteli yatakapojengwa wataweza kupata hizo ajira.

Mheshimiwa Spika, miradi ya ujirani mwema inayotekelezwa na *TANAPA* na nichukue fursa hii kumpongeza Mkurugenzi wa *TANAPA* kwa jinsi ambavyo wanatekeleza sera ya ujirani mwema. *TANAPA* wamekuwa wakisaidia wananchi wanaoishi maeneo majirani na hifadhi zetu kwa kujenga hospitali na kuboresha miundombinu ya elimu katika maeneo haya. Kwa hiyo, niwapongeze sana *TANAPA*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, uwepo wa Uwanja huu wa Ndege ambaao kwa kweli kwa muda mrefu umekuwa ukizungumzwa sasa tunaona busara za Mheshimiwa Rais wetu kwa kuona mbali kwamba sasa watalii wataweza kufika kwa haraka zaidi pale na kuweza kutembelea hizi hifadhi zetu. Tunafahamu Geita imebarikiwa na Mwenyezi Mungu kuwa na madini, kwa hiyo, wawekezaji wataweza kufika kwa urahisi zaidi. Madini haya pia yataweza sasa kutangazwa kwa undani zaidi kutokana na hifadhi hizi kwa hiyo wawekezaji wengi watapenda kwenda kule kuwekeza mahotelii na miradi mbalimbali. Kwa hiyo, kwa kweli tunaona kabisa kwamba Geita itakwenda kubadilika lakini na maeneo mengine jirani na uwanja huu sasa ndiyo utakaokuwa chachu kubwa ya maendeleo. Vilevile uanzishwaji wa hifadhi hizi kutachangia utunzaji wa mazingira. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niende tu haraka katika kuishauri Serikali kwa sababu tunafahamu kwamba faida ni nyingi. Hivi karibuni Mheshimiwa Waziri Mkuu alizindua *channel* ya kutangaza utalii *Channel* ya Safari pale *TBC* na Waheshimiwa Mawaziri walikuwepo. Kwa hiyo, sasa ni wakati muafaka kabisa wa kuitumia hii *Safari Channel*/kuweza kutangaza utalii wetu na hasa hifadhi hizi mpya ili wananchi waweze kutambua na kupata ule muamko wa kwenda kutembelea hifadhi zetu. Kwa maana kwamba wananchi watakapokwenda kutembelea hifadhi hizi, kwanza ni njia mojawapo ya kupunguza msongo wa mawazo unapokwenda kule unasahau mengine na kuona utalii uliopo kule. Kwa hiyo, nashauri sana kuitumia hii *channel* ili iweze kutagaza huo utalii wetu.

Mheshimiwa Spika, wito wangu vilevile wananchi wanaoishi maeneo jirani na hifadhi hizi kuona kwamba wao ndiyo wanakuwa chachu ya kutunza mazingira na kuhifadhi hifadhi hizi.

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Amina.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii, Mungu ibariki Tanzania, Mungu mbariki Rais wetu, bariki Baraza la Mawaziri, wewe mwenyewe Spika na Watanzania wote kwa ujumla. *A Luta continua*, mapambano bado yanaendelea. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Amina Mollel. Tunaendelea na Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko.

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Spika, nami nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja hii muhimu sana. Hata hivyo, nina mambo mawili. La kwanza ni kuwakumbusha wenzetu kwamba mapori haya ya Burigi na Biharamulo yako jirani na Mkoa wa Kigoma na pori letu mashuhuri sana la Kigosi Moyowosi. Nilitarajia katika kufanya Burigi, Biharamulo ziwe *National Parks* na Kigosi Moyowosi ingekuwa *National Park* kwa sababu haya mapori yanategemeana na yako jirani sana. Isitoshe katika Pori la Kigosi Moyowosi kuna eneo la *Ramsar site*, eneo chepechepe ambalo kwa kweli kwa wenzetu wa *UNESCO* wameshalitangaza kama ni urithi wa dunia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nilitarajia kwa muktadha huu na kwa dhamira hii njema kwamba Burigi, Biharamulo inge-incorporate na *Kigosi Moyowosi National Park* kwa sababu ikolojia ile ni moja sisi tunatoka maeneo yale tunafahamu. Hofu yangu ni nini sasa? Endapo Kigosi Moyowosi mtaiacha tafsiri yake ni kwamba wale majangili na watu wabaya wataacha Burigi na Biharamulo *National Parks* watashuka huku, ni kushuka tu pale, kwa sababu kutoka Biharamulo kuja Kigosi Moyowosi ni chini ya kilomita 60, ni jirani sana. Kwa hiyo, angalizo langu kwa nia njema hiihii, naomba sana Mheshimiwa Waziri na timu yako hata ikiwapendeza basi Kigosi Moyowosi na Malagarasi *wetland* iwe chini ya uangalizi wa *TANAPA* vinginevyo yale maeneo yanaharibika sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lingine ni kulinda Mto Malagarasi. Mto huu jiografia yake ilivyo unapita katikati ya Pori la Kigosi

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Moyowosi na umeharibika sana kwani umevamiwa sana. Kwa hiyo, nasema tena ni hoja njema sana, ni jambo jema sana tena isitoshe limechelewa kwa sababu mimi nimewahi kuhudumu kwenye Tume ya Wanyamapori katika mambo tuliyoyapendekeza miaka ya 2013 ilikuwa ni kufanya mapori haya yote yawe *National Park* ili kupunguza uhalifu, ujangili na kadhalika. Ombi langu na angalizo langu kwa Serikali ni kwamba angalieni namna bora sasa ya kuilinda Kigosi Moyowosi kwa sababu wewe Spika ni Mhifadhi ni ikolojia ile ile tu na wanyama ni wale wale tu, mkibana huku Biharamulo maana yake uhalifu utashuka Kigosi Moyowosi. Kwa hiyo, angalizo langu kwa Serikali lilikuwa ni hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia nadhani Mheshimiwa Waziri anakumbuka kwamba wale ndege wasiopatikana popote duniani mwezi wa Juni na Julai wanakwenda Kigosi Moyowosi. Uwanja wa Ndege wa Kigosi Moyowosi ulijengwa na wawekezaji, kwa hiyo, Uwanja wa Ndege wa Chato utasidia sana kwani watalii watatoka Chato wanashuka kwa ndege na ni dakika 20 au 15 wanakuja Uwanja wa Ndege wa Kigosi Moyowosi. Ule uwanja wa ndege bado upo na ni uwanja muhimu sana. Kwa hiyo, maeneo haya ni mazuri sana kwa ajili ya *ku-promote* utalii katika Taifa letu. Nina hakika kupandisha hadhi mapori haya na ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Chato eneo lile sasa litaimarika katika tasnia hii ya utalii.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, nilitaka niongezee hayo kwa ajili ya umuhimu wa Kigosi Moyowosi. Ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa James Mbatia dakika tano.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Kwanza, Tanzania tumebahatika kuwa kwenye eneo zuri sana la vivutio hivi vyaa utalii. Ukiangalia ikolojia yetu Tanzania na ukiangalia vivutio vyaa utalii Tanzania na tukijilinganisha na dunia sisi tuko katika wale watano bora duniani kwenye vivutio vyaa utalii. Kwa mfano, ukiangalia *GDP*

ya Taifa letu na ukiangalia fedha za kigeni za Taifa letu leo utalii unaongoza nchi yetu hii kwenye fedha za kigeni. Kwa takwimu za mwaka jana zilikuwa ni shilingi bilioni 2.4 ambayo ni asilimia 28 ya fedha zote za kigeni zinatokana na utalii.

Mheshimiwa Spika, sasa utalii huu unawezeshwa na zile hifadhi zetu za Serengeti ikiongoza, *KINAPA*, Tarangire, Manyara, Arusha na Ngorongoro pia. Tunahitaji Wizara ikawa na *vision* yenye mwelekeo au mpango mkakati sahihi. Watuambie ule mpango mkakati wa 2022 umefikia wapi ili ku-*double GDP*na *forex* kwenye utalii? Kwa mfano, *Southern Corridor*, Ruaha, Mikumi na kwingine, hizi hifadhi tano ambazo ndio zina *break even*, ambazo zinazalisha zile nyingine na *TANAPA* wanafanya kazi nzuri sana chini ya Jenerali Waitara kama Mwenyekiti wa Bodii, Allan Kijazi - Mkurugenzi wa Bodii, kwa kweli nawapongeza sana *TANAPA* kwa kazi kubwa sana wanayoifanya, wanafanya kazi kubwa sana na nzuri katika Taifa letu lakini tujiangalie kidunia miundombinu hii ya utalii ikoje? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa takwimu za mwaka juzi tunaonekana kwenye ushindani wa miundombinu ya utalii zikiwepo barabara zetu, viwanja vyetu vya ndege, vyuo vinavyohudumia watalii, hoteli kwa pamoja tunashika nafasi ya 110 kati ya nchi ya 133. Sasa ni namna gani tunaimarisha hii miundombinu kwenye hifadhi zetu iweze kwenda sambamba na kuhakikisha tuna- *double GDP*na *forex* yetu na kuhakikisha hifadhi zote hizi mpaka za Moyowosi anazosema Mheshimiwa Nsanzugwanko na Tanzania yote Mwenyezi Mungu aliyotujalia mambo haya yanakuwa ni endelevu. Tukiwekeza vizuri hapa, hata sekta nyingine zikisuasua lakini hii Mwenyezi Mungu aliyotupatia tuhakikishe inakwenda kwa kasi kubwa. Kwa hiyo, tuwekeze miundombinu ya kutosha kwenye sekta hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia ile asilimia 10 ambayo *TANAPA* wanachangia kwenye Mfuko Mkuu basi iondolewe moja kwa moja irudi kwenye miundombinu ya utalii. Vilevile *Southern Corridor* ambayo imeshaanza tusiachie katikati na hizi

nyingine zote ambazo zimeletwa kwa Azimio hili tuziangalie ili Tanzania iwe ni sehemu nzuri na salama kwa vivutio vyetu.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa muda ulionipatia. (*Makof*)

SPIKA: Mheshimiwa Angelina Mabula, dakika tano tafadhali atafuatliwa na Mheshimiwa Kanyasu dakika tano.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA

MAKAZI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii na mimi nichangie Azimio la Bunge la Kuridhia Ubadilishaji wa Hadhi ya Mapori ya Akiba ya Biharamulo, Burigi, Kimisi, Ibanda na Rumanyika ili kuwa Hifadhi za Taifa. Nianze pia kwa kuwapongeza sana ndugu zetu wa *TANAPA* chini ya Kijiji ambao wanafanya kazi moja nzuri sana. Nawapongeza pia kwa kuwa na mahusiano mazuri na majirani zao. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya Waheshimiwa Wabunge ambao wamezungumzia habari ya migogoro pengine inaweza ikaongezeka kwa sababu watu wengine walikuwa wanapata kipato katika maeneo yale. Naomba niwatoe hofu kwanza katika zoezi hili zima ambalo litakwenda kufanyika baada ya Azimio kupita maana yake elimu itakuwa ni endelevu katika maeneo yale inavyofanyika kwa wananchi wengine wanaokaa jirani na Mapori ya Akiba. Wananchi wale huwa wanapewa elimu ya kuwa walinzi wa maeneo yale na kuelezwfa faida watakazozipata kutokana na ule Mfuko wa Ujirani Mwema ambao wenzenetu wa *TANAPA* wanawasaidia.

Mheshimiwa Spika, mbali na kuimarisha uhifadhi pia, watakuwa na zoezi hilo lingine la kuona kwamba, wanajivunia nchi yao kwa kuwa na rasilimali ambazo zinaongeza kipato, lakini pia katika suala zima la kuvutia watalii wanapokuwa wanakuja katika maeneo yale, wananchi walioko kule watakuwa na fursa pia, za kuweza kufanya mambo mengine, ikiwa ni pamoja na kuwa na bidhaa za kiutamaduni ambazo itakuwa ni manufaa kwoo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pia naomba niwaambie tu Waheshimiwa Wabunge kwamba, tumekuwa na zoezi ambalo limekuwepo chini ya *TANAPA* wamelfadhili katika kupanga mpango wa matumizi ya ardhi katika maeneo yanayozunguka mapori. Nina imani na nina uhakika katika hili ambalo linakwenda kufanyika sasa watu wale pia, watapata huduma hiyo ya kuwa na mpango wa matumizi bora ya ardhi kwenye yale maeneo, watapata fursa zote kama ambavyo wanapata wengine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ile hofu ya migogoro naomba tuiondoe kwa sababu, pia Serikali imedhamiria kuhakikisha kwamba, migogoro yote katika maeneo ya hifadhi, migogoro yote kwa wale wanaopakana na hifadhi inaondolewa. Kubwa ni kutoa elimu, pia kuwafanya wale wananchi wajitambue kwamba, zile ni rasilimali zao na ni sehemu ya ulinzi katika maeneo yale. Kwa hiyo, hayo wakiyajua yatakuwa hayana shida yoyote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia, napenda niseme jambo lingine katika wale watu wanaokaa katika maeneo yale, usalama utaongezeka. Tumekuwa wote tunajua unakwenda maeneo unasindikizwa na Polisi na uko ndani ya nchi yako. Usalama wa maeneo yale ulikuwa ni mdogo sana. Kwa hiyo, kwa kuyafanya kuwa hifadhi usalama utaimarishwa, lakini pia wananchi wenyewe watajiona wako salama ndani ya nchi yao. Ni maeneo ambayo kidogo yalikuwa na changamoto. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri nimefanya kazi Kagera na nilikuwa Muleba na Pori la Burigi linapakana katika maeneo hayo, kwa hiyo, maeneo yale hata ukienda kikazi ilikuwa unatakiwa uende na askari. Sasa unakwenda na askari mchana kwenye eneo lako, kwa hiyo, nina imani ulinzi utakwenda kuimarka. Kwa hiyo, tuwatoe hofu wananchi hasa wale waliokuwa wanafaidika na mapori haya. Nia ya Serikali na dhamira ni njema sana ni kuwawezesha pia wao kiuchumi katika kufungua fursa zingine ambazo zitawafanya wao pia waweze kufaidika na rasilimali iliyoko katika nchi yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa fursa hii.
(Makofii)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Sasa Mheshimiwa Kanyasu, Naibu Waziri wa Maliasili, dakika tano tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii ambayo umenipatia. Naomba niwashukuru wote ambaao wamepata nafasi ya kuchangia, lakini pia niwashukuru kwa sababu asilimia kubwa ya wachangiaji wameunga mkono hoja na sisi ambaao tumeleta hoja hii tumeifarijika kuona kumbe ulikuwa ni mtazamo wa kila mtu kuona umuhimu wa hifadhi hii kuwa *National Park*.

Mheshimiwa Spika, kama alivyomalizia kusema Mheshimiwa Angelina Mabula, watu wengi ambaao hawajawahi kufika BBK hawaifahamu vizuri. Ukiwa BBK upande ambaao tunapakana na nchi jirani kuna vijiji vinakwenda mpaka kwenye mto, mpaka wetu ni mto, lakini ukivuka mto peke yake unaingia kwenye BBK hizi ambazo tunazungumzia hii Kimisi, Burigi pamoja na Biharamulo. Maana yake ni kwamba, upande wa pili palikuwa na watu ambaao wana *access* ya moja kwa moja na *game reserve*, lakini upande wetu huu kwa sababu, mpaka ni mrefu na kwa sababu ya uwezo ambaao *TAWA* walikuwa nao tulikuwa tunshindwa kwa kweli kimsingi kusimamia ulinzi vizuri.

Mheshimiwa Spika, sasa tunafarijika kuona kwamba, baada ya kuwapatia *TANAPA* na kama walivyosema Wajumbe wengi ni kwamba, *TANAPA* kimsingi wanazo *financial muscles* ambazo zitatusaidia sana kwenye kuimarisha ulinzi. Katika kuhakikisha kwamba, hili linaungwa mkono na kauli hii, baada tu ya sisi kuonesha kwamba, tunataka kuichukua hii kuwa *TANAPA*, tayari *TANAPA* wamekwishatengeneza kilometra 121 za barabara, wamekwishapeleka magari matano kwa ajili ya kuimarisha doria, wamenunua maboti mawili kwa ajili ya usimamizi kwenye Ziwa Burigi na Ziwa Ngoma. Pia lakini tayari

wametambua maeneo nyeti ya uwekezaji kwa ajili ya ujenzi wa hoteli na wameongeza idadi ya wafanyakazi katika eneo hili na kupeleka wafanyakazi 70. Kwa hiyo, utaona utayari wa *TANAPA* katika kuhudumia eneo hili ni mkubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, suala la ushirikishwaji; tangu tulipokuja na wazo hili tumezitumia Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya, lakini Viongozi wa Vijiji wa maeneo husika. Wote hawa wametumika katika kutoa elimu na kuwaeleza faida ambazo zitapatikana kutokana na eneo hili kuwa hifadhi ya Taifa. Hata hivyo, elimu itaendelea kutolewa kwa sababu, elimu ni suala la kudumu. Naamini kwamba, wananchi wa maeneo haya wamejiandaa vizuri zaidi kupokea eneo hili kuchukuliwa na *TANAPA* kwa sababu za historia ya *TANAPA* yenyewe namna inavyofanya kazi, lakini faida ambayo wanaipata.

Mheshimiwa Spika, tunategemea watapata faida gani; la kwanza, tunaamini kwamba, eneo lile likishafanyika uwekezaji wa kutosha, ukiacha suala la usalama lipo suala la biashara. Maeneo yale yatachangamka sana kibiashara, kutajengwa hoteli za ndani na nje ya eneo hilo ambazo zitafanya mzunguko wa pesa katika eneo hilo kuwa mkubwa, lakini tutaimarisha zaidi *cultural tourism*. Maeneo mengi sana ukiwa unatoea Arusha ukija kufika Serengeti wananchi wa maeneo yale wanaona umuhimu wa uwepo wa Ngorongoro na Serengeti kwa sababu, wakati watalii wanaelekea kwenye kitalii Serengeti na Ngorongoro wanapita kwenye maeneo ya wananchi na kuona namna ambavyo wananchi wanashiriki kwenye utalii. Vile vile, tunaamini kwamba, usimamizi mzuri wa mazingira utaimarika ikiwa ni pamoja na ongezeko kubwa la ajira. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Msigwa ameonesha dalili ya kwamba, nikitafsiri vizuri lugha yake ni kama anaona kunafanyika upendeleo kupeleka *TANAPA* sasa hivi BBK na kuacha *REGROW*, Mheshimiwa Waziri wangu atazungumzia vizuri kuhusu *REGROW*, Lakini nataka nimtoe wasiwasi kwamba, nchi hii ni moja, mtazamo ambao Serikali inao kuhusu Kusini ni mtazamo uleule ambao inao kuhusu Kaskazini,

kuhusu Magharibi na sehemu nyingine zote na kwamba, haya hayafanyiki ili kuondoa umuhimu wa eneo la *Southern Circuit*.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa mchango wako mzuri sana, dakika zenyewe chache tu. Labda Waheshimiwa Wabunge niseme mawili matatu kidogo, kama alivyosema Mheshimiwa Nsanzugwanko, ni mdau kwenye mambo haya ya uhifadhi, kwa hiyo, jambo kama hili linanigusa kwelikweli maana nimetokea huko na nimekulia huko. (*Makof*)

Hifadhi hizi kupandishwa hadhi kuwa *National Park* ni jambo la msingi sana ambalo naliunga mkono. Tunatengeneza *circuit* nyingine sasa ya Kaskazini Magharibi mwa nchi yetu ambayo itakuwa na Kisiwa cha Saanane, itakuwa na *Rubondo Island* na hizi hifadhi tano Burigi, Biharamulo, Kimisi, Ibanda na Rumanyika Urugundu. Pia tukumbuke hizi hifadhi zinakuwa ziko karibu na nchi mbili Rwanda na Burundi, kwa hiyo, kule Rwanda kuna hifadhi ile ya Kagera, lakini Uganda kuna *Lake Mburo* na nyingine ambazo ziko Masaka, Mbarara na kadhalika. Nimeshazunguka zunguka kote kule miaka hiyo, enzi hizo. (*Makof*)

Kwa hiyo, kwa kadiri muda unavyoenda kutakuwa na mzunguko fulani wa utalii katika kuimarisha pia, Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki *as we go*. Kwa hiyo, ni jambo jema sana litaufanya Uwanja wa Chato uwe *busy*, inatakiwa wananchi sasa wapokee jambo hili kwa sababu, zitatakiwa hoteli zenye viwango, yatatakiwa magari kwa ajili ya watalii ambayo sekta binafsi inatakiwa iingie, wananchi wenyewe, halmashauri zilizoko kule lazima watu wajipange katika namna ya kuhudumia watalii, *customer care* hata kama wewe ni dereva *tax*, hata kama wewe una hoteli ndogo na kadhalika wote lazima wawe na mtazamo wa kuhudumia utalii, haya yote yanahitaji mchakato mkubwa. (*Makof*)

Bahati mbaya sana Waziri wa Fedha hayupo, lakini Naibu wake yupo nataka sana nisemee kuhusu *TANAPA*, wenzangu wamegusa kidogo hapa kwamba, *TANAPA* inahifadhi tano ambazo ndizo zinaleta kipato cha uhakika angalau. Ina hifadhi 11 hadi sasa ambazo zinabebwa na hizi tano sasa tunazi-*load* tano nyingine zinaingia kwenye *box*, kwa hiyo, maana yake mzigo wa *TANAPA* unazidi kuwa mkubwa sana. (*Makof*)

Sasa kwa upande wa Wizara ya Fedha, *TANAPA* huyo analipa *Treasury* asilimia 15 ya mapato yake *gross* kwa mwaka, 15 percent anapeleka *Treasury*. Halafu analipa tena six percent ya *gross* yake, three percent ikiwa inaenda kwenye mambo ya *research* na *training* kwa maana ya Chuo cha Pasiansi na Mweka na hivi vyta utalii na kadhalika na three percent anapeleka kwenye Mfuko wa Utalii unaoitwa *Tourist Development Levy*. Halafu *TANAPA* anapofanya miradi ya maendeleo wako Waheshimiwa Wabunge wamesema ni vizuri wananchi wafaidike na ndio sera ya *TANAPA* ya ujirani mwema; akijenga zahanati kwenye kijiji cha jirani lazima ali pe kodi ya kile alichokifanya. Akijenga madarasa ya shule, akishamaliza kujenga madarasa hayo lazima ali pe kodi ya madarasa yale aliyojenga, yaani ukitafuta *logic* ya mambo hayo huwezi kuipata, tunalibebesha shirika mizigo mizito mno. Pamoja na hayo *TANAPA* haohao lazima walipe 30 percent kodi ya *net income* kama *corporate tax*, 30 percent! (*Makof*)

Taxes zingine zote wao wanakuwa subjective to them, waki-import magari, waki-import mitambo, waki-import nini, lazima walipe kodi, lakini sasa kubwa zaidi imeongeleta hapa *REGROW*; wamesema akina Mheshimiwa Msigwa na wengine hata Mheshimiwa Naibu Waziri amejibu hapa, ni mradi wa zaidi ya dola milioni 150. Mradi ule ni wa kukuza utalii pamoja na maeneo mengine Kusini pia. Huko Kusini *infrastrucure* hakuna, kama ambavyo tunapoanzisha hizi hifadhi tano, *TANAPA* wana mzigo wa kuchonga barabara, kujenga nyumba na makazi ya askari, kutengeneza viwanja vyta ndege vidogo, air strips na kadhalika, miundombinu mingi lazima utengeneze. Kwa hiyo, lazima wa-import ma-grader,

ma-D6, sijui madudu gani, yale yote wakiyaleta lazima walipe kodi kama kawaida. (*Makofi*)

Sasa mradi kama huu *REGROW* ambao unatusaidia sisi wanashindwa kuuanza na miradi hii yote ina *time limit, time iki-expire* mradi unakufa. Hawawezi kuacha kwa sababu, pamoja na kwamba kwenye mikataba imo ile *tax exemption*, lakini kiuhakika hawana hakika kama wakileta ma-grader pale bandarini yatapita kwa maana hiyo, wanachotaka ni *assurance* tu ya Wizara ya Fedha; kwenye mkataba mmekubaliana, lakini *assurance* ipo kwamba, wakileta hii mitambo kweli watapitisha? Ndio hilo ambalo nilipenda niwaombe Wizara ya Fedha msaidie jambo hili, msaidie jambo hili, vinginevyo *TANAPA* peke yake hawawezi, hawataweza. (*Makofi*)

Kuna fedha za inaitwa *CEDCP* ambayo ni *Euro 20 million* na wenyewe mradi karibu uta-expire kwa sababu hizo hizo, kwenye makubaliano iko *tax exemption in practice* haiko. Sasa hawawezi kuleta mitambo na nini katika mazingira haya na *TANAPA* wanahitaji sana hizi *equipments* na zinafanya kazi, huo mradi ukiisha mitambo ile inabaki Tanzania inaendelea kuchonga barabara na kurekebisha mambo mengi mengine. Miradi hii ni muhimu sana naomba sana Wizara ya Fedha muwasikie Wizara ya Maliasili na Utalii ili jambo hili liweze kupita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri wa Maliasili, wenzetu wote *Southern* huko, iwe ni *South Africa*, Namibia, Zimbabwe na wenzao hata Botswana pia, wanazo *department* za uhamishaji wa wanyama ndani ya *TANAPA*, ndani ya *TAWA* wanakuwa na Idara ya Uhamishaji wa Wanyama. Enzi za kuamini kwamba, eneo likishakuwa *National Park* kwa hiyo, hakuna *intervention* yoyote inayoweza kufanyika, wakati huo umeshapita. Kwa mfano mapori haya, ng'ombe walikuwa wamejaa huko ndani, majangili walikuwa wamejaa huko ndani, wakimbizi waliingia, yaani yameharibika kwa kiwango kikubwa, *TANAPA* ana kazi kubwa sana ya kuyatangeneza. Kilichotakiwa ni kwamba, lazima *study* ifanyike kujua ni wanyama gani ambao walikuwepo kutoka zamani. Sasa

wale wanyama wale lazima wawe *stocked*, lazima wakamatwe mahali ambako wako nje ya hifadhi na nini, wasafirishwe waongezwe katika maeneo yale ili huo utalii uwe na maana vinginevyo mtalii aje kuangalia nini? Itakuwa ni ngumu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri, wanyama hawawezi kunyesha kama mvua, lazima wakamatwe katika maeneo ambayo sio ya hifadhi, wapelekwe katika maeneo ya hifadhi. Jambo hili tumekuwa hatulifanyi Tanzania, lakini sasa lazima tulifanye, kule nyuma liliwahi kufanyika; Hifadhi ya Rubondo wanyama wote unaowaona Rubondo pale walihamishwa wale na *Frankfurt Zoological Society* kwa hiyo, sasa hawa akina *KfW* wanaotusaidia na wengine hili jambo la kuhamisha wanyama lazima sasa tuelekee huko. (*Makofi*)

Tuwapate wanyama toka maeneo ambayo wako nje wanazurura hovskyo, wanaharibu mazao ya watu, unaona Waheshimiwa Wabunge wanalamika, ningombwa wale wakamatwe, wawe *captured* wapelekwe katika maeneo *strategically* ambayo na hizi hifadhi zitahitaji hilo zoezi liweze kufanyika na maana yake ni kwamba, lazima yaagizwe magari yanayofaa kwa ajili ya zoezi hilo la *capture*, makubwa ambayo yana *facilities* hizo kutegemea na aina za wanyama, lakini pia ili ku-*capture* wanyama lazima uwe na *helicopter* ikusaidie kufukuza wanyama wale na nini, ziko njia za kukamata wanyama. Huo uwekezaji ni mkubwa kama *TANAPA* hapati hizo *exemptions* anazozihitaji hawawezi kufanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri wa Maliasili, mwisho, nataka kusema kwamba, sasa hebu Ngorongoro nayo ianz kubeba mizigo maana tunaibebesha *TANAPA* tu, tunabebesha *TANAPA* tu, Ngorongoro nao wabebe wenzao. Kuna mapango kama haya ya Kondoa, kuna maeneo kama yale ya Eyasi kule ambako wenzetu hawapendi kuitwa Watindiga wanaitwa Wahadzabe, yale maeneo kama yale ambayo yana taratibu za *cultural tourism almost like Ngorongoro* na maeneo mengine Tanzania nao wabebe mzigzo wana ka-

extra, kidogo, itasaidia sana katika kuimarisha uhifadhi wetu. (Makofii)

Baada ya maneno hayo, nikukaribishe Mheshimiwa Waziri, karibu sana. Mtoa hoja tunakupa dakika 15, ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, Mhifadhi, ahsante kwa fursa hii, Nashukuru kwanza kwa kukubali hoja hii iletwе hapa kwenye Bunge lako Tukufu, lakini pili kwa mchango ambao umeutoa hapa. Japokuwa umenirushia nondo kwelikweli ukijua kabisa ni Daktari Bingwa wa Afya ya Jamii, lakini najifunza haraka.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote kwanza nianze kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Awamu ya Tano kwa kukubali ushauri wetu mbalimbali ambao tumekuwa tukiupeleka kwake, hususan jambo moja kubwa ambalo mwezi Januari, tarehe 15 alilifanyia uamuzi, kwamba, uhifadhi katika Awamu ya Tano ubadilike kidogo tutoke katika misingi ya uhifadhi ya zamani ambayo ilikuwa inajikita kwenye dhana ya *command and control* zaidi tuhamie kwenye uhifadhi ambao unahuishisha maendeleo ya jamii, unafaidisha watu, kwa maana fupi *community based conservation*.

Mheshimiwa Spika, imefika mahali Mheshimiwa Rais ametoa ridhaa yake, lakini pia ametoa mwongozo ambao sasa unatupa dira ya kuweza kutekeleza azma pana tuliyonayo ya kuichora upya tasnia ya uhifadhi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, mambo mengi yamekuwa yakizungumziwa katika nchi yetu kuhusu uhifadhi, lakini mengi yamekuwa yakikwama kwa sababu, wewe bahati nzuri ni Mhifadhi unafahamu ni jinsi gani sheria za uhifadhi zilivyo *rigid*, sheria hizi ni ngumu sana. Ukiwa Waziri wa Maliasili na Utalii unataka kufanya ubunifu kwenye maeneo haya utapata tabu sana kwa sababu, ni lazima upate ridhaa ya

Mheshimiwa Rais, Baraza la Mawaziri limshauri, akupe ridhaa yake, uje upate ridhaa ya Bunge, halafu mrudishie tena Mheshimiwa Rais ndio sasa kitu kitokee. Kwa hivyo, unaweza ukawa Waziri ambaye pengine unapata tabu sana kufanya *innovation* kwenye eneo ambalo umepewa kusimamia kwa sababu ya *rigidity* ambayo ipo kwenye sheria mbalimbali za uhifadhi.

Mheshimiwa Spika, kwa hatua tuliyofikia na mwongozo ambao Mheshimiwa Rais ameutoa sasa tunafarijika kwamba, tunaweza kusonga mbele na kufanya ubunifufutu katika maeneo mbalimbali ambayo tunakusudia kuyafanya kazi. Mheshimiwa Rais ameturuhusu turekebishe mipaka ya maeneo ya uhifadhi na hii ni mojawapo ya jithada ambazo tunafanya.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hilo, kwa mfano, kuna baadhi ya misitu ya *reserve*, tutaikata tatarudisha kwa wananchi ili kupunguza *pressure* kwenye maeneo haya ya Hifadhi za Taifa, ndiyo ile dhana ya *community based conservation* itafanya kazi ipasavyo. Kwanza lazima tutatue changamoto za wananchi, wananchi wanahitaji maeneo kwa ajili ya kuchunga, makazi, kilimo na uchimbaji wa madini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, maeneo kwa kiasi kikubwa katika mikoa ile yalikuwa yamehifadhiwa, kama si Mapori ya Akiba basi ni misitu ambayo inaifadhiwa kwa mujibu wa sheria, Misitu ya Halmashauri ama misitu ya Serikali Kuu. Kwa hiyo, katika kuchora upya ramani ya uhifadhi katika mikoa ile, tutaweza kufikia azma ya kuwapa wananchi maeneo ambayo watayatumia kwa shughuli hizo mbalimbali ambazo wamekusudia. Jambo hilo tu peke yake lilihitaji kwa kweli ridhaa ya Mheshimiwa Rais mwenyewe wala siyo uamuzi wa Waziri wa Maliasili na Utalii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba ya kwako yote niyachukue kama ushauri na tutayafanya kazi. Hili la kuhamisha wanyama tunalifahamu na tayari kazi hiyo imeshaanza kufanyika. Nikuhakikishie tu kwamba nimefanya

ziara mara tatu katika Mapori haya ya BBK katika maandalizi ya kuleta hoja hii ya Azimio ya Kuyapandisha hadhi kwenda kuwa Hifadhi za Taifa, maeneo yale yame-recover kwa kiasi kikubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge ambaao tulifanya nao ziara mwaka jana ni mashahidi, tulikutana na makundi makubwa ya tembo yakihama kutoka Burigi na kuhamia upande pili wa barabara ambaao ni upande wa Hifadhi wa Kimisi na pia kuna makundi makubwa ya nyati yapo katika maeneo haya. Vilevile wawekezaji ambaao wamefika kufanya *survey* kwa ajili ya kuja kuwekeza pale ambapo tutatoa fursa ya kufanya hivyo wameanza kupigana vikumbo, kuwania maeneo mbalimbali kwa ajili ya kuwekeza. Hii ni dhahiri kwamba hata kama *private sector* nao wanafikiria kuwekeza mle ni dhahiri kwamba maeneo haya yana vivutio ambavyo vitaleta tija katika kukuza utalii katika eneo husika. Kwa hiyo, tutafanya kazi ndogo za kuhamishia wanyama kama ambavyo umetushauri ambaao hawapatikani kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, lakini kufafanua tu kidogo hili la *Ngorongoro Conservation Area Authority* tayari tumeshawapa maeneo mengi. Maeneo hayo ya Kolo, Miambani na Mapango ya Amboni. Wiki iliyopita nimesaini *administrative directive* ambayo sasa ni Waraka wa kisheria kuyahamisha kutoka taasisi moja kuyapeleka taasisi nyingine. Ngorongoro ana maeneo kadhaa ambayo yana urithi wa kiutamaduni ama yana hadhi ya kuwa *Geopark* kwa sababu ana maeneo mawili ambayo yana hadhi hiyo na yametambuliwa na *UNESCO*. Kwa hiyo, tumeona tumuongeze pia Mapango ya Amboni, Michoro ya Miambani na *Irrigation Scheme* ya jadi pale Engaruka, zote hizi atakuwa akizisimamia na kuziendeleza, kwa hiyo, naye Ngorongoro tumempa mzigo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia taasisi zote za uhifadhi tumezipa mizigo mingine ya kuendesha maeneo mbalimbali ya mali kale. Maeneo ya Kalenga tumempa *TANAPA* kwa sababu yapo karibu na Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, maeneo

ya Isimila tumempa *TANAPA*, Nyumba ya Mwalimu Nyerere ile ya pale Magomeni tumempa *TANAPA* na Kilwa, Songo Mnazi tumewapa *TAWA*. Tumewagawia haya maeneo ili kukamilisha hizi *circuit*.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, ndugu yangu Mheshimiwa Msingwa asiwe na wasiwasi, hiki kichwa kilichokalia hapa ikifika mwaka 2020 tufanye tathmini pamoja na utaona tofauti. Kwa sababu kuna mambo mengi tunayafanya kazi na kwa hakika yataichora upya ramani ya uhifadhi wa nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuunganisha na hoja tu ya Mheshimiwa Nsanzugwanko katika eneo hilo, tunapoelekea kuichora upya ramani ya uhifadhi nchini, pamoja na kupandisha hadhi haya Mapori ya Akiba matano kwenda kuwa Hifadhi za Taifa pia tunakusudia kupandisha hadhi kiini cha mapori ya akiba mengine matatu katika ikolojia hiyo hiyo moja. Pori la Akiba la Kigosi tunachukua kiini tunapandisha kinakuwa *national park*, tunaacha eneo la nje linabaki kuwa *game reserve*. Pori la Akiba Moyowosi tunapandisha hadhi kiini pamoja na ile *Ramsar site* inakuwa *national park*, pembezoni tunaacha inabaki kuwa *game reserve*. Pori la Akiba Ugala tunapandisha hadhi eneo la kiini ile *satellite area* tunaiacha inaendelea kuwa *game reserve*, tunaunganisha na misitu ya hifadhi ambayo ipo katika maeneo hayo ambayo tunaipandisha hadhi pia inakuwa *natural reserves*.

Mheshimiwa Spika, malengo yetu ni kuichora upya ramani ya uhifadhi. Pembezoni kabisa mwa misitu ya hifadhi tunarekebisha maeneo ya vijiji, tunakata ardhi ya misitu tunawarudishia wananchi ili wawe na ardhi ya kutosha. Tunaweka alama za kudumu na baada ya kuweka alama za kudumu sasa tunasisitiza na kuimarisha ulinzi wa maliasili hizo kwamba zisivamiwe. Pamoja na kupunguza maeneo hayo lakini pia kuna maeneo mengine ambayo tutayapandisha hadhi na maeneo mengi mapya tutayaazisha kwa sababu ya umuhimu wake kiuhifadhi. (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, eneo la Wembele na Nyahua Mbuga ni *the only connection* kati ya hifadhi zilizoko Kusini; kwa maana ya *ecosystem* ya Ruaha, Rungwa kuja kuunga kwenye hifadhi zilizopo Kaskazini kuititia Nyahua, Wembele mpaka kutokea Maswa *Game Reserve*. *That's the only connection* ambapo wanyama wanatoka Kusini wanakuja Kaskazini, wanatoka Kaskazini wanaenda Kusini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile maeneo muhimu kama hayo niliyosema *connection* kati ya Burigi, Biharamulo na Kimisi ukiunganisha na Kigosi Moyowosi kwenda mpaka Mahale, Katavi *National Park* mpaka Gombe, hiyo pia ni ikolojia moja. Kwa hivyo, kuna maeneo ambayo tunayapandisha hadhi, kwa mfano misitu iliyopo kule Uvinza, Masito East, Masito West, Misitu ya Tongwe East, Tongwe West tunaiunganisha na *North East Mpanda* yote tunaipandisha hadhi na tunahifadhi katika ngazi ya Kitaifa ama ngazi ya Halmashauri za Wilaya ili kuwe na uhakika wa *corridor* ambazo zinapitika mwaka wote. Kwa sasa hivi maeneo mengine hayo niliyoyataja ni *general land*, kwa hiyo, wanaweza kufanya lolote sasa tunaamua kuyahifadhi kwa mujibu wa sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lengo letu ni kutimiza hilo nililolisema la kuichora upya ramani ya uhifadhi. Vijiji ambavyo kwa mfano viro katikati ya kiini cha maeneo yaliyofadhiwa tunavihamisha, tunavikatia maeneo pembezoni ili kuwa na uhakika kule ndani pako salama na maisha ya huko kwenye hifadhi yanabaki kuwa salama na wanyama hawatolewi katika njia yao ya kila siku na matokeo yake kuvamia vijiji vya watu na kusababisha migogoro ambayo ulikuwa unaizungumzia.

Mheshimiwa Spika, tunafanya hivi kwa msingi mmoja, sisi watoto wa Tanzania tukitembea nchi za nje huko tunajivuna sana kwamba tunatoka Tanzania. Katika mambo ambayo tunajivuna nayo ni urithi wa maliasili ambao tunao na urithi huu unatambulika kimataifa na sisi ni mionganoni mwa nchi ambazo zimetenga eneo kubwa la ardhi yake kwa ajili

ya kuhifadhi maliasili mbalimbali ambazo ni urithi kwa sisi tunaoishi leo na vinavyokuja hapo baadaye.

Mheshimiwa Spika, huu ni urithi wa kipekee, ni *unique feature* ya nchi ya Tanzania na ni urithi ambao unaweza kujizalishazalisha, unaweza kuji-renewhaushi. Ni utajiri ambao haufilisiki kama tutaweza kuuhibadhi na kuutunza na ni utambulisho wa nchi yetu nje ya mipaka ya nchi yetu. Kwa hiyo, jukumu la uhifadhi kwa kweli tunalichukua katika viwango vya juu sana na katika umuhimu wa kipekee na ndiyo maana tumeona tuichore upya ramani ya hifadhi zetu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, ni kweli *TANAPA* inaongezewa mzigo lakini inategemea unalinganisha *TANAPA* na kitu gani. Uongozi wa Jenerali Waitara na Mkurugenzi wetu, Ndugu Kijazi ni dhabiti na imara. Mimi kama Waziri najiridhisha katika taasisi ambazo nimepewa kuzisimamia *TANAPA* ina viwango vya juu sana vya utendaji na ndiyo maana kila mtu hapa anawawmagia sifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, *TANAPA* wana hifadhi 16 tu, kati ya hizo tano (5) kweli zinajиendesha na zinatoa faida ambayo inasaidia kuendesha hifadhi nyingine. Ukitaka kulinganisha sasa *TANAPA* ambaye ana hifadhi 16 na *TAWA* ambaye ana hifadhi zaidi ya 100, utaona migogoro kwa kiasi kikubwa na hizo operesheni zinazozungumziwa hapa zililazimika kufanyika si kwa sababu ya uzembe wa *TANAPA*, hapana, kwa sababu *TANAPA* analinda vizuri maeneo yake, ni kwa sababu kulikuwa na uzembe chini Wizara ya Maliasili na Utalii na mamlaka za Serikali za Mitaa na wakati huo *TAWA* ilikuwa hajaazishwa. Kwa hiyo, kuhamisha baadhi ya majukumu kutoka *TAWA* kuyapeleka *TANAPA* mbali na sababu ambazo tumezisema wakati tunatoa hoja yetu ya msingi ni jambo ambalo pia linapunguza mzigo kwa *TAWA* lakini pia linaimarisha ramani ya uhifadhi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaona pengine ni vyema kwa maeneo ambayo yana umuhimu wa kipekee tukayapeleka *TANAPA* ili yakapata ulinzi wa kutosha. Kwa

mfano, Moyowosi hatuchukui hifadhi yote, tunachukua kiini tu tunampa *TANAPA*, nje ya kiini tunamuacha *TAWA* aendele kusimamia. Lengo letu ni moja, kuongeza idadi ya *men in the boots*, ya askari ambao wako katika eneo husika.

Mheshimiwa Spika, tunafanya hivi siyo tu kwa sababu za ulinzi wa maliasili iliyoko pale lakini kwa sababu za ulinzi mpana wa nchi yetu. Kwa sababu mapori haya yamekaa katika eneo ambalo ni *conflict zone*; kuna wakimbizi na wahalifu wanaotoka katika nchi za jirani. Kwa hiyo, tunavyoongeza *men in the boots* kwenye maeneo haya maana yake pia tunaimarisha ulinzi katika nchi yetu, kwa sababu *patrol* na miundombinu itakuwa mingi na maeneo haya yatabaki kuwa salama. Linakuwa ni jambo la ajabu sisi tunazuia watu wetu wasitumie maeneo haya kwa shughuli zao za kila siku halafu watu wa nchi nyingine wanakuja kuyatumia, ni jambo ambalo halikubaliki kidogo. Kwa hiyo, tumeona bora tuyahifadhi na tuyalinde kwa nguvu zaidi kuliko ilivyokuwa hapo awali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hoja nyingi wamezizungumzia Mheshimiwa Mabula na Mheshimiwa Kanyasu naomba nisizirudie, labda niseme moja hii ya *REGROW* na Sungura Wawili. Mradi wa *REGROW* upo pale pale, fedha zimeshaingia ndani ya Serikali. Nilifafanua hapa siku tatu au nne zilizopita, tunachokifanya ni kuendelea kupatana na wenzetu ili mradi ule uwe na tija zaidi. Kuna haja gani ya kujengewa viwanja vya ndege vya changarawe kwa pesa ya mkopo ambayo nchi yetu italipa wakati tuna uwezo wa kuwataka wanaotukopesha watujengee kiwanja ambacho ni cha *hard surface* (sakafu ngumu) ili kiweze kudumu zaidi. Tunaona *economically hai-make sense* kuwa na *project* ambayo itakuwa ya muda mfupi kiasi hicho, halafu *project* yenyewe si rafiki kwa mazingira.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ukitaka kufanya ukarabati wa kiwanja cha changarawe maana yake ni lazima uchukue *material* humo humo ndani ya hifadhi, kwa hiyo, pia *it is not environmental friendly*. Kwa hiyo, tunaona bora tujenge kiwanja cha ndege ambacho ni cha sakafu

ngumu na ndilo jambo pekee ambalo tumbeki tukizungumza na watu wa *World Bank*. Pesa wameshatoa, ruhusa ya kuendelea na mradi imeshatoka na Mradi wa Kuku utalii Kusini unaendelea. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sambamba na mradi huo, tumepata pesa pia baada ya kuonyesha nia ya kuyapandisha hadhi Mapori ya Akiba kuwa *National Park* kutoka *Global Climate Facility* ambao watatupa pia dola za Kimarekani milioni 100 ambazo zitatusadia kufanya maboresho katika Mapori haya ya Akiba kwa sababu na wao wameona kwamba sisi wenyewe tuna nia ya kufanya hivyo. Malengo yetu ni kutimiza azma ya llani ya Uchaguzi ambayo sasa imedumu takribani miaka 10 ikizungumzia jambo moja; Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano sasa mwaka wa tisa huu wanazungumzia jambo moja kubwa nalo ni *diversification* ya kijilografia ya vivutio vya utalii hapa nchini, haiwezekani tuka-concentrate watalii kwenye kanda moja tu ya nchi yetu, tufungue kanda nyingine. Ndiyo maana tunafungua *Circuit* ya Kusini na Kaskazini Magharibi. Lengo letu ni ku-diversify geographical shughuli za utalii katika nchi yetu ukiacha *Circuit* ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, pia tunafungua *circuit* ya utalii wa fukwe katika ukanda wa fukwe utakaoanzia Bagamoyo kwenda mpaka Tanga. Sasa hivi tuko katika mipango ya awali, tunachora ramani na ile *water front* yote tunaiwekea mkakati. Pia *water front* ya Kilwa sambamba na kutambua umuhimu wa kipekee wa magofu yaliyopo pale Kilwa Kisiwani pamoja na jitihada zinazoendelea za kuifungua *Circuit* ya Kusini pale kuunganisha la *Selous National Park* kwa upande ule wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, tunaichora upya ramani ya utalii na uhifadhi katika nchi yetu na hii ni moja ya jitihada.

*(Hapa kengele illilia kuashiria
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa fursa hii, naunga mkono hoja na naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Dkt. Hamis Kingwangalla, Waziri wa Maliasili na Utalii.

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema hoja imeshatolewa, naomba sasa niwahoji kama mnaridhia ubadilishaji wa hadhi wa Mapori ya Akiba ya Biharamulo, Burigi, Kimisi, Ibanda, Rumanyika -Orugundu kuwa Hifadhi za Taifa.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

(Azimio la Bunge la Kuridhia Ubadiilishaji Hadhi Mapori ya Akiba ya Biharamulo, Burigi, Kimisi, Ibanda na Rumanyika-Orugundu kuwa Hifadhi za Taifa liliridhiwa na Bunge)

SPIKA: Bunge zima limeafiki kwa kauli thabiti kabisa. Jambo hili limepata baraka zote za Wabunge toka pande zote. Ni jambo ambalo kwa kweli linatusogeza mbele kiuhifadhi, kiutalii na aspectnyingine nyingi sana za kimapato katika nchi yetu. Tunakupongeza sana Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Serikali kwa ujumla lakini pia Katibu Mkuu wa Wizara, Mkurugenzi Mkuu wa TANAPA, Bodi nzima na Mwenyekiti wa Bodi. Tunawataki kila kheri TANAPA. (*Makofi*)

Tunajua na tunatambua kwamba ni majukumu makubwa zaidi, mtalazimika kuajiri zaidi na kuwekeza zaidi na yale ambayo tumeyasema tunatumaini Wizara ya Maliasili

na Wizara Fedha mtajaribu kukaa kuangalia hii nira ambayo *TANAPA* wanayo shingoni kwa kweli ilegezwelegezwe kwenye baadhi ya maeneo ili waweze kutekeleza haya majukumu tunayowapa. Vinginevyo tutakuja kuwalaumu baadaye kwamba hawatekelezi kwa matarajio tuliyowapa. Maombi yao ni *genuine* kabisa ni vizuri yakafanyiwa kazi. Kwa sababu tunaelekea kwenye kipindi cha bajeti cha Bunge linalokuja itakuwa ni wakati mwafaka Kamati ya Bajeti nanyi mliangalie jambo hili ili tuwawezeshe hawa wanaotubebea bendera ya uhifadhi katika nchi yetu *TANAPA* na Ngorongoro wawe na unafuu fulani.

Tukumbuke pamoja na juhudi za ndani tunashindana na majirani zetu. Tunashindana na jirani wa hapo Kaskazini, tunashindana na jirani mwingine pale Kaskazini Magharibi, tunashindana na jirani mwingine mdogo mdogo yule naye anakuja mblo, ye ye ana hifadhi mbili tu lakini dah, anajitahidi kweli kweli. *In actual sense* ni moja tu ya wale *gorillas*. Sisi tuna rasilimali za kila aina ambazo Mungu ametupa, ni nchi ya ajabu sana hii, tuna rasilimali kwelikweli.

Mheshimiwa Waziri wa Maliasili enzi hizo niliwahi kutembelea *Tsavo National Park* ambayo ndiyo kubwa kwa jirani; nikazunguka mle kama siku nne au tano. Hifadhi ile ina udongo mwekundu, kwa hiyo, mkizunguka na magari mkitoka huko mko wekundu kama hivi viti vilivyo, vumbi moja kwa moja.

Nikajiuliza mbona wanyama hatuoni na watalii nao wanazunguka. Baadaye tunakuta mabango yameandikwa kwa Kingereza, yameandikwa kwamba kuwaona wanyama katika hifadhi hii ya *Tsavo* si jambo rahisi linataka umakini wa hali ya juu na ukibahatika kumuona mmoja utakuwa umetumia juhudi kubwa. Wanawapa moyo watalii na *binocular* kuangalia hivi kumbe hamna kitu mle, lakini wanatengeneza hela pamoja na maneno yao hayo yote. Sisi hifadhi za kwetu zote ukifika kwenye geti hata hujalingia kwenye *park* tayari umeshaanza kuona wanyama hata hujalipa bado. Kwa hiyo, ni baraka ambayo tumepeewa na Mwenyezi Mungu. (*Makofi/Kicheko*)

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Nimewahi kuzunguka Namibia pia kule, tukaangalia masuala ya michoro ya kwenye mapango. Wakawa wanatupeleka kwenye maeneo unaikuta ile michoro ukitazama sana unaona hii imechorwa na mtu hii hapa katikati hapa hii lakini sisi tunayo michoro *original*/kabisa. Sasa kule wenzetu magari ya watalii yanavyopishana wanaoneshwa kitu ambacho hakipo lakini sisi ni *original* kabisa, kwa hiyo, tuzidi kujitahidi.

Pale jirani na Serengeti kwa jirani zetu kuna hifadhi moja wanaita Maasai Mara ni maarufu sana lakini unakuta simba mmoja amezungukwa na magari 40, 50. Hivi kutwa nzima huyo simba anawinda saa ngapi apate chakula kama kutwa nzima wamezungukwa na magari wanapiga picha, simba wenyewe kumbe hata watano hawafiki, wa kwetu ni *natural* kabisa. Kumbe usiku wanachukua nyama ya ng'ombe wanawalisha, ni simba wa nyumbani siyo simba wa porini. (*Makofi/Kicheko*)

Nilitaka tu kuonyesha tofauti ya *potential* ya utalii tuliyonayo sisi na ule uigizaji ambao wenzetu wanafanya japo wanatengeneza pesa katika uigizaji wanaoufanya. Kwa hiyo, tunawatakia kila la heri, ahsanteni sana na tuna matumaini makubwa.

Naipongeza sana Kamati ya Ardhi, Maliasili ya Utalii, Kamati hii katika miaka yake mitatu hii imefanya ziara ya kwenda kwenye maeneo magumu kabisa. Vile vile wameshatembelea baadhi ya hizi hifadhi ambazo leo tumezipandisha hadhi. Kwa kweli kwa Waheshimiwa Wabunge kuwatoa hapa mpaka kuwapeleka huko Burigi, Kimisi na kadhalika, siyo jambo rahisi sana, linataka wajipange kweli kweli. Pia wameshatembelea Kanda ya Kusini huko, mpaka Ifakara, Mahenge, wapi huko. Juzi hapa wametoka Ruaha huko ndani, ni maeneo ya ndani kweli kweli! Nawapongeza sana Kamati na nawaomba mwendelee kufanya kazi katika mazingira hayo ya kutia moyo. (*Makofi*)

Katibu tuendelee.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Marekebisho Mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka 2019 (*The written Law Miscellaneous Amendment (No. 2) Bill, 2019*)

(Kusomwa Mara ya Pili)

SPIKA: Muswada umesomwa mara ya pili, sasa moja kwa moja nimwite Mwanasheria Mkuu wa Serikali. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, Muswada huu ni muhimu, naomba muwepo muusikilize vizuri. Karibu Mwanasherini.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Spika, kwa unyenyekevu mkubwa na kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 86 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la mwaka 2016, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka 2019 (*The Written Laws Miscellaneous Amendments (No. 2) Acts, 2019*) kama ulivyorekebishwa kwa mujibu wa jedwali la marekebisho, sasa usomwe Mara ya Pili na Bunge lako Tukufu lijadili na hatimaye lipitishe Muswada huu kuwa sehemu ya Sheria za nchi.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru tena Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali Na. 2 wa Mwaka 2019. Naomba pia nitumie nafasi hii kumpongeza tena Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuiongoza nchi hii kwa malengo, ujasiri na uzalendo wa hali ya juu. Nawashauri Watanzania wote tuendelee kumuunga mkono na pia kumwombea kwa Mwenyezi Mungu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia nawapongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Ally Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mawaziri wote kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuwalettea maendeleo Watanzania wote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Mawaziri wote kwa ushirikiano wanaoipatia Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali katika utekelezaji wa majukumu yake. Kwa namna ya pekee, naomba nimshukukru Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Philip Mpango; Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Selemani Jaffo; na Waziri wa Madini, Mheshimiwa Dotto Biteko kwa ushirikiano wao mkubwa walioipatia Ofisi hii ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali, katika uandaaji wa Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, nakupongeza wewe mwenyewe, Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyevitii wa Bunge, kwa kuongoza na kusimamia vikao na mijadala ndani ya Bunge letu kwa umahiri na kwa kuzingatia sheria na kanuni zinazoliongoza Bunge hili. Pia nawapongeza Waheshimiwa Wabunge, kwa kuendelea kutekeleza ipasavyo wajibu wao wa kikatiba wa Kutunga Sheria pamoja na kusimamia Serikali.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Ofisi ya Bunge na Wabunge wote kwa ushirikiano mnaoipatia Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali. Nawapongeza pia watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali wakiongozwa na Naibu Mwanasheria Mkoo wa Serikali, Dkt. Evaristo Emmanuel Longopa, kwa kuendelea kutekeleza majukumu na kazi za Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali kwa ufanisi ipasavyo licha ya kukabiliana na changamoto mbalimbali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali Na. 2 wa 2019, (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 2) Act, 2019*) ambao

uko mbele ya Bunge lako Tukufu. Napenda kuishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti inayoongozwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Mbunge na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge kwa ushirikiano na ushauri walioitupatia wakati wa kupitia Muswada huu Mbele ya Kamati hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati hii ilifanya kazi kubwa na nzuri sana ya kuchambua Muswada huu kwa makini na kusikiliza na kuchambua maoni yaliyowasilishwa na wadau mbalimbali walioitwa mbele ya Kamati hiyo na kuishauri Serikali kuboresha huu. Serikali imezingatia ushauri wa Kamati na imeleta jedwali la marekebisco kwa kuzingatia ipasavyo ushauri huo muhimu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu sasa Muswada wa Sheria ya Marekebisco ya Sheria mbalimbali Na. 2 wa mwaka 2019 wenye lengo la kurekebisha sheria zifuatazo:-

Sheria ya Kwanza, Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, ambayo ni Sura ya 147; pili, Sheria ya Kodi ya Mapato ambayo ni Sura ya 332; tatu, ni Sheria ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya utozaji wa Kodi ya Majengo, Sura 289; nne, Sheria ya Madini ambayo ni Sura 123; na tano, Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura 148.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya marekebisco ya sheria hizi, pamoja na mambo mengine ni utekelezaji wa azma ya Serikali ya kuondoa changamoto mbalimbali kwa wachimbaji wadogo wa madini, wakulima wa zabibu ndani ya nchi na viwanda vinavyotumia zabibu hiyo katika uzalishaji pamoja na kuweka viwango mfuto (*Fixed Rate*) vya Kodi ya Majengo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza azma hii marekebisco husika yanahusisha masuala yafuatayo:Kwanza kupunguza kiwango cha ushuru wa bidhaa kwenye pombe kali, (*spirits*) inayotengenezwa nchini kwa kutumia zabibu zinazozalishwa

nchini kutoka shilingi 3,315 kwa lita hadi shilingi 450 kwa lita; pili, kuondoa kodi ya zuio (*Final Withholding Tax*) kutoka 5% inayotozwa kwenye bei ya kuuzia madini aina zote kwa wachimbaji wadogo hadi asilimia sifuri. (*Makof*)

Tatu, kuweka viwango mfuto, (*Fixed Rate*) kwa kodi ya Majengo badala ya utaratibu wa hivi sasa ambapo kodi ya majengo kwa majengo yaliyofanyiwa uthamini inatofautiana kutokana na thamani ya kila jingo; nne, kuanzisha vituo vya ununuzi wa madini katika maeneo ambayo masoko ya madini hayatakuwepo; tano kuweka taratibu za uingizaji madini nchini; sita, kuweka mfumo madhubutti utakaowezesha wachimbaji wadogo wa madini kununua na kuuza madini katika Vituo vya Ununuzi na Masoko ya Madini; na saba, kuhakikisha kodi zinazohusu leseni za madini zinalipwa kabla ya leseni kuhamishwa, au kufanyiwa sihia kwenda kwa umiliki mwiningine; na nane, kuhakikisha mapato yanayotokana na biashara ya madini yanakusanywa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeona upo umuhimu wa kuwasilisha Muswada huu kwa haraka kupitia Hati ya Dharura ili kuondoa changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja: moja, kupunguza utoroshaji wa madini, unaofanywa na wachimbaji wadogo wa madini kwenda nje ya nchi na hivyo kukwepa kodi wanazotozwa kwenye madini hayo; pili, kuondoa tatizo la wakulima wa zabibu hapa nchini, kukosa soko la kuuza zabibu kutokana na wazalishaji wa vinywaji vikali vinavyotumia zao hilo kutonunua kwa wingi, kutokana na ushuru mkubwa wa bidhaa kwenye vinywaji vikali vinavyozalishwa kwa zao hili; na tatu, kuondoa tatizo la ukwepajji kodi ya majengo na kuhamasisha wananchi kulipa kodi hiyo kwa hiari. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegawanyika katika sehemu kuu sita kama ifuatavyo: Sehemu ya Kwanza yenye Ibara ya kwanza hadi ya pili, inahusu masharti ya utangulizi ambayo yanajumuisha jina la Muswada na namna ambavyo sheria zinazopendekezwa kurekebishwa, zitakavyorekebishwa ndani ya Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili ya Muswada yenye Ibara ya 3 na 4 inapendekeza kurekebisha jedwali la 4 la Sheria ya Ushuru wa Bidhaa (Sura ya 147). Kwanza kwa kufanya marekebisco ya kiuandishi ili kuleta maana iliyokusudiwa; na pili, kupunguza viwango vya ushuru wa bidhaa kwenye pombe kali (*spirits*) inayotengenezwa nchini kwa kutumia zabibu zinazozalishwa nchini kutoka shilingi 3,315/= kwa lita hadi shilingi 450/= kwa lita.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza, lengo la hatua hii ni kuhamasisha viwanda vinavyozalisha vinywaji vikali hapa nchini kutumia mchuzi wa zabibu unaozalishwa na zabibu zilizolimwa ndani ya nchi ili kuhamasisha wawekezaji wengi kuwekeza katika uzalishaji wa vinywaji vinavyotumia mchuzi wa zabibu hiyo na hivyo kuongeza ajira, kuchochea kilimo cha zabibu na kuwaimarisha kiuchumi wakulima wa zabibu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu ya Muswada yenye Ibara za 5 na 6 na 7 inahusu marekebisco ya Sheria ya Kodi ya Mapato (Sura ya 332). Muswada unapendekeza kufuta kifungu cha 83 (b) na aya ya 4(d) ya jedwali la kwanza la Sheria ya Kodi ya mapato ili kuondoa Kodi ya Zuio (*Withholding Tax*) kutoka 5% hadi 0% kwenye bei ya kuuzia madini ya aina zote kwa wachimbaji wadogo. Lengo la hatua hii ni kuwahamasisha wachimbaji wadogo kuuza madini yao katika Masoko ya Madini yaliyoanzishwa chini ya Sheria ya Madini (Sura ya 123) na hivyo kuzuia utoroshwaji nje ya nchi kwa madini hayo.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nne ya Muswada huu inahusu marekebisco ya Sheria za Serikali za Mitaa ya Utozaji wa Kodi ya Majengo, (Sura ya 289). Muswada unapendekeza kufanya marekebisco katika vifungu vya 3, 6, 16, 18 (a) na 29 na kufuta vifungu vya 18, 19, 20 na 22 ili kufanya yafuatayo:-

(a) Kuweka viwango mfuto vya Kodi ya Majengo (*Fixed Rated*) kama ifuatavyo: shilingi 10,000/= kwa nyumba ya kawaida na shilingi 20,000/= kwa nyumba ya ghorofa kwa maeneo ya Makao Makuu ya Halmashauri za Wilaya na

Mamlaka za Miji Midogo. Pili, shilingi 10,000/= kwa nyumba za kawaida na shilingi 50,000/= kwa kila sakafu ya nyumba ya ghorofa iliyopo katika maeneo ya Majiji, Manispaa na Halmashauri za Miji.

(b) Kutoza kodi ya majengo kwa kila kiwanja badala ya kila jengo lililopo ndani ya kiwanja husika kwa maeneo ya Halmashauri za Wilaya pamoja na Miji midogo.

(c) Mamlaka ya Mapato kuendelea kukusanya Kodi ya Majengo katika Majiji, Manispaa na Halmashauri za Miji na Halmashauri za Wilaya, ikishirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hatua hii inatarajiwa kuongeza uhiari wa wananchi kusajili majengo yao na kulipa kodi kwa wakati na hivyo kuongeza mapato ya Serikali yanayotokana na kodi hii.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tano ya Muswada inahusu marekebisho ya Sheria ya Madini (Sura ya 123). Sheria hiyo inafanyiwa marekebisho ya jumla kwa madhumuni ya kutumia msamati sahihi kwa kufuta maneno "*mining rights*" popote yalipotumika katika sheria na badala yake kuweka "*mineral rights*." Madhumuni ya marekebisho hayo ni kutumia msamati sahihi kama ulivyotafsiriwa na Sheria ya Madini ya mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 4 cha sheria hiyo kinafanyiwa marekebisho kwa kuongeza tafsiri mpya ya maneno "*small scale miner, mineral and game houses, mineral or tailings*" na "*raw minerals*." Sababu ya marekebisho haya ni kutoa ufanuzi ili kuleta uelewa wa maneno katika kutekeleza sheria hiyo. Aidha, kifungu cha 9 cha sheria hii kinapendekeza kurekebishesha kwa kuweka masharti ya kuhakikisha mmiliki wa leseni awe amelipa kodi, tozo na ada za leseni kabla ya kusihia leseni kwa mmiliki mwingine. Lengo la marekebisho haya ni kudhibiti upotevu wa mapato ya Serikali. Vile vile kifungu cha 18 kinarekebishesha kwa madhumuni ya kuweka ukomo wa chini wa adhabu kwa makosa ya kufanya biashara ya madini kinyume cha sheria. Kifungu cha 27 cha sheria kinarekebishesha kwa madhumuni

ya kuongeza kifungu kidogo cha (2) na kinachoweka masharti kwa wachimbaji wadogo na wafanyabiashara (*brokers and dealers*) wa madini kuuza na kununua madini yote katika masoko ya madini (*mineral and game houses*), isipokuwa kwa wamiliki wa leseni kubwa na za kati.

Mheshimiwa Spika, vile vile inapendekezwa kuongeza kifungu cha 27C(3) kinachoruhusu wamiliki wa leseni za wachimbaji madini wa kati na wakubwa kuuza madini ndani au nje ya Soko la Madini nchini. Kwa sehemu zisizokwu na masoko ya madini, kifungu 27C(4) kimeongezwa ili kuweka ulazima kwa Tume ya Madini kuanzisha Vituo vya Ununuzi wa Madini vinavyotembea (*mobile stations*) au kuanzisha Vituo vya Uuzaji na Ununuzi sehemu zenye wachimbaji wengi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 27E kinachoanzisha (*Government Minerals Warehouses*) kinarekebishwa kuondoa ulazima kwa wachimbaji wadogo kuhifadhi madini yao katika *Government Minerals Warehouses* na lengo la marekebisho hayo ni kuwapa uhuru wa kuhifadhi madini yao mahali popote watakapoona inafaa.

Mheshimiwa Spika, aidha, vifungu vya 55, 76, 80 na 83 vinarekebishwa kwa madhumuni ya kuakisi kuanzishwa kwa masoko ya madini. Sambamba na marekebisho hayo, inapendekezwa Vituo vya Ununuzi wa Madini vianzishwe katika maeneo ambayo hakuna Masoko ya Madini. Marekebisho hayo yanategemewa kuweka mfumo madhubuti utakaowezesha wachimbaji wadogo kuuza madini yao. Aidha, marekebisho hayo yanalenga kuhakikisha mapato yanayokana na biashara ya madini yanakusanywa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, pia sheria inarekebishwa kwa kuongeza vifungu vipyta vya 86A, B na C vinavyoweka masharti kuhusu uingizaji wa madini nchini. Aidha, inapendekezwa kuweka masharti ya kumpa Waziri mamlaka ya kutengeneza kanuni kuhusu haki na wajibu wa mmiliki wa kibali cha kuingiza madini nchini na pia kutengeneza fomu

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

za tamko la madini na mambo mengine yanayohusiana na utoaji wa vibali vyat kuingiza madini nchini.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kifungu kipywa cha 100E kinaongezwa ili kuruhusu wachimbaji wadogo wa madini kufanya biashara ya makinikia kwa maana ya *mineral ore and tailings*.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Sita ya Muswada yenye vifungu vya 28 na 29 inahusu marekebisho Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (Sura ya 148). Sehemu hii inapendekeza kurekebisha sehemu ya kwanza ya jedwali kwa kuongeza kipengele cha 25 ili kutoa msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwa wachimbaji wadogo wa madini watakaouza madini yao katika masoko ya madini na vituo vya ununuzi wa madini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya; na kwa mara nyingine tena ninashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maelezo ya hoja kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali Na. 2 wa Mwaka 2019 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) No. 2 Act, 2019*). Naomba Bunge lako Tukufu liujadili na kuupitisha katika hatua ya kusomwa kwa mara ya pili na mara ya tatu ili hatimaye uwe sehemu ya sheria za nchi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Tunakushukuru sana kwa maelezo yako ya ufasaha kabisa na jinsi ulivyotupitisha katika nini kinachopendekezwa na hoja yako. Tunashukuru sana.

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

No. 1

5th February, 2019

SPECIAL BILL SUPPLEMENT

*to the Gazette of the United Republic of Tanzania No.1. Vol.99 dated 5th February, 2019
Printed by the Government Printer, Dodoma by Order of Government*

THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO.2)
ACT, 2019

ARRANGEMENT OF SECTIONS

Section Title

PART I
PRELIMINARY PROVISIONS

1. Short title.
2. Amendment of Certain Written Laws.

PART II
AMENDMENT OF THE EXCISE (MANAGEMENT AND TARIFF) ACT,
(CAP.147)

3. Construction.
4. Amendment of Fourth Schedule.

PART III
AMENDMENT OF THE INCOME TAX ACT,
(CAP.332)

5. Construction.
6. Repeal of section 83B.
7. Amendment of First Schedule.

PART IV
AMENDMENT OF THE LOCAL GOVERNMENT AUTHORITIES
(RATING) ACT,
(CAP.289)

8. Construction.
9. Amendment of section 3.
10. Amendment of section 6.
11. Amendment of section 16.
12. Repeal of section 18.
13. Amendment of section 18A.
14. Repeal of sections 19, 20 and 22.
15. Amendment of section 29.

PART V
THE AMENDMENT OF THE MINING ACT,
(CAP.123)

16. Construction.
17. General amendment.
18. Amendment of section 4.
19. Amendment of section 9.
20. Amendment of section 18.
21. Amendment of section 27C.
22. Amendment of section 25.
23. Amendment of section 76.
24. Amendment of section 80.
25. Amendment of section 83.
26. Amendment of section 86.
27. Addition of section 100E.

PART VI
AMENDMENT OF THE VALUE ADDED TAX ACT,
(CAP.148)

28. Construction.
29. Addition of section 55B.

NOTICE

This Bill to be submitted to the National Assembly is published for general information to the general public together with a statement of its objects and reasons.

Dar es Salaam,
5th February, 2019

JOHN W. H. KIJAZI,
Secretary to the Cabinet

A BILL
for

An Act to amend certain written laws.

ENACTED by Parliament of the United Republic of Tanzania.

PART I
PRELIMINARY PROVISIONS

Short title **1.** This Act may be cited as the Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.2) Act, 2019.

Amend-
ment of
certain
written
laws
 2. The Written Laws specified in various Parts of this Act are amended in the manner specified in their respective Parts.

PART II
AMENDMENT OF THE EXCISE (MANAGEMENT AND TARIFF) ACT,
(CAP.147)

Construc-
tion
Cap.147
 3. This Part shall be read as one with the Excise (Management and Tariff) Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

Amend-
ment of
Fourth
Schedule
 4. The principal Act is amended in the Fourth Schedule by-
(a) deleting figure.22.08 appearing in the second column and substituting for it the figure 2208.20.00;

(b) deleting the description "locally produced products of this heading" and the rates thereof appearing under the HS.Code 2208.20.00 and substituting for them the following:

	Description	Unit	Old Excise Rate	New Excise Rate
2208.20.00	Spirits obtained by distilling grape wine or grape marc from locally produced grapes.	/	Tshs.3,315.00 per litre	Tshs. 450.00 per litre
	Other locally produced spirits under this heading	/	Tshs. 3,315.00 per litre	Tshs. 3,315.00 per litre

PART III
AMENDMENT OF THE INCOME TAX ACT,
(CAP.332)

Construction
Cap.332

5. This Part shall be read as one with the Income Tax Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

Repeal
of
section
83B

6. The principal Act is amended by repealing section 83B.

Amend-
ment of
First
Schedule

7. The principal Act is amended in paragraph 4 of the First Schedule-

- (a) in subparagraph (c), by deleting the word "and" appearing at the end of item (v);
- (b) by deleting subparagraph (d).

PART IV
AMENDMENT OF THE LOCAL GOVERNMENT AUTHORITIES (RATING) ACT,
(CAP. 289)

Construction
Cap. 289

8. This Part shall be read as one with the Local Government Authorities (Rating) Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

Amendment
of section 3

9. The principal Act is amended in section 3 by deleting the definition of the terms "authority" and "rateable property" and substituting for them the following new definitions-

"authority" means the Tanzania Revenue Authority;

"rateable property" means-

(a) in the case of a plot with a single building, a building within the jurisdiction of an authority which is in actual occupation and all improvements on, in or under any such building;

(b) in the case of a plot with more than one building, only one building which generates highest rates revenue in that plot,

but does not include mud huts, thatched houses, mud houses and such other similar houses;"

Amendment
of section 6

10. The principal Act is amended in section 6(1) by adding immediately after the word "Municipal Council" the word "District Council,"

Amendment
of section
16

11. The principal Act is amended in section 16 by:

(a) deleting subsections (1) and (1A) and substituting for them the following:

 "(1) There shall be charged property rate at the rate of -

 (a) in the case of city council, municipal council and town council areas:

 (i) ten thousand shillings for ordinary building;

- (ii) fifty thousand shillings for each storey in a storey building; and
- (b) in the case of district council areas:
- (i) ten thousand shillings for ordinary building;
 - (ii) twenty thousand shillings for a storey building;
- Cap .416 Provided that, a fraction of a building belonging to one or several co-owners in accordance with the Unit Titles Act shall be treated as a separate building.”;
- (b) deleting subsections (3), (4), (5), (6), (7) and (8) and substituting for them the following new subsections:
- “(3) The Tanzania Revenue Authority shall have powers to collect rate at a rateable area.
- (4) For purposes of this section, “ordinary building” excludes mud huts, thatched houses, mud houses and such other similar houses ordinarily used for residential purposes.”

Repeal
of
section
18

12. The principal Act is amended by repealing section 18.

Amend-
ment of
section
18A

13. The principal Act is amended in section 18A by deleting the words “rating property and collecting property rate” and substituting for them the words “collecting property rate in collaboration with the local government authority”.

Repeal
of
sections
19,20
and 22

14. The principal Act is amended by repealing sections 19, 20 and 22.

Amend-
ment of
section
29

15. The principal Act is amended in section 29 by deleting the words "general or special rate" appearing in the marginal note and subsection (1) and substituting for them the word "rate".

Construc-
tion
Cap.123

16. This Part shall be read as one with the Mining Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

General
amend-
ment

17. The principal Act is amended generally by deleting the words "mining rights" wherever they appear and substituting for them the words "mineral rights".

Amend-
ment of
section 4

18. The principal Act is amended in section 4 by adding in the appropriate alphabetical order the following new definitions:

"small scale miner" means a holder of a primary mining licence;

"Mineral and Gem Houses" means the Mineral and Gem Houses established under section 27C;

"Minerals Import Permit" means a Minerals Import Permit issued under section 86A;

"mineral ore" means the naturally occurring material in the form of rocks or sediments from which economically valuable minerals can be extracted;

"tailings" means materials left over after the mineral ore is crushed and valuable minerals are extracted from it;".

Amend-
ment of
section 9

19. The principal Act is amended in section 9 by deleting subsection (4) and substituting for it the following:

 "(4) Consent of the licensing authority where it is required under subsection (2) shall not be given unless-

 (a) there is a proof that substantial

developments have been effected by the holder of a mineral right;

(b) there is a Tax Clearance Certificate issued by the Tanzania Revenue Authority; and

(c) there is proof that other charges, fees and payables have been cleared."

Amend-
ment of
section
18

20. The principal Act is amended in section 18 by:

- (a) adding the words "a holder of import permit" immediately after the words "licensed broker" wherever they appear in subsection (1);
- (b) by deleting paragraphs (a) and (b) of subsection (4) and substituting for them the following:
- (a) in the case of an individual, to a fine of not less than five million shillings but not exceeding ten million shillings or to imprisonment for a term of not less than one year but not exceeding three years or to both;
- (b) in the case of a body corporate, to a fine of not less than twenty million shillings but not exceeding fifty million shillings."

Amend-
ment of
section
27C

21. The principal Act is amended in section 27C, by-

- (a) adding immediately after subsection (1) the following new subsections:
- (2) A person who wishes to buy or dispose minerals shall buy or dispose minerals at the Mineral and Gem Houses established under subsection (1).
- (3) Notwithstanding subsection (2), a holder of mining licence and special mining licence may dispose of mineral extracted from their respective licence areas at any market of choice.
- (4) Where there is no Mineral and Gem Houses the Commission shall-
- (a) establish buying stations

whether mobile or stationed within the area where there is active mining activities;

(b) issue broker's licence in respect of specific buying station or stations.

(5) The Minister may, for the purpose of this section and by notice published in the *Gazette*, exempt certain minerals from the requirement of this section.";

(b) by renumbering subsection (2) as subsection (6).

Amend-
ment of
section
55

22. The principal Act is amended in section 55(3) by adding immediately after the word "recovered" appearing in paragraph (c) the words "to a holder of a dealer's or broker's licence".

Amend-
ment of
section
76

23. The principal Act is amended in section 76 by adding immediately after the word "acquire" appearing in paragraph (a) the words "minerals from the Mineral and Gem Houses".

Amend-
ment of
section
80

24. The principal Act is amended in section 80(2) by-

(a) adding immediately after paragraph (b) a new paragraph as follows:
"(c) specify the buying stations from which the applicant may buy minerals;"

(b) renaming paragraph (c) as paragraph (d).

Amend-
ment of
section
83

25. The principal Act is amended in section 83 by deleting subsection (1) and substituting for it the following:

"(1) A broker's licence shall authorize the holder to buy or acquire gold or gemstones in a designated buying station as the licence may specify, and to sell or dispose of minerals so acquired to a licensed dealer at the Mineral and Gem House."

Amend-
ment of
section
86

26. The principal Act is amended-

(a) by adding immediately after section 86 the following subheading:

"(iii) Minerals Import Permit;"

(b) by adding immediately after the proposed sub-heading (iii) the following new sections:

"Conditio **86A.**-(1) A person shall not import any minerals without a Minerals Import Permit issued by the Commission prior or at the entry point.

(2) Subject to the provisions of this Act, a person who wishes to import minerals for processing, disposing or dealing in or marketing purposes shall apply to the Commission for grant of a Minerals Import Permit in respect of the type of minerals he wants to import.

(3) The Commission shall, upon being satisfied with the contents of application, issue a Mineral Import Permit to the applicant in respect of minerals intended to be imported and upon payment of prescribed fees.

(4) The permit holder shall be required to comply with laws and regulations governing the importation of minerals.

Importati
on of
diamon
ds

86B. Subject to section 86A, importation of diamonds shall, in each round of import be subject to the following specific conditions:

(a) the permit holder shall apply for diamond import clearance from

the Commission; and
(b) the permit holder shall submit proof of holding a certificate of compliance to the Kimberly Process Certification System.

Regulation
s on
importatio
n of
minerals

86C.-(1) The Minister may make regulations prescribing:
(a) conditions for Minerals Import Permit;
(b) procedures for application and issuance of Minerals Import Permit;
(c) rights and obligations of the holder of Minerals Import Permit; or
(d) such other matters as may be required for purposes of Minerals Import Permit under this section.

(2) The Minerals Import Permit issued under this section shall be valid for such time as may be stated in the permit."

Addition
of
section
100E

27. The principal Act is amended by -

(a) adding immediately after section 100D the following new section:

"Mineral
ores and
tailings to
be trading
commodit
y

100E. Mineral ores or tailings owned or dealt with by small scale miners shall be a trading commodity in Tanzania."

(b) renumbering sections 100E and 100F as sections 100F and 100G respectively.

PART VI
AMENDMENT OF THE VALUE ADDED TAX ACT,
(CAP.148)

Construction
Cap.148

28. This Part shall be read as one with the Value Added Tax Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

Addition
of section
55B

29. The principal Act is amended by adding immediately after section 55A the following new section:

"Zero-rating supply of minerals by small scale miners
Cap.
123

55B.-(1) Supply of precious metals, gemstones and other precious stones by a small scale miner at the buying station designated by the Mining Commission under the Mining Act or at the Mineral and Gem House shall be zero-rated.

(2) The Minister may make Regulations for the better carrying into effect the provisions of this section.

(3) For the purpose of this section- "Mineral and Gem Houses" shall have the meaning ascribed to it under the Mining Act;

"small scale miner" shall have the meaning ascribed to it under the Mining Act."

OBJECTS AND REASONS

This Bill proposes to amend five Acts namely; the Excise Management and Tariff Act, (Cap.147), the Income Tax Act, (Cap.332), the Local Government Authorities (Rating) Act, (Cap.289), the Mining Act, (Cap.123) and the Value Added Tax Act, (Cap.148).

The proposed amendments to the respective laws are intended to cure the shortfalls occasioned during the implementation of the respective laws.

This Bill is divided into Six Parts. Part I deals with Preliminary Provisions which include the title of the Bill and the manner in which the laws proposed to be amended are amended in their respective Parts.

Part II of the Bill proposes to amend the Excise Management and Tariff Act, Cap.147. The Fourth Schedule is intended to be amended so as to reduce the excise duty for spirits made of locally produced grapes. The aim of the proposed amendments is to encourage manufacturers to use locally produced grapes. The proposal is intended to promote grape farming.

Part III of the Bill proposes to amend the Income Tax Act, Cap 332. Section 83B and paragraph 4(d) of the First Schedule are proposed to be repealed with the view of removing the obligation to withhold tax of 5% payable by small scale miners.

Part IV of the Bill proposes to amend the Local Government Authorities (Rating) Act, Cap.289 whereby sections 6,16, 18A and 29 are proposed to be amended and sections 18, 19, 20 and 22 of the Act are proposed to be repealed. The aim of the proposed amendments is to set a flat rate for property tax and enable the Tanzania Revenue Authority to be the sole collector of property tax in the country. The proposed rates are Ten Thousand shillings for ordinary buildings situated in rural and urban areas, Twenty Thousand Shillings for each storey building situated in rural areas and Fifty Thousand Shillings for each storey building situated in urban areas.

Part V proposes amendment to the Mining Act, Cap.123. The Act is amended generally with a view to using proper terms “mineral rights” instead of “mining rights”. Section 4 of the Act is amended for the purpose of adding interpretation of new terms that have been used in various provisions of the Act and section 9 is amended to include tax clearance as a precondition for transfer of mineral rights. The proposed amendments are intended to ensure that taxes relating to mineral rights are paid before effecting transfer of such rights. Section 18 is amended to provide minimum penalties for offences relating to unauthorised trading of minerals.

Section 27C of the Act is amended to make buying and disposing of minerals in the Mineral and Gem Houses compulsory save for holders of mining licences or special mining licences. In the same vein, the Act is amended in sections 55, 76, 80 and 83 so as to reflect the introduction of Mineral and Gem Houses. It is further proposed that buying stations be established in mineral areas where there is no Mineral and Gem Houses. The said amendments are expected to put in place vibrant mechanism that will enable small scale miners to sell their minerals. Further, the amendments aims at regulating and controlling trading in minerals with a view to ensuring that revenues relating to trading in minerals are efficiently collected. Furthermore, the Act is amended by adding new sections 86A, 86B and 86C to provide for matters relating to Minerals Import Permits.

Part VI of the Bill proposes to amend the Value Added Tax Act, Cap. 148. The Act is proposed to be amended by adding a new section 55B with a view of zero-rating supply of precious metal and gemstones by small scale miners at Mineral and Gem Houses.

MADHUMUNI NA SABABU

Muswada huu unapendekeza marekebisho katika Sheria tano zifuatazo; Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147, Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332, Sheria ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya Utozaji wa Kodi ya Majengo, Sura 289, Sheria ya Madini, Sura 123 na Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura 148.

Lengo la kupendekeza marekebisho haya ni kuondoa upungufu uliodhihirika wakati wa utekelezaji wa baadhi ya masharti yaliyomo katika Sheria hizo.

Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Kuu Sita. Sehemu ya Kwanza inahusu masharti ya Utangulizi ambayo yanajumuisha, jina la Muswada na namna ambavyo Sheria zinazopendekezwa kurekebishwa zitakavyorekebishwa ndani ya Muswada huu.

Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147 ambapo Jedwali la Nne linapendekezwa kurekebishwa kwa kupunguza kiwango cha Ushuru wa Bidhaa kwenye pombe kali (spirits) inayotengenezwa nchini kwa kutumia zabibu zinazozalishwa nchini. Lengo la marekebisho haya ni kuhamasisha viwanda kutumia mvinyo unaozalishwa nchini na hivyo kuinua kilimo cha zao la zabibu.

Sehemu ya Tatu ya Muswada inahusu marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332. Muswada unapendekeza kufanya marekebisho kwa kufuta Kifungu cha 83B na aya 4(d) ya Jedwali la Kwanza. Lengo la marekebisho haya ni kuondoa kodi ya zuio ya 5% kwa wachimbaji wadogo wa madini ili kuwahamasisha wachimbaji wadogo kuuza madini yao katika masoko ya madini.

Sehemu ya Nne ya Muswada inahusu marekebisho ya Sheria ya Serikali za Mitaa ya Utozaji wa Kodi ya Majengo, Sura ya 289. Muswada unapendekeza kufanya marekebisho katika vifungu vya 6,16,18A, 29 na kufuta vifungu vya 18,19,20 na 22. Lengo la marekebisho haya ni kuweka viwango mfuto yya kodi ya majengo na kuiwezesha Mamlaka ya Mapato (TRA) kuwa mkusanyaji pekee

wa kodi ya majengo nchini. Viwango vinavyopendekeza ni Shilingi elfu kumi kwa majengo ya kawaida kwa maeneo ya mijini na vijijini; Shilingi elfu ishirini kwa nyumba za ghorofa katika maeneo ya Vijijini na Shilingi elfu hamsini kwa kila sakafu kwa nyumba za ghorofa katika maeneo ya mijini.

Sehemu ya Tano ya Muswada inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Madini, Sura ya 123. Sheria hiyo inafanyiwa marekebisho ya jumla kwa madhumuni ya kutumia istilahi sahihi kwa kufuta maneno "*mining rights*" na badala yake kutumia maneno "*mineral rights*". Kifungu cha 4 cha Sheria hiyo kinapendekeza kurekeblishwa kwa kuongeza tafsiri ya istilahi mpya zilizotumika katika Sheria hiyo. Kifungu cha 9 cha Sheria hiyo kinapendekeza kurekeblishwa kwa madhumuni ya kujumuisha cheti cha uthibitisho wa kutodaiwa kodi kama moja ya masharti ya uhamishaji wa umiliki wa leseni za madini. Marekebisho hayo yanakusudiwa kuhakikisha kwamba kodi zinazohusu leseni za madini zinalipwa kabla ya leseni hizo kuhamishiwa katika umiliki mwengine. Kifungu cha 18 kinarekeblishwa kwa madhumuni ya kuweka ukomo wa chini wa adhabu kwa makosa ya kufanya biashara ya madini kinyume cha Sheria.

Kifungu cha 27C cha Sheria kinarekeblishwa kwa madhumuni ya kuweka ulazima wa ununuzi na uuzaji wa madini kufanya katika masoko ya madini isipokuwa kwa wamiliki wa leseni kubwa na za kati. Aidha, vifungu vya 55, 76, 80 na 83 vinarekeblishwa kwa madhumuni ya kuakisi kuanzishwa kwa masoko ya madini. Sambamba na marekebisho hayo, inapendekeza vituo vya ununuzi wa madini vianzishwe katika maeneo ambayo hakuna masoko ya madini. Marekebisho hayo yanategemewa kuweka mfumo madhubuti utakaowezesha wachimbaji wadogo kuuza madini yao. Aidha, marekebisho hayo yanalenga kuhakikisha mapato yanayotokana na biashara ya madini yanakusanywa ipasavyo. Pia, Sheria inarekeblishwa kwa kuongeza vifungu vipyta vya 86A, 86B na 86C vinavyoweka masharti kuhusu uingizaji wa madini nchini.

Sehemu ya Sita ya Muswada inahusu marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148. Muswada unapendekeza kufanya marekebisho kwa kuongeza kifungu kipyta cha 55B ili kutoza Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa kiwango cha asilimia sifuri kwenye

madini ya metali na vito yatakayouzwa na wachimbaji wadogo wa madini kwenye masoko ya madini. Lengo la mapendeleko haya ni kuwahamasisha wachimbaji wadogo kuuza madini yao katika masoko ya madini na kudhibiti utoroshaji wa madini.

Dodoma,
30 Januari, 2019

ADELARDUS L. KILANGI,
Mwanasheria Mkuu wa Serikali

**SCHEDULE OF AMENDMENTS TO BE MOVED BY THE HON. ADELARDUS L. KILANGI THE
ATTORNEY GENERAL AT THE SECOND READING OF
THE BILL ENTITLED "THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS)(NO.2) ACT, 2019"**

Made under S.O. 86(10)(b)

The Bill entitled "The Written Laws (Miscellaneous Amendments)(No.2) Act, 2019" is amended as follows:

A: In Clause 9 by deleting the proposed definition of the term "rateable property" and substituting for it the following:

"rateable property"

(a) in City Councils, Municipal Councils and Town Councils, means -

- (i) in the case of a plot with a single building, a building which is in actual occupation including all improvements on, in or under any such building;
- (ii) in the case of a plot with more than one building, all buildings in actual occupation in that plot including improvements on, in or under such buildings;

(b) in District Councils, means-

- (i) in the case of a plot with a single building, a building which is in actual occupation including all improvements on, in or under any such building;
- (ii) in the case of a plot with more than one building, only one building which shall be charged the highest rates in that plot, but rateable property under paragraphs (a) and (b) does not include mud huts, thatched houses, mud houses and such other similar houses;"

B: By deleting Clause 10 and substituting for it the following:

"Repeal and
replacemen
t of section 6

10. The principal Act is amended by repealing section 6 and replacing it with the following:

"Declaration
of rateable
area

6.-(1) An area declared as City Council, Municipal Council, Town Council or District Council shall be a rateable area for purposes of this Act:

Provided that, in District Council only the areas within the boundaries of head quarters of the District Council and Township authorities shall be rateable areas.

(2) For the purpose of subsection (1), the Minister may, in consultation with the Minister responsible for local government and by notice published in the *Gazette* declare-

(a) the boundaries of the head

quarters of District Council and Township authority; and

(b) any other area within the District Council to be a rateable area."

C: In Clause 11(b), in the proposed subsection (4) by inserting immediately after the word "excludes" the words "storey buildings";

D: In Clause 18 by adding immediately after the proposed definition of the term "mineral ore" the following new definition:

"raw minerals" means minerals which are not yet processed, beneficiated or value added, and this meaning shall be subject to regulations governing value addition and shall be without prejudice to the meaning contained in Mineral Development Agreements;"

E: In Clause 19 by deleting the proposed subsection (4)(a) and substituting for it the following:

(a) there is a proof that substantial developments have been effected by the holder of mineral right in accordance with the programme of mining operations under sections 41(3) and 49(2);"

F: In Clause 26(b)-

(a) by deleting the proposed section 86A and substituting for it the following:

"Minerals Import Permit

86A.-(1) A person shall not import any minerals without a relevant Minerals Import Permit.

(2) A person importing minerals shall make a declaration in a prescribed form indicating the type and quantity of minerals intended to be imported and the purpose for importation.

(3) Upon making a declaration under subsection (2), the Commission shall, without prejudice to subsection (5) and sections 86B and 86C, issue to the declarant a Minerals Import Permit prior to importation or at the entry point.

(4) A permit holder shall, upon disposal of minerals imported, pay royalties and inspection fees at the rate applicable.

(5) A permit holder shall comply with laws and regulations governing the importation of minerals."

(b) by deleting the proposed Clause 86B and substituting for it the following:

"Importation of diamonds

86B. A person intending to import diamonds shall submit proof of holding a certificate of compliance with the Kimberly Process Certification System."

- (c) by adding immediately after the proposed section 86B the following:
- "Importation of radioactive minerals shall comply with the provisions of section 125."
- (d) by designating the proposed section 86C as section 86D;
- (e) in the proposed Clause 86D as designated by deleting subsection (1) and substituting for it the following:
- (1) The Minister may make regulations prescribing-
- (a) rights and obligations of the holder of a Minerals Import Permit;
- (b) declaration forms for minerals to be imported;
- (c) format and content of the Minerals Import Permit;
- (d) such other matters as may be required for purposes of Minerals Import Permit."

G: By deleting Clause 29 and substituting for it the following:

29. The principal Act is amended in Part I of the Schedule by adding immediately after item 24 the following exempted item:

" **25.** Supply of precious metals, gemstones and other precious stones by a small scale miner at buying stations or at the Mineral and Gem Houses designated by the Mining Commission under the Mining Act. "

H: By adding immediately after Clause 21 the following new clause:

"Amendment of section 27E of the principal Act is amended in section 27E by adding immediately after subsection (1) the following proviso:

27E

"Provided that, for small scale miners the requirement of this section shall be optional."

Dodoma,
....., 2019

A.L.K
AG

SPIKA: Nichukue fursa hii kidogo kuwatambua wageni wetu. Tunao wageni 30 wa Mheshimiwa Doto Biteko, Waziri wa Madini, ambao ni viongozi na wanachama wa Shirikisho la Vyama vya Wachimbaji Madini Wadogo Tanzania (*FEMATA*) wakiongozwa na Rais wa Shirikisho hilo, Ndugu John Bina. *FEMATA* naomba msimame. Ahsanteni na karibuni sana. Tunashukuru sana kwa uwepo wenu. Tunajua mlikuwa na kikao na Mheshimiwa Rais, mnaona jinsi ambavyo Serikali imewasikiliza. Katika muda mfupi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali analeta mabadiliko yanayohusiana na masuala ya madini. Naamini Waheshimiwa Wabunge wakishafanya maamuzi hapa, ni katika mtakaofurahia maamuzi ya siku ya leo. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Bhagwanji Meisuria ambao ni Vlongozi wa CCM kutoka Chwaka Visiwani Zanzibar wakiongozwa na Ndugu Mlenge Khatib. Ooh, karibuni sana wageni wetu kutoka Zanzibar. Karibuni sana Dodoma.

Yupo mgeni wa Mwantumu Dau Haji ambaye ni mjukuu wake wa kwanza kutoka Kusini Unguja, Ndugu Ayuna Taleed. Karibu, yule pale. Karibu sana. Pia tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Margaret Sitta kutoka Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Anicet Mlay. Karibuni sana. Mwisho ni wanafunzi 200 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma wakiongozwa na Mwalimu wao Dkt. Mnata Resani. UDOM, karibuni sana.

Pia nina wageni wa Spika, *brass band*, mpo! Karibu sana, simameni. Karibuni sana, mnapendeza kweli kweli. Ahsanteni sana maafande. (*Makofi*)

Sasa tunaendelea Waheshimiwa Wabunge na hatua ya Mwenyekiti wa Kamati, naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, ili aje atupitishe katika maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusiana na mapendekezo haya yaliyoletwa mbele yetu na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Mheshimiwa Simbachawene, tafadhali. Ukiweza dakika 20 nitashukuru.

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI: Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati ya Bajeti kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka 2019.

Mheshimiwa Spika, utangulizi, kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni ya Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2016, naomba kutoa maoni na ushauri wa Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka 2019.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeona upo umuhimu wa kuwasilisha Muswada huu kwa haraka kupitia hati ya dharura ili kuondoa changamoto mbalimbali kwa wachimbaji wadogo wa madini, wakulima wa zabibu, viwanda vinyavotumia zabibu hiyo katika uzalishaji wa mvinyo na pombe kali (*valuer brandy*) pamoja na kuweka viwango mfuto vyta ya majengo.

Mheshimiwa Spika, kupitia Muswada huu sheria zifuatazo zinafanyiwa marekebisho: Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147; Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332; Sheria ya Serikali za Mitaa (Utozaji wa Kodi za Majengo), Sura 289; Sheria ya Madini, Sura 123; na Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura 148.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti imejadili kwa kina Muswada huu na Kamati inapenda kuwashukuru wadau wafuatao ambao walifika kutoa maoni yao mbele ya Kamati. Wadau hao ni Shirikisho la Wachimbaji wa Madini Tanzania (*SEMATA*), Umoja wa Wachimbaji Wakubwa Nchini, Umoja wa Mawakala wa Madini Tanzania (*TAMIDA*), Umoja wa Wanawake Wachimba Madini Tanzania (*TAWOMA*), Wawakilishi kutoka Viwanda vya Mvinyo vya *Domia* na *Alko Vintage*, Mjiolojia wa Wachimbaji Wadogo wa Madini ya dhahabu (*Medium Scale Gold Mining Geologist*), Mtandao wa Watoa Msaada wa Kisheria Tanzania, (*Tanzania Network for Legal Aid Providers*), Asasi ya Kiraia ya *Tangible Initiative for Local Development in Tanzania*.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya Muswada; Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka 2019, una lengo la kufanya marekebisho ya sheria tano zilizoainishwa katika utangulizi ili kuondoa upungufu uliojitekeza wakati wa utekelezaji wa sheria hizo. Hatua hii itasaidia:-

- (i) Kupunguza utoroshwaji wa madini kwenda nje ya nchi unaofanywa na wachimbaji wadogo na hivyo kukwepa kodi;
- (ii) Kuondoa tatizo la wakulima wa zabibu hapa nchini na kukosa soko la uhakika la kuuza zabibu kutokana na wazalishaji wa vinywaji vikali vinavyotumia zao hilo kutonunua kwa wingi mchuzi wa zabibu unaozalishwa nchini; na
- (iii) Kukabiliana na changamoto ya ukwepajji kodi ya majengo na kuhamasisha wananchi kulipa kodi hiyo kwa hiari.

Mheshimiwa Spika, Kamati imepitia Muswada huu kifungu kwa kifungu kwa madhumuni ya kujielimisha maudhui ya kila ibara. Baada ya kujiridhisha na maudhui yake Kamati ilifanya majadiliano ya kina na Serikali kuhusu mapendekezo ya marekebisho ya sheria tano zilizopo kwenye Muswada huu. Katika majadiliano hayo Kamati ilikubaliana na Serikali kufanya marekebisho katika baadhi ya vifungu. Pamoja na hayo Kamati ingependa kuwasilisha maoni na ushauri wake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147. Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza marekebisho ya Ibara ya 4 ya Muswada ili kupunguza kiwango cha ushuru wa bidhaa unaotozwa kwenye pombe kali zinazotengenezwa nchini kwa kutumia zabibu, zinazozalishwa hapa nchini kutoka Sh.3,315 hadi Sh.450. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua ya pendekezo hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hatua hii kwanza, itasaidia kuondoa tatizo la upatikanaji wa soko la zabibu kwa wakulima wetu. Aidha, hatua hii itasaidia kupunguza bei ya mchuzi wa zabibu unaozalishwa ndani ya nchi kwa kuwa sasa utakuwa unapatikana kwa bei ya gharama nafuu ukilinganisha na ule unaotoka nje;

Mheshimiwa Spika, pili, itahamasisha na kuendeleza uzalishaji wa zao la zabubi nchini;

Mheshimiwa Spika, tatu, itahamishia uzalishaji na uendelezaji wa viwanda vya kusindika zao la zabibu nchini na hivyo kuongeza ajira na mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya Sheria ya Mapato, Sura 332; Ibara ya 6 na 7 ya Muswada inapendekeza kufuta kifungu cha 83B na aya ya 4(d) ya jedwali la kwanza la Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332 kwa lengo la kuondoa kodi ya zuio ya asilimia tano inayotozwa kwenye bei ya kuuzia madini ya aina zote nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii kwani imejibu haraka kilio cha wachimbaji wadogo kuhusu kodi hiyo. Aidha, hatua hii sasa itahamasisha wachimbaji wadogo kuuza madini yao katika masoko ya madini ambayo Serikali inakusudia kuyaanzisha hapa nchini. Katika maeneo yenye uchimbaji wa madini na hivyo kusaidia upatikanaji wa mapato na takwimu za uzalishaji wa madini tofauti na ilivyokuwa awali ambapo madini mengi yalikuwa yanatoroshwa nje.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya Sheria ya Serikali za Mitaa na Utozaji wa Kodi ya Majengo, Sura. Ibara ya 9 na 11 ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Serikali za Mitaa ya Utozaji wa Kodi ya Majengo kwa lengo la kuweka viwango mfuto (*flat rate*) ya kodi ya majengo, lengo hasa ya mabadiliko haya ni kutoa unaafuu katika ulipaji wa kodi na kuhamasisha wananchi wachangie katika mapato ambayo kimsingi ndio huleta maendeleo.

Hivyo marekebisho hayo yanalenga kutoza kodi kwa maeneo yafuatayo:-

Kwanza, kutoza kodi ya majengo kwa jengo moja linalotumika kwa makazi katika kiwanja kimoja kwa kiwango cha Sh.10,000 kwa nyumba ya kawaida na Sh.50,000 kwa kila sakafu ya nyumba ya gorofa iliyopo katika maeneo ya majiji, manispaa na halmashauri za miji;

Pili, kutoza kodi ya majengo kwa kila jengo ndani ya kiwanja kimoja kwa kiwango cha Sh.10,000 kwa nyumba ya kawaida na Sh.50,000 kwa kila sakafu ya nyumba ya ghorofa kwa maeneo ya majiji, manispaa na halmashauri za miji;

Tatu, kutoza kodi ya majengo kwa jengo moja linalotumika kwa makazi katika kiwanja kimoja kwa kiwango cha Sh.10,000 kwa nyumba ya kawaida na Sh.20,000 kwa nyumba ya gorofa katika maeneo ya Makao Makuu ya Wilaya na Miji Midogo na maeneo ambayo Waziri mwenye mamlaka atatangaza kwenye gazeti la Serikali;

Nne, kutoza kodi ya majengo kwenye jengo moja lenye thamani ya juu katika kiwanja chenye majengo zaidi ya moja kwa kiwango cha Sh.10,000 kwa nyumba ya kawaida na Sh.20,000 kwa ghorofa kwa maeneo ya halmashauri za wilaya; na

Tano, majengo yenye gorofa yenye wamiliki tofauti kwa kila ghorofa chini ya Sheria ya *Unit Tittles* yatatozwa kodi ya majengo kwa kila ghorofa kulingana na umiliki.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo haya yote yanalenga kupanua wigo wa ukusanyaji wa mapato kutoka katika maeneo ya halmashauri za majiji, miji na manispaa hadi kufikia maeneo ya halmashauri za wilaya na mamlaka za miji midogo. Baada ya majadiliano ya kina Serikali ilikubalika kwamba kwa maeneo ya halmashauri za wilaya kodi hii ikusanywe katika mipaka ya makao makuu ya wilaya tu na siyo hadi maeneo ya vijijini. Aidha, Serikali ilikubali kufanya mabadiliko kama inavyoonekana katika jedwali la

marekebisheso ambaye waziri mwenye dhamana amepewa mamlaka ya kutangaza eneo nje ya maeneo haya endapo ataona hali ya uchumi na kimaendeleo ya eneo husika inaruhusu kodi hiyo kkusanywa.

Mheshimiwa Spika, vilevile ilikubalika kwamba kwa maeneo ya miji, majiji na manispaa, endapo kuna nyumba zaidi ya moja zote zitatozwa kiwango mfuto. Hatua hii inalenga hasa wale wamiliki wa nyumba ambao wana nyumba zaidi ya moja kwenye eneo moja lakini huzitumia ama kuajiri ya kupangisha au kwa ajili ya kibishara, sharti hili halitatumika katika halmashauri za wilaya na badala yake endapo kuna majengo zaidi ya moja katika eneo hilo basi jengo moja linalotozwa kodi kubwa ya majengo ndiyo pekee litakalolipiwa.

Mheshimiwa Spika, Marekebisheso ya Sheria ya Madini, Sura 123; Serikali imechukua uamuzi thabiti wa kudhibiti usafirishaji wa madini ghafi nje ya nchi ili iongezwe thamani hapa nchini. Uamuzi huu ulikuwa na lengo la kushawishi la kuchochaea uongezaji wa thamani ya madini yanayozalishwa nchini. Hata hivyo, tatizo linalojitokeza ni kwamba tafsiri ya maneno *raw minerals* bado halijatolewa katika Sheria ya Madini. Hivyo basi, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuboresha zaidi Ibara ya 18 ya Muswada na kuweka tafsiri ya maneno *raw minerals*.

Mheshimiwa Spika, vilevile Kamati bado inaona haja ya kufanya marekebisheso ya tafsiri ya maneno *small scale miners*, ilitafsiri hiyo iweze kuwajumuisha *dealers* na madalali yaani *brokers*. Aidha, Kamati inashauri badala ya kutumia maneno ya '*a person*' kama inavyoonekana katika Ibara ya 21A(2) yatumike maneno *small scale miners* ambayo yatakuwa yametafsiriwa.

Mheshimiwa Spika, katika Ibara ya 19 ya Muswada ilikuwa inafannya marekebisheso katika kifungu cha 9 cha Sheria ya Madini; Kamati ilikubaliana na Serikali kuiondoa ibara hiyo yote kwa kuwa Sheria ya Madini, Sura 123 ilivyo sasa ina maudhui yanayopendekezwa katika kifungu hicho

cha 9(4). Aidha, maudhui yaliyopo katika kipengele cha (b) na (c) cha Muswada yanaweza kutengeneza kifungu kidogo ili kukidhi maudhui hayo yaani jedwali la marekebisho limeainisha maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 20 ya Muswada inapendekeza kutoa adhabu kwa makosa yanayotokana na kufanya biashara ya madini kinyume cha sheria kwa kutoza kiasi cha shilingi milioni tano na isiyozidi shilingi milioni kumi pamoja na kifungo kati ya mwaka mmoja hadi miaka mitano endapo kosa limefanywa na mtu binafsi na shilingi milioni ishirini na isiyozidi shilingi milioni hamsini.

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na hatua hii nzuri kwa kuwa itasaidia wachimbaji wadogo kufuata taratibu za kisheria za biashara ya madini. Vilevile hatua hii itasaidia Serikali kuwa na takwimu sahihi za mapato yanayotokana na biashara ya madini pamoja na uzalishaji nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Ibara ya 21, ambayo inafanya mabadiliko katika kifungu cha 27C cha Sheria ya Madini, yana lengo ya kuanzisha maeneo ya kuuzia na kununua madini yaani *minerals and gem house*, pamoja na kuweka utaratibu unaowaruhusu wamiliki wa leseni kubwa za wachimbaji wa madini yaani *mining na special mining license* kuuzwa mahali popote madini yao.

Mheshimiwa Spika, vilevile katika ibara hiyo Serikali inapendekeza kuweka utaratibu wa kuanzisha maeneo ya mauzo pale ambapo hakuna *gem house*. Aidha, Waziri amepewa mamlaka ya kutunga kanuni ambazo pamoja na mambo mengine ni kutoa msamaha yaani (*exemption*) kwa baadhi ya madini kufuata utaratibu huo.

Mheshimiwa Spika, lazima nikiri kwamba hili ni moja ya maeneo ambayo tulijadiliana kwa kina na kufikia maamuzi kwamba masharti haya yasitumike kwa wachimbaji wadogo ili kuhamasisha:-

Kwanza, kutumia maeneo maalum ya kuuzia madini; Pili, kuihalalisha sekta ndogo ya uchimbaji wa madini; na Tatu, kuhamasisha wachimbaji wadogo wachangie katika uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, jedwali la marekebisho ya Serikali limezingatia hayo yote tuliyokubaliana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na Serikali kuhusu marekebisho ya mapendekezo katika Ibara ya 22, 23, 24 na 25.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 26 ya Muswada inayofanya marekebisho katika kifungu cha 86 cha Sheria ya Madini ina nia ya kuweka utaratibu wa kuingiza madini nchini. Kamati ilibaini kwamba utaratibu ullopendekezwa na Serikali katika Muswada utaleta ugumu katika uingizaji wa madini nchini kuliko kutoa unafuu, lengo ikiwa ni kurahisisha uingizwaji wa madini nchini kutoka mahali popote duniani. Ibara hii inaweka masharti ya kutoa tamko yaani *declaration* kuhusu aina ya madini, kiwango cha madini na sababu za kuingiza madini husika nchini. Aidha, baada ya kutoa tamko hilo atapatiwa kibali kinachomruhusu kuingiza madini hayo.

Mheshimiwa Spika, Kamati imekubaliana na mapendekezo yaliyopo katika Ibara ya 26, ambayo yanabadilisha vifungu cha 86B na 86C vya Sheria ya Madini ambayo kimsingi yanaweka utaratibu wa uingizaji wa almasi nchini pamoja na kumpa Waziri Mamlaka ya kutunga kanuni na utaratibu wa kuingiza madini kama hayo.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura namba 148. Katika Ibara ya 29 ya Muswada Serikali imekubaliana na mapendekezo ya Kamati kuhusiana na msamaha yaani *ku-exempt* kodi ya ongezeko la thamani kwa wachimbaji wadogo. Hii itasaidia na kuhamasisha wachimbaji wadogo wa madini kuuza madini ndani ya nchi kupitia masoko yanayoanzishwa na hivyo kupunguza utoroshwaji wa madini nje ya nchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, maoni ya jumla; kwanza Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kwamba kanuni zinazotungwa ili kutekeleza mabadiliko haya ziwe na nia na dhamira iliyokusudiwa kwenye sheria iliopitishwa.

Mbili, Kamati imebaini kwamba pamoja na kwamba Serikali imedhamiria madini ya vito yaongezewe thamani hapa nchini, hakuna mkakati wowote wa kutoa msamaha wa mashine za ukataji na uchongaji wa vito. Hivyo ili sekta hiyo iweze kukua ni lazima Serikali kuleta mpango mkakati wa kiutaalam wa kikodi utakaosaidia kufanya ujuzi huo na ufundu huo uweze kuongezeka nchini.

Tatu, Kamati pia imebaini kwamba suala la ukataji na uchongaji wa madini ya vito, kwa kiasi kikubwa ni kipaji na si kwamba inasomewa vyuoni kama inavyodhaniwa, hivyo kuna ugumu wa wenyе vipaji hivyo kupata vibali vyа kazi na kuishi nchini kwa sababu ya Sheria ya Uhamiaji inayotambua utaalam wenyе yeti na sio vipaji. Kwa sababu utaalam huo haupo nchini hivi sasa, Kamati inashauri Serikali kuangalia uwezekano wa kuruhusu watu wenyе ujuzi huo kuingia nchini kwa urahisi katika kipindi fulani ili Taifa liweze kunufaika na ujuzi wao kwa kuwa utaalam huo ni adimu.

Nne, wadau wa sekta ya madini wameiomba Serikali kutenga siku ya madini nchini ambayo watakutana wanunuzi wa madini, wauzaji wa madini pamoja na wauzaji wa teknolojia ya uchimbaji na utafutaji wa madini. Siku hii wanaamini itasaidia kuitangaza zaidi rasilimali hii duniani. Aidha, Serikali iangalie utaratibu wa kurudisha maonesho ya madini ya vito yale ya *Arusha Gem Fair*.

Tano, Kamati inashauri Serikali kuangalia uwezekano wa kuondoa kodi ya ongezeko la thamani na ushuru wa forodha kwenye malighafi zinazotumika katika usindikaji wa mvinyo na pombe kali zinazozalishwa kutohana na zao la zabibu inayolimwa hapa nchini ili kuhamasisha kilimo cha zabibu. (*Makof*)

Sita, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanza kutoa vibali nya kusafirisha baadhi ya madini ghafi, kwa mfano madini ya ujenzi, viwandani na kwa kipindi cha mpito wakati inajipanga vizuri kuongeza thamani ya madini. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa malizia.

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI: Mheshimiwa Spika, hitimisho, naomba kuchukua fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha na maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka 2019. Aidha, nipende kumshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mawaziri, Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Dotto Biteko, Waziri wa Madini na Waheshimiwa Mawaziri wengine waliofika kwenye Kamati.

Mheshimiwa Spika, aidha, niwashukuru Wajumbe wa Kamati na nisisahau kumshukuru Kamishna wa *TRA*, Mheshimiwa Charles Kichere, kwa ujumla na Serikali nzima kwa ushirikiano mkubwa ambao wametupa Kamati. Napenda pia kumshukuru Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki pamoja na Wajumbe wa Kamati kwa umahiri wao katika kutoa ushauri na mawazo mbalimbali katika kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda, nitaomba nisisome majina ya Wajumbe lakini yaingie kwenye *Hansard*. Aidha, nimshukuru Katibu wa Bunge na Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti na Msaidizi wake na wataalamu wote wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, kazi hii ilikuwa ngumu sana, tumetoka saa sita karibu kila siku toka ulipotupa kazi hii. Nataka nikuhakikishie kwamba tumeifanya kwa uaminifu mkubwa na tumepata ushirikiano mkubwa kutoka kwa Serikali lakini tumepata ushirikiano mkubwa sana kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge waliokuja wengi tu kwenye Kamati yetu hadi kuikamilisha kazi hii, napenda niwashukuru wote.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, naomba kuwasilisha, ahsante sana. (*Makofi*)

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI KUHUSU MUSWADA WA
SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI (NAMBA 2)
WA MWAKA 2019 KAMA YALIVYOWASILISHWA BUNGENI**

1.0. UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 86 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2016 naomba kutoa maoni na ushauri wa Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.2) wa Mwaka 2019 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.2) Act, 2019*].

Mheshimiwa Spika, Serikali imeona upo umuhimu wa kuwasilisha Muswada huu kwa haraka kupitia Hati ya Dharura ili kuondoa changamoto mbalimbali kwa wachimbaji wadogo wa madini, wakulima wa zabibu, viwanda vinavyotumia zabibu hiyo katika uzalishaji wa mvinyo na pombe kali (Valuer Brandy) pamoja na kuweka viwango mfuto (*fixed rate*) vya kodi ya majengo.

Mheshimiwa Spika, kupitia Muswada huu Sheria zifuatazo zinafanyiwa marekebisho: -

- i) Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147 [*The Excise (Management and Tariff) Act, CAP 147*];
- ii) Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332 [*The Income Tax Act, CAP 332*];
- iii) Sheria ya Serikali za Mitaa ya Utozaji wa Kodi ya Majengo, Sura 289 [*The Local Government Authorities (Rating) Act, CAP 289*];
- iv) Sheria ya Madini, Sura 123 [*The Mining Act, CAP 123*]; na
- v) Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura 148 [*The Value Added Tax Act, CAP 148*].

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti imeujadili kwa kina Muswada huu, Kamati inapenda kuwashukuru wadau wafuataao ambao walifika kutoa maoni yao mbele ya Kamati. Wadau hao ni:-

- i) *Shirikisho la Wachimbaji Madini Tanzania* (*Federation of Miners Association of Tanzania - FEMATA*);
- ii) Umoja wa Wachimbaji Wakubwa Nchini (*Tanzania Chamber of Minerals*);
- iii) Umoja wa Mawakala wa Madini Tanzania (*Tanzania Mineral Dealers Association - TAMIDA*);
- iv) Umoja wa Wanawake Wachimba Madini Tanzania (*Tanzania Women Miners Association-TAWOMA*);
- v) Wawakilishi Kutoka Viwanda Vya Mvinyo vya Domia na Alko Vintage;
- vi) Mjiolojia wa Wachimbaji Wadogo na wa Kati wa madini ya dhahabu (Medium Scale Gold Mining Geologist);
- vii) Mtandao wa Watoa Msaada wa Kisheria Tanzania (*Tanzania Network of Legal Aid Providers- TANLAP*);
- viii) *Asasi ya kiraia ya Tangible Initiatives for Local Development in Tanzania (TIFLD)*; na

2.0. MADHUMUNI YA MUSWADA

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.2) wa Mwaka 2019 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.2) Act, 2019*] una lengo la kufanya marekebisho ya Sheria Tano zilizoainishwa katika utangulizi ili kuondoa mapungufu yaliyojitekeza wakati wa utekelezaji wa Sheria hizo. Hatua hii itasaidia: -

- i) Kupunguza utoroshwaji wa madini kwenda nje ya nchi unaofanywa na wachimbaji wadogo na hivyo kukwepa kodi;
- ii) Kuondoa tatizo la wakulima wa zabibu hapa nchini la kukosa soko la uhakika la kuuza zabibu kutokana na wazalishaji wa vinywaji vikali vinavyotumia zao hilo kutonunua kwa wingi mchuzi wa zabibu unaozalishwa nchini; na
- iii) Kukabiliana na changamoto ya ukwepajji kodi ya majengo na kuhamasisha wananchi kulipa kodi hiyo kwa hiyari.

3.0. MAONI NA USHAURI WA KAMATI KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI (NAMBA 2) WA MWAKA 2019

Mheshimiwa Spika, Kamati imepitia Muswada huu kifungu kwa kifungu kwa madhumuni ya kujielimisha maudhui ya kila Ibara. Baada ya kujiridhisha na maudhui yake, Kamati ilifanya majadiliano ya kina na Serikali kuhusu mapendekezo ya marekebisho ya **Sheria Tano (5)** zilizopo kwenye Muswada huu. Katika majadiliano hayo Kamati ilikubaliana na Serikali kufanya marekebisho katika baadhi ya vifungu. Pamoja na hayo, Kamati ingependa kuwasilisha maoni na ushauri wake kama ifuatavyo:-

**3.1. Marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147
[The Excise (Management and Tariff) Act, CAP 147]**

Mheshimiwa Spika, sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza kurekebisha **Ibara ya 4** ya Muswada ili kupunguza kiwango cha ushuru wa bidhaa unaotozwa kwenye pombe kali (*spirits*) zinazotengenezwa nchini kwa kutumia zabibu zinazozalishwa hapa nchini kutoka **shilingi 3,315.00** kwa lita hadi **shilingi 450.00** kwa lita. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuja na pendekezo hili. Hatua hii, **Kwanza**; itasaidia kuondoa tatizo la upatikanaji wa soko la

zao la zabibu kwa wakulima wetu. Aidha, hatua hii itasaidia kupunguza bei ya mchuzi wa zabibu zinazozalishwa ndani kwa kuwa sasa utakuwa unapatikana kwa gharama ya nafuu ukilinganishwa na ule unatoka nje; **Pili**, itahamasisha na kuendeleza uzalishaji wa zao la zabibu nchini; **Tatu**, itahamasisha uanzishwaji na uendelezaji wa viwanda vya kusindika zao la zabibu nchini na hivyo kuongeza ajira na mapato ya Serikali.

3.2. Marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332 [The Income Tax Act, CAP 332]

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 6 na 7 ya Muswada kinapendekeza kufuta Kifungu ya **83B** na aya ya 4(d) ya Jedwali la Kwanza la **Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332 [The Income Tax Act, CAP 332]** kwa lengo la kuondo a kodi ya zuio ya asilimia 5 (*withholding tax*) inayotozwa kwenye bei ya kuuzia madini ya aina zote nchini. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii kwani imejibu haraka kilio cha wachimbaji wadogo kuhusu kodi hiyo. Aidha, hatua hii sasa itahamasisha wachimbaji wadogo kuuza madini yao katika masoko ya madini ambayo Serikali inakusudia kuyaanzisha hapa nchini, katika maeneo yenye uchimbaji wa madini na hivyo kusaidia upatikanaji wa mapato na takwimu za uzalishaji wa madini tofauti na ilivyokuwa awali ambapo madini mengi yalikuwa yanatoroshwa nje.

3.3. Marekebisho ya Sheria ya Serikali za Mitaa ya Utozaji wa Kodi ya Majengo, Sura 289 [The Local Government Authorities (Rating) Act, CAP 289]

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 9 na 11 ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Serikali za Mitaa ya Utozaji wa Kodi ya Majengo kwa lengo la Kuweka viwango mfuto (fixed rate) vya kodi ya majengo. Lengo hasa la mabadiliko haya ni kutoa unafuu katika ulipaji kodi na kuhamasisha wananchi wachangie katika mapato ambayo kimsingi ndio huleta maendeleo, hivyo marekebisho hayo yanalenga kutoza kodi kwa:-

- i) Kutoza Kodi ya Majengo kwa jengo moja linalotumika kwa makazi katika kiwanja kimoja kwa Kiwango cha Shilingi 10,000/= kwa nyumba ya kawaida na shilingi 50,000/= kwa kila sakafu ya nyumba ya ghorofa iliyopo katika maeneo ya Majiji, Manispaa na Halmashauri za Miji;
- ii) Kutoza kodi ya majengo kwa kila jengo ndani ya kiwanja kimoja kwa kiwango cha Shilingi 10,000/= kwa nyumba ya kawaida na shilingi 50,000/= kwa kila sakafu ya nyumba ya ghorofa kwa maeneo ya Majiji, Manispaa na Halmashauri za Miji;
- iii) Kutoza Kodi ya Majengo kwa jengo moja linalotumika kwa makazi katika kiwanja kimoja kwa kiwango cha shilingi 10,000/= kwa nyumba ya kawaida na shilingi 20,000/= kwa nyumba ya ghorofa katika maeneo ya Makao Makuu ya Wilaya na Mamlaka za Miji midogo na maeneo ambayo Waziri mwenye mamlaka atatangaza kwenye Gazeti la Serikali;
- iv) Kutoza Kodi ya Majengo kwenye jengo moja lenye thamani ya juu katika kiwanja chenyе majengo zaidi ya moja kwa kiwango cha shilingi 10,000/= kwa nyumba ya kawaida na shilingi elfu 20,000/= kwa ghorofa kwa maeneo ya halmashuri ya Wilaya
- v) Majengo ya ghorofa yenyе wamiliki tofauti kwa kila ghorofa chini ya Sheria ya *Unit Titles* yatatozwa kodi ya jengo kwa kila ghorofa kulingana na umiliki.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo hayo pia yalilenga kupanua wigo wa ukusanyaji wa kodi kutoka katika maeneo ya Halmashauri za Jiji, Miji na Manispaa hadi kufikia maeneo ya Halmashauri za Wilaya na Mamlaka ya Miji midogo. Baada ya majadiliano ya kina, Serikali ilikubali kwamba, kwa maeneo ya Halmashauri za Wilaya kodi hii ikusanywe katika mipaka ya Makao Makuu ya Wilaya tu na **sio hadi maeneo ya vijijini**. Aidha, Serikali ilikubali kufanya mabadiliko kama

yanavyoonekana katika jedwali la marekebisho ambapo Waziri mwenye dhamana amepewa Mamlaka ya kutangaza eneo nje ya maeneo hayo endapo ataona hali ya kiuchumi na kimaendeleo ya eneo husika inaruhusu kodi hiyo kukusanya.

Mheshimiwa Spika, vilevile ilikubalika kwamba kwa maeneo ya miji, maji na manispaa endapo kuna nyumba zaidi ya moja zote zitatozwa kiwango mfuto. Hatua hii inalenga hasa wale wamiliki wa nyumba ambao wana nyumba zaidi ya moja kwenye eneo moja lakini zinatumika ama kwa ajili ya kupangisha au kwa ajili ya kibiasara. Sharti hili halitatumika katika Halmashauri ya Wilaya na badala yake endapo kuna majengo zaidi ya moja katika eneo hilo basi jengo moja linalotozwa kodi kubwa ya majengo ndilo pekee litakalolipiwa.

3.4. Marekebisho ya Sheria ya Madini, Sura 123 [*The Mining Act, CAP 123*]

3.4.1. Mheshimiwa Spika, Serikali imechukua uamuzi thabiti wa kudhibiti usafirishaji wa madini ghafi (*raw mineral*) nje ya nchi ili yaongezwe thamani hapa nchini, Uamuzi huu ulikuwa na lengo la kushawishi na kuchochea uongezaji wa thamani ya madini yanayozalishwa nchini. Hata hivyo, tatizo linalojitokeza ni kwamba tafsiri ya maneno raw mineral bado haijatolewa katika sheria ya madini. Hivyo basi Kamati inaipongeza Serikali kwa kuboresha zaidi **Ibara ya 18 ya Muswada** kwa kuweka tafsiri ya maneno *raw minerals*.

3.4.2. Mheshimiwa Spika, vilevile Kamati bado inaona haja ya kufanyia maboresho ya tafsiri ya maneno “*small scale miner*” ili tafsiri hiyo iweze kuwajumuisha “*dealers*” na madalali “*Brokers*”. Aidha, kamati inashauri badala ya kutumia maneno “*a person*” kama yanavyoonekana katika ibara ya 21 (a), (2) yatumika maneno “*small scale miner*” ambayo yatakuwa yametafsiriwa.

- 3.4.3. Mheshimiwa Spika, Katika Ibara ya 19 ya Muswada** ilikuwa inafanya mabadiliko katika kifungu cha 9 cha Sheria ya Madini, Kamati ilikubaliana na Serikali kuiondoa ibara hiyo yote kwa kuwa Sheria ya Madini Sura ya 123 ilivyo hivi sasa ina maudhui yanayopendekezwa katika kifungu hicho hicho cha 9 kifungu kidogo cha 4. Aidha, maudhui yaliyoko katika vipengele (b) na (c) vya Muswada yanaweza kutengeneza kifungu kidogo ili kukidhi maudhui hayo (jedwali la marekebisho limeainisha marekebisho husika)
- 3.4.4. Mheshimiwa Spika, Ibara ya 20 cha Muswada** imependekeza kutoza adhabu kwa makosa yanayotokana na kufanya biashara ya madini kinyume cha Sheria kwa kutoza kiasi cha **shilingi milioni tano** na isiyozidi **milioni kumi** pamoja na kifungo kati ya mwaka mmoja hadi mitano endapo kosa limefanywa na mtu binafsi (*Individual*) na Shilingi **milioni ishirini** na isiyozidi shilingi milioni hamsini. Kamati inakubaliana na hatua hii nzuri kwa kuwa itasaidia wachimbaji wadogo kufuata taratibu na sheria za biashara ya madini. Vilevile, hatua hii itasaidia Serikali kuwa na takwimu sahihi za mapato yatokanayo na biashara ya madini pamoja na uzalishaji nchini.
- 3.4.5. Mheshimiwa Spika, Ibara ya 21 ya Muswada** ambayo inafanya mabadiliko katika kifungu cha **27C** cha Sheria ya Madini yana lengo la kuanzisha maeneo ya kuuza na kununulia madini "Gem House" pamoja na kuweka utaratibu unaowaruhusu wamiliki wa leseni kubwa za uchimbaji wa madini (*mining licence* na *special mining licence*) kuuza mahali popote madini yao. Vilevile, Katika Ibara hiyo Serikali inapendekeza kuweka utaratibu wa kuanzisha maeneo ya mauzo pale ambapo hakuna "Gem House". Aidha, Waziri amepewa mamlaka ya kutunga kanuni ambazo pamoja na mambo mengine ni kutoa msamaha "*exempt*" kwa baadhi ya madini kufuata utaratibu huo.

Mheshimiwa Spika, lazima nikiri kwamba hili ni moja ya eneo ambalo lilijadiliwa kwa kina na tukafikia maamuzi kwamba masharti haya yasitumike kwa wachimbaji wadogo ili kuwahamasisha **Kwanza** Kutumia maeneo maalumu ya kuuzia madini; **Pili**, kuihalalisha sekta ndogo ya uuzaji na uchimbaji madini; na **tatu**, kuwahamasisha wachimbaji wadogo wachangie katika uchumi wa Taifa. Endapo masharti haya yatatumika kama yalivyo yanaweza yasilete matokeo ambayo yamekusudiwa na Serikali. **Jedwali la marekebisho la Serikali limezingatia mapendekezo hayo ya Kamati.**

- 3.4.6. Mheshimiwa Spika**, aidha, Kamati inakubaliana na Serikali kuhusu marekebisho yanayopendekezwa katika **ibara za 22, 23, 24, na 25**, za Muswada huu, ambazo kwa pamoja zinarahisisha ufanyaji wa biashara ya madini nchini kwa wachimbaji wadogo hasa kwa kuweka mfumo madhubuti utakaowezesha wamiliki wa leseni za uchimbaji madini wa katni na wakubwa kuuza madini ndani au nje ya soko la madini nchini.
- 3.4.7. Mheshimiwa Spika, Ibara ya 26 ya Muswada** inayofanya marekebisho katika kifungu cha **86A** cha Sheria ya Madini ina nia ya kuweka utaratibu wa uingizaji wa madini nchini. Kamati ilibaini kwamba utaratibu uliopendekezwa na Serikali katika muswada unaleta ugumu katika uingizaji wa madini nchini kuliko kutoa unafuu. Lengo ikiwa ni kurahisiha uingizwaji wa madini nchini kutoka mahali popote Duniani. Ibara hiyo inaweka masharti ya kutoa Tamko "*Declaration*" kuhusu aina ya madini, kiwango cha madini na sababu za kuingiza madini husika nchini. Aidha, baada ya kutoa tamko hilo atapatiwa kibali kitakachomruhusu kuingiza madini hayo nchini.
- 3.4.8. Mheshimiwa Spika**, Kamati imekubaliana na Mapendekezo ya Serikali yaliyopo katika **ibara ya 26** ambayo yanabadilisha kifungu cha 86B na 86C ya

Sheria ya Madini ambayo kimsingi yanaweka utaratibu wa uingizaji wa almasi nchini pamoja na kumpa Waziri mamlaka ya kutunga kanuni za utaratibu wa kuingiza madini hayo nchini.

3.5. Marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura 148 [The Value Added Tax Act, CAP 148]

Mheshimiwa Spika, katika **Ibara ya 29 ya Muswada**, Serikali imekubaliana na mapendekezo ya Kamati kuhusu kutoa msamaha (exempt) wa kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwenye madini ya metali na vito yatakayouzwa na wachimbaji wadogo kwenye masoko ya madini hapa nchini. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii, kwani marekebisho haya **Kwanza**, yatasaidia kuhamasisha wachimbaji wadogo wa madini kuuza madini yao ndani ya nchi kupitia masoko yatakayoanzishwa na hivyo kupunguza utoroshwaji wa madini nje ya nchi kwa njia ya magendo; **Pili**, yataondoa ushikilaji wa mitaji ya wafanyabishara wadogo wa madini, **Tatu**, yatasaidia kuwatambua wachimbaji wadogo kupitia masoko ya madini yatakayoanzishwa na kuongeza wigo wa mapato ya Serikali na kukuza uchumi kupitia sekta ya madini.

4.0. MAONI YA JUMLA

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena Kamati inapenda kuipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu ikiwa ni utekelezaji wa maoni ambayo Kamati iliyatoa kupitia Taarifa zake mbalimbali ilizowasilisha Bungeni.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba nitoe maoni na ushauri wa jumla kama ifuatavyo: -

- 4.1. Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba Kanuni zitakazotungwa ili kutekeleza mabadiliko haya ziwe na nia na dhamira iliyokusudiwa kwenye Sheria itakayopitishwa.
- 4.2. Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kwamba pamoja na kwamba Serikali imedhamiria madini ya vito

yaongezwe thamani hapa nchini, hakuna mkakati wowote wa kutoa msamaha kwa mashine za ukataji na uchongaji wa vito hivyo ili sekta hiyo ikue nchini. Kamati inashauri katika mwaka ujao wa fedha Serikali iangalie masuala ya kikodi na kiutawala katika kuongeza ujuzi na ustadi kwa wakata madini ya vito.

- 4.3. Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kwamba suala la ukataji na uchongaji wa vito kwa kiasi kikubwa ni kipaji na si kwamba inasomewa vyuoni kama inavyodhaniwa. Hivyo kuna ugumu wa wenye kipaji hicho kupata kibali cha kazi na kuishi kwa sababu sheria ya uhamiaji inatambua utaalamu wenye yeti tu na sio vipaji. Kwa sababu utaalamu huo haupo nchini hivi sasa. Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kuruhusu watu wenye ujuzi huo kuingia nchini kwa urahisi katika kipindli fulani ili Taifa liweze kunufaika na ujuzi wao kwa kuwa utaalamu huo ni adimu.
- 4.4. Mheshimiwa Spika**, Wadau wa Sekta ya Madini wameiomba Serikali kutenga siku ya Madini nchini ambapo watakutana wanunuzi wa madini, wauzaji wa madini pamoja na wauzaji wa teknolojia ya uchimbaji na utafutaji wa madini. Siku hii wanaamini itasaidia kuitangaza zaidi rasilimali hii Duniani. Aidha, Serikali iangalie utaratibu wa kurudisha maonesho ya madini ya vito (Arusha Germ Fare)
- 4.5. Mheshimiwa Spika**, aidha Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kuondoa kodi ya Ongezeko la Thamani na ushuru wa forodha kwenye malighafi zinazotumika katika usindikaji wa mvinyo na pombe kali zinazozalishwa kutohana na zao la zabibu linalolimwa hapa nchini ili kuhamasisha kilimo cha zabibu.
- 4.6. Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanza kutoa vibali vyaa kusafirisha baadhi ya madini ghafi kwa mfano madini ya ujenzi na viwandani kwa

kipindi cha mpito wakati ikijipanga vizuri kuongeza thamani ya madini hayo hapa nchini. Hata hivyo inaishauri Serikali pindi wanapopanga bei elekezi ya madini ya ujenzi ni vyema kuwashirikisha wazalishaji wa madini ujenzi kwa sababu wao ndio wanaojua ghamama halisi za uchimbaji na usafirishaji wa madini hayo.

5.0. HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii kukushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha taarifa ya maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Namba (Na.2) wa Mwaka 2019, mbele ya Bunge lako Tukufu. Vilevile napenda nimshukuru Mheshimiwa Prof. Adelardus L. Kilangi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango (Mb), Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dotto Biteko, Waziri wa Madini, Mheshimiwa Januari Makamba, Waziri wa Nchi (OMR) – Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Selemani Jaffo, Waziri Ofisi ya Rais- TAMISEMI, Mheshimiwa Aashatu Kijaji (Mb), Naibu Waziri wa Fedha na Mipango na Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, Naibu Waziri wa Madini kwa ushirikiano wao walizoutoa kwa Kamati. Aidha, napenda kuwashukuru Watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango, Ndg. Charles Kichere, Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Tanzania pamoja na watendaji wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa maoni na ushauri wao ulioiwezesha Kamati kuchambua Muswada huu hadi hatua hii. Kamati pia inawashukuru wadau wote waliofika mbele ya Kamati na kutoa maoni yao kuhusu Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Makamu Mwenyekiti Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, pamoja na Wajumbe wote wa Kamati hii kwa umahiri wao katika kuchambua vifungu vya Muswada huu na kuweza kufanya maamuzi sahihi. Naomba niwatambue Wajumbe hao kama ifuatavyo.

1. Mhe. George Boniface Simbachawene, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb – Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. David Ernest Silinde, Mb
4. Mhe. Dkt. Immaculate Sware Semesi, Mb
5. Mhe. Mbaraka Kitwana Dau, Mb
6. Mhe. Mendrad Lutengano Kigola, Mb
7. Mhe. Maria Ndilla Kangoye, Mb
8. Mhe. Oran Manase Njeza, Mb
9. Mhe. Riziki Said Lulida, Mb
10. Mhe. Freeman Aikael Mbowe, Mb
11. Mhe. Hasna Sudi Katunda Mwilima, Mb
12. Mhe. Makame Cassim Makame, Mb
13. Mhe. Balozi Adadi Mohamed Rajab, Mb
14. Mhe. Abdallah Majurah Bulembo, Mb
15. Mhe. Prof. Anna Kajumulo Tibaijuka, Mb
16. Mhe. Stephen Julius Masele, Mb
17. Mhe. Ali Hassan Omar, Mb
18. Mhe. Martha Jachi Umbulla, Mb
19. Mhe. Dkt. Dalaly Peter Kafumu, Mb
20. Mhe. Albert Obama Ntabaliba, Mb
21. Mhe. Marwa Ryoba Chacha, Mb
22. Mhe. Balozi Dkt. Diodorus Buberwa Kamala, Mb
23. Mhe. Andrew John Chenge, Mb
24. Mhe. Hussein Mohamed Bashe, Mb
25. Mhe. Shally Josepha Raymond, Mb
26. Mhe. Suleiman Ahmed Saddiq, Mb

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee kabisa, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Ndg. Stephen Kagaigai, Katibu wa Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake katika kipindi chote. Aidha, napenda kuishukuru Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti ikiongozwa na Kaimu Mkurugenzi Ndg. Lina Kitosi, Kaimu Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Michael Kadebe na Makatibu wa Kamati hii Ndg. Godfrey Godwin, Emmanuel Rhobi, Lilian Masabala na Maombi Kakozia kwa kuratibu shughuli za Kamati pamoja na wanasheria wa Ofisi ya Bunge, Ndg Mossi Lukuvi na Ndg. Thomas Shawa kwa kutoa ushauri wa kitaalam na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

George B. Simbachawene, Mb
MWENYEKITI
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI
9 Februari, 2019

SPIKA: Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, Mheshimiwa George Simbachawene. Tunashukuru sana pamoja na Wajumbe wako wa Kamati kwa kazi kubwa ambayo mmeefanya. Ahsanteni sana mmeefanya kwa niaba yetu.

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunakwenda upande wa Upinzani, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa David Silinde, nawe pia nakupa dakika zisizozidi ishirini.

MHE. DAVID E. SILINDE - MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 2 wa mwaka 2019.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyenzi Mungu kwa uweza wake mkubwa kwa kunipa nguvu na afya njema na hivyo kusimama mbele ya ukumbi ili kutoa maoni ya Kambi Rasmi Upinzani Bungeni. Aidha, shukrani za Watanzania wengi kwa Mola wetu kwa kuendelea kumponya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Tundu Antiphas Lissu. Pia tunawashukuru tena kwa rehema zake ambazo hazina kiwango na kipimo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kipekee nitoe salamu za pekee kwa Kiongozi wa Kambi Rasmi Upinzani, Mheshimiwa Freeman Mbowe, pamoja na Mbunge Esther Matiko walioko huko jela Segerea. Napenda kusema kwamba yote yanayotokea kwao ni chachu ya kufanya sisi kuwa imara zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Muswada huu ambaeo umeletwa kwa Hati ya Dharura, kama kawaida ya Serikali unafanya marekebisho ya sheria tano ambazo ni Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147; Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332; Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa ya Utozaji wa Kodi ya Majengo, Sura ya 289; Sheria ya Madini, Sura ya 123; na Sheria ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148.

Mheshimiwa Spika, mbali ya kuwa Muswada huu umeletwa kwa Hati ya Dharura na pia umeletwa kwa lugha ya Kiingereza badala ya kuwa na Muswada ulitafsiriwa pia kwa lugha ya Kiswahili, jambo hili limewafanya wadau wakuu katika Muswada huu yaani wachimbaji wadogo kukosa fursa nzuri ya kupitia kwa makini kila kifungu na kujua mapendekezo yake. Ni ukweli kwamba kusomewa na kutafsiriwa ni lugha tofauti kabisa na kujisomea mwenyewe na kuelewa jambo hilo. Kwa mantiki hiyo, huu ni uzembe mwengine wa makusudi unaofanywa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia baadhi ya sheria zinazofanyiwa marekebisho katika Muswada huu, zina uhusiano wa moja kwa moja na bajeti ya Serikali ya mwaka wa fedha 2018/2019, ambayo ilipitishwa na Bunge lako Juni, 2018 na ambayo tunaitekeleza hadi sasa. Uhusiano huu wa moja kwa moja, unapunguza au kuongeza mizania ya bajeti yetu kwa maana ya mapato na matumizi. Hivyo, lingekuwa nijambo jema kama ambavyo mara zote wakati wa kupitisha Sheria ya Fedha kwamba marekebisho yanayotarajiwu kufanya kwenye Sheria ya Kodi yanatarajia kuongeza ama kupunguza kiasi gani cha fedha kwenye bajeti yetu. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani tunaitaka Serikali itueleze kwa mabadiliko haya itaongeza ama itakosa kiasi gani.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya Muswada. Kama ambavyo tumeeleza hapo awali kwamba Muswada huu unafanya Marekebisho Sheria tano na umegawanyika katika sehemu kuu sita. Sehemu ya kwanza ikiwa inahusu masharti ya utangulizi ambayo yanajumuisha jina la Muswada na namna sheria zinavyopendekezwa kurekebishwa zitakavyorekebishwa ndani ya Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 4 kinachohusu marekebishesho ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147 kinafanya marekebishesho Jedwalilala Nne la Sheria Mama, kwa kupunguza kiwango cha Ushuru wa Bidhaa za pombe kali zinazozalishwa kwa zabibu zinazolimwa hapa nchini. Hili ni jambo jema na Kambi Rasmi ya Upinzani hatuna pingamizi nalo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini kwa kuweka kumbukumbu sawa, wakati Bunge lako hili linapitisha Sheria ya Fedha tarehe 21 Juni, 2017 nikisoma maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani hapa Bungeni kwa mwaka wa fedha 2017/2018, nilisema kuwa kuongeza ushuru kwenye bidhaa zinazozalishwa kutokana na malighafi ya kilimo ni jambo linalovunja sana moyo wakulima na hivyo kuikosesha sekta ya kilimo soko la uhakika kwa bidhaa zao. Katika wasilisho letu kwa Sheria za Fedha kwa mwaka 2016 - 2018 tulitahadharisha jambo hilo la kuongeza ushuru kwa bidhaa ambazo zinategemea malighafi kutoka kwa wakulima hapa nchini lakini mapendelekezo hayo yalikataliwa kwa sababu tu yalitolewa na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa hivi mapendelekezo yanaletwa katikati ya mwaka wa fedha baada ya kuona mlifanya makosa ya makusudi ya kuua zao la zabibu. Hii ni sawa na kuonja sumu wakati unajua kabisa itakuua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani kama ambavyo tulishauri miaka iliyopita mapendelekezo haya ni mazuri lakini bado hayaondoi tatizo la moja kwa moja kwenye ununuzi wa zao la zabibu kwa wakulima kwa sababu hatua hii itapunguza ukubwa wa tatizo kwa asilimia 30 - 40

kwa sasa kwani bado kuna matatizo yaliyobakia kutokana na kodi nydingi hasa katika uagizaji wa malighafi kutoka nje za kutengenezea zabibu hiyo, kama vifungashio au chupa kwa ajili ya bidhaa hiyo inayozalishwa viwandani. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali kuwa ushuru wa chupa kwa ajili ya *packaging* ya pombe kali na *wine* urejewe ili kutoa unafuu zaidi kwa wakulima na hasa kwa waagizaji ambao wanununa zabibu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya Sheria ya Serikali za Mitaa ya Utozaji wa Kodi ya Majengo. Mabadiliko hayo yanayopendekezwa na Serikali ni kuiwezesha Mamlaka ya Mapato ya Tanzania kukusanya mapato ambayo tangu awali yamekuwa na mapungufu makubwa. Mamlaka ya Mapato nchini *TRA* katika kipindi ambacho imekusanya Kodi ya Majengo zimejitokeza changamoto mbalimbali ikiwemo Serikali kushindwa kurejesha fedha hizo katika Halmashauri mbalimbali ili ziweze kutekeleza majukumu yake kama ilivyoahidiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, taarifa ya mwaka kuhusu utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha Januari, 2018 hadi Januari, 2019 pamoja na tathmini ya utekelezaji wa bajeti katika kipindi cha nusu mwaka 2018/2019, Sehemu ya 5(h), inabainisha wazi na kuthibitisha hoja ya Kambi Rasmi Upinzani Bungeni kwamba Mamlaka ya Mapato Tanzania haina uwezo mkubwa wa kukusanya mapato ya majengo na chanzo hicho kilipaswa kuachwa kwenye Halmashauri. Taarifa hiyo inasema na ninukuu: "Kamati inaona kuwa kiwango cha ukuaji wa Kodi ya Majengo kimeshuka kwa asilimia 44.5". Kambi ya Upinzani Bungeni inaendelea kuishauri Serikali kuacha chanzo hiki chini ya Halmashauri zetu na kuitaka Serikali Kuu ipanue wigo wa kukusanya mapato kwa kuangalia vyanzo vingine.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 13 cha Muswada wa Sheria ya Serikali za Mitaa ya Utozaji wa Kodi za Majengo, Sura ya 289 kinapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 18(a) cha sheria husika na kuingiza jukumu jipya la Serikali za Mitaa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato nchini

TRA kukusanya Kodi ya Majengo. Hoja ya *TRA* ikusanye mapato ikishirikiana na Serikali za Mitaa inaungwa mkono na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti ambayo taarifa yake ya mwaka kuhusu utekelezaji wa majukumu katika kipindi cha Januari, 2018 hadi Januari, 2019 katika kipengele (h) kinachohusu ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi, Kamati inashauri na ninanukuu: "Serikali kuongeza bidii ya ukusanyaji wa Kodi ya Majengo kwa kushirikiana na Halmashauri husika.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaona kwamba kifungu hiki hakijakaa sawa kwa kuwa hakielezi ushirikiano huu kati ya Mamlaka ya Mapato nchini na Serikali za Mitaa ni ushirikiano wa aina gani. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuweka wazi aina hii ya ushirikiano kwa kuwa Mamlaka ya Mapato (*TRA*) na wafanyakazi wake na inafanya kazi lakini pia Mamlaka za Serikali za Mitaa zinajitegemea. Kwa ushirikiano huu mpya, washirika hawa wawili yaani *TRA* na Serikali za Mitaa watanufaikaje?

Mheshimiwa Spika, Serikali za Mitaa zitanufaika na ushirikiano huu katika mazingira ambayo *TRA* inakusanya mapato kwa ajili ya Serikali Kuu kwa mujibu wa sheria hii. Ni nani kati ya washirika hawa watagharamia gharama za ukusanyaji wa kodi hiyo kwa watumishi wanaotoka Serikali za Mitaa ambao watahusika katika zoezi hilo? Ni maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwamba wakati Waziri anatunga Kanuni, Serikali iweke jambo hili bayana kisheria kuwa ushirikiano baina ya *TRA* na Serikali za Mitaa uwe katika dhana ya asilimia 60 kwa 40 katika zoezi zima la ukusanyaji wa Kodi za Majengo kwa maana kwamba asilimia 60 iende *TRA* na asilimia 40 ibaki katika Halmashauri kama moja ya chanzo cha mapato. Jambo hilo litaondoa mkanganyiko huu ili kuwezesha urejeshwaji wa fedha za majengo kwa Halmashauri. Huu ndiyo ushirikiano ambao hata Kamati ya Bajeti ilikuwa inashauri kutokana na ukweli kwamba *TRA* imeshindwa kuiflikia lengo ambalo tulikuwa tumeliweka.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 15 cha Muswada kinarekebisha Kifungu cha 29 cha sheria kuu. Pamoja na

marekebisho yaliyofanywa katika kifungu hicho cha 29 bado kinapaswa kufanyiwa marekebisho zaidi kwa kuwa sheria isiporekebishwa itasababisha tataruki kubwa huko vijijiini kwa wananchi. Aidha, matakwa ya kulipa kodi ndani ya miezi miwili na nyongeza ya taarifa ya maandishi kwa siku ishirini na moja vikifuatiwa na mchakato wa kuuzwa kwa nyumba za wananchi ili kufuta deni la Kodi ya Majengo litasababisha mtafaruku kwa wananchi. Ili kuepusha hilo, ni maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwamba mabadiliko ya kifungu cha 29 yaangalie pia suala la kuuzwa kwa majengo kufidia kodi inayodaiwa.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya Sheria ya Madini, Sura ya 123. Kifungu cha 17 cha Muswada kinafanya marekebisho ya jumla kwenye sheria kwa kufuta maneno '*mining rights*' sehemu yoyote kwenye sheria yanapojitokeza maneno hayo na kuweka maneno '*mineral rights*'.

Mheshimiwa Spika, kwa uelewa wetu ni kuwa haya maneno yana maana mbili tofauti na hivyo ni vyema yakatumika '*mining rights*' ambapo ni haki ya kuchimba ambayo mwenye haki anaipata kutokana na mikataba baina yake na mmiliki wa madini. Aidha, hii ya pili '*mineral rights*' ni haki ambayo mmiliki wa hayo madini na mara zote inatokana na mmiliki wa ardhi yenye hayo madini.

Mheshimiwa Spika, katika kupata tafsiri zaidi kwa wajui wa mambo hayo inaonyesha kwamba: "*Mining rights- This right to mine is an action also referred to as a "right of self-initiation". This right to mine is an action (prospecting and extraction), as distinguished from idle ownership*". Aidha, *Mineral rights:* "*are a landowner's rights regarding natural resources located on his or her land*". Pia *mineral rights*, give ownership of these resources to the landowner, as well as the right to gain monetarily (in whole or in part) from the sale of such natural resources. Kwa muktadha huu ni kwamba maneno hayo mawili yanaweza kutumika kwenye sheria hii ya madini bila ya mkinzano wowote wa kimantiki.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 18 cha Muswada kinachofanya marekebisho kifungu cha 4 cha sheria kwa kuongeza tafsiri ya maneno, ama kutoa tafsiri ya neno '*tailings*' ambayo kwa lugha maarufu kwa jamii yetu ya Kitanzania ni magwangwala. Kwa mujibu wa tafsiri ya neno hilo, kutoka Wikipedia ni kwamba: "*Tailings, is also called mine dumps, culm dumps, slimes, tails, refuse, leach residue or slickens, terra-cone, are the materials left over after the process of separating the valuable fraction from the uneconomic fraction of an ore*". Kwa maneno mengine ni kwamba hizi zinazoitwa '*tailings*' ni bidhaa ambazo hazina *economic value* yoyote ile kwa mujibu wa tafsiri hiyo na pia inategemeana ni teknolojia gani iliyotumika katika uchenjuaji wa madini hayo ya dhahabu.

Mheshimiwa Spika, katika muendelezo wa kifungu hicho, kifungu cha 27 cha Muswada kinachofanya marekebisho kifungu cha 100 kwa kuongeza kifungu kipyta cha 100E, kinasema kuwa hayo mabaki yanayomilikiwa na wachimbaji wadogo sasa itakuwa ni biashara kama biashara zingine. Tukumbuke kwamba hii *tailings* siyo *concentrates* au makinikia bali ni magwangwala.

Mheshimiwa Spika, hoja hapa ni je biashara hii nayo itakuwa inafanyika kwa mujibu wa kifungu cha 27 cha sheria na itakuwa inalipiwa kodi? Kwani hakuna biashara ambayo itafanyika katika sekta ya madini bila ya kuwa na utaratibu wa jinsi itakavyofanya. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa itakuwa ni vyema kama kifungu hiki kipyta kinachotaka biashara kufanyika kama neno la '*Tailings*' litafutwa na kubakia na maneno "*Mineral ores*" kwani *mineral ores* ni makinikia ambayo ndani yake kuna madini ya aina mbalimbali na uchenjuaji wake kwa maana ya *smelting* unaweza kufanyika ili kupata madini mengine zaidi ya yale yaliyokuwemo hapo awali.

Mheshimiwa Spika, aidha, Muswada umeingiza kitu kipyta cha maneno kwa maana ya *mineral and Gem Houses* na kikitolea tafsiri yake. Kambi Rasmi ya Upinzani naona badala ya kutumia neno '*Houses*' litumike neno '*Centres*' au

'Stations' kwani neno hilo litaleta maana zaidi katika biashara nzima ya soko la madini kwa wachimbaji wadogo na neno *Houses* linaweza kutumika vibaya na hivyo kupoteza dhana nzima ya uanzishajji wake.

Mheshimiwa Spika, pia tafsiri ya mchimbaji mdogo imetolewa kuwa ni yule ambaye anamiliki leseni, kwa maana ya *Primary Mining Licence*. Tafsiri hii au utambuzi huu wa mchimbaji mdogo kwa ufahamu wetu ni kuwa unaacha nje wachimbaji wengi ambaao kwa Kiingereza wanaitwa *Artisanal Small Scale miners*. Wengi wa watu hawa bado ni *informal* hivyo hawamiliki leseni lakini maisha yao yote ni uchimbaji na hilo la kutokuwa na leseni ni kutokana na mitaji yao kuwa midogo na pia ukiritimba katika tasnia ya urasimishajji.

Mheshimiwa Spika, kwa muktadha huo basi ni bora tasfiri ya wachimbaji wadogo ikawahuisha na wachimbaji wa aina wa hii ili kwa ujumla wao, wanufaike na soko linaloanzishwa na sekta ili liweze kukua kama ambavyo matarajio ya sheria yalivyo. Ni ukweli kwamba dhana nzima ya marekebisho ya vifungu vya 21 - 25 vya Muswada huu, inalenga katika kuhakikisha kuwa biashara ya madini kutoka kwa wachimbaji wadogo inarasimishwa na hivyo udhibiti wa mapato kutokana na biashara hiyo unaliilingizia Taifa fedha na pale pale wahusika wanazidi kubakia kwenye biashara hiyo.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya mwisho ni marekebisho ya Sheria ya Ongezeko la Thamani, kifungu cha 29 cha Muswada kinaongeza Kifungu cha 55B kwenye Sheria hii, kifungu hicho kinatoa msamaha wa kodi kwa maana ya zero rated on VAT kwa dhahabu itakayouzwa na wachimbaji wadogo kwenye Kituo cha Mauziano kwa maana ya *Mineral and Gem Houses*. Kambi Rasmi ya Upinzani haina tatizo na hatua hiyo kwani itasaidia uchimbaji huo mdogo kuwa na gharama nafuu kutokana na vifaa vinavyotumika katika uzalishajji kupata msamaha wa kodi ya VAT.

Mheshimiwa Spika, jambo hili litapelekea madini yatakayouzwa kwenye kituo hiki kuwa na bei shindani kwa

wanunuzi. Aidha, kutokana na ukweli kwamba Serikali imekuwa na tabia ya kutokulipa *VAT refunds* kwa wafanyabiashara, mfano, wafanyabiashara wanaoingiza sukari za viwandani, ile 15% ya *VAT* hawajawahi kulipwa fedha zao zaidi ya shilingi bilioni 32 na makampuni ya madini kudai zaidi shilingi bilioni 500. Hivyo wadau wengi waliomba wawe *exempted* na sisi hatuna tatizo na kifungu hicho.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kwa ujumla Kambi ya Upinzani haipingani na marekebisho yaliyoletwala bali ina mtazamo kwamba utaratibu huu wa Hati ya Dharura unatunyima haki ya msingi ya kufanya tafakuri ya kina kwa kile kilicholetwa na kutopata nafasi ya kupata maoni ya upande wa watusika wakuu kwa maana ya wadau wa sheria husika. Sambasamba na tatizo hilo la kimfumo juu ya utungwaji wa sheria, tumejitahidi kupitia vifungu husika na kutoa mtazamo wetu kwa maeneo husika na hivyo kuitaka Serikali kutoa ufanuzi zaidi na pengine kuvifanyia marekebisho ili kutimiza azma iliyokuwa imekusudiwa wakati marekebisho haya yanafanywa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema maneno naomba kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani, japo tulipata muda mfupi, ahsante. (*Makofî*)

**MAONI YA MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI
KUHUSU MUSWADA WA MAREKEBISHO YA SHERIA
MBALIMBALI NAMBA 2 WA MWAKA 2018 (THE WRITTEN
LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) NO.2 ACT, 2019
KAMA YALIVYOWASILISHWA BUNGENI**

(*Yanatolewa chini ya Kanuni ya 86(6) ya Kanuni za Bunge,
Toleo la Januari 2016*)

A. UTANGULIZI:

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu kwa uwezo wake mkubwa wa kunipa nguvu na afya njema na hivyo kusimama mbele ya ukumbi huu ili kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bunge. Aidha

shukrani za watanzania wengi kwa Mola wetu kwa kuendelea kumponya vyema Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa Wizara hii ya Sheria na Katiba na pia Mnadhimu Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Mheshimiwa Tundu Antiphas Lissu. Tunashukuru tena kwa rehema zake ambazo hazina kipimo wala kiwango.

Mheshimiwa Spika, kwa kipekee nitoe salaam kwa Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani, mbunge wa Jimbo la Hai na Mwenyekiti wa Taifa wa Chadema Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe pamoja na Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko Mbunge wa Jimbo la Tarime Mjini walioko katika gereza la Segerea kwa kesi za kisiasa kwamba; sisi Kambi Rasmi ya Upinzani na watanzania wengi, kwamba kuwa kwao magereza ni chachu ya kutufanya kuwa imara zaidi katika kuendeleza kile ambacho kitaifanya nchi yetu kutoka katika hali hili iliyo sasa na kwenda kule kunakotarajiwa na watanzania wengi.

Mheshimiwa Spika, muswada huu ambaeo umeletwa kwa hati ya dharura kama kawaida ya Serikali, unafanya marekebisho kwenye sheria tano, ambazo ni Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147, Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332, Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa ya Utozaji wa Kodi ya Majengo, Sura ya 289, Sheria ya Madini, Sura ya 123 na Sheria ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148.

Mheshimiwa Spika, mbali ya kuwa muswada huu umeletwa kwa hati ya dharura, na pia umeletwa kwa lugha ya kiingereza badala ya kuwa na muswada uliotafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili, jambo hili limewafanya wadau wakuu katika muswada huu yaani wachimbaji wadogo kukosa fursa nzuri ya kupitia kwa makini kila kifungu na kuja na mapendekezo. Ni ukweli kwamba kusomewa na kutafsiriwa lugha ni tofauti kabisa na kujisomea mwenyewe na kueleza uelewa wako katika jambo hilo. Kwa mantiki hiyo, huo ni uzembe mwingine wa makusudi uliofanywa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia baadhi ya sheria zinazofanyiwa marekebisho katika muswada huu zina uhusiano wa moja

kwa moja na bajeti ya Serikali ya Mwaka wa Fedha 2018/2019 ambayo iliyopitishwa na Bunge Mwezi Juni, 2018 na bajeti inayotekelawa kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, uhusiano huo wa moja kwa moja unapunguza au kuongeza mizania ya bejeti yetu (MAPATO NA MATUMIZI), hivyo lingekuwa ni jambo jema kama ambavyo mara zote wakati wa kupitisha sheria ya fedha kwamba marekebisho yanayotarajiwa kufanywa kwenye sheria za kodi yanataraja kuongeza au kupunguza kiasi cha fedha kwenye bajeti yetu. Hivyo, basi Serikali itueleze kwa mabadiliko haya itaongeza ama itakosa kiasi gani?

B. MAPITIO YA MUSWADA

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo tumeeleza hapo awali kwamba muswada huu unafanya marekebisho sheria tano na megawanyika katika sehemu kuu sita na sehemu ya kwanza ikiwa inahusu masharti ya utangulizi ambayo yanajumuisha, jina la Muswada na namna ambavyo sheria zinazopendekezwa kurekeblishwa zitakavyorekeblishwa ndani ya muswada.

i. Marekebisho ya sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 4 cha muswada kinafanya marekebisho Jedwali la nne la sheria mama kwa kupunguza kiwango cha ushuru wa bidhaa za pombe kali zinazozalishwa kwa zabibu zinazolimwa hapa nchini. Hili jambo ni jema na Kambi Rasmi ya Upinzani. Kwa kuweka kumbukumbu sawa, wakati Bunge hili tunapitisha sheria ya fedha tarehe 21 Juni, 2017 nikisoma maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwa Mwaka wa Fedha 2017/ 2018 nilisema kuwa kuongeza ushuru kwenye bidhaa zinazozalishwa kutokana na malighafi ya kilimo ni jambo linalovunja moyo wakulima na hivyo kuikosesha Sekta ya Kilimo soko la uhakika kwa bidhaa zao. Katika wasilisho letu kwa sheria za fedha za mwaka 2016 hadi 2018 tulitahadharisha jambo hilo la kuongeza ushuru kwa bidhaa ambazo zinategemea malighafi kutoka wakulima wa nchi,

Lakini mapendekezo hayo yalikataliwa kwa sababu tu yalitolewa na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi mapendekezo yanaletwa katikati ya mwaka wa fedha baada ya kuona mlifanya makosa ya makusudi ya kuua zao la zabibu. Hii ni sawa na kuonja sumu wakati unafahamu kabisa kuwa itakuua.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi kama ambavyo ilishauri miaka hiyo, mapendekezo haya ni mazuri lakini bado hayaondoi tatizo la moja kwa moja kwenye ununuzi wa zao la zabibu kwa wakulima kwa sababu hatua hii itapunguza ukubwa wa tatizo kwa asilimia 30-40. Kwani bado kuna matatizo yaliyobakia kutokana na kodi nyingi hasa katika uagizaji wa malighafi toka nje za kutengenezea zabibu kama vifungashio au chupa kwa ajili ya hiyo bidhaa inayozalishwa viwandani.

Hivyo basi Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri kuwa ushuru kwa chupa kwa ajili ya "packaging" ya pombe kali urejewe ili kutoa nafuu hadi kwenye bei za zabibu.

ii. Marekebisho ya sheria ya Serikali za Mitaa ya Utozaji wa Kodi ya Majengo, Sura ya 289.

Mheshimiwa Spika, Mabadiliko haya yanayopendekezwa na serikali ya kuiwezesha mamlaka ya mapato Tanzania kukusanya mapato, tangu awali yamekuwa na mapungufu makubwa. Mamlaka ya Mapato nchini (TRA) katika kipindi ambacho imekusanya kodi ya majengo zimejitokeza changamoto mbalimbali ikiwemo Serikali kushindwa kurejesha fedha hizo katika Halmashauri mbalimbali ili ziweze kutekeleza majukumu yake kama ilivyoahidiwa.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya mwaka kuhusu utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha Januari, 2018 hadi januari, 2019 pamoja na tathimini ya utekelezaji wa bajeti katika kipindi cha nusu mwaka 2018/2019, Sehemu ya 5 (h) inabainisha wazi na kuthibitisha hoja ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni

kwamba, Mamlaka ya Mapato Tanzania haina uwezo wa kukusanya kodi ya majengo na chanzo hicho kinapaswa kuachwa kwenye Halmashauri.Taarifa hiyo inasema na ninanukuu "*Kamati inaona kuwa kiwango cha ukuaji wa ukusanyaji wa kodi ya majengo kimeshuka kwa asilimia 44.5*"

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaendelea kuishauri Serikali kuacha chanzo hiki chini ya Halmashauri zetu na kuitaka Serikali Kuu ipanue wigo wa kukusanya mapato kwa kuangalia vyanzo vingine.

Mheshimiwa Spika, kifungu hicho hicho cha 11 cha mswada, kinarekebisha kifungu cha 16 cha sheria husika na kuweka viwango mfuto vya kodi ya majengo. Sasa mheshimiwa spika, katika sheria ya zamani Halmashauri zilikuwa na uwezo wa kufanya makadirio kulingana na hali ya uchumi wa Halmashauri husika, sasa kwa sheria hii kuweka viwango sawa bila kuzingatia hali ya uchumi katika Halmashauri husika siyo sawa, na Kambi Rasmi ya Upinzani inataka serikali kufanya mabadiliko, ili viwango vya kodi pamoja na mambo mengine vizingatie hali ya kiuchumi kwa eneo husika.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 13 cha mswada sheria ya serikali za Mitaa ya utozaji wa kodi za majengo, Sura ya 289 kinapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 18A cha sheria husika na kuingiza jukumu jipya ya serikali za Mitaa kushirikiana na Mamlaka ya Mpato nchini (TRA) kukusanya Kodi ya Majengo. Hoja ya kwamba TRA ikusanye mapato ikishirikiana na serikali za mitaa inaungwa mkono na kamati ya kudumu ya Bunge ya bajeti, ambayo katika taarifa yake ya mwaka kuhusu utekelezaji wa majukumu katika kipindi cha januari, 2018 hadi januari, 2019 katika kipengele (h) kinachohusu ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi, kamati inasema na ninanukuu "*kamati inashauri serikali kuongeza bidii ya ukusanyaji wa kodi ya majengo kwa kushirikiana na Halmashauri husika*"

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba kifungu hiki hakijakaa sawa kwa kuwa hakielezi ushirikiano huu kati ya Mamlaka ya Mapato nchini na Serikali za Mitaa ni ushirikiano wa aina gani. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni

inaitaka serikali kuweka wazi aina hii ya ushirikiano kwa kuwa mamlaka ya Mapato nchini TRA inawafanyakazi wake na inafanya kazi lakini pia mamlaka za serikali za mitaa zinajitegemea, kwa ushirikino huu mpya washirika hawa wawili, yaani TRA na Serikali za Mitaa watanufaikaje.

Mheshimiwa Spika, Serikali za Mitaa, zitanufaikaje na ushirikiano huu, katika mazingira ambayo TRA inakusanya mapato kwa ajili ya Serikali kuu, kwa mujibu wa sheria hii, nani, kati ya washirika hawa wawili, atagharamia gharama za ukuswanyaji wa kodi hiyo kwa watumishi wanaotoka serikali za mitaa, ambao watahusika katika zoezi hili?

Mheshimiwa Spika, ni maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kwamba wakati Waziri anatunga kanuni serikali iweke jambo hili bayana kisheria kuwa ushirikiano huo baina ya TRA na LGA uwe katika dhana ya 60% kwa 40% katika zoezi zima la ukuswanyaji wa kodi za majengo, kwa maana kwamba 60% iende TRA na 40% ibakie katika halmashauri, jambo hilo litaondoa mkanganyiko kuhusu urejeshwaji wa fedha za majengo kwa halmashauri. Huu ndio ushirikiano ambao hata Kamati ya Bajeti illikuwa inashauri kutokana na ukweli kwamba TRA imeshindwa kufikia lengo tarajiwa.

Mheshimiwa spika, kifungu cha 15 cha muswada, kinarekebisha kifungu cha 29 cha sheria kuu, pamoja na marekebiso yanayofanywa katika kifungu hicho cha 29, bado kifungu hicho kinapaswa kufanyiwa marekebiso zaidi kwa kuwa sheria hii isporekebishwa itasababisha tataruki kubwa huko vijijini kwa wananchi. Aidha matakwa ya kulipa kodi ndani ya kipindi cha miezi miwili na nyongeza ya taarifa ya maandishi kwa siku 21, vikifualiwa na mchakato wa kuuzwa kwa nyumba za wananchi ili kufikia deni la kodi ya majengo litasababisha mtafaruki kwa wananchi na ili kuepusha hilo, ni maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwamba, mabadiliko ya kifungu cha 29 yaangalie pia swala la kuuzwa kwa majengo kufidia kodi inayodaiwa.

iii. Marekebisho ya sheria ya Madini, Sura ya 123

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 17 cha muswada kinafanya marekebisho ya jumla kwenye sheria kwa kufuta maneno “mining rights”, sehemu yoyote kwenye sheria yanapojitokeza maneno hayo na kuweka maneno “mineral rights”.

Mheshimiwa Spika, kwa uelewa wetu ni kuwa haya maneno yana maana mbili tofauti na hivyo maneno hayo ni vyema yakatumika. “Mining rights” ni haki ya kuchimba ambayo mwenye haki anaipata kutokana na mikataba baina yake na mmiliki wa madini. Aidha hii ya pili ya “mineral rights” ni haki ambayo mmiliki wa hayo madini na mara zote inatokana na mmiliki wa ardhi yenye hayo madini.

Mheshimiwa Spika, katika kupata tafsiri zaidi kwa wajubi wa mambo hayo, inaonesha kwamba; “*Mining rights-This right to mine is an action also referred to as a “right of self-initiation”.* *This right to mine is an action (prospecting and extraction), as distinguished from idle ownership*”. Aidha, Mineral rights; “are a landowner’s rights regarding natural resources located on his or her land”. Pia mineral rights, *give ownership of these resources to the landowner, as well as the right to gain monetarily (in whole or in part) from the sale of such natural resources*.

Mheshimiwa Spika, kwa muktadha huo ni kwamba maneno hayo mawili yanaweza kutumika kwenye sheria hii ya madini bila ya mkinzano wowote wa kimantiki.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 18 cha muswada kinachofanya marekebisho kifungu cha 4 cha sheria kwa kuongeza tafsiri ya maneno, na kutoa tafsiri ya neno “tailings” lakini kwa lugha maarufu katika jamii yetu ya Kitanzania ni “magwangala”.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa tafsiri ya neno hilo kutoka Wikipedia ni kwamba; “*Tailings, is also called mine dumps, culm dumps, slimes, tails, refuse, leach residue or slickens,*

terra-cone, are the materials left over after the process of separating the valuable fraction from the uneconomic fraction of an ore". Kwa maneno mengine ni kwamba hizi zinazoitwa Tailings ni bidhaa ambazo **hazina economic value (uneconomic fraction of an ore)** yoyote ile kwa mujibu wa hiyo tafsiri na pia itategemea ni teknolojia gani imetumika katika uchenjuaji wa madini hayo ya dhahabu.

Mheshimiwa Spika, katika muendelezo wa kifungu hicho, kifungu cha 27 cha muswada kinachofanya marekebisho kifungu cha 100D kwa kuongeza kifungu kipyga cha **100E**, kinachosema kuwa hayo mabaki yanayomilikiwa na wachimbaji wadogo sasa itakuwa ni biashara kama biashara zingine. Tukumbuke kwamba hii Tailings sio **concentrates au Makinikia** bali ni "**Magwangala**". Hoja hapa ni je biashara hii nayo itakuwa inafanyika kwa mujibu wa kifungu cha 27C cha sheria? Na itakuwa inalipiwa kodi? Kwani hakuna biashara ambayo itafanyika katika sekta ya madini bila ya kuwa na utaratibu wa jinsi itakavyofanyika.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa itakuwa ni vyema kama kifungu hiki kipyga kinachotaka biashara kufanyika kama neno la Tailings litafutwa na kubakia na maneno "**Mineral ores**" kwani **mineral ores** ni makinikia ambayo ndani yake kuna madini ya aina mbalimbali, na uchenjuaji (*smelting*) wake unaweza kufanyika ili kupata madini mengine zaidi ya yale yaliyokuwemo hapo awali.

Mheshimiwa Spika, aidha, muswada umeingiza kitu kipyga cha "Mineral and Gem Houses" na kikitolea tafsiri yake, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona badala ya kutumia neno **Houses** litumike neno **Centre au Stations**, kwani neno hilo linaleta maana zaidi katika biashara nzima ya soko la madini kwa wachimbaji wadogo. Na neno houses linaweza kutumika vibaya na hivyo kupoteza dhana nzima ya uanzishwaji wake.

Mheshimiwa Spika, pia tafsiri ya mchimbaji mdogo imetolewa kuwa ni yule ambae anamiliki leseni ya "primary mining license", tafsiri hii au utambuzi huu wa mchimbaji mdogo,

kwa ufahamu wetu ni kuwa unaacha nje wachimbaji wengi ambao kwa kwa kiingereza wanaitwa "*artisanal Small Scale miners*", wengi wa watu hawa bado ni *informal* hivyo hawamiliki leseni lakini maisha yao yote ni uchimbaji na hilo la kutokuwa na leseni ni kutokana na mitaji yao kuwa midogo na pia ukiritimba katika tasnia hiyo ya urasimishaji.

Mheshimiwa Spika, Kwa mktadha huo basi, ni bora tafsiri ya wachimbaji wadogo ikawahuisha na wachimbaji wa aina hii ili kwa ujumla wao wanufaike na soko linaloanzishwa na sekta iweze kukua kama ambavyo matarajio ya sheria hii yalivyo.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli kwamba dhana nzima ya marekebisho ya vifungu vya 21 hadi 25 vya muswada huu vinalenga katika kuhakikisha kuwa biashara ya madini kutoka kwa wachimbaji wadogo ina rasimishwa na hivyo udhibiti wa mapato kutokana na biashara hiyo unallingizia taifa fedha na pale pale watusika wanazidi kubakia kwenye biashara.

iv. Marekebisho ya Sheria ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 147.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 29 cha muswada kinachoongeza kifungu cha 55B kwenye sheria, kifungu hicho kinatoa msamaha wa kodi (Zero-rated on VAT) kwa dhahabu itakayouzwa na wachimbaji wadogo kwenye kituo cha mauziano (Mineral and Gem House). Kambi Rasmi ya Upinzani haina tatizo na hatua hiyo kwani itasaidia uchimbaji huo kuwa wa gharama nafuu kutokana na vifaa vinavyotumika katika uzalishaji kupata msamaha wa kodi ya VAT. Jambo hili litapelekea madini yatakayouzwa kwenye kituo hiki kuwa na bei shindani kwa wanunuizi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ukweli na hali halisi ya wafanyabiashara wanaoagiza Sukari ya Viwanda na kutokurudishiwa 15% ya fedha zao VAT kama sheria inavyohitaji, na hivyo wengi wao kupata hasara kubwa. Kwa muktadha huo, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema badala

ya kutoa **Zero rated tax** kwa wachimbaji wadogo, itakawa vyema wachimbaji wadogo wadogo wawe **exempted** na kodi hiyo.

C. HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla Kambi Rasmi ya Upinzani haipingani na marekebisho yaliyoletwa bali ina mtazamo kwamba utaratibu huu wa hati ya dharura unatunyima haki ya msingi ya kufanya tafakuri ya kina kwa kile kinacholetwa na pia kutupa nafasi ya kupata upande wa wahusika wakuu(wadau) wa sheria husika.

Mheshimiwa Spika, sambamba na tatizo hilo la kimfumo juu ya utungwaji wa sheria, tumejitahidi kupitia vifungu husika na kutoa mtazamo wetu kwa maeneo husika na hivyo kuitaka Serikali kutoa ufanuzi zaidi na pengine kuvifanyia marekebisho ili kutimiza azma iliyokuwa imekusudiwa wakati marekebisho hayo yanatayarishwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya ksema hayo kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha.

.....
David Ernest Silinde (Mb)

K.n.y: **MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI
WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO**

09 Februari, 2019

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa David Silinde. Tunakushukuru sana kwa maoni hayo.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuangalia muda wetu ulivyo na tungependa tumalize *on time* maana Wasukuma wengi wanataka kuondoka leo, kwa hiyo, nипитиshe tu *general rule* kwamba tujitahidi tutumie dakika tano tano ndugu zangu ili twende vizuri. (*Makofii*)

Tunaanza na Mheshimiwa Dkt. Dalaly Kafumu, atafuatiwa na Mheshimiwa Bashe kwa dakika tano tano.

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nianze kabisa kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kwenye jambo hili kubwa alilolifanya la kuiangalia sekta ya uchimbaji mdogo. Kwa kweli amefanya jambo kubwa, wachimbaji hawa wamekuwa na kilio kikubwa, tunamshukuru sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, napenda niseme kwamba Muswada huu ni muhimu sana na ultakiwa uje kwa Hati ya Dharura na sisi tumeutendea haki kwenye Kamati. Sina maneno mengi sana ya kusema kwenye Muswada huu lakini niseme tutakapokuwa tunatekeleza Muswada huu kuna mambo yanaweza kujitokeza ambayo labda hatukuyatazama vizuri. Napenda niseme mambo mawili tu ambayo nategemea yanaweza kutuletea changamoto wakati tunatekeleza Muswada huo.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza, ni Kifungu cha 21(2) ambacho kinazungumzia utoaji wa *import permit* kwa wanaoleta madini nchini. Najua tumevutana vutana sana, lakini tumerekebisha mpaka hapo tulipofika, lakini bado naamini kuna namna tunaweza tukarebisha zaidi, kwa sababu majirani zetu hawana utaratibu huo unaovuta sana. Kwa hiyo, wao wataweza kuendelea kupata madini yetu kutoka hapa yakienda kwao kuliko sisi. Kwa hiyo, huu utaratibu kadiri tutakapotekeleza ikileta changamoto hizi ambazo nazitegemea, basi msisite kuleta tukarekebisha jambo hilo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tunatakiwa anayetaka kuleta madini Tanzania asipate tabu yoyote ajue anaenda kwenye madini atapita vizuri, akipita kwenye soko madini yake yanaandikishwa anauza, lakini tukianzia kuwazuia kule kule mpakani tunaweza tukatapa tabu kidogo. Nasema tu kwamba kwa sasa tupite lakini kama kuna changamoto itajitokeza, tuikebishe. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili na la mwisho ni Kifungu namba 26 ambacho nilichokizungumza ni Kifungu

26(b) sasa nazungumzia Kifungu 21(2). Kifungu hiki kinaweza kabisa kuzuia baadhi ya wachimbaji kufanya biashara kwenye soko la nje kwa sababu wao wamelazimika kwenda kwenye soko tulilonalo. Sasa katika kutekeleza kuna wengine wanaweza kuwa na *Dealer's License* basi kwa namna fulani waruhusiwe ku-export madini kama wanaweza badala ya kulazimisha kila mmoja aende kwenye soko, anayeweza kwenda nje basi aende lakini tuhamasishe zaidi watokeze kwenye soko.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kusema naunga mkono hoja na naishukuru sana Serikali kwa kuleta Muswada huu ambao utasaidia sana wachimbaji wadogo. Mungu ibariki sekta ya uchimbaji mdogo, Mungu ibariki Tanzania. Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Dalaly Kafumu, Kamishna wa Madini Mstaafu. Nilikutaja Mheshimiwa Hussein Bashe, utafuatiwa na Mheshimiwa Halima Mdee.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa. Awali ya yote nitumie fursa hii kuishukuru kwa dhati kabisa Serikali, lakini vilevile nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa maamuzi makubwa aliyoyafanya kukutana na wachimbaji wadogo na kusikiliza kero zao. Jambo la pili, nishukuru Wizara ya Fedha na Wizara ya Nishati na Madini na Ofisi ya AG, tumekuwa na *engagement* ya siku mbili wame-give in katika mambo mengi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nataka nitoe ushauri hasa katika zao la zabibu. Tumechukua hatua ya awali ya kutatua changamoto ya zao la zabibu kwa kubadilisha tozo ya *excise duty*, nataka niiombe Serikali kwa dhati kabisa hii ni asilimia 40 tu ya tatizo la sekta ya zabibu, asilimia 60 bado imebaki katika gharama za *import* za *component* zinazohusika kama *input* kwenye uzalishaji wa mazao yanayotokana na zabibu kama vifungashio na chupa. Kwa hiyo, ningeshauri Serikali kwa kuwa tunaanza kuiandaa na mwaka wa fedha unaokuja, ni vizuri kukutana na wadau hawa kwa kina ili tuweze kulinyanya zao la zabibu vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo nataka nishauri, kaliongea kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Dalaly Kafumu. Kwa sisi tunaotoka kwenye maeneo ya uzalishaji wa dhahabu, tunafahamu na hii aliongea kwenye Kamati, kwa mara ya kwanza tumeanza kujadili dhahabu baada ya uhuru kwa uwazi. Ni sawasawa na *gorilla fighters* mnawatoa porini sasa mnawaleta waje waweke silaha chini waache *smuggling*.

Mheshimiwa Spika, naiomba kwa dhati Serikali wakati wanaenda kutengeneza *regulation* ya utekelezaji wa mabadiliko ya sheria hizi, ni vizuri wakafanya *engagement* ya kutosha na hawa wanaojihusisha katika sekta hii ndogo ya madini. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, suala la *import license*; yaani Serikali tumeongea nao sana na naamini huu ni mjadala wanaweza wakaleta hapa *additional amendment*. Hivi kifungu hiki kinasema hivi, naomba ninukuu:

"A person shall not import any minerals without a relevant Mineral Import Permit."

Mheshimiwa Spika, kwa *nature* ya wafanyabiashara wa madini mtu ana-smuggle kupeleka nje kwa sababu ya ghamama za tozo na soko la kwake la ndani. Sasa tujuilize tumezungukwa na *Mozambique* mtu kalipua shimo lake kapata dhahabu yake, utaratibu uliopo kule ni shida kwa nini hii *declaration* isifanyikie sokoni? Yeye aingie na dhahabu yake, aingie moja kwa moja sokoni auze. Kwa nini tuna complicate mipaka yetu, hebu tujuilize swali wakati *Tanzanite* yetu inakatiza kwenda Kenya waliwekewa hii *import license* barabarani? Sisi tuna become very holy wakati sisi tumepoteza sana rasilimali, wenzetu wamefaidika na rasilimali zetu. Naishauri tuondoe hii, *declaration* ikafanyikie sokoni, ni muhimu sana tukifanya namna hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, la tatu kwenye *regulation*; kule kwenye uchimbaji wa madini ya dhahabu na Mheshimiwa Waziri wa Madini anafahamu, kule hakuna kulipana

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

mshahara kule mtu akiingia chini ya ardhı hata miezi sita siku akizalisha wanagawana mifuko, huyu hana *PML, Dealer License* na *Broker License*. Kwa hiyo, yule mchimbaji (nyoka) aliyepo kule aki-crush dhahabu akapata dhahabu zake ndogo anaweka mfukoni, hapa katikati hana leseni yoyote. Yeye kavumbua Nzega anataka kurudi Dodoma nyumbani kwao ndio akauze. Anaweza kukamatwa na polisi na kufanya nini. Kwa hiyo, nashauri tutakapoenda kutengeneza *regulation*, tunayo *Dealer's License, Broker's License, PML*, ni vizuri waangalie namna gani hawa wachimbaji wadogo wanawenza kufanya biashara yao bila kuwekewa vikwazo. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Spika, otherwise naishukuru sana kwa hatua hii iliyochukua. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Hussein Bashe. Hata jana kuna vijana wa Kongwa wapiga kura wangu wameniaga wanaenda Msumbiji, wanaenda kuchimba dhahabu na wakipata mzigo wanakuja nao, sasa tena hapa tunafanyaje? Mheshimiwa Waziri angalia haya mambo. (*Makof/Kicheko*)

Nilikutaja Mheshimiwa Halima Mdee, atafuatiwa na Mheshimiwa Bulembo.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwanza kwa kuongeze hapo uliposema, naamini Serikali itaacha ubishi ama itapokea ushauri wa Kamati ambao ultaka ipunguze masharti magumu na mazito ya kifungu cha 86A na 86B ili kuruhusu *minerals* ziweze kutoka maeneo mengine ziingie nchini, *thensisi* kama nchi tu-export. Kwa hiyo, naamini Serikali licha ya kwamba Kamati tulishauri kwa muda mrefu wakaja na msimamo wao mkali baada ya kauli za Spika watalegeza. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, la pili, ni muhimu kupitia Muswada huu Serikali ikiri kwamba wakati wa Bunge la Bajeti ina wajibu

wa kusikiliza, kwa sababu ukiangalia mambo yanayohusiana na 18% ya wachimbaji wadogo, 5% ya *withholding tax* na 18% ya *VAT*kuondoa kwa wachimbaji wadogo, hili suala la zabibu lilzungumzwa kwenye bajeti, Kamati ya Bajeti ikaleta, Kambi Rasmi ya Upinzani ikashauri, Serikali ikakataa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa swali linakuja, je Serikali imeleta mabadiliko haya ya *Finance Bill*, actually ukisoma between the lines tunafanya marekebisho ya *Finance Act* lakini kwa sababu haiwezi kuletwa katikati, tunatumia *miscellaneous*. Sasa Serikali imeona imepanua wigo wa kodi ngumu na nzito, fedha zimekosekana, tumeamua kuchenjia gia hewani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ni ushauri tu Serikali ilenge kusikiliza sababu pale ambapo tumeweka kodi mpaka zinakuwa kero, tunafanya watu wakwepe kodi. Tunafanya watu badala ya kutumia rasilimali za ndani, wa-*import* kutoka nje. Walisema juzi kwamba Mheshimiwa Dkt. Mpango ameanza kusikiliza, naona kwa mabadiliko haya Mheshimiwa Dkt. Mpango ataanza kusikiliza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la tatu, suala *property tax*, kodi za majengo, dhamira ya uanzishaji wa vyanzo vya mapato ya halmashauri mbalimbali ni kuziwezesha kuijendesha. Ndio maana Serikali Kuu ina vyanzo vyake na Serikali za Mitaa zina vyanzo vyake. Tunatambua kwamba *TRA* ndio *custodian* wa makusanyo, lakini pale ambapo wanakusanya kodi ya majengo Kawe, *spirit* ya kodi ya majengo ni Mama Mollel aliipe kodi, halmashauri ikamrekebishia barabara yake, hiyo ndio *spirit*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa leo Serikali inakusanya vyanzo vya halmashauri, inaweka kwenye kapu kuu pesa ambayo wananchi wake ambao wanatozwa kodi zingine, hizi zinazotozwa na halmashauri hawa -*feel* mchango wao kwenye halmashauri zao. Sasa katika *spirit* ya kusikiliza na ninyi mnajua kwamba Serikali Kuu, halmashauri inacholeta kikubwa ni mishahara ya watumishi na miradi michache

mikubwa. Ujenzi wa madarasa, zahanati, ununuzi wa madawati na utengenezaji wa barabara ni wa halmashauri. Pamoja na kwamba *TARURA* imeanzishwa inategemea halmashauri, tutaendeshaje hizi halmashauri? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nikuombe na nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwamba hatuwezi kuua *decentralization* iliyojengwa *for more than 20 years*. Kama nchi lazima tuwe tuna vitu vinavyotu-guide, haya mambo ya kila awamu ikija inakuja na mambo yake tunalipoteza Taifa. (*Makof!*)

SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Halima Mdee. Nilishakutaja Mheshimiwa Bulembo atafuatiwa na Mheshimiwa Mariam Ditopile.

MHE. ALHAJI ABDALLAH M. BULEMBO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Awali ya yote kwanza nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na Baraza lake la Mawaziri na viongozi wote kwa kukubali hii *agenda* ya wachimbaji wadogo, nawapongeza sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, suala hili ni kubwa sana na Serikali imeonesha wazi ina nia njema katika suala la wachimbaji wadogo. Tumekaa kwenye Kamati ya Bajeti mpaka karibu saa sita za usiku, nampongeza Mwanasheria Mkuu, Waziri wa Fedha, Waziri wa Madini ni kama tulitaka kukesha, lakini hatimaye tumekubalina na ajenda imekuja hapa, nawapongeza sana kwa yale tuliyokubaliana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi, shida yangu ni ndogo sana hata dakika tatu sifiki. Mheshimiwa Waziri Mkuu alikaa na Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya, ombi langu kwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wasiingilie zoezi hili kwa sababu Rais ameshasema wafanyabiashara wachimbaji wadogo wapewe haki zao na waruhusiwe, wasiingilie. Hii ni kwa sababu atachimba mtu pale Nyamongo au Majimoto lakini bei nzuri iko Shinyanga, huyu mtu ana leseni ni *broker/dealer* asizuiwe kwenda kuza Shinyanga kwa

sababu Shinyanga ndio kuna mapato. Kwa hiyo, hapa kuna hatari Wakuu wa Mikoa hapa wakataka kila mtu kuonesha amekusanya kiasi gani katika Mkoa/Wilaya yake kuanza kuwasumbua wachimbaji wadogo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, *agenda* yangu kubwa iko pale wachimbaji wadogo nia ya Rais imeonekana, tunampongeza sana tumekaa naye siku mbili, sheria ni nzuri, kodi zimeondolewa, mchimbaji yejote Tanzania hii ana raha. Kwa kweli tunampongeza Rais, lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu Wakuu wake wa Wilaya na Mikoa awaambie wakae mbali na zoezi hili kwa sababu tutakuwa tunapiga simu nydingi, wasituweke kikwazo njiani. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mwisho kwa sababu ni mchimbaji na nawakilisha wachimbaji wenzangu mtuache raia Rais aliyofanya tulipe kodi, tusipeleke madini nje na Serikali ipate mapato yake.

Mheshimiwa Spika, ya kwangu ni hayo tu, nakushukuru sana. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Bulembo. Mheshimiwa Mariam Ditopile atafuatiwa na Mheshimiwa James Milly.

MHE. MARIAM D. MZUZURI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwa kweli leo hii nitajikita kwenye kuongelea mchuvi wa zabibu. Kila siku nikiwa nachangia masuala ya kilimo nasema tujikite kwenye *agricultural zone*. Leo hii kulibeba zao la zabibu kwa Mkoa wa Dodoma, ndio mambo yenyewe tunaenda kuyatengeneza vizuri. Msimu uliopita wakulima wetu zabibu ziliozea kwenye mashamba na sababu inajulikana. Wale wenye viwanda vikubwa hapa Dodoma ambao *CETAWICO* pamoja na *Alko Vintage* yake matanki yao ya kuhifadhi michuzi yalijaa kutokana na tozo ilivyokuwa kubwa walishindwa kwenda kuuza ule mchuvi, kwa hiyo *effect* yake ikashuka kwa mkulima, walishindwa kuuza zabibu, zabibu

zikaoza. Kwa hiyo, niseme hatua ya kupunguza punguzo kubwa sana litaenda kuwahakikishia soko la zabibu za wakulima wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Waswahili wanasema usione vinaelea vimeundwa. kwa namna ya kipekee nikupongeze umekuwa *pioneer* kwenye kutetea punguzo hili; mbele ya Waziri Mkuu na Rais uliongea. Mwingine pia Mbunge wangu wa Dodoma Mjini Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde ambaye anajinasibu kwa kusema yeye ni mtumishi wa watu (*De populo servorum*)sijui kama nimepatia Kigogo hiki. Mbele ya Rais tarehe 3 Novemba, wakati wa ufunguzi wa *NMB* aliomba hili punguzo mbele ya Waziri Mkuu na Mbele ya Makamu wa Rais aliomba hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuna siku nimeambatana naye mpaka Ofisi za *TRA* akititea punguzo hilli, hawezi kujisemea humu ndani lakini naomba niwahakikishie wakulima wote wa Dodoma Mjini kwenye hili Mbunge wenu amelipigania na fadhila mumrudishe 2020 kijana wenu, aliwasemea na kweli amehakikisha yeye ni mtumishi wenu. Atapita bila kipingwa, hilo linajulikana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nasema mbona tunaanza kusutana? Wameongea wamesikika, mambo yamerekebishika wanaanza tena kusuta ooh! Mheshimiwa Dkt. Mpango hasikii, amesikia. Asingerekibisha wangesema nini? Kwa hiyo, ifike hatua kama kweli tunashauri ili mambo yawe vizuri, basi tusifie tuendelee kuongezea nyama sio tunaanza tena kusutana sutana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, napenda pale pale uliposema wewe kuhusu hii *import permit*. Jamani hata kwenye suala la uchenjuaji walivyosema kwamba kama kuchenjua kufanyike kwenye mkoa ule ule ambao, tumeona *effectyake*. Kulikuwa wanaoleta madini yao kutoka Congo na Kenya kuja kuchenjua, tumekosa mapato kutokana na hilo. Kama leo vijana wetu wanapata uwezo wanaenda huko *Mozambique* na wapi kuchukua madini kuja *ku-process* hapa kwa nini

tuanze kuleta vikwazo? Kwa kweli kwenye hili Mheshimiwa Waziri wa Fedha kama vile tunavyom-*appreciate* yeye ni msikiu na mwelewa, hebu aangalie namna ya kuliweka sawa. Yote haya tunataka vijana wetu wapate ajira na vilevile nchi yetu iweze kupata mapato kama wanavyofanya Awamu ya Tano wanajenga vituo vya afya, tunaona kodi, hata *TRA* acheni wachukue kodi ya majengo, wananchi wanaona namna Serikali ya Awamu ya Tano inavyorudi kwao na mapato yanatumika vizuri na kwa uwazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa nafasi uliyonipa. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mariam Ditopile. Mheshimiwa James Millya nilikwishakutaja.

MHE. JAMES K. MILLYA: Mheshimiwa Spika, ilikuwa nisisimame kabisa, lakini kwa namna ambavyo tumetendewa wachimbaji wadogo nchi hii na Mheshimiwa Rais imebidi nisisimame kushukuru. Maana ni siku 17 tu tangu kikao hicho kiishe, leo sheria inakuja Bungeni kuwasaidia wachimbaji wadogo nchi nzima. Hii ina maana gani? Kwamba Mheshimiwa Rais ni msikiu sana, anajali watu na anawapenda sana wachimbaji wadogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa umewataja wageni waklongozwa na Rais wa Shirikisho la Vyama vya Wachimbaji Madini Wadogo ndugu Bina na wengine wa Simanjiro waliotoka hapa kwa kweli huu ni ushuhuda wa kipekee kwamba baada ya kulia kwa muda mrefu leo hii *withholding taxile* ya asilimia 5 na VAT. Tena leo tumeletewa *schedule of amendment* asubuhi na Serikali baada ya kusikiliza jana kutwa nzima na Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na mamlaka zinazohusika, wamekuja na *schedule of amendment* ya kuondoa kabisa kusema wachimbaji wadogo wapo *exempted* kwa VAT. Kwa hili tunashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nina dogo tu. Wakati msomaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani anasoma ule ukurasa wa pili

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

anasema tunaleta marekebisho haya sasa hivi wakati tayari tumeshapitisha Bajeti ya 2018/2019. Hivi kweli kama wewe ni kiongozi wa nchi unataka watu wako waendelee kuumia usifanye marekebisho ya sheria ili usubiri mpaka bajeti ifike? Siyo sahihi. (*Makof*)

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Spika, taarifa.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila utaratibu)

MHE. DAVID E. SILINDE: Kama anasoma roborobo lazima arekebishwe.

SPIKA: Mheshimiwa Silinde.

T A A R I F A

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda nimpe taarifa mchangiaji, kazi yetu ilikuwa ni kuhoji na kama ambavyo anasema tumehoji kwamba imekuja katikati, mbele nimeandika pale kwamba haya mambo yana *financial implications*. Kwa hiyo, tunataka majibu ya Serikali ndiyo watakuja kutujibu kwamba kuna ongezeko la fedha ama kuna upungufu kutokana na haya marekebisho, *so*, jibu kitaalam mzee. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa James, unapokea hiyo taarifa?

MHE. JAMES K. MILLYA: Mheshimiwa Spika, siipokei hata kidogo kwa sababu *in the first premise* ile ya ku-question tu kwa nini leo yaletwe haya mabadiliko kwa sababu ina *implication* ya bajeti maana yake nia yao si njema. (*Makof*)

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila utaratibu)

MHE. JAMES K. MILLYA: Mheshimiwa Spika, naomba niende kwenye marekebisho ya Sheria ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, Utunzaji wa Kodi, Sura ya 289. Kwenye *Schedule of Amendment* ya Serikali ile *clause 9(a)(ii)*, naomba Serikali

iongeze *clause* (iii) ya kusema kwamba badala ya kutoza nyumba zote, hata za *residential*, wa-*qualify* pale kwamba isiwe ya biashara tu bali na *residential*, waflikirie hiyo ili kuweka usawa nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, naomba niishukuru sana Kamati ya Madini. Kwa muda mrefu na Mheshimiwa Waziri amekataza madini ya vito yasitoke nje bila kukatwa. Hatuna wataalam wa kutosha, tunaomba mtupe muda wa kutosha kusafirisha kwanza kwa sababu madini ya *ruby* na tanzanite hatuna uwezo wa kukata hapa nchini, mturuhusu kwa sasa tuyasafirishe nje. Chukueni kodi yenu nyingine yoyote lakini mturuhusu tusafirishe *rough* kwa muda huu mpaka ambapo Serikali na nchi itakuwa tayari kwa ajili ya kukata.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri alisema kwamba kwenye *regulations* ambazo watatunga wadau wote wa madini watawahusishwa ili aweze kuruhusu kipengele hiki. Nimpongeze sana kuanzia jana ameanza kutoa leseni za kusafirisha madini yetu nje ya nchi, hongera sana Mheshimiwa Waziri. Naomba iwe kwenye hivyo madini ya vito, tanzanite na mengine yote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru pia kwa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa James, muda hauko upande wako. Tunaendelea na Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, atafuatiwa na Mheshimiwa Cecil Mwambe.

MHE. LOESIA J. BUKWIMBA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye Muswada huu wa Sheria ambao umeletwa mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa nianze kwa kuipongeza Serikali hasa Mheshimiwa Rais pamoja na Baraza la Mawaziri kwa kazi kubwa mnayoifanya. Kikubwa zaidi kwa

hii hatua ambayo kwa muda mfupi tu wachimbaji wadogo na wachimbaji mbalimbali wametoa maelezo fulani kwa ajili ya kuomba Serikali kufanyiwa marekebisho leo hii tumeletewa Muswada kwa ajili ya marekebisho. Kwa hiyo, naipongeza sana Serikali na Mheshimiwa Rais, kwa kweli amewajali wachimbaji wadogo wa nchi hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi na wachimbaji wadogo wa Geita na Tanzania nzima, nichukue nafasi hii kipekee kabisa kumpongeza na kumshukuru sana, hasa kwa ajili ya Muswada huu ambao umeletwa kwa ajili ya kupendekeza kuondoa kodi (*withholding tax*) kwa wachimbaji wadogo. Kwa hiyo, nashukuru sana kwa jambo hili, ni kubwa sana kwa ajili ya wachimbaji wadogo wa madini katika nchi ya Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika Sehemu ya Sita ya Muswada ambayo imekusudia kufanya marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148 ambapo sasa hivi ni asilimia zero, kwa maana kwamba wachimbaji wadogo hawatoi kodi yoyote ya Ongezeko la Thamani. Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kupongeza sana Serikali pamoja na Wizara kwa ujumla kwa jambo hili kubwa ambalo limeweza kufanyika kwa wachimbaji wadogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo sasa, naomba tukishapitisha Muswada huu kuwa sheria Mheshimiwa Rais aweze kusaini ili hatimaye iweze kuwa sheria iweze kutumika kwa haraka. Pia niombe Wizara inayohusika iweze kuanda zile taratibu na kanuni mapema zaidi ili hatimaye sheria hii iweze kutumika mapema kabisa na wananchi tuweze kunufaika na sheria hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa kuleta Muswada huu hasa kwa ajili ya zabibu. Ni kwa muda mrefu tumekuwa tukisikiliza jinsi ambavyo watu wa Dodoma walikuwa wakilalamikia suala hili kwa sababu ya kodi mbalimbali ambazo zimekuwepo. Napongeza sana hatua hii, nina imani kabisa hata Wagogo sasa wataweza kunufaika zaidi na kwa sababu ndiyo Makao Makuu ya Nchi

ya Tanzania itaneemeka vizuri sana kwa sababu masuala yao ya zabibu yameweza kuchukuliwa hatua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sikuwa na mengi sana kikubwa zaidi ni kushukuru na kupongeza Muswada huu ambaao umeletwa kwa haraka hapa Bungeni. Nilikuwa nashangaa yule anayehoji kwamba kwa nini umeletwa kwa haraka, mimi nashukuru sana kwa sababu Serikali inachukua hatua haraka kwa ajili ya kuondoa matatizo ya wananchi ili wananchi waweze kunufaika zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono Muswada huu kwa haraka zaidi. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana, tunakushukuru Mheshimiwa Lolesia kwa kututetea. Mheshimiwa Waziri wa Fedha, mwaka 2018 zabibu kwa wastani ilizaa vizuri zaidi. Wako wakulima maskini lakini wako katika umoja wao walikuwa wamekopa *TIB* na shamba lao likawa limezaa vizuri sana, lakini zabibu ile haikuwa na mnunuzi. Nikatafuta mtu mwenye hela zake nikamwambia hebu wasaidie hawa watu bwana zabibu zao zinunuliwe, akasema mimi sifanyi biashara ya zabibu lakini ngoja tuongee na wenye viwanda. Wakaenda kwa wenye viwanda kule Hombolo wakazungumza nao kwamba yeye yule tajiri atoe pesa awape wenye kiwanda lakini *interest free* na watalipa *any time in three years* mradi wanunue zile zabibu za wale wananchi, wenye kiwanda wakakataa bado, pamoja na kutupa hela hiyo bure na haina riba, hatuwezi kununua kwa sababu ya hii kodi. Kwa hiyo, hii kodi ilikuwa ina athari kubwa sana, tunaishukuru kweli Serikali. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Mwambe, atafuatiwa na Mheshimiwa Nyinamtemi.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye hoja hii ili yopo mbele yetu hapa ya Muswada unaohusu masuala ya madini lakini pia zabibu.

Mheshimiwa Spika, nakwenda moja kwa moja kwenye *section 5*. Kwanza nianze kwa kulikumbusha Bunge lako kwamba kuna wakati tunakuwepo humu ndani kwa nia nzuri kabisa ya kutaka kuishauri Serikali lakini kwa bahati mbaya kabisa kuna watu wanaamua kufanya propaganda badala ya kutekeleza wajibu wetu. Kutokana na hizo propaganda na kushindwa kutekeleza wajibu wetu ndiyo maana leo tupo hapa Siku ya Jumamosi, kinyume kabisa na utaratibu sisi tuliozoea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mwaka jana wakati tunajadili huu Muswada kuhusiana na sheria hiihii ambayo leo tunakuja hapa kuigeuza, tena kwa *speed* kubwa sana, baada ya Mheshimiwa Rais kuona kwamba kuna matatizo na wachimbaji hawa wa madini walipokwenda kuongea naye wakamueleza matatizo wanayoyapata kutokana na sheria hii, leo tunakutana hapa tunasema tunataka kubadilisha wenyewe. Tatizo hili tulillianzisha sisi wenyewe kwa sababu tulishindwa kutimiza wajibu wetu wakati huo. Wabunge wengi tu wa Upinzani, tena watu wakaja na *reference*; hawa watu tumewaona Morena wamekaa na watu ambao wameamua kuwabandika majina sasa wanaitwa mabeberu, wakiwa wanawapa pesa ili kuona sheria hii sasa inakwenda kubadilishwa ili kuweza kuwalinda mabeberu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Mpango tulisoma sisi pale taarifa yetu ya Kambi Rasmi ya Upinzani tukimueleza kwamba unachokwenda kukifanya sasa hivi unakwenda kuonesha au kuwasaidia watu wanaofanya *smuggling* ya biashara ya madini. Leo hii umeona kwamba hakuna pesa zinazopatikana kutokana na ubovu wa sheria iliyoko kule unaamua kulturudishia hapa ili tuweze kuijadili.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya sana tulitumia muda mrefu kuitengeneza sheria hii. Kuna vifungu vingi ambavyo navyo bado ni vibovu vinahitaji kuletwa humu ndani vifanyiwe marekebisho. Muda wa saa moja hautoshi sisi kama Wabunge kuishauri Serikali. Kwa hiyo, tunachokifanya sisi sasa hivi, tumechukua maoni ya wadau lakini tumechukua maoni machache sana ambayo

tunakwenda kuyapeleka pale lakini baada ya muda hatutaweza kupata kile ambacho tulikuwa tunakitarajia. Tusifanye nchi yetu kuwa ni nchi ya majaribio kwenye vitu ambavyo vinakwenda kutuangamiza sisi wenyewe. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tukae sisi hapa leo tuijulize, hivi toka tulipopitisha hii sheria mpaka sasa hivi Serikali yetu imepata hasara kiasi gani? Hayo ndiyo maswali ya msingi ya kujuliza. Pia niwaulize na ninyi wataalam kwamba wakati mnatengeneza hizi sheria, hivi ni kweli mliwa-*consult* wataalam wanaofahamu mambo haya? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, jana kwa bahati mbaya, nasikia baadaye mliamua ku-*withdraw*, ulivuja mpaka mwongozo wa namna ya kwenda kuzitumia hizi sheria lakini bado kwenye zile kanuni zenu mnakwenda kuleta mambo mengine ya ajabu ambayo hayawezekani. Endeleeni kukaa na wadau muweze kuboresha, mumsaidie Rais kuweza kuwasaidia hawa watu.

Mheshimiwa Spika, mmekwenda huku ndani mnakwenda kuongeza vitu vingine. Sasa hivi mnakuja hapa na *issue* mnasema kutakuwa na suala la *warehouse gems* pale, lakini pia kule ndani kutakuwa na masuala ya eti mtu aliyechimba madini huko anakwenda kuya-*deposit* anapewa stakabadhi, hili suala limeharibu sana kwenye mazao ya korosho. Sisi tuna utaratibu wa stakabadhi ghalani kwenye korosho, mnaleta stakabadhi ya ghala kwenye madini, nani anafahamu *quality* ya hayo madini, nani atakwenda kupima, nani atakwenda kufanya *valuation* hiyo siku mnakwenda kufanya vile vitu? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nashauri waangalie haya mambo kwa makini, wakae na wataalam wawashauri. Hatujaweza kuititia kwa sababu ya huu muda tuliokuwa nao ni mfupi sana, lakini huku ndani kwenye sheria iliyoletwa pamoja na mabadiliko vile vifungu tulivyovipitisha wakati ule vinahitaji kuwa *scrutinized* zaidi na zaidi ili Sheria yetu ya Madini iweze kuwa bora zaidi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini kwenye kanuni, wanakwenda kuongeza vitu ambavyo uwezekano wa kuvitekeleza ni mdogo. Serikali hii inadaiwa *about 500 billion* kwa ajili ya ushuru na kodi mbalimbali zinazolipwa kule, leo tunakwenda tunasema eti kila madini yaliyopo yapelekwe kwenye *warehouse*. Tunawaambia haiwezekani roli la mchanga kwa sababu nayo ni madini ya ujenzi tuyapeleke kwenye *warehouse gems*, tutafanyaje hizi kazi? Hivi vitu vingine Serikali wavikubali, tuache, tusiingize vitu visivyowezekana.

Mheshimiwa Spika, niombe muda uongezwe jambo hili lijadiliwe kwa kina. Ahsante sana. (*Makof*)

SPIKA: Nakushukuru sana. Nilishakutana Mheshimiwa Joseph Musukuma atafuatiwa na Mheshimiwa Mama Kilango Malecela.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie.

Mheshimiwa Spika, naomba niipongeze sana Serikali kwa hatua kubwa ambayo imechukua ya kuweza kutusaidia hasa sisi tunaotoka kwenye dhahabu. Namsikiliza rafiki yangu anaongea anadhani hizi ni korosho, dhahabu ina wenyewe, hii sio Kangomba. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kweli sheria ni nzuri lakini tunabishana hapa kana kwamba tumeshaweka ushawishi wa nchi jirani kuja kuingiza dhahabu hapa kwetu. Bado tunayo kazi kubwa ya kuendelea kubadilisha mambo mengine ili na wenzetu wale tunao-*compete* nao kama Uganda na Rwanda na Burundi waweze kuja kuuza Tanzania. Ukienda Uganda wao wanatoza asilimia moja tu. Sasa kwa masharti haya kwamba dhahabu inavyofika *border lazima iwekwe warehouse*, naomba nikwambie hakuna mtu atakwenda ku-*declare* dhahabu yake, kwanza huo ushawishi hatuna.

Mheshimiwa Spika, kuna watu wanatembea na kilo kama zilizoshikwa Mwanza tu, akifika pale *border a-declare* halafu arudi aje aziuze Geita, atembee nazo, nani atakubali hata kupanda hilo gari alimo humo ndani? Kwa hiyo, niombe tu masharti haya yaliyowekwa yaondolewe, dhahabu iwe *free* kama pesa. Ni kama vile wewe unavyoweza kuweka Sh.100,000 kwenye *wallet* na mtu awe na uhuru wa kuweka pesa yake mfukoni, tusiweke masharti kabisa kwenye dhahabu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri ananisikia, pamoja na kupunguza hizi kodi lakini kuna shida kule machimboni. Kule machimboni tunapotoa mifuko yetu 100 kwa mfano kwenye duara, lazima jioni watu wa Madini waje wachukue mifuko sita kama *share*, sasa hilo ni tatizo kubwa. Toka nimekuwa kiongozi sijawahi kuona ile mifuko inayochukuliwa kama kodi na madini inapigwa mnada kwa Sh.1,000,000, huwa inapigwa mnada kwa Sh.10,000 watu wanakula mgao. Kwa hiyo niombe, kama tumeamua kufuta kodi hakuna sababu ya watu wa Madini kwenda kusumbua watu wetu kule kwenye machimbo, waondoke tubaki kwenda kulipa kodi inayostahili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, liko suala la uhaba wa watumishi...

SPIKA: Mheshimiwa Musukuma, nitakuongeza dakika moja, unaweza ukalirudia hilo maana sijalipata kabisa. Hao watu wa Madini ni watu wa Serikali kabisa?

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Spika, kule machimboni kuna utaratibu kwamba mchimbaji anapotoa jioni mifuko yake 100 anaweka juu. Kabla ya zile kodi ambazo tumezijadili humu, watu wa Madini lazima wawe pale wachukue mgao wa mifuko sita kwenye mia. Ile mifuko wanakwenda kui葬za kama mnada kesho yake, inauzwa tu labda Sh.5,000, Sh.10,000 wakati uliyotoka nayo inauzwa Sh.1,000,000.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri ni shahidi, anaweza akathibitisha toka tunawapa ile mifuko sita, sita ni lini ofisi yake imewahi kula pesa ya mifuko hiyo ya madini kutoka Tanzania nzima? Kwa hiyo, tunatengeneza wizi tu wa watumishi wetu walioko kule. londo ke hiyo kodi ya kuchukulia kule wabaki wanachimba *free halafu tukapambane* kwenye kodi ambayo mnaipunguza kule. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tuna uhaba sana wa watumishi. Naomba nichukue mfano wa Geita. Geita peke yake tuna *elusion* kama 300 au 400, watumishi walioko pale ni watano tu na Geita pale kwa uchache kwenye mkoa wetu unaweza ukakuta kuna *rush labda* 30 mpaka 40 na magari yako mawili, hao watu watano wanaamka kila siku kwenda kufungua kwenye *elusion* kuchukua kodi ya Serikali. Watu watano hawa wanagawana sasa kwenda kupambana na zile *rush zilizopo* Geita labda kwa siku zipo 200 au 300, hawana hata usafiri wa kwenda nao, inabidi kama mtu wa *elusion* umfuate kwa gari lako, mnakwenda mnajadili kwenye gari. Kwa hiyo, mpaka mnafika kule Mheshimiwa Waziri yataendelea tu yale uliyoyakamata juzi Dodoma, utakuta mtu ame-*declare* kilo moja kumbe ana kilo 30. Kwa hiyo, pia hilo suala la watumishi ni vizuri mkaliangalia na vitendeakazi vikawepo.

Mheshimiwa Spika, liko suala la msamaha wa vitu vinavyo-*process* dhahabu halikuzungumzwa hapa. Tumesikia wenzenetu watani zetu Wagogo wakati wanaomba hapa wamesema wanaomba zile mashine za kuchakata mvinyo na zenyewe ziondolewe ushuru. Hata kwenye dhahabu *process* ya kuipata ni vitu vingi vinashirikishwa. Kwa hiyo, vile vi-*attachment* vya ku-*process* dhahabu nashauri pia Serikali ikaondoa kodi.

Mheshimiwa Spika, dhahabu ni pesa, tusiiwekee masharti. Sisi wachimbaji, naweza kuwa nachimba kwenye *rush* napata gram kumi au mbili, nakula kidogo tu Sh.30,000 nyingine natunza ili siku nikirudi kwa mke wangu nikamuoneshe dhahabu. Si lazima niiuze leo, naweza nikaitunza siku nina shida nikaja kuiiza hata Dodoma. Sasa haya mambo ya kuweka masharti lazima dhahabu ukitaka

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

kutoka hapa uwe na leseni ya *import*, haiwezekani hivi vitu. Tutakuwa bado tunamuongezea Rais mzigo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho, naungana na mwenzangu Mheshimiwa Bashe, pamoja na kwamba itasainiwa lakini naomba kwenye kutunga kanuni ni lazima washirikishe wadau kwa nia nzuri tu. Wadau washirikishwe watoe maoni yao...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Musukuma.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

SPIKA: Tunaendelea na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela atafuatiwa na Mheshimiwa Bobali.

MHE. ANNE K. MALECELA: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba *ku-decalre interest* kwamba mimi ni mwananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro, Wilaya ya Same lakini mimi pia ni mwananchi wa Mkoa wa Dodoma, Jimbo la Mtera. Kwa niaba ya walima zabibu, ndugu zangu Wagogo, nitoe shukrani za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Rais kwa jinsi ambavyo ametugusa wakulima wa Mkoa wa Dodoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikiri kabisa tulikuwa tunapata shida sana. Niseme ukweli, mume wangu ni mkulima mkubwa wa zabibu, ana ekari 11 pale Chinangali. Nimuombe Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa unyenyekevu mkubwa, Bunge Ilijalo la Bajeti uje Chinangali uone ni kiasi gani wakulima wa zabibu pale tuna shida. Serikali kwa hili mlilolifanya la kupunguza huu ushuru wa mchuzi wa zabibu mmewapa usingizi wakulima wa zabibu hapa Dodoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama ulivyozungumza, mwaka 2018 zabibu zilioza, zabibu ni zao tofauti na nazi na mazao

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

mengine. Siku ya kuvuna ikifika usipovuna ndani ya wiki moja unapoteza kabisa. Wakulima wa zabibu kwa Mkoa wa Dodoma, *including* mume wangu, Mzee Malecela, mwaka 2018 tulipoteza moja kwa moja. Kwa hiyo, kwa unyenyekevu mkubwa nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa jinsi ambavyo ametufikiria sisi wakulima wa zabibu.

Mheshimiwa Spika, sina mengi ya kusema, nashukuru sana, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Nilishakutaja Mheshimiwa Bobali.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nitajikita kwenye eneo moja la mabadiliko ya kodi (*Property Tax*) kwenye Serikali za Mitaa. Niliposoma hili *amendment* kifungu cha 11, kidogo nimepata *shock*, sijaelewa, labda Mwanasheria Mkuu ama Waziri atatufafanulia. Inasema, *in the case of City Council, Municipal Council and Town Council areas; na ikaongezewa kifungu cha District Council areas.*

Mheshimiwa Spika, kwenye Halmashauri za Vijiini wakati mwingine unakuta Makao Makuu ya Halmashauri zile yako kwenye Makao Makuu ya Mikoa. Nitatolea mfano, Halmashauri yetu sisi ya Lindi Vijiini, Makao Makuu yetu yako Lindi Mjini pale. Kwa hiyo, ukiweka eneo la Halmashauri ya Wilaya, maana yake ni vijiini vyote vya Jimbo la Mchinga na vijiini vyote vya Jimbo la Mtama.

Mheshimiwa Spika, sasa nataka kupata ufanuzi, kinachokusudiwa hapa kwenda kutozwa kodi katika hizi nyumba, ni zile nyumba mpaka za vijiini au zile Makao Makuu ya pale ilipo Halmashauri? Nitatolea mfano huu kwa sababu ya kesi hiyo kwamba ziko halmashauri ambazo Makao Makuu yake yako maeneo ya mijini.

Mheshimiwa Spika, kuna jambo limezungumzwa kuhusu suala la utunzi wa sheria hii ya bajeti ya tarehe 21

Juni, 2017. Haya leo ambayo tunaona ni mabadiliko makubwa kabisa, nami niseme ukweli, kistaarabu kabisa kwamba Mheshimiwa Mpango tulikushauri mwaka 2017 na mwaka 2018, umekuja nayo umeyafanya. Sisi kama Bunge, bila kujali kwamba hawa Wapinzani ama hawa ni Chama Tawala, tuna haja pia ya kujipongeza kwamba ushauri wetu umepokelewa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nashukuru. Pia Mheshimiwa Waziri alipaswa ku-*admit* kwa kazi kubwa tuliofanya Waheshimiwa Wabunge kwenye kushauri hili. Kwa kuwa ushauri huo ameupokea, wakati mwingine anapokuja kwenye Bajeti, asisite pia kusikiliza ushauri wa Waheshimiwa Wabunge. Tuepuke hii aibu ya leo tunatunga sheria, kesho kutwa inakuja kufanyiwa *amendment*. Imekuwa ni *trend* ya Bunge la sasa kuwa tunafanya *amendments* nydingi sana ya sheria ambazo hazijadumu kwa muda mrefu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili nalo nadhani kitichako italionia kwamba marekebisho mengi ya shera yanayoletwa ni sheria hizi ambayo tumetunga kwenye Bunge hili la 11. Ina maana kwamba wakati tunatunga hatukuangalia ama hatuku-*consult* wadau.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa na *interest* na eneo la Serikali la Mitaa, naomba sana ufanuzi kwa sababu suala liliopo huko, watu wanajua kwamba sasa ni nyumba zote, vijijiini na kwenyewe wataenda kutoza hiyo kodi ya shilingi 10,000/=. Tungepata ufanuzi ili leo tukiondoka tukawaambie. Kwa mfano, wale wananchi wangu wa Mchinga, Kilolambwani, Melola na wapi ambako ni maeneo tu ya Halmashauri ya Vijijiini basi wajue kwamba wao hawahusiki juu ya jambo hili.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Agness Marwa.

MHE. AGNESS M. MARWA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Rais

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

na Mheshimiwa Mpango kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuondoa ushuru kwa wachimbaji wadogo wadogo. Pia naipongeza Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kuitia Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kutusikiliza Wabunge wake tunapokuwa tunashauri. Ndiyo maana huwa tunawashauri wenzetu. Unaposhauri kwa uzuri, hata unayemshauri anakusikiliza. Kwa mfano, nilishauri kuhusu suala la malipo au fidia ya watu wanaodai madai yao Tarime, waliokuwa wanaitwa Tegesha na sasa Mheshimiwa Rais amenisikiliza; alimtuma Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri wake wa Madini na sasa wanalipwa kuanzia wiki ijayo, watapewa malipo yao yote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kipekee namshukuru pia Mheshimiwa Rais kwa kukubali kutoa mapori ya akiba kuwa hifadhi ya Taifa kwa sababu ni suala zuri kwa maana ya kwamba tutaongeza pato la Taifa baada ya kuwa tuna hifadhi nydingi za Taifa.

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wenzetu humu ndani wanatakiwa watafutiwe hifadhi ya ziada ili kusudi wakaishi huko kwa sababu wana tabia za wanyama. Hawaoni mambo yanayofanyika na Mheshimiwa wetu Rais, hawakubaliani na mambo yanayofanyika na Mheshimiwa wetu Rais, utadhani wao sijui wanaishi wapi! Aliiomba dada yetu *JD*, naomba ninukuu kidogo, "Hawaijui walipotoka, watajuaje wanakokwenda? Ya kwao yamewashinda, yetu hawatoweza." (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo,...

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu. (*Kicheko*)

SPIKA: Mheshimiwa Agness. (*Kicheko*)

MHE. AGNESS M. MARWA: Ndiyo Mheshimiwa Spika.

SPIKA: Nyimbo haziruhusiwi. Endelea Mheshimiwa Agness. (*Kicheko*)

MHE. AGNESS M. MARWA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pia, napongeza kipekee pia Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, pia kupunguza ushuru wa mchuzi ...

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu.

SPIKA: Mheshimiwa Agness, kuna...

MHE. AGNESS M. MARWA: Ndiyo!

SPIKA: Kuna Mheshimiwa amesimama hapa.

KUHUSU UTARATIBU

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa, naomba Mheshimiwa Mbunge ambaye anaendelea, amekiuka kanuni ya 64 kwa kutumia lugha ya kuudhi pale aliposema kwamba Waheshimiwa Wabunge wengine wana tabia za kinyama.

Mheshimiwa Spika, kama hukisikia, amesema hivyo. Hiyo ni lugha ya kuudhi, Waheshimiwa Wabunge hawana tabia za kinyama, ni binadamu, wamechaguliwa na wananchi, wanakubalika, wanaeleweka na wako vizuri.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa heshima kubwa hiyo lugha ya kuudhi Mheshimiwa Mbunge ni vema akaiondoa. Afute kabisa. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Agness, kama ulisema hilo, futa tu ili uendelee.

MHE. AGNESS M. MARWA: Mheshimiwa Spika, sawa nimefuta. (*Kicheko*)

SPIKA: Endelea Mheshimiwa.

MHE. AGNESS M. MARWA: Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi

na kupitia Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa mambo mazuri anayoyafanya ya kuwatetea hasa Wajasiriamali wadogo wadogo wanyonge na haswa kwa kupunguza tozo ndogo ndogo kama vile kutoa tozo kwenye huu mvinyo ambao kwa maana moja au nyingine wajasiliamali wadogo wadogo ambao wanauza huu mchuzi wa zabibu, sasa watapa soko zuri na watapandisha kipato chao juu zaidi.

Mheshimiwa Spika, naamini kabisa Mheshimiwa Mpango ataangalia pia kuondoa ushuru kwenye mahindi ili kusudi sasa hatu gongo baadaye itengenezwe kwa kutumia mahindi ili kusudi baadaye ibadilishiwe jina na kupandishwa hadhi ili ipewe jina la mvinyo mzuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Kwa kweli Serikali ya Chama cha Mapinduzi imefanya kazi kubwa, imefanya kazi nzuri...

*(Hapa Kengele ililia kuashiria
kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

SPIKA: Mheshimiwa Agness kengele imeshalia. Nakushukuru sana, ahsante sana.

MHE. AGNESS M. MARWA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Magufuli oyee! (*Makof/Kicheko*)

SPIKA: Mwaka wa Uchaguzi huu, lazima watu wachangamke. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Profesa Maghembe, kwa upande wa Wabunge huyo ni wa mwisho, halafu atafuatia Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Jafo. Mheshimiwa Maghembe, dakika tano.

MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kutoa mawazo kidogo tu katika Muswada huu. Ni siku 17 tu wachimbaji

wadogo walitoa matatizo yao mbele ya Mheshimiwa Rais na kwa *speed* aliyofanya kuleta Muswada huu, anastahili tumpongeze sana, Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli. Hii ni kazi nzuri na tusiibeze kwa njia yoyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nimeangalia kifungu cha 26 cha sheria hii ambacho kinaongelea juu ya *import permit*. Wako watu wanachimba na kutafuta madini hapa Tanzania kutoka Thailand; wako watu wanatoka nchi hata ya Afghanistan wanachimba hapa; wako Wa-Senegal wanachimba hapa na wanaondoka na madini yetu, kwa sababu wanapokwenda nyumbani kwao kule, wanapokelewa kama wao ni mashujaa.

Mheshimiwa Spika, sisi tunakuwa Wakatoliki zaidi ya *Pope*. Mtu anakwenda anachimba madini yake popote anapoyachimba, naomba tukifute hiki kifungu kilichorekebishwa na Serikali, kinaitwa 86 (a) katika mabadiliko haya ya Serikali. Hiki kifungu nawaomba sana; na uzee wangu leo nataka niwapigie magoti, tukifute kabisa. Mtu yejote ambaye ameleta madini huku Tanzania, afanye *declaration* ndani ya soko anapouzia ili Serikali iweze kuweka *record*. Kusiwe na *application* yoyote kule mpakani au *application* yoyote huko njiani, apeleke madini mpaka sokoni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nchi zote hizi za dunia zinajengwa kwa mambo mengi; na yako mambo mengi ambayo katika Bunge lililoko wazi namna hii, hatuwezi kusema kila kitu. Kwa hili, imenibidi nikuombe sana kwamba nisimame na nili-*convince* Bunge lako Tukufu katika hili. Tufute hiki kifungu cha 26 kabisa. Kama Mheshimiwa Waziri nataka kukileta kwa namna, akiweke kwenye kanuni ya kumtaka mtu aliyeleta madini afanye *declaration* kwenye soko.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Nakushukuru sana Profesa. Natumaini tutakapoingia kwenye vifungu huko, tutaelewana Kiswahili. Maana kifungu hicho ni sawa sawa na mtu kwenye

familia yako kusema watoto wangu ni marufuku kuleta mali ambayo imepatikana nje ya Kijiji chetu, ni marufuku. Sasa hiyo si unataka familia yako iwe masikini! Mtoto akileta mali nyumbani, anapigiza kigelegele. Sisi tunapiga marufuku watoto wetu wasiletie mali. Wanaweza kutufafanulia vizuri, labda hatujaelewa sawasawa.

Mheshimiwa Waziri Jafo, dakika tano, Mheshimiwa Waziri wa Madini, dakika tano.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumpongeza sana mtoa hoja, AG wetu katika Muswada huu wa Mabadiliko ya Sheria Mbalimbali. Pia yangu ni mafupi.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuunga mkono hoja hii iliowasilishwa hapa. Pia ni wazi kwamba sheria hii inagusa sehemu ya *Property Tax* ambapo nami tuna eneo ambalo tunalismamia. Kikubwa zaidi, napenda kumshukuru sana AG kwa hii kazi kubwa ambayo ameifanya kwa kuleta Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, pili, kwa sababu nasimamia Mamlaka ya Serikali ya Mitaa na ninajua kila jambo tunalofanya, lengo letu ni kwa ajili ya kuhakikisha tunalipeleka nchi yetu mbele. Kikubwa, naishukuru sana Wizara ya Fedha kwa ujumla. Katika kipindi hiki cha sasa ambacho mwanzo kidogo kulikuwa na changamoto kubwa sana katika Bunge letu kuhusu mambo ya *Property Tax*, ikionekana kwamba imeleta hali mbaya sana hasa katika sehemu za Miji.

Mheshimiwa Spika, kwa ushahidi wa karibu, kwanza naishukuru sana Serikali hasa Wizara ya Fedha, katika kipindi cha Awamu ya Kwanza mwezi Nne mwaka 2018 iliweza kutoa takribani shilingi bilioni 131.6 kwa ajili ya miradi mikakati ambayo imekuja katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Katika hizo, juzi nilikuwa naongea na wenzangu wa Manispaa ya Kinondoni na wengine kwamba Kinondoni mpaka hivi sasa

wamepokea zaidi ya shilingi bilioni 32 katika miradi ya mikakati. Hata *Property Tax* wangekusanya, hailingani na fedha walizopewa wao. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Manispaa ya Ilala, ukiangalia Machinjio ya Vingunguti, Soko la Kisutu linalojengwa pale hivi sasa imechukua zaidi ya shilingi bilioni 20. Jiji la Dar es Salaam wamepata takribani shilingi bilioni 50. Hizi zote ni kwa ajili ya miradi mikakati. Manispaa ya Moshi wamepata takribani shilingi bilioni saba kwa ajili ya ujenzi wa stendi ya Moshi pale Mjini, ambayo hata ile *Property Tax* wangekusanya isingefika kiasi hicho. Juzi tulianza kwa ndugu yangu Mheshimiwa Mch. Msigwa pale, zaidi ya shilingi bilioni moja, sasa tutaenda kuimarisha machinjio ya pale Iringa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kikubwa zaidi, ukiangalia *trend* ya kwanza, upatikanaji wa fedha zaidi ya shillingi bilioni 131; safari hii, juzi tu, katika Mkutano wa juzi *PST* alikuwa na timu ya wataalam katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa, imetoka zaidi ya shilingi bilioni 137. Hii ni *trend* nzuri.

Mheshimiwa Spika, kikubwa zaidi nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge, tushirikiane kwa pamoja. Lengo letu ni kwamba sheria hizi zikipita, lakini kwa pamoja tukiwa na lengo moja la kuhakikisha nchi yetu inasonga mbele; na hasa pale penye upungufu Waheshimiwa Wabunge wanaposhauri, tuchukue vizuri, itasaidia nchi yetu hii kuweza kusonga mbele.

Mheshimiwa Spika, kikubwa zaidi niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge tuendelee kuishauri Serikali kwa wema kwa kujua kwamba ushauri huu unaotolewa katika njia moja au nyingine, unaenda kuimarisha Mamlaka za Serikali zetu za Mitaa, kuimarisha Serikali yetu kwa ujumla na mwisho siku tuweze kupata mabadiliko makubwa kwa ajili ya nchi yetu hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya haya machache, kuna jambo moja ambalo Mheshimiwa Bobali alizungumza kuhusu Halmashauri zetu, nadhani hili limezungumzwa katika kifungu

cha 10 ambacho ukiangalia *amendment* kimefanuliwa vizuri na AG wetu hapa. Nadhani jambo hilo limekuwa addressed vizuri kuhusu wapi eneo katika Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya inaenda kukusanya.

Mheshimiwa Spika, *otherwise*, namshukuru sana AG na ninaomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa wa Nchi, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Jafo. Sasa nimkaribishe Mheshimiwa Waziri wa Madini, Mheshimiwa Doto Biteko, dakika tano pia.

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii. Nitumie nafasi kuunga mkono hoja na nimpongeze sana mtoa kwanza kwa kuwasilisha, lakini kwa kazi kubwa aliyoifanya. Nawashukuru sana Kamati ya Bajeti ambao walishughulikia Muswada huu, tumefanya nao kazi kwa karibu sana, chini ya Mwenyekiti, Mheshimiwa Simbachawene. Kwa kweli ni Kamati makini, wamefanya kazi kubwa sana. Kama walivyosema, tumefanya nao mpaka usiku wa manane; na kwa kiasi kikubwa yale yote ambayo wao walipendekeza yaweze kurekebishiwa, wameyarekebisha.

Mheshimiwa Spika, nataka kuongelea jambo moja tu. Jambo lenyewe ni kumpongeza sana Mheshimiwa Rais. Mabadiliko haya yaliyoletwa, kwa kweli *champion* wake aliyesababisha tufike hapa ni Mheshimiwa Rais. Kwenye Mkutano ule ambao tulikutana na wadau wa madini pale Dar es Salaam, tulipomwalika Mheshimiwa Rais kuja kutufungulia Mkutano, yeye aliamua ku-*dedicate* siku zima kukaa na kuwasikiliza wachimbaji wadogo. Hatua hii ni kubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sifa ya Serikali inayotokana na watu, ni kuwasikiliza watu wake. Ndiyo maana mnapoona tunaleta mabadiliko ya sheria hizi, ni kwa sababu sifa hiyo Serikali ya Chama cha Mapinduzi inayo, kwamba inawasikiliza

watu wake. Sheria hizi ziko kwa ajili yetu, kutuhudumia sisi. Wakati wa kutekeleza tukiona kuna ugumu mahali fulani siyo dhambi kurekebisha. Hiki ndicho kilichofanyika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kiashiria kikubwa kabisa kinachoonesha kwamba tunawasikiliza watu, kwanza ni ule mikutano wenyewe tuliofanya na wadau. Kiashiria kingine kikubwa ni ulr mwitikio ambao Serikali imekuwa nao wa kuja kurekebisha sheria hizi ili kuondoa kero zilizokuwepo kwenye Sekta ya Madini. Naomba nitoe nafasi nimpongeze na kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kutoa nafasi hiyo ili wachimbaji wadogo waweze kuongeza mchango kwenye Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Spika, limesemwa neno moja hapa, nami naamini aliyesema alikuwa anazungumza kwa maana ya kutania tu kwamba tumeamua kubadilisha kwa ajili ya *change gear* angani. Wadau wa madini wamekaa hapo juu. Kwa muda mrefu walikuwa na mambo ambayo wanalamikia na ambayo sisi wenyewe wasimamizi wa sheria tulikuwa tunayaona kweli ni changamoto. Tumeamua kurekebisha ili tuweze kuongeza tija ili tuweze kudhibiti utoroshaji. Kwa mara ya kwanza kwenye historia ya nchi hii, marekebisho haya yanatengeneza masoko ya madini kwenye nchi yetu, hatukuwahi kuwa nayo. Kila mtu alikuwa anachimba, anajua atapeleka wapi. Sasa wamewekewa utaratibu, wapi watakwenda kuuza, wamewekewa utaratibu wa namna gani watasimamiwa pale kwenye masoko ya madini.

Mheshimiwa Spika, wito wangu kwa wachimbaji wadogo ni kwamba fursa hii tumeipata, tuitumie vizuri ili tuweze kuongeza manufaa. Yameongelewa maneno hapa kwamba sasa wale wenyе *Dealer License*, kwa sababu ya uwepo wa masoko haya, watazuiwa ku-*export*, hapana. Wale *Dealership License* wataendelea ku-*export* kwa mujibu wa sheria. Kwa sababu kifungu hicho kinachowaruhusu ku-*export* bado kipo.

Mheshimiwa Spika, ilikuwepo changamoto ya kuwazuia kusafirisha madini ghafi. Tumerekebisha kifungu hicho cha sheria na sasa tumetoa mwongozo ambao kila mtu mwenye madini atapaswa kuongeza thamani kwa kiwango fulani. Kama alivyosema Mheshimiwa Millya, tayari tumeanza kutoa vibali vya watu wanaotaka ku-export.

Mheshimiwa Spika, wachimbaji wadogo wamekaa kwenye *gallery* yako, tatizo hilo tumeliondoa. Nawaomba sana wachimbaji wadogo watumie fursa hii waweze kuomba vibali, waweze kusafirisha madini ili walipe kodi. Kodi ambayo ilikuwa inawaudhi ni hizo ambazo zimezungumzwa. Naamini Mheshimiwa Waziri wa Fedha atakuja kuziongelea.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kuwahakikishia wachimbaji wadogo wote Tanzania, Serikali ya Awamu ya Tano ya Chama cha Mapinduzi inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, ipo kwa ajili yao, ndio maana tunachukua muda mwingi wa kuwasikiliza. Hata siku waliyopendekeza uwepo wa Siku ya Madini Nchini, sisi tumeshaanza kuifanyia kazi kwa kushirikiana nao.

Mheshimiwa Spika, hata ukiwaauliza wachimbaji wadogo kama wanasilizwa ama hawasilizwi, wao ni mashahidi tunawasilikiza sana, tena hatuwasilikizi ofisini tu, tunawafuata huko waliko kwenye migodi. Pia tunazungumza nao kwenye vikao, tunazungumza nao kwa kuandikiana na mapendekezo yao ndio tutakayowatumia hata wakati wa utengenezaji wa kanuni tutawashirikisha kwa sababu ni takwa letu kwamba twende pamoja, hakuna mtu anayetaka kumvizia mwenzie, tunachotaka ni wote tuwe kwenye boti moja ili tuweze kuimarisha sekta ya madini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na nakushukuru kwa nafasi hii. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Nimkaribishe Mheshimiwa Waziri wa Fedha Dkt. Mpango, dakika saba.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa fursa hii. Nianze pia kwa pongezi kwa mtoa hoja Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, lakini pia Kamati ambayo ilichambua vizuri sana Muswada huu. Vile vile niwapongeze Mawaziri wenzangu, Mheshimiwa Waziri wa Madini, Mheshimiwa Waziri anayesimamia TAMISEMI, lakini na wachimbaji wadogo ambao kwa kweli pindi Muswada huu utakapopitishwa na Bunge lako utakwenda kuwanufaisha.

Mheshimiwa Spika, nianze na maoni ya Kamati kwa haraka; niseme tu kwamba kwa kweli tutajitahidi kuhakikisha kwamba kanuni zinabakia na nia na dhamira ambayo imeoneshwa na Mheshimiwa Rais kupitia Muswada huu, kwa hiyo msiwe na wasiwasi. Pili, kuhusu kodi kwenye mashine za ukataji wa madini pia *VAT* kwenye mashine za kusindika mvinyo, naomba niseme tu kwamba tutayangalia haya katika uchambuzi wa mapendekezo ya marekebisho ya kodi kwa ajili ya mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Spika, nikikimbia kwa haraka kwenye maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani, Muswada huu kwa hakika utaandikwa pia kwa lugha ya Kiswahili, utatafsiriwa, kwa hiyo wananchi wetu wataweza kusoma bila wasiwasi. Kwa upande wa kama mabadiliko haya yameongeza mapato au yamepunguza niwahakikishie tu kwamba uchambuzi ulifanyika na kwa mfano nitatoa tu mfano kwa upande wa ushuru wa bidhaa mapato yatapungua kwa takribani bilioni 5.7, upande wa *exemption* ya *VAT* yatapungua kwa milioni 741, lakini *withholding tax* nayo itapungua kwa milioni 104. Jambo kubwa sana ni kwamba kwanza kwa upande wa mrabaha huu utaongezeka kwa miezi iliyobaki kufikia bilioni 10, pia tunajua kwamba kodi zinatokana na ajira, *voluntary compliance* ya watu wetu na shughuli za madini ambazo zitaongezeka kutokana na hatu hizi zitatuongeza mapato.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kodi ya majengo napenda tu niwahakikishie kwamba, *TRA* inaendelea kukusanya vizuri kwa kipindi cha Julai impaka Disemba kama ambavyo tulitolea ufanuzi kwenye Kamati, *TRA*

ilishakusanya bilioni takribani tisa ambazo ni kama asilimia 62 ya lengo, lakini pia tunafanya jitihada nyingine kuhakikisha kwamba *TRA* inakusanya zaidi. Mwaka jana tulajiri wafanyakazi 400, tunakwenda kuongeza wafanyakazi wengine 167 tunawaongezea vitendea kazi hususan magari kwa mwaka huu tutawaongezea magari 74, lakini jambo la msingi zaidi tunakwenda kuongeza ushirikiano wa Mamlaka ya Mapato na Halmashauri za Wilaya na wanashirikiana katika kutambua maeneo na nyumba.Pia kama nilivyosema, kuna taratibu nyingine za kiutawala za kuziwesha Mamlaka za Halmashauri kuweza kuisaidia Mamlaka ya Mapato kukusanya.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa majengo kuuzwa kwa kudaiwa kodi ya nyumba, napenda tu nisitizie kwamba, tumechukua hatua za kupunguza kodi ya majengo na kuifanya iwe ya mfuto. Kwa hiyo inakuwa *flat rate* ambayo ni ndogo ya asilimia 10 kwa lengo hilo la kuondoa adha hiyo. Pia niwakumbushe wote, sisi wote ambao tuna *properties* zinazodaiwa kodi kwamba kodi hii inalipwa mara moja tu kwa mwaka na kwa hiyo kila mtu ana wajibu wa kuijandaan kulipa hizo Sh.10,000. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile sisahau kwamba katika mapendekezo tunayoleta hapa, tunaondoa nyumba zile ambazo kwa kweli wanaishi wananchi wetu maskini, tumesema wazi nyumba za tope, za majani zote tunaziondoa kwenye wigo wa kutozwa hii kodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, labda lingine nimeambiwa hapa kwamba wakati wa bajeti tuwe tunasikiliza ushauri wa Waheshimiwa Wabunge, naomba tu niseme kwamba, kuleta mabadiliko sio udhaifu, kuleta mabadiliko ni pamoja na Serikali kuwa *flexible*, lakini pia ni muhimu sana kukumbuka kwamba wajibu wangu mwingine ni kulinda mapato ya Serikali. Pia msisahau kwenye ushuru wa bidhaa kwenye mvinyo kwa mfano, kwenye zabibu ambazo zinazalishwa hapa nchini kwa kiwango cha asilimia 75 tulipunguza ushuru wa bidhaa, kwa hiyo tunaendelea kluyashughulikia mambo

haya kila tunaposikia malalamiko ambayo tunaona ni *genuine* kutoka kwa wananchi wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ilisemwa hapa kwamba pengine utaratibu huu wa Mamlaka ya Mapato kukusanya kodi ya majengo na huu wa *D by D*, naomba tu nisisitize kwamba Serikali inaendelea kupeleka fedha kwenye Halmashauri kuititia kwenye bajeti zao, lakini vilevile kwa miradi mingine ambayo inapata fedha kutoka kwa wafadhili kama *P4Rbado* tunaendelea kupeleka pia fedha kwenye halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hofu ile ya nyumba za vijiji kutozwa kodi, kwenye marekebisho tumebadilisha kifungu cha 10 na tumebadilisha na kukiweka sasa kifungu cha 6(1) ambako tunaeleza kwamba tozo hii sasa itahusu Makao Makuu ya Wilaya ndani ya mipaka ya Makao Makuu ya Wilaya na *townships* na kwa hiyo hicho kifungu kinachofanya kimsingi ni kuondoa vijiji katika maeneo ambayo yanatozwa hii kodi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba niwashukuru sana wale wote waliochangia kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuja na hatua hii ya kusikiliza wananchi wake na kutuagiza sisi wasaidizi wake ili tuweze kuleta mabadiliko haya.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, najua wewe ni mdau mkubwa sana wa mchuzi wa zabibu, tulikusikia kwa niaba ya wakulima wote wa zabibu na mimi nikiwa mmoja wao, ahsante kwa mwongozo wako. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Mpango. Sasa nimkaribishe mtoa hoja Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Profesa Kilangi, dakika 10, tafadhali.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kukushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kufanya majumuisho ya mjadala kuhusu Muswada

wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2019. Katika mijadala huu jumla ya Waheshimiwa Wabunge 10 wamechangia kwa kuzungumza na hatukupata michango wka maandishi.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mizuri. Tumepokea maoni mazuri ambayo yamelenga kuboresha si tu Muswada, bali hata masharti mengine ya Sheria mama husika na kwa ujumla maoni na ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge ni ushahidi kwamba suala la marekebisho ya sheria kwa lengo la kuboresha utekelezaji madhubuti wa sheria zilizopo linamhusu kila mmoja wetu. Katika Bunge hili, hili ni jambo endelevu na ndiyo maana mara kwa mara Serikali inakuja na Miswada ya aina hii kwa ajili ya kuboresha sheria zetu hasa tunapoona kwamba utekelezaji umetupatia changamoto kidogo.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja mbalimbali zilizotolewa, nawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri wote ambao wamechangia katika kuhitimisha hoja hii na wamezijibu baadhi ya hoja hizo na nafikiri sitakuwa na haja tena ya kurudia hizo hoja ambazo wamesaidia kueleza kwa ufasaha kabisa.

Mheshimiwa Spika, nafikiri liko jambo moja ambalo pengine ingekuwa ni vizuri nikalitolea ufanuzi na hili ni suala la *import permit* kwa wale wanaotaka kuingiza madini kutoka nje ya Tanzania na tumeyasikia maoni ya Waheshimiwa Wabunge, nafikiri hata wakati wa mijadala kwenye Kamati jambo hili lilibuka sana na hofu nyingi zillioneshwa kwamba kwa mfano, majirani zetu hawana masharti kama haya tubadilishe masharti isiwe kwamba mtu anapewa *permit* labda anapokuwa anaingia au kabla ya kuingia, lakini turahisiche utaratibu na tuitoe *permit* hii kwenye maeneo watakapokuwa wanauzia yaani kwenye masoko.

Mheshimiwa Spika, sasa napenda kueleza haya machache yafuatayo: Kwanza hili suala la *import permit* kwa madini siyo jipya, zipo *import permit* ambazo tayari zinatolewa

na Wizara ya Madini hasa kwa madini yanayotoka nje kupitia bandarini yanayohitajika kwa ajili ya viwanda vyetu. Hawa wote wanaoingiza madini haya wanapata *import permit* inayowawezesha kuingiza madini haya. Kwa hiyo kwa kweli Kisheria na kiutaratibu siyo jambo jipya, tunachotaka kufanya sasa, tulilingize kwenye Sheria Mama.

Mheshimiwa Spika, ni kwa nini tuwe na *import permit*? *Import permit* ni kama jicho linalosaidia kuangalia madini yote yanayoingia na tukiiondoa hii import permit kwanza tutaingiza mgongano na Sheria iliyopo kwa sasa hivi kwa sababu tuna kifungu cha tano cha Sheria ya Madini (*Mining Act*) kinachozungumza kwamba madini yote katika nchi hii popote yalipo ardhini, juu ya ardhni na kadhalika ni mali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na huu huwa ni msingi unaowekwa katika Sheria zote za Madini za nchi mbalimbali. Ukienda kusoma Sheria yoyote ya nchi yoyote itasema, madini yale yote ni mali ya Serikali ile au ni mali ya nchi ile na sasa wanaruhusu mtu mmoja mmoja aweze kuyamiliki hayo kupitia utaratibu wa kisheria kupitia leseni. Kwa hiyo tukiodoa *import permit* tutaanza kuwa na mgogoro na kifungu hicho.

Mheshimiwa Spika, pia kuna kifungu kinachosema kwamba, mtu hataruhusiwa kuchimba au kufanya jambo lolote kuhusiana na madini, hiki ni kifungu cha sita bila kuwa na leseni au kitu chochote kinachomruhusu kufanya namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, zaidi liko tatizo kwenye kifungu cha 18 ambacho kinafanya ni kosa kwa mtu kukutwa na madini ya namna hii vinginevyo awe ama ana leseni ya uchimbaji ile *primary mining license* au *mining license* au *special mining license* au *Broker's license* au *Dealer's license* na sisi tukasema huyu anayeyaleta haya madini nchini yeye tunam-cover namna gani? Ndiyo tukasema afadhali tuwe na *import permit* kwa sababu ile *import permit*tampa ruhusa ya kuwa na haya madini na popote pale atakapokutwa nayo atakuwa ana haki ya kuwa nayo kwa mujibu wa hiyo *import permit*.

Mheshimiwa Spika, pia tukiiondoa kabisa tutapata shida na baadhi ya madini. Tunayo madini kama almasi ambayo yana masharti na masharti hatukuyatengeneza wenyewe, yako katika ngazi ya Kimataifa, yanatokana na mambo ya *Kimberly process*. Kwa mfano, kuna mambo ya *blood diamond* na kwa hiyo kuna masharti ambayo yamewekwa, mtu akiingiza almasi lazima tujiridhishe kwamba almasi ile hajatoka tunasema kwenye *conflict places* na imepitia ule utaratibu uliowekwa Kimataifa. Vile vile kuna madini sijui yanaitwaje kwa Kiswahili (*Radioactive minerals*) ambayo pia ni lazima tuyawekee udhibiti wa namna fulani. Sasa tusipokuwa na hii *import permit* madini kama haya yanayosema almasi, *radioactive minerals* pengine na madini mengine ya aina mbalimbali tutakuwa tumeyapa nafasi ya kuingia kwa kweli bila kujiridhisha kwamba yamefuata utaratibu. Kama nilivyosema kwa sehemu kubwa lengo la *import permit* ni kumlinda huyu anaye-*import* haya madini, kwa sababu hataweza kusema kwamba amevunja sharia, atakuwa yuko-*covered* vizuri sana na Sheria.

Mheshimiwa Spika, katika majadiliano kwa mfano, wakati wa Kamati kuna baadhi ya Wabunge walisema, sasa mtu huyu akija na haya madini akayaiza akapata fedha zake labda Dola 200,000 anaondoka nazo namna gani? Ni wazi ilielezwa na Waziri wa Fedha kwamba iko Sheria inayomtaka tu afanye *declaration* anapofika mpakani kwamba ana fedha hizi ametoka nazo. Hata hivyo, anaweza kuulizwa zaidi kwamba ulipoingia hukuwa na hizi fedha umezipata wapi? Hivyo, *import permit* itamsaidia, atasema nilikuja na madini na hii ni *import permit* nilioingia nayo, atakapouza pale atapata *receipt* atakapolipa zile *royalties* na zile *charges* zingine, atakuwa na *receipt* na hii itamsaidia zaidi, itamfanya mazingira yake yawe rahisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kikubwa hapa ni kuhusu utaratibu na napenda kusema kwamba katika majadiliano haya tumezungumza sana kuhusu utaratibu na naomba nikuhakikishie tena na Wabunge wote na naomba waliamini

hili, kwamba tumeurekebisha na kuufanya rahisi sana. Katika jedwali letu la marekebisho ukienda kile kifungu cha 86A(2) katika ile lbara ya 26(b) ya jedwali la marekebisho tumesema:

"(2) A person importing minerals shall make a declaration in a prescribed form indicating the type and quantity of minerals intended to be imported and the purpose of importation."

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo atatuambia, anajaza tu *form* halafu anatuambia ni madini gani, ni kiasi gani na ameleta kwa kusudi gani; kuyauza, ku-process au ni *transit*, au lengo lingine lolote. Halafu kinachofuata kinasema:

"(3) Upon making a declaration under subsection (2), the Commission shall" hatusemi "the commission may" tumesema "the Commission shall, without prejudice subsection (5) and section 86B and 86C issue to the declarant a Minerals Import Permit prior to importation or at the entry point."

Mheshimiwa Spika, hii maana yake ni kwamba, anaweza kujaza hii *form* kabla kabisa hajayaleta madini au anaweza kujaza hii *form* wakati anaingia kwenye nchi. Kwa hiyo hii ndiyo *requirement* peke yake ya msingi, *declaration* peke yake, akishaweka *declaration*, anapewa *permit*.

Mheshimiwa Spika, basi naomba ninapohitimisha hoja yangu hii niwashukuru tena Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mizuri, nawashukuru Kamati na wote waliohudhuria Kamati. Nawashukuru pia wadau kwa maoni mbalimbali waliyoyatoa ambayo tumeyazingatia yametusaidia katika kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba tena kutoa hoja.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Ahsante sana. Hoja imetolewa na imeungwa mkono tunakushukuru sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Katibu.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:

KAMATI YA BUNGE ZIMA

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu

NDG. STEPHEN KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali (Na.2) wa Mwaka 2019 [The Written Laws Miscellaneous Amendments] (No.2 Bill, 2019]

Ibara ya 1

Ibara ya 2

Ibara ya 3

Ibara ya 4

Ibara ya 5

Ibara ya 6

Ibara ya 7

Ibara ya 8

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 9

MWENYEKITI: Mheshimiwa Halima Mdee, nimekuona.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali inipatie uafanuzi kwenye maeneo mawili. Eneo la kwanza, natambua kwamba sasa hivi kuna watu ambaao wanalipa fedha tofauti kwenye nyumba ambazo zimekuwa *evaluated*. Kwa mabadiliko haya, hii shilingi elfu hamsini *flat rate* kwa maghorofa na shilingi elfu kumi kwa nyumba za kawaida zinahusisha na wale watu ambaao

nyumba zao zilikuwa *evaluated*, kwa maana kwamba watalipa fedha nydingi zaidi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini linalohusiana na hiki kifungu mahsus, nilikuwepo kwenye Kamati ya Bajeti, kwenye kifungu cha 9 ambacho kinafanya marekebisho kifungu cha (3) kinasema kwenye *City Councils, Municipal Councils* na *Town Councils* inamaanisha ikiwa kwenye kiwanja kimoja ambacho kina jengo zaidi ya moja kila jengo liliokuwa kwenye kiwanja hicho litatozwa fedha. Tunafahamu kwamba unaweza ukawa na kiwanja kimoja una nyumba yako unakaa, nyumba ya mlinzi, nyumba ndogo ya familia, nyumba ya ng'ombe, nyumba ya wazazi na nyumba ya duka, sasa kwa maelezo ya kipengele hiki tafsiri yake ni kwamba *plot* moja inaweza ikatozwa hata mara tatu, nne ama tano, nadhani hii itakuwa inawaumiza watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilijadiliana kwa kina sana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Serikali wakakubali kwamba hii ita-*apply* kwenye maeneo ambayo ni ya *commercial purposes* lakini siyo kwenye makazi ya kawaida. Nilitaka nipate ufanuzi wa Serikali kwa sababu Serikali iliji-*commit* kwenda kurekebisha lakini hajarekebisha. Tafsiri yake kesho sheria hii ikianza kufanya kazi, Halima nina vibanda vyangu vitano, ama Spika una vibanda vyako cha mbwa, ng'ombe yaani kila kimoja kinatozwa kivyake. Nilitaka Serikali itoe ufanuzi kwenye hili labda walipitiwa hawakufanya marekebisho ili twende vizuri. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana umeelewka. Umenipa tabu kidogo Mheshimiwa Halima, kwenye marekebisho kuna ile 9(b).

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vifungu viwili; cha kwanza kinahusu *City Councils, Municipal Councils* na *Town Councils*.

MWENYEKITI: Okay na cha *District Councils*.

MHE. HALIMA J. MDEE: Cha pili kinahusu *District Councils*.

MWENYEKITI: Kwenye *District Councils* wame-cover vizuri.

MHE. HALIMA J. MDEE: Ndiyo kwenye *District Councils* wame-cover vizuri.

MWENYEKITI: Hapo nimekuelewa, ahsante. Ufafanuzi wa jambo hili, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mdee akisoma hii *Schedule of Amendments* ambayo Serikali imeleta katika hicho kifungu cha 9(a)(ii) tumeeleza: "*In the case of a plot with more than one building, all buildings in actual occupation in that plot including improvements on, in or under such buildings.*" Kama tulivyo sema pale mwanzo kwenye (i) tumesema: "*In the case of a plot with a single building, a building (maana yake hilo jengo moja) which is an actual occupation including all the improvements on, in or under any such building*", yaani kwa maana kwamba tunalihesabu hili jengo moja na hivyo vibanda, sijui vitu gani vyote vinahesabika ni sehemu ya hilo jengo moja na ndiyo lugha ya kisheria ilivyo na Mheshimiwa Mdee anafahamu vizuri. Kwa hiyo, tumechukua maelezo hayo hayo tumeyaweka na kwenye (ii) kwamba hayo majengo utakapokuwa unayaangalia basi hautahesabu vile vibanda sijui vya mlinzi na kadhalika siyo nyumba zinazojitegemea ni sehemu ya ile nyumba utakayokuwa unaiangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Halima.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele cha (ii) kinasema hivi: "*in the case...*"

MWENYEKITI: Hiyo (ii) inagongana na ile (i)?

MHE. HALIMA J. MDEE: Yes.

MWENYEKITI: Endelea.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, inasema: “*In the case of of a plot with more than one building, pana comma na Mwanasheria anajua kwenye sheria comma ina maana yake, all buildings in actual occupation in that plot including improvements ...*”. Kwa hiyo, kwenye *plot* moja na majengo mengine yoyote ambayo yako ndani ya *plot* pamoja na *improvements*, sijui kama tunaelewana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu hapa ni kwa nini kwenye *plot* moja tuweke hizo *complications*? Kwa hiyo, tukikitoa hiki kipengele cha (ii) kikabaki kipengele hicho cha (i) peke yake itakuwa imejibu hilo ambalo ninalisema ama hiki kipengele cha (ii) *tu-focus* kwenye masuala ya *commercial* kama *target* ilikuwa ni hiyo kwamba inawezekana Halima nina kiwanja halafu nimeweka *apartments*, sasa hiyo ni *different case*. Kwa hiyo, nilikuwa nasema katika *scenario* hiyo, hiki kipengele cha (i) tukiache, hiki kipengele cha (ii) kitoke ama kifanyiwe *qualification* ili kisiumize watu ambao kwenye *plot* moja wana majengo mengi. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Umeeleweka Mheshimiwa. Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tofauti ya namna ambavyo *City Councils, Municipal Councils* na *Town Councils* zitakavyokuwa *treated* ukilinganisha na *District Councils*. Hiki kifungu anachokielezea Mheshimiwa Mdee kinahusu *City Councils, Municipal Councils* na *Town Councils* na hapa tunatengeneza *principle* na *principle* ni kwamba, kipengele cha (i) ukiwa na jengo moja katika *plot* litatozwa hilo jengo moja, hayo maeleo ya nyongeza ni kwamba hautahesabu vile vitu vidogo vidogo kama mabanda na kadhalika. Kipengele cha (ii) lengo lake ni kwamba ukiwa na jengo zaidi ya moja katika kiwanja

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

kimoja basi hayo majengo yote yatatozwa lakini hautaangalia vile vibanda na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni tofauti na unapokuja kwenye *District Councils* na kwenye *District Councils* inahusisha pia zile *Township Authorities*. Kule tumesema, *in the case of a plot with a single building*, ukiwa na jengo moja basi litatozwa jengo hilo moja lakini *in the case of a plot with more than one building* yaani ina majengo mengi, *then only one building which shall be charged the highest rate in that plot*.

Mheshimiwa Mwenyeiti, kwa hiyo, hapa tumetofautisha. Lile suala la ku-charge jengo moja katika *plot* litatusika tu kwenye *District Authorities*, *District Councils* na kwenye *Township Authorities* lakini ukija kwenye Jiji, *Municipals* na *Town Councils* pakiwa na majengo mengi katika *plot* moja tunaya-charge. Haya maoni yalitoka kwa Wabunge wenyewe kwamba kuna watu wana *estates* katika Miji na amejenga majengo 30 siyo *fairku-charge* jengo moja tu sawa na yule aliyeko kwenye *District Councils*. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mnapiga makofii lakini hamjui mnatengeneza mzinga wa tatizo na mtaanza kulia wenyewe tu wala haupiti muda mrefu maana siku hizi hatujengi kama yale matembe ya Kigogo kwamba ukijenga moja basi moja tu, siku hizi lazima utakuta kuna nyumba nyingine. Sidhani kama kuna haja ya kuendeleza mjadala. (*Kicheko*)

MBUNGE FULANI: Bado haijaka sawa.

MWENYEKITI: Ndiyo haijaka sawa lakini tumeshafika mahali pakuhoji kwa sababu hamkuleta *amendment*, kwa hiyo, hamna *right* hiyo. Waheshimiwa Wabunge, sijui kama mna-copy za *amendments*?

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa
Wabunge waliongea bila utaratibu)*

MWENYEKITI: Maana mkiwa mmekaa tu hamsomi wala hamuangalii, muwe nazo maana hizi kodi mnakwenda kulipa wenyewe pamoja na wapiga kura. Uksoma utaona kwenye *District Councils* hakuna mgongano wowote kila kitu kimenyooka kabisa ila kwenye Majiji, Manispaa na kadhalika, kile cha kipengele cha (i) hakina shida lakini kipengele cha (ii) kimeingiaingia pale, aah jamani hamkuleta *amendments* sasa nitawahoji.

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)

Ibara ya 10

MWENYEKITI: Mheshimiwa Japhary, hoja yako ni Ibara ya 10 au 11?

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Ibara ya 11.

MWENYEKITI: Sawa.

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)

Ibara ya 11

MWENYEKITI: Mheshimiwa Japhary.

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ibara ya 11 naomba kuondoa neno “each storey” na ibaki “for a storey” katika maeneo ya Mjini. Hoja yangu ni kwamba kama ilivyo kwenye maeneo ya wilayani au vijijini ni kwamba kwa nini tuweke kila sakafu badala ya kuweka kwenye ghorofa moja, kutoza shilingi elfu hamsini kwa kila ghorofa kwenye maeneo ya mjini na siyo kwenye kila sakafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo ilikuwa hoja yangu.

MWENYEKITI: Sababu yako ni nini sasa?

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu, sheria inataka kwenye maeneo ya mjini kila sakafu ya nyumba ya ghorofa itozwe shilingi elfu hamsini kama sheria ilivyo na upande wa wilayani ghorofa moja itatozwa shilingi elfu ishirini. Hoja yangu ni kwamba maeneo ya mjini nayo itozwe kwa ghorofa shilingi elfu hamsini na siyo kwa sakafu.

MWENYEKITI: Yaani hayo maneno unayoyasema tumeshakusikia, tunachotaka ni sababu yako.

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu yangu ni kwamba...

MWENYEKITI: Au sababu ni kwa sababu unataka?

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu yangu kwanza ni kuoanisha kati ya mjini na vijiji. Pili, lengo la *property tax* siyo ku-*discourage* watu kujenga nyumba ni pamoja na ku-*encourage* watu kujenga nyumba. Unapoweka hiyo kila sakafu na wakati *policy* za miji mingi ni kwamba maeneo ya mji tujenge ghorofa hata Dodoma leo kuna maeneo ambayo yanalamisha ujenge ghorofa mbili, tatu sasa huku unawawekea tena sheria ya kuwaongezea malipo katika kila sakafu wanayojenga ni kuwa-*discourage* watu kujenga ghorofa. Kwa hiyo, nafikiri tungetoza kwa ghorofa na siyo kwa sakafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ndiyo yalikuwa maoni yangu na kama maelezo hayataridhisha basi nitaomba kutoa hoja Wajumbe wengine wajadili.

MWENYEKITI: Huko ni kupoteza muda, Mheshimiwa ulikuwa Meya unajua?

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana natetea hilo kwa sababu nilikuwa Meya. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Aaah, hiyo hoja yako hiyo, tunaipa nafasi kwa vile ulileta huku, Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabla ya hapo Mheshimiwa Mbunge anatakiwa akumbuke kwamba zilikuwa zinatozwa kwa kuangalia thamani ya jengo. Kwa hiyo, tumeipunguza sana na kusema sasa hatutatumia thamani ya jengo badala yake itakuwa ni *flat rate*, hilo moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, tunatafuta mapato ya Serikali. Kwa hiyo, kwa sababu hizo mbili ni muhimu kwa mijini ambako ndiko kuna majumba makubwa yenye maghorofa angalau Serikali iweze kupata mapato kwa ajili ya kuwahudumia wananchi wake. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ameridhika Mheshimiwa Japhary.

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Mwenyekiti...

MWENYEKITI: Yaani pendekazo lako Mheshimiwa Japhary ni kwamba mtu mwenye ghorofa moja alipe sawasawa na mwenye ghorofa 20, ndiyo pendekazo lako au nakuwekea maneno mdomoni? Hebu jaribu kufafanua.

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo kosa mtu kujenga ghorofa 20 na huyo mtu anayejenga ghorofa 20 ana malipo mengi ya kodi kwa Serikali kuliko huyo mwenye ghorofa moja, hilo la kwanza. Kwa hiyo, kodi siyo moja tu, tunapoiangalia kodi katika *scenario* ya *property tax* peke yake nadhani hatuko sawa, hayo ndiyo mawazo yangu. Tunatakiwa tuiangalie katika upana kwamba huyo mtu anaweza akawa na kodi nyingi. Kwa hiyo, nilichokuwa nafikiria ni kwa nini ioneckane kwamba huyo mtu lazima hizo ghorofa azilipie sakafu zote, kwa nini asilipie ghorofa moja aliyonayo, lengo ni kuto-*discourage* watu kujenga hizo ghorofa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kwamba tunataka mapato tuisubiri mpaka walalamike tena kwa Mheshimiwa

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Rais ndiyo tuje tena kubadilisha hapa. Kwa hiyo, nadhani tusiende hivyo tulione katika jicho hilo.

MWENYEKITI: Yaani nikuhakikishie hueleweki kabisa, uko peke yako.

WABUNGE FULANI: Tumelewa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, TAMISEMI.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemwelewa Mheshimiwa Japhary lakini tuelewe sasa hivi umiliki wa nyumba unavyokwenda. Hivi sasa kwa mfano, Wabunge wengine ni mashahidi kuna eneo moja linaitwa Medelii, pale kila *floor* ina mmiliki wake maalum. Kwa hiyo, chukua *scenario* hiyo tu, ukiangalia nyuma ya jengo letu la Bunge kuna maghorofa ya Medelii lakini kila *apartment* ina mmiliki wake, ndiyo *logic* ya jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Japhary.

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, najua labda unakataa kunielewa na hoja aliyozungumza Waziri iko kwenye sheria, watu wenye *apartment* wanalipa tofauti. Mimi nazungumzia mmiliki mmoja kwenye jengo moja, hiyo nyingine Mheshimiwa Waziri iko kwenye sheria inaeleweka vizuri tu lakini nazungumzia mmiliki mmoja kwa nini aliipe lile jengo shilingi laki tatu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, una jengo lako la ghorofa mbili...

MWENYEKITI: Hivi sisi kwa nini tuhangaike na mmiliki mmoja, sijui miliki ngapi, badala ya kuweka kodi kama ilivyowekwa hapa sisi tuanze kuhangaika na mmiliki, kwa mfano wamiliki ni watatu halafu sasa hapo inakuwaje? (*Makof!*)

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Watatu watalipa kama *unit titles* na sheria iko hapa imeandikwa.

MWENYEKITI: Sasa hapa wanalipa kwa *floor*, wawe 10, wawe wawili wanalipa kwa *floor*.

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia mtu mmoja katika *building*, labda mimi hujanielewa vizuri.

MWENYEKITI: Hujaeleweka na leo muda wetu mdogo. Mimi sioni kama ni jambo ambalo...

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe hoja.

MWENYEKITI: Umeshindwa kutushawishi. Uklona jambo unaongea tu wenzako hawakuelewi, wala hawako na wewe unakubali wewe ndiyo huelewi, unakaa chini tu, ndiyo *principle* ya vikao kama hivi, uko peke yako Mheshimiwa. (*Kicheko*)

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)

Ibara ya 12

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 13

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jafary, 13.

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, *Clause* ya 13 inaonesha kwamba, *TRA* wanakusanya lakini wanashirikiana na halmashauri. Sasa hoja yangu hapa ni kwamba, tangu mwanzo tumekuwa tukiomba kwamba, bado halmashauri wakusanye hii kodii ya *Property Tax*, lakini Serikali imeendelea kusema kwamba, *TRA* wakusanye. Sasa

na sheria inasema kwamba, washirikiane na halmashauri. Sasa ninachotaka kuomba Bunge lako ni kwamba, washirikiane na halmashauri kwa namna gani, huo ushirikiano uwe wa namna gani?

Mheshimiwa Spika, nikapendekeza kwamba, labda ushirikiano uwe kwamba, kama halmashauri wanakuwa ni wakala basi wakusanye wapate asilimia 40 na Serikali ipate asilimia 60, ndio hoja yangu ambayo nimeleta hapa. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Sasa, sawa Mheshimiwa Jafary, lakini nilisema hapa wiki iliyopita nadhani, kwamba mnapofanya marekebisho kama haya, tunayo Idara hapa ya Sheria Bungeni, mwende kule wawasadie katika kuweka maneno kidogo au mnao Wanasheria mionganoni mwenu akina Mheshimiwa Halima hao, wawewekee kidogo katika lugha ya kisheria. Sasa pale ukisoma maana lazima sisi tuangalia ulichokipendekeza, sasa pale kwa kweli, yaani hata ulichokipendekeza wewe sijui kama hata wewe mwenyewe unakielewa?

Unapotueleza kwa mdomo hivyo, lakini sasa sisi tunaangalia ulichokiandika. *Provided that the regulations made under Section 18(a) shall allocate 60 percent of the collected property rate, eeh! Collected property rate to TRA and 40 percent shall remains at Local Government Authority.*

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Mwenyekiti *remains* ni *typing error* hiyo s, lakini...

MWENYEKITI: Si umesaini hii? Kabla hujasaini si unatakiwa usome tena?

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hatuwezi kushindana kwa *technicalityza* Kingereza kwa sababu, kwanza sisi ni waswahili. Mimi nilichokuwa najaribu kuangalia ni kwamba, lengo kinachozungumzwa kimeelewaka...

MWENYEKITI: Shida yako unabishana na hueleweki. Tumekwambia wapo watu wa msaada, tunao watu wanalipwa hapa kukusaidia, kwa hiyo, wakati mwingine unaawaona, lakini pia unao kwenye Kambi, kabla hujasaini unawapitishia wenzako wanatazama kidogo wanakuwekea sawasawa. (*Makofi*)

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 14
Ibara ya 15
Ibara ya 16
Ibara ya 17

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 18

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jafary bado una muda, endelea, *Clause 18.*

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, *Clause 18* wakati anajibu Mwanasheria nimeelewa alichomaanisha, kwa hiyo, hayo marekebisho nimyaondoa. (*Makofi*)

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 19

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 20
Ibara ya 21

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)

NDG. STEPHEN N. KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:
Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Marekebisho ya Serikali
yameleta Ibara Mpya ya 22.

Ibara Mpya 22

(Ibara iliyotajwa hapo juu illipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)

NDG. STEPHEN N. KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:
Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo itabidi kuwe na
mpangilio sasa, iliyoandikwa Ibara ya 22, isomeke Ibara ya
23.

Ibara ya 23

Ibara ya 24

Ibara ya 25

Ibara ya 26

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 27

(Ibara iliyotajwa hapo juu illipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)

Ibara ya 28

MWENYEKITI: Hii ndiyo ile ya 27 Waheshimiwa
Wabunge mlikuwa mnaiongelea au nytingine? Mheshimiwa
Profesa... Naam, ambayo sasa ni 28?

MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE: Mheshimiwa
Mwenyekiti, itakuwa 27 ndio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia maelezo ya AG ni maelezo mazuri sana, lakini lengo letu ni kuongeza mapato ya Serikali, kwamba, kama hakuna vikwazo mapato ya Serikali yataongezeka sana na ndio lengo letu tunapokaa humu ndani ni kujaribu kuisaidia Serikali kuongeza mapato. Kwa hivi, pamoja na maelezo mazuri tungeiomba Serikali ifikirie tena kuhusu jambo hili. Labda ambalo lingebaki kama lilivyo ni ile *radioactive materials and so on* lakini haya mengine nadhani yanaweza kufanywa vizuri na yakaiongezea Serikali *phenomenally* kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Wajumbe wa kamati kama mnataka kuongezea hapo! Mwenyekiti?

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi kweli eneo hili hata kwenye Kamati tulipatanalo shida sana. Wajumbe kwa kiasi kikubwa ni kama vile hii *permit* na sisi ilikuwa inatupa shida, maelezo ya Serikali yalikuwa ni haya haya, lakini kwenye Kamati tuna mtu kama Mheshimiwa Profesa Kishimba; Mheshimiwa Profesa Kishimba uzoefu wake unatuambia, ukifika pale mpakani una madini yako, una dhahabu na uka-*declare* pale ukapata hiyo *permit* halafu unaondoka na usafiri gani uje ufile kwenye hiyo *gem house?* (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, anasema unapata *escort*, yaani unafanyaje kwa sababu, usalama wako kuanzia pale ni matatani na mashaka yenewe yanaanzia kwa huyohuyo hata aliyekuwa anakupa hiyo *permit* kwa sababu, kama ni dhahabu *it is money*, kama ni *ruby it is money...*

MWENYEKITI: Ukichukulia ni jioni jioni hivi, saa 10.00 jioni. (*Kicheko*)

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI: Mheshimiwa

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mwenyekiti, yes na ruby unawenza ukatia mfukoni tu hivi, lakini una hela nyingi. Sasa ukisha-*declare* pale usalama wako uko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tulipata shida nalo sana hili jambo hadi tukafikia tukasema basi, *option* iwe tuanzie ile (b) ambayo ilikuwa inasema, *a person importing minerals shall make a declaration in a prescribe...* ianzie, sasa bado tatizo linakuwa ni lile lile kwa sababu hapa, unajua, labda tu sasa niseme kwamba, tumeibiwa sana madini, yanakwenda yanatokea kwenye nchi za wenzetu, majirani zetu na sasa mpaka ambao unaondoa madini mengi ni huu unao-*border* na Rwanda.

Mheshimiwa Spika, sasa na sisi tunajua wako watu wetu wanaochimba nje, lakini wako nje ambao kwa kufungua haya masoko watataka kuja kuuza ndani. Kwa kipengele hiki si rahisi mtu akapita aka-*declare*, kwa hiyo, njia za panya zitaendelea kutumika tu na zikitumika Polisi watakamata kwa hiyo, tutaleta mkanganyiko ambao hatutafikia lengo pamoja na *issue* za kiusalama na maelezo ya AG, ni mazuri kabisa, lakini labda tutenganishe yepi tunayotarajia yaende kwenye soko, ili hayo tusiweke hiyo *requirement* ya *declaration* na yale ambayo tunaona yanastahili *declaration*, basi yawe *declared*. Haya sisi tunalenga dhahabu yetu, tunalenga dhahabu na hizi *gemstones* na *precious metals*, yaani haya madogo madogo haya ili yaje kwenye soko, masoko haya yachangamke, sisi yakinika yakiuzwa huko tupate dola. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, huo ndio ulikuwa msimamo, lakini sasa...

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI: ...haimo kwenye *schedule*, lakini sasa Kiti chako kiangalie busara hiyo na Serikali iangalie busara hii, kama tunawenza tukatenganisha ili tutoke hapo. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Sijui kama kuna haja ya Mheshimiwa Kishimba kuongezea, yupo leo? Eeh, Profesa hebu weka maneno kidogo, Mheshimiwa Profesa Kishimba nimempa nafasi; Mheshimiwa Kishimba hayupo eeh!

Yaani ni hivi, labda tuelewane, Wanakamati sisi tumewaeleweni na maelezo ya Serikali nayo ni mazuri pia, lakini sisi hapa *intention* yetu ni kwamba, kama kwa mfano; nafikiri nilisikia siku ile ya kikao cha kule kwa Mheshimiwa Rais kwamba, inaelekea kama Uganda kwenye eneo letu ndio muuzaji namba moja wa dhahabu na Kenya ndio muuzaji namba moja wa *tanzanite*, na kadhalika. Mnadhani wangekuwa na sheria kama hii tunayotunga hapa wangekuwa namba moja? (*Makof!*)

MWENYEKITI: Wasingekuwa! Sasa sisi tunataka kutengeneza kitu wanaita kwenye sayansi, *osmosis*, tunataka uvute maji yaje huku Tanzania, Watanzania walioko huko nje walete, wageni walioko nje, yaani kwa maana ya majirani zetu wote wale wafanye Tanzania iwe soko lao walete mali hapa wauze. Ndio namna ambavyo Serikali itapata fedha zaidi na nchi yetu itainuka. Sasa kwa kuweka namna hii kidogo tunajifungia tena ile kama tulivyozowea siku zote, sasa tunazidi kuchelewa.

Nimekuona Mheshimiwa Kafumu eeh!

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana maelezo ya Mwenyekiti wangu, lakini ningependekeza kwamba, hii *permit* ibaki kwa madini ya ujenzi, madini yanayoenda kwenye viwanda yanayobebwa na malori na nini, tunaweza tukaibakisha, lakini kwenye madini ya almasi kuna kibali cha *Kimberly Process* cha Kimataifa cha *UN* chenyewe kitabaki. Haya madini mengine haya tuyaondolee ili kweli tushindane na Kenya, tushindane na Uganda na nchi za jirani. Tukifanya hivyo, nina hakika kabisa mwaka kesho tutarudi hapa. Nakushukuru. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Chenge, nilikuona umesimama.

MHE. ANDREW J. CHENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana na pia niwashukuru na wengine wajumbe walioliona hili, lakini hasa wewe, kwani umeliona mapema sana, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani tunaweza tukaenda mbele kwa njia ya Mheshimiwa Kafumu, lakini sasa hapa tu-focus kwenye madini na lilisemwa kwenye Kamati, tunaangalia yale madini *metallic minerals*. Sasa unaiondoa almasi kwa sababu kuna utaratibu wake halafu unakuja na *gemstones*. Sasa hizi ndio rasilimali za Tanzania ambayo tunataka ya kwetu ambayo tunayo ibaki, iende, lakini kwa utaratibu na inayokuja ije kwa utaratibu mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nadhani kama Serikali itapenda kuliangalia hilo unachotakiwa sasa marekebisho ya Serikali waliyoleta kwenye ile (2) ndogo inaongeza:

*"A person importing..., madini yapi sasa? Kama watakubali dhana yangu unayaingiza hapo, ...*metallic minerals or gemstones shall make a declaration in a prescribed form at buying stations or at mineral or gem houses designated by the Commission.*"*

Kwa hiyo, yeye ataingia na ule usiri ule, lakini aende moja kwa moja sokoni. Kule ndio atapewa ile fomu ataijaza, ana madini gani, uzito gani, lakini tunajua hatasema madhumuni amekuja sokoni. Atapewa ile fomu na kama bei siku hiyo haikuchanganya atafungasha pamoja na kale kananihii kake, mhuri ule aliopewa, anaondoka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani tukienda hivyo, tutakuwa tume-capture vizuri. Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ngoja, wakati Serikali wanaendelea kufikiri, basi tuendelee kusikiliza mawili matatu, Mheshimiwa nimekuona.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nataka niongezee kidogo hapo kwenye hili suala la uingizwaji wa madini kutoka nchi jirani. Mfanyabiashara ama mchimbaji wa madini Sh.500/= ama Sh.1,000/= ni nydingi sana kwake. Mfano, jirani labda Kenya kuna maeneo inayochimbwa, labda Migori pale; mtu amepata kama kilo tatu, akasikia Tanzania kwenye soko lilitoko Mwanza *gram* moja kwa Kenya iko Sh.90,000/= lakini Mwanza ikawa iko kwa 91,000/= yuko tayari kutoka Kenya kuleta hayo madini Mwanza, lakini kwa sababu ana kilo tatu akisikia ukifika mpakani pale lazima u-*declare*, sasa kilo tatu ni fedha nydingi sana na yeze ni mara yake ya kwanza kuingia nchini, sasa lazima atakuwa na wasiwasi. Pia tutakuwa na watu wangapi wa kuweza kuwasindikiza hao wenyewe mali ambao wanatoka nje? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala ni gumu sana, nadhani libaki palepale kwamba, yale madini ambayo yako kimataifa sana, kama vile almasi, ibaki hivyo hivyo, lakini kwa madini kama dhahabu na madini mengine yaingie yaje yasajiliwe kwenye soko palepale. Ushauri wangu ni huo kwa sababu, kidogo nina uzoefu na hii kazi tangu mwaka 1976.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Amar. Mheshimiwa Hawa Ghasia.

MHE. HAWA A. GHASIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nataka tu kuchangia kwamba, lengo letu ni nini, kukuza biashara hii ya madini kwenye nchi yetu au kuzuia madini yetu yasiende nje? Ukiangalia kwa kiasi kikubwa ni kuvutia watu walete madini kutoka nje ili na sisi tuweze kunufaika na mipaka inayotuzunguka. Kwa hiyo, mapendeleko yangu huku kwetu ambako tunataka yaingie, hebu tupunguze haya masharti mengine mengine. Mfano, kama sisi tuko tunapakana na Mozambique, lazima tuweke mazingira dhahabu ivutike itoke Mozambique ije Tanzania. sisi tujikite kuhakikisha ile inayotoka nje ya mipaka yetu ndio itoke ikiwa na masharti magumu, lengo tupate mapato. (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikichukulia uzoefu wa korosho wakati huo kabla stakabadhi ya mazao ghalani na wakati huo kila halmashauri ilikuwa na kiwango chake cha kutoza ushukuru. Kwa hiyo, mtu alichokuwa anafanya ukiona Lindi wao wameweka Sh.30/= wewe unafanya Sh.25/= na unaenda kuweka kituo cha kununulia korosho mpakani kabisa na Lindi kwa hiyo, korosho zote za Lindi zinakuja kwako. Kwa hiyo, napendekeza *declaration* ikafanyike sokoni, mtu akipata alikopata anatoka Congo, anatoka Mozambique, mipakani huko kwa usalama wake, lakini pia kwa kumvutia apite bila masharti yoyote. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ole-Millya, ulikuwa umesimama.

MHE. JAMES K. MILLYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ina amani. Miaka fulani kabla Sheria ya 2017 hajapitishwa tulikuwa na *gem shows* pale Arusha, zilikuwa zinafanyika na zilikuwa zinavutia wageni wengi kutoka nje, Madagascar, Msumbiji, Zambia, Congo. Baada tu ya kuweka *restriction* kama hiyo tayari *gem show* hajafanyika kwa miaka karibu mitatu sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana kabisa na wenzangu waliotangulia. Kwa mfano, kama Serikali inataka kulinda kutoingiza madini fulani wa-*qualify* kwenye hicho kifungu kwamba, hatutaki mpaka u-*declare industrial minerals* zinazotakiwa kuingia, lakini kwenye *gemstone* na *gold* waruhusu iingie bila kupewa *restriction* yoyote.

MWENYEKITI: Naangalia huku kwa Mheshimiwa Selasini huku, hakuna hata mmoja, eeh! Uwanja huu mgeni eeh? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mbunge wa Muheza, halafu Mheshimiwa Getere. Mheshimiwa Adadi.

MHE. BALOZI ADADI A. RAJAB: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kunipa nafasi hii; labda

Mwenyekiti pia, alisahau, wakati tunaongea na wadau kwenye kifungu hiki walisema mambo mazuri sana ambayo yamefanyika na Mheshimiwa Rais pamoja na marekebisho haya, lakini wakasema kabisa kwamba, hamtaona kabisa madini yanakwenda kwenye hayo maduka ambayo yamefunguliwa, hatutapeleka kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kwenye Kamati tuliwaambia kwamba jamani hebu tufungue mipaka, tuzuie kwenye kutoka, kama ni kodi tuta-coverkule kwenye kutoka. Haya masharti madogo madogo haya yanazidi kuleta migogoro. Kenya sasa hivi ndio wanaonekana wanatoa tanzanite ilhali tanzanite inatoka kwetu, ni kwa sababu masharti kama hayo hakuna, sasa kwa nini tunaweka haya mambo? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutoe haya mambo mtu aingize aende mpaka kwenye soko, utatoona mambo yamechangamka. Kifungu hiki kikiendelea kuwa kama kilivyo, haya mazuri yote ambayo yamefanyika yatakwama. Ukiangalia Serikali imekubali kubadilisha mambo mengi sana lakini hiki wamekataa. Kama *issue* ni *security* kuna sheria ambazo zipo, kama ni *radioactive* kuna sheria yake inashughulikia, kama mtu ataingiza *explosives* kuna sheria yake, kwa nini wanakataa kuondoa suala hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri wawe *understanding*, wakubali ili watu wafanye biashara vizuri. Nakushukuru. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. *Actually* mjadala huu Waheshimiwa Wabunge hauhusishi tu madini haya tunayoyazungumzia hapa na ndiyo maana tumeipa muda, ni *principle* fulani tunaitengeneza ambayo *imedisadvantage* Tanzania kwa miaka mingi kwenye maeneo mengi. Utakamatwa na kahawa huku Tanzania kama uko Bukoba kule ikishafika Uganda unasindikizwa. Utakamatwa na roli la machungwa huku Tanzania ukishavuka *border* ya Kenya unasindikizwa, uko salama kabisa na ndiyo hivyo hivyo kwa wenzetu wote kitu kikishaingia kwao basi wana-

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

facilitate, sisi tunalinda hata mali ya jirani isiingie kwetu. Tuna nia njema na nzuri sana lakini sasa katika dunia ya leo kidogo. (*Makof/Kicheko*)

Nilikutaja Mheshimiwa Getere halafu Mheshimiwa David Silinde.

MHE. BONIPHANCE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nakubali kwamba hiyo sheria ya kwenda sokoni iwepo lakini najuliza maswali mengi sana. Hivi tunamtaka nani alete madini hapa kwetu? Kwa mfano mtu wa Kenya *value* ya hela ya Kenya ni kubwa kuliko ya kwetu, hata ukienda kuuza ng'ombe 300 kule Kenya unakuja kupata hapa zaidi ya shilingi milioni moja na kitu au shillingi millioni mbili. Wenzetu wa Congo ndiyo wana madini, Kenya hawana madini mengi, unajua nchi yetu kama mnavyoona kwenye jiolojia tuna madini yote yaani sisi ndio kichaka, sasa tunataka nani aje kwenye madini haya? Ukienda Congo wana madini lakini hela yao ni dola, hakuna mtu wa Congo ataacha dola aje kuuza kwenye madafu ya kwetu hapa. Kwa hiyo, nafikiri kwamba sheria hii iwepo lakini pia naomba...

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. BONIPHANCE M. GETERE: ...uwazi wa madini yetu humu ndani uwe mkubwa zaidi kuliko ya Congo. Uwazi ya madini yetu na Sheria zetu za Madini za ndani ziwe wazi kweli
...

MBUNGE FULANI: Kaa chini.

MHE. BONIPHANCE M. GETERE: ...kuliko madini ya nje. Kwa hiyo, mimi nakubali lakini naona madini yetu tuyalinde zaidi kuliko yanayotoka nje kwa sababu ni machache.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, haelewi huyo.

MWENYEKITI: Ni ushauri wake na namlinda kabisa. Mheshimiwa David nimeshakutaja.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na nashukuru sana walau kuruhusu mjadala huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ambalo watu wengi hawafahamu, madini si mihogo, mahindi wala si magonjwa. Unapoleta mahindi ndani ya nchi yako maana yake unaruhusu uchumi wako uwe mkubwa. Nchi zote duniani nenda Hong Kong hata na tani kumi, ukifika pale wao ndiyo wanakulinda. Ukishauza yale madini kutoka na ile hela, hapo hutoki na hela zaidi ya dola 5,000. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi nyngi zilizotuzunguka na zillzoendelea, mfano mdogo Kenya na hili nafikiri hata watu wa Madini wanajua, tumezungumza na wachimbaji wadogo, mrabaha huu kwa madini ya *gemtones* pamaja na dhahabu, Kenya, Uganda hawahawa jirani zetu ni asilimia moja, sisi kwetu hapa ina-*depend* kuanzia 4% kwenye dhahabu mpaka 6% kwenye madini haya ya vito. Hicho tu kifungu kimoja unaona kabisa kinatubana sisi wenye kwenye biashara. Sasa unakwenda kuongeza kitu kingine kwamba sasa hata kuleta ndani kwa ajili ya biashara ni tatizo wakati yanapokuja inaongeza mzunguko wa fedha ndani ya nchi yetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kwenye Kamati ya Bajeti, uzuri tulizungumza vizuri sana na Serikali tukawaambia jamani duniani kote haya mambo hayafanyiki. *The good thing* leo wakati tunafanya marekebisho ya sheria hii, kwenye zabibu pia tuliwaambia na wakati tunapitisha hapa Kamati ya Bajeti tuliwaambia, sasa kwa sababu mwaka 2016/2017 zabibu ilikuwa na bei juu Serikali ikapandisha ushuru toka 450 mpaka 3,315, mwaka 2018 mambo yakawa hayaendi. Tukawaambia jamani sisi tuliwashauri, wakulima walifaidika ndiyo lakini ninyi mkaona kama kile chanzo, matokeo yake leo tumekuja kubadilisha na sisi kama Kambi ya Upinzani tumekubaliana na jambo hilo kwa nia njema ya kuwasaidia watu wa zabibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzuri wa hesabu hizi, unajua namba huwa hazidanganyi na hawa wachimbaji wadogo walitueleza vizuri kwamba Waheshimiwa Wabunge kwa mfano, kwa hizi kanuni pamoja na maelezo ya Serikali ambayo walikuwa wametoa, hii *smuggling* walieleza na ipo kwenye *Hansard* wakasema wataendelea na biashara ya *black*. Sisi tukasema hapana hatutaki tufikie huko, tunataka huu mzunguko uendelee kubaki, kwa hiyo, Serikali tusikilizeni, kwa bahati mbaya Serikali ikawa imeweka msimamo wake kwenye jambo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiri kwa ushauri wa Serikali na maoni ya Wabunge tuliookaa pamoja tungeomba hili tutengeneze utaratibu mzuri, kama ule ule, mtu *a-declare* kwenye soko lakini tutengeneze sheria ambayo haitamruhusu mtu kutoka na fedha mara baada ya kuza. Kama ni gari anunue hapa, kama vifaa ananunue hapa, fedha hiyo ibaki kwa maslahi ya wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Sasa Serikali wapo tayari tuwasikilize, Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, Prof. Kabudi tafadhalii.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Serikali lilikuwa ni hilo ambalo Waheshimiwa Wabunge wamelizungumza tuweze kuhakikisha kwamba madini haya yanaletwa nchini. Niwafahamishe tu kwamba madini haya yatakayoletwa nchini hayataletwa tu na hawa wachimbaji wadogo wadogo tu. Mara baada ya kujenga *smelter* na *refinery* na hivi sasa ukichukua kampuni ambayo imenunua hisa nydingi za Barick yenye migodi yake nchini Congo hao pia sasa watataka kuleta madini yao hapa kwa ajili ya kuya-*refine* katika *refineries* ambazo wao wako tayari kuzijenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hao ni hakika kabisa, wataomba *import permit* ya kuleta madini yao kutoka Congo, Benin, na Mali kuja kwenye *refineryambayo* baadaye itatajengwa hapa Tanzania. Kwa hiyo, hilo lilikuwa ni kundi moja ambalo litahitaji kabisa kuwa na *prior application* ili dunia nzima ijue madini yao yanayotoka Benin, Mali, Congo na Burkina Faso sasa yanakuja Tanzania kwa ajili ya kuwa *refined* kwa sababu kampuni hiyo imenunua hisa nyingi katika Kampuni ya Barick na imekuwa ndiyo kampuni kubwa ya utengenezaji wa dhahabu duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kundi la pili sasa ni hili la hawa wachimbaji wadogo wadogo. Hofu ya Serikali iliyokuwepo ilikuwa tusije na utaratibu ambao sasa mtu yeьте atakayekamatwa Tarime kwa Mheshimiwa Waitara akasingizia kwamba nilikuwa naipela *Buying station*. Hata hivyo, baada ya kusikiliza hoja hizi, Serikali imetrafakari, sijui kama tunaruhusiwa kufanya mabadiliko bila kuleta *Schedule of Amendments*, kama inakubalika basi tunayo mabadiliko ambayo tungeyapendekeza. (*Makof*)

MWENYEKITI: Tuendelee, kwa sasabu nitawahoji baadaye.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafanya marekebisho na baadaye tutaomba yawe *refined* na Waandishi wa Sheria, tunataka tupendekeze kwamba: “*A person importing metallic minerals, gemstones except tanzanite, shall make a declaration in prescribed form at the Mineral and Gem House or at a buying station*”. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya pili tunasema: “*A person importing diamonds, radioactive minerals, tin, tungsten, tantalum, shall obtain an import permit upon making a declaration in a prescribed form and upon providing proof of compliance to International Conventions and obligations*”. (*Makof*)

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hayo yanakubalika, basi tungependa mabadiliko hayo tuwasilishe kwako ingawa ni kwa utaratibu huo. (*Makof*)

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Musukuma.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumuuliza Waziri.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Musukuma umefuatilia lakini? (*Kicheko*)

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefuatilia isikupe tabu mtani wangu.

MWENYEKITI: Endelea Mheshimiwa Musukuma. Jamani ni mtani wangu huyo. (*Kicheko*)

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na mawazo ya Waziri, Mheshimiwa Kabudi, lakini swali langu pamoja na kuwa ameenda kufanya *declaration* kwenye kituo cha kuuza baada ya kuuza zile pesa, nishauri, kuna mchangiaji ametoa mfano wa Hong Kong kwamba ukienda Hong Kong ukiuza kutoka na pesa ndiyo hairuhusiwi. Sasa tukiweka sharti la kwamba baada ya kuuza hela ziwe hivi, hilo ndilo tatizo la kwanza watu hawataleta dhahabu hapa, tunawaambia haya kwa usoefu. (*Makof*)

MWENYEKITI: Hilo katika mjadala Mheshimiwa Musukuma halipo kwa sasa na kama litakuwepo basi ni kwa Waziri wa Fedha katika utaratibu mwingine kabisa. Ahsante. (*Kicheko*)

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na
Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 29
Ibara ya 30

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zillipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima Pamoja na Marekebisho ya Serikali)*

MWENYEKITI: Katibu.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imemaliza kupitisha Ibara zote za Muswada kama ulivyowasilishwa.

MWENYEKITI: Bunge linarejea.

(Bunge lilitrudia)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Mheshimiwa mtoa hoja, taarifa.

TAARIFA

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu ya Kanuni ya 89(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka 2019 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendment) (No. 2) Bill, 2019*] Ibara kwa Ibara na kuukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali (Na.2) wa Mwaka 2019 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 2) Bills, 2019*]kama ulivyorekebishwa katika Kamati ya Bunge Zima sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:
Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Hoja imetolewa na imeafikiwa. Sasa kama ilivyo ada, naomba niwahoji sasa kuhusu Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali Na.2 wa Mwaka 2019 pamoja na marekebisho yake.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

(Muswada wa Sheria wa Serikali Ullipitishwa na Bunge)

SPIKA: Ahsante sana, umepita bila kupingwa kabisa.
Katibu.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

Muswada wa Sheria kwa ajili ya kufanya Marekebisho katika Sheria mbalimbali zipatazo tano (5) kwa lengo la kuondoa mapungufu ambayo yamejitokeza katika Sheria hizo wakati wa utekelezaji wa baadhi ya masharti katika Sheria hizo [A Bill for An Act to Amend Certain Written Laws]

(Kusomwa Mara ya Tatu)

SPIKA: Ahsante sana. Sasa hatua za Muswada huu kwa upande wa Bunge zimefikia mwisho wake. Tutaupeleka mbele ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano ili ikimpendeza tupate baraka zake na baadaye iwe sheria kamili ya nchi yetu. *(Makofi)*

Nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Waziri wa Madini, Waheshimiwa Mawaziri wote wakiongozwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu na timu ya wataalam kutoka Wizara zote hizo nilizozitaja. Kipekee niwashukuru sana Kamati ya Uongozi kwa kukubali jambo hili kwamba tulifanyie kazi leo

na Kamati ya Bajeti kwa kufanya kazi *overtime*, mmechapa kazi kwelikweli, mmeutendea haki Muswada huu na Wabunge wote maana tukiwa kwenye Kamati ya Bunge Zima hapa kwa kweli tumeurekebisha Muswada huu.

Kwa wale wanaofuatilia mienendo ya Bunge watakulaliana na mimi labda kwamba Miswada ambayo imekuwa ikija hapa Bungeni imekuwa ikichambuliwa vilivyo kabisa kabisa. Kila Kamati ambayo tumeipelekea kuchambua Muswada kazi hiyo inafanyika *thoroughly*. Waheshimiwa Mawaziri wamekuwa *very responsive*, wanakubali pale wanaposhauriwa na wamekuwa wakifanya mabadiliko mengi ya maana kabisa na matokeo yake sheria ambazo tunazipata kwa kweli zimekuwa ni sheria ambazo zimetokana na mchakato ambaao ni wenye afya. (*Makofi*)

Naomba wenzetu upande wa Serikali muendelee na moyo huo wa kushirikiana nasi katika kupitia Miswada yetu inayokuja hapa ili tuwe na sheria shirikishi na sheria nzuri kabisa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hatua hiyo nimuite Katibu kwa ajili ya shughuli inayofuata.

NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:

TAARIFA YA KATIBU WA BUNGE

NDG. STEPHEN N. KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:
Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 29(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kutoa taarifa kwamba shughuli zote zilizowekwa kwenye Orodha ya Shughuli za Mkutano wa Kumi Nne wa Bunge sasa zimemalizika.

SPIKA: Ahsante sana, Katibu.

NDG.STEPHEN N. KAGAIGAI – KATIBU MEZANI:

HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu, karibu sana. (*Makofi*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, kwanza hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia afya na uzima na kutuwezesha kukamilisha shughuli zote za Mkutano wa Kumi na Nne wa Bunge la Kumi na Moja kama zilivyopangwa.

Mheshimiwa Spika, sasa ni takribani mwezi mmoja na siku kadhaa tangu kuanza kwa mwaka mpya wa 2019. Aidha, kwa kuwa huu ni Mkutano wa kwanza tangu kuingia kwa mwaka 2019, nitumie fursa hii kukutakia wewe Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge, Waheshimiwa Wabunge wenyewe, watumishi wote wa Bunge na Watanzania wote kheri ya mwaka mpya wa 2019. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wakati tukiendelea na kikao hiki cha Bunge wako baadhi ya Waheshimiwa Wabunge na wananchi tulinaowawakilisha katika Majimbo yetu, walipata misiba ya ndugu, jamaa na marafiki. Nitumie nafasi hii kuwapa pole wote waliofikwa na misiba hiyo.

Aidha, kwa masikitiko makubwa, niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu na Watanzania kwa ujumla kutoa salamu za pole kwa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (*TECH*) kwa kifo cha Mhashamu Baba Askofu Evaristo Chingula, aliyekuwa Askofu wa Jimbo Katoliki la Mbeya, tarehe 21 Novemba mwaka 2018.

Vile vile natoa pole kwa Shehe Abubakar Bin Zubeir, Mufti na Shehe Mkuu wa Tanzania, kutokana na kifo cha mkewe Bibi Hidayah Omari aliyefariki tarehe 30 Januari, 2019 huko Korogwe Mkoani Tanga. Vile vile nitoe salamu za pole kwa familia ya Mwanasiasa Mkongwe Nchini, Mzee wetu marehemu Pancras Ndejembji.

Mheshimiwa Spika, natoa pole kwa Mheshimiwa Mahmood Hassan Mgimwa, Mbunge wa Mufindi Kaskazini, kwa kufiwa na binti yake; Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa kufiwa na baba yake mzazi, Mzee Mathew Rubango; na Mheshimiwa Capt. Mst. George Huruma Mkuchika, Mbunge na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora kwa kufiwa na mama yake mzazi Bi. Tekla Mkuchika. Mwenyezi Mungu apumzishe roho za Marehemu mahali pema Peponi, amina.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kuwapa pole Waheshimiwa Wabunge wenzetu, nianze na Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala, Mbunge wa Viti Maalum ambaye pia alipata ajali kule Wilayani Kondoa tarehe 24 Desemba, 2018 iliyogharimu maisha ya watu watatu naye kukimbizwa Hospitali ya Taifa Muhimbili. Pia Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, Mbunge wa Manyoni Magharibi ambaye alipata ajali ya gari, tarehe 5 Desemba, 2018 eneo la Nala Dodoma na kugharimu kifo cha mtu mmoja. Tunamshukuru Mwenyezi Mungu kuwa hivi sasa wote wanaendelea vizuri na tupo nao katika shughuli za Bunge, ingawa wengine wako kwenye mapumziko mafupi.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu Mheshimiwa Abdallah Ally Mtolea ameweza kuapishwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Temeke, kuititia Chama cha Mapinduzi CCM. Nampongeza sana kwa kupita bila kipingwa katika uchaguzi uliopangwa kufanyika tarehe 20 Desemba, 2018. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mwezi Januari, 2019 Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alifanya mabadiliko madogo ya Baraza la Mawaziri. Napenda kutumia fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Angellah Kairuki, Mbunge kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, anayeshughulikia Uwekezaji na Mheshimiwa Dotto Biteko, Mbunge kuwa Waziri wa Madini na Mheshimiwa Dkt. Mpoki Ulisubisya kuwa Balozi.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko haya ya Baraza la Mawaziri, yalikwenda sambamba na uteuzi wa viongozi

wengine wa Serikali ukihusisha Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu, Makatibu Tawala wa Mikoa, Majaji wa Mahakama za Rufani na Majaji wa Mahakama Kuu, Wakuu wa Wilaya pamoja na Wakurugenzi wa Halmashauri zetu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, rai yangu kwa viongozi na Watendaji waliopata uteuzi ni kwamba wajiridhishe na wahakikishe kuwa wanatembelea wananchi ili kupokea kero zao na kutafuta njia nzuri ya kutatua kero hizo.

Mheshimiwa Spika, Viongozi na Watendaji wote wa Serikali wanapaswa kujielimisha kuhusu sheria, kanuni na taratibu mbalimbali zinazoongoza utendaji wao sehemu za kazi. Maamuzi mtakayoyafanya yazingatie sheria, kanuni na taratibu.

Mheshimiwa Spika, tuje kwenye shughuli za Bunge. Katika Mkutano huu, Waheshimiwa Wabunge wamepata fursa ya kuuliza maswali ya kawaida ya msingi yapatayo 122 na maswali 222 ya nyongeza, na kujibiwa na Serikali. Aidha, maswali ya papo kwa papo yapatayo saba, yalielekezwa kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Miswada ya Serikali, Bunge lako Tukufu lilipokea, kujadili na kujitisha kwa hatua zake zote Miswada sita. Miswada hiyo; wa kwanza ni Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 4) ya Mwaka 2018; Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Mwaka 2018; Muswada wa Sheria za Mamlaka ya Udhhibit wa Usafiri wa Ardhini wa Mwaka 2018; Muswada wa Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira wa Mwaka 2018; na Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa ya Mwaka 2018 na Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) ya Mwaka 2019.

Mheshimiwa Spika, kwa hatua iliyofikiwa, napenda kutumia nafasi hii kuwapongeza sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa kujitisha Miswada hiyo wakati tukisubiri maamuzi ya Mheshimiwa Rais kuidhinisha kuwa Sheria kamili.

Mheshimiwa Spika, katika Bunge hili pia, Bunge lako Tukufu liliridhia azimio la kubadilisha Hadhi ya Mapori ya Akiba ya Biharamulo, Burigi, Kimisi, Ibanda na Rumanyika, Urugundu kuwa Hifadhi za Taifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie Kamati za Kudumu za Bunge. Kama ambavyo unafahamu kuwa Mkutano huu ulikuwa mahsus kwa ajili ya Bunge lako Tukufu kupokea na kujadili Taarifa za Mwaka za Kamati za Kudumu za Bunge. Hivyo Kamati zote za Kudumu ziliwasilisha Taarifa zake kama ilivyopangwa. Nitumie fursa hii pia kuwapongeza Wenyeviti, Makamu Wenyeviti, na Wajumbe wote wa Kamati za Kudumu za Bunge, kwa kuwasilisha taarifa zilizosheheni maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali kwa Serikali yetu.

Mheshimiwa Spika, Serikali inapokea hoja zilizoibuliwa wakati wa vikao vya Kamati za Bunge na inaahidi kuzifanya kazi hususan wakati huu wa maandalizi ya Mpango mpya wa Bajeti ya mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kwa uchache kutoa tathmini ya mapitio na mwenendo wa utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Serikali, kwa kipindi cha Julai hadi Desemba 2018 na mwelekeo wake hadi Juni 2019.

Mheshimiwa Spika, hali ya uchumi imeendelea kuimarika. Mathalan kati ya Januari hadi Septemba, 2018, pato la Taifa lilikua kwa wastani wa asilimia 6.7 ikilinganishwa na asilimia 6.2 katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2017. Ongezeko hilo la ukuaji wa uchumi limechochewa zaidi na uwekezaji mkubwa kwenye miundombinu, hususan ujenzi wa barabara, reli na viwanja vya ndege.

Mheshimiwa Spika, masuala mengine yaliyochangia ukuaji mzuri wa uchumi ni kutengemaa kwa kupatikanaji wa Nishati na hali nzuri ya hewa kwa upande wa kilimo. Shughuli za kiuchumi zilizoendelea, zimeendelea kutoa mchango mkubwa katika pato la Taifa. Kwa kipindi cha Januari hadi Septemba 2018, ni kilimo kilichoongeza kwa asilimia 33.4; ujenzi, asilimia 15.7; na biashara, asilimia 10.2.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa Sekta ya Kilimo, Serikali itaendelea kuimarisha sekta hiyo kwa kuendeleza uboreshaji wa miundombinu ya umwagiliaji, kuhakikisha pembejeo za kilimo zinapatikana kwa wakati, kuimarisha huduma za ugani na kuboresha upatikanaji wa miundombinu ya hifadhi na masoko na lengo la Serikali ni kuongeza tija kwenye uzalishaji wa mazao ya kilimo na hivyo kumwongezea kipato mkulima, kitakachomwezesha kujikimu na kujkwamua na umasikini.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza wakulima wote nchini, wafugaji, wavuvi, wadau wa Sekta ya Ujenzi na wafanyabiashara kwa mchango wao mkubwa kwenye ukuaji wa uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, mfumuko wa bei umeendelea kutengamaa ambapo ulikuwa na wastani wa asilimia 3.5 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 5.3 kwa mwaka 2017. Kiwango hiki ni kidogo kabisa kuwahi kutokea katika kipindi takriban miaka 40 iliyopita.

Mheshimiwa Spika, kiwango cha chini cha mfumuko wa bei kimetokana na kuimarika kwa hali ya upatikanaji wa chakula katika masoko ya ndani na nchi jirani, pamoja na utekelezaji madhubuti wa Sera za Fedha na za Bajeti.

Mheshimiwa Spika, tunayo akiba ya fedha ya kigeni, imeendelea kuwa ya kuridhisha ambapo hadi kufikia Novemba, 2018, ilifikia Dola za Marekani bilioni 5.079. Kiasi hicho cha fedha za kigeni kinatosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi takriban miezi mitano. Kiwango hiki ni zaidi ya lengo la nchi la kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa bajeti wa kipindi cha nusu mwaka umeendelea kuwa wa kuridhisha. Katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2018, Serikali ilitarajia kukusanya na kutumia jumla ya shilingi trilioni 15.97. Aidha, hadi kufikia Desemba, 2018 kiasi cha shilingi trilioni 12.84

kilipatikana kutohana na vyanzo vya ndani na nje ambacho ni sawa na asilimia 80.4 ya makadirio ya nusu mwaka.

Mheshimiwa Spika, Matumizi ya Serikali kwa kipindi cha Julai hadi Desemba, 2018, yalikuwa shilingi triliuni 12.83. Fedha hizo zilitolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo, ulipaji wa mishahara ya watumishi, ugharamiaji wa deni la Taifa, uendeshaji shughuli za Serikali, ulipaji wa madeni ya watumishi waliohakikiwa, wazabuni pamoja na Wakandarasi.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, utekelezaji wa bajeti ya Serikali kwa kipindi cha Julai hadi Desemba, 2018 umekukwa na mafanikio makubwa. Miiongoni mwa maeneo yaliyopewa kipaumbele ni kama ifuatavyo:-

Moja, kuendelea na ujenzi wa miundombinu wezeshi ya kiuchumi ikiwemo reli kwa kiwango cha Kimataifa, bwawa la kufua umeme utokanao na nguvu za maji katika Bonde la Mto Rufiji, kukamilisha ununuzi wa ndege mpya mbili aina ya Airbus A220-300, ambapo moja iliwasili nchini Desemba, 2018 na nyiningine imewasili nchini Januari, 2019 na kufanya ndege ambazo zimenunuliwa na Serikali ya Awamu ya Tano, kuwa sita. (*Makofii*)

Pili, kutekeleza Sera ya Elimu Msingi Bila Ada na kuwezesha upatikanaji wa chakula kwa wanafunzi wa bweni, ruzuku kwa ajili ya uendeshaji wa shule na posho za Walimu Wakuu na Waratibu wa Elimu Kata. (*Makofii*)

Tatu, kutolewa mikopo kwa wanafunzi 119,214 wa elimu ya juu ambapo wanafunzi 40,114 ni wa mwaka wa kwanza; na 79,100 wanaendelea na masomo vile vile. Ruzuku imeendelea kutolewa kwa wanafunzi 871 wanaoendelea na masomo ndani na nje ya nchi.

Nne, kuimarika kwa kupatikanaji wa dawa muhimu kwa asilimia 96, kukamilisha kwa ujenzi wa jengo la kusimika vifaa vya uchunguzi na kununua vifaa vya tiba ya mionzi katika Hospitali ya Rufaa ya Mbeya.

Tano, kuimarisha utoaji wa chanjo kwa asilimia 97, sambamba na kuimarisha huduma za matibabu ya kibingwa kwa kuboresha miundombinu ya kutolea huduma, ununuzi wa vifaa tiba vya kisasa na hivyo kupunguza Rufaa za wagonjwa nje ya nchi. (*Makofii*)

Sita, kuendeleza utekelezaji wa miradi ya kimkakati 22 ya kuongeza mapato na kupunguza utegemezi wa Mamlaka za Serikai za Mitaa. Aidha, Serikali imesaini miradi mipyaa 15 kwa Halmashauri 12 iliyokidhi vigezo na utekelezaji wake unaanza mara moja. (*Makofii*)

Saba, upanuzi wa mtandao wa maji katika Miji ya Dar es Salaam, Arusha, Sumbawanga, Kigoma, Lindi na Kibaha, upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Kukamilika kwa miradi 65 ya maji vijijini kunafanya jumla ya miradi yote iliyokamilika kufikia 1,660, ikiwa na vituo vya kuchotea maji 90,907. Aidha, miradi 492 inaendelea kutekelezwa katika Halmashauri zote nchini na ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Nane, kuendelea na utekelezaji wa awamu ya tatu ya mradi kabambe wa kupeleka umeme vijijini kuptitia Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*), ambapo vijiji 1,039 vimeshaunganishwa na umeme. (*Makofii*)

Tisa, ununuzi na ukarabati wa meli katika Maziwa Makuu kuendelea na ujenzi wa meli mpya katika Ziwa Victoria, Nyasa na Tanganyika; kuendelea na ukarabati wa meli za MV Victoria, MV Butiama, MV Liemba, MV Umoja, MV Serengeti na MV Songea. (*Makofii*)

Kumi, ujenzi wa jengo la tatu la abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere, umekamilika kwa asilimia 90.7; na upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mwanza na viwanja vya ndege vingine vya mikoani kazi zinaendelea.

Kumi na moja, kukamilika kwa *Mfugale Flyover*, TAZARA na kuanza kutumika, kufikia asilimia 28 ya ujenzi wa

Ubungo Interchange, kuwekwa kwa jiwe la msingi na kuanza maandalizi ya ujenzi katika daraja la *Surrender*, kuzinduliwa na kuendelea na ujenzi wa barabara ya njia nane, kutoka Kimara hadi Kibaha na kuendeleza ujenzi na ukarabati wa madaraja na barabara kuu za Mikoa vile vile za Wilaya. (*Makofi*)

Kumi na mbili, kutengamaa kwa viashiria vya uchumi jumla, ikiwemo ukuaji wa pato la Taifa, mfumuko wa bei na thamani ya shilingi.

Kumi na tatu, kuendeleza na upanuzi wa barabara za Dar es Salaam, Mtwara na Tanga, na kuongeza kiwango cha upakiaji wa mizigo na uondoaji wa shehena katika maeneo ya Bandari za Ukanda wa Bahari na Maziwa Makuu, kwa lengo la kuimarishe, biashara ya ndani na Kimataifa.

Kumi na nne, kugharamia shughuli za uendeshaji wa ofisi ambazo ulifikia asilimia 121 kwa Wizara, Idara na Sekta zote zinazojitegemea, Taasisi na Wakala wa Serikali, asilimia 101 kwa Sekretarieti za Mikoa na asilimia 91 kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Kumi na tano, kuanza ujenzi wa ofisi 23 za Wizara katika eneo la Mji wa Serikali, Ihumwa, hapa Jijini Dodoma na ujenzi huo sasa umefikia zaidi ya asilimia 90.

Kumi na sita, kuimarishe Utawala wa Sheria na kuboresha usikilizwaji wa Mashauri ya Jinai, Madai, na Rufaa katika ngazi mbalimbali za Mahakama na kupitia upya mikataba inayolinda maslahi mapana ya rasilimali na vitega uchumi vya Taifa ikiwemo Mkataba wa Uendeshaji wa Kampuni ya BAT au Airtel.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuongeza mapato na kuimarishe usimamizi wa matumizi ya fedha na rasilimali za Umma ili kufikia malengo katika kipindi kilichobaki cha mwaka 2018/2019. Miiongoni mwa mikakati hiyo ni kama ifuatayo:-

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Moja, kuhakikisha kwamba Wizara na Taasisi zote za Umma zinatumia mfumo wa Serikali wa Kielektroniki wa kukusanya na kusimamia wa maduhuli, kabla ya Juni 2019.

Pili, kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani, kwa lengo la kupunguza utegemezi.

Tatu, kutumia mfumo wa kielektroniki wa *Stamp* za Kodi kwenye viwanda vinavyozalisha bidhaa zinazotozwa ushuru na zile zinazoingizwa nchini. Pia mfumo huu utasaidia kupata taarifa sahihi za uzalishaji na kupunguza uvujaji wa mapato ya Serikali.

Nne, kudhibitii biashara ya magendo kuitia bahari, maziwa, mipaka na njia zisizokuwa rasmi kwa kuitia vyombo vyote vya Ulinzi na Usalama kwa kushirikiana na Taasisi nyingine za Serikali kama Wakala wa Barabara (*Tanroads*) na Mamlaka ya Bandari Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie kuimarika kwa mifumo ya ukusanyaji mapato. Watanzania siku zote tunamuenzi Rais wetu kipenzi Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa hatua za makusudi anazozichukua katika kuhakikisha anaimarisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato. Binafsi, naamini Mheshimiwa Rais anafanya haya yote kwa lengo la kuona Tanzania inapunguza utegemezi wa misaada. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mifano ya hatua hizo za Mheshimiwa Rais ni maelekezo yake ya tarehe 10 Desemba, 2018 kwa Mawaziri na Wakuu wa Mikoa, kuwasilisha mapendekezo kuhusu namna bora ya kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa tayari Serikali imeshapokea mapendekezo ya namna bora ya kuboresha vyanzo vya mapato ya ndani kutoka kwa Mawaziri na Wakuu wa Mikoa na inafanya kazi mapendekezo hayo. Tutatoa maagizo mahsus kwa *TRA* na *TAMISEMI* kushirikiana katika kukusanya kodi za majengo.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imeendelea kutekeleza maelekezo ya Mheshimiwa Rais aliyo yatoa tarehe 22 Januari, 2019 alipokutana na wadau wa Sekta ya Madini. Serikali imefuta Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*) na kodi ya Zui o ya 5% ya mwisho (*Final Withholding Tax*) inayotozwa kwenye bei ya kuuzia madini ya aina zote kwa wachimbaji hao?

Mheshimiwa Spika, hatua hii inatarajiwa kupunguza utoroshwaji wa madini, kuwatambua wachimbaji wadogo kuitia masoko ya madini yatakayoanzishwa. Yatawapunguzia gharama wachimbaji wadogo na hivyo kuendesha shughuli zao kwa ufanisi mkubwa pamoja na kuongeza wigo wa mapato kwa kuwa madini sasa yatauzwa ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, nitoe rai kwa wachimbaji wote wadogo kushirikiana na Mamlaka mbalimbali za Serikali, kutekeleza maazimio yaliyofikiwa katika kikao na Mheshimiwa Rais. Aidha, naziagiza tena Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala wa Taasisi za Serikali zote na Serikali za Mitaa kuhakikisha zinajiunga na mfumo wa Serikali wa kielektroniki wa ukusanyaji wa mapato kabla ya tarehe 30 Juni, 2019.

Mheshimiwa Spika, sambamba na maelekezo haya, naielekeza pia *TRA* kusimamia uwekaji wa mifumo ya kukusanya Kodi za Vileo kwa kutumia *Stamp* za kielektroniki kwa viwanda vinavyozalisha vinywaji hivyo. Aidha, ifikapo tarehe 28 mwezi huu wa Februari, 2019 kila kiwanda kiwe kimeshafunga mfumo huo. *TRA* ni jukumu lao kusimamia hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vitambulisho kwa wafanyabiashara wadogo wamachinga, nitumie fursa hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ubunifu na uamuzi wake wa kugawa Vitambulisho Maalum kwa Wajasiriamali Wadogo kwa ajili ya kuwatambua na kuwarasimisha.

Mheshimiwa Spika, utambuzi wa wajasiriamali wadogo ulilenga kuziwezesha Halmashauri kuwapangia

mipango ya kuwaendeleza kama vile kuwatengea maeneo ya kufanya biashara zao bila kubughudhiwa, lakini hata kuwapatia mikopo na hivyo kuchangia pato la ndani katika ngazi za mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 4 Februari, 2019, jumla ya vitambulisho 284,945 vilishatolewa kwa wafanyabiashara kati ya vitambulisho 675,000 vilivyotolewa awamu ya kwanza na asilimia 42 ya vitambulisho vilivyotolewa. Utaratibu huo wa kugawa vitambulisho kwa wafanyabiashra wadogo umesaidisa Serikali kukusanya takribani shilingi bilioni 5.70.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua nia njema ya kuwatambua na kuwarasimisha Wajasiriamali wadogo kwa kuwapa vitambulisho, nawashihi Waheshimiwa Wabunge wenzangu na wananchi wote kuunga mkono jitihada hizi za Serikali na nyote mtakubaliana nami kuwa tukiwaendeleza wajasiriamali hawa wadogo tutakuwa katika nafasi nzuri ya kujenga sekta binafsi imara ya Watanzania ambaa baadaye wataweza kufanya biashara za ndani na za kimataifa kwa umahiri na ushindani mkubwa.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie sekta ya utalii; Serikali imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali kwa lengo la kuimarisha sekta ya utalii hapa nchini. Mionganoni mwa mikakati hiyo ni uanzishaji wa masoko mapya ya utalii sambamba na uimarishaji wa Shirika la Ndege la Tanzania (*ATCL*) kwa ununuzi wa ndege mpya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kufuatia ziara ya utangazaji, utalii katika Miji ya Shanghai, Guangzhou, Hong Kong, Sheldon na Beijing iliyofanyika Novemba, 2018, kundi la awali la watalii 350 kutoka China, litatembelea hapa Tanzania mwezi Machi, 2019. Lengo la Bodi ya Utalii Tanzania ni kuleta nchini watalii wapato 10,000 kutoka China. Kuongezeka kwa idadi ya watalii watakaotembelea Tanzania kunatarajiwa kuchocheara ukuaji wa shughuli mbalimbali za kiuchumi pamoja na mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa tarehe 15 Disemba, 2018 nilipata fursa ya kuzindua channel mpya ya utalii ijulikanayo kama Tanzania Safari *Channel*, ambayo ni sehemu ya utekelezaji wa maelekezo ya Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli. Agizo alilotoa kwa Shirika letu la Utangazaji Tanzania.

Mheshimiwa Spika, uwepo wa *channel* hii si tu utaendeleza taswira na sifa nzuri ya Tanzania ya Kimataifa, lakini pia kuongeza thamani katika mnyororo mzima wa biashara ya utalii nchini. Kupitia fursa hiyo Serikali imeongeza wigo wa utangazaji wa vivutio vya utalii na kuwawezesha wananchi kuvitambua na kujua namna ya kuvifiki. Hatua ambayo inatarajia kuongeza idadi ya watalii wa ndani. Kwa sasa *channel* hii inaonekana kwenye visumbuzi maarufu kama ving'amuvi vya *Startimes channel* Na. 331 na *channel* Na. 542. Na kishumbuzi cha Azam kinapatikana *channel* Na. 109. Taratibu zinakamilishwa ili *channel* hiyo pia iweze kuonekana kwenye kishumbuzi cha DSTV.

Mheshimiwa Spika, rai yangu kwa Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na Shirika la Utangazaji Tanzania zianzishe ushirikiano na *channel* za ndani na nje ya nchi kama vile *National Geographic* na *Discovery Channel* ili kuongeza wigo na kuijjengea uwezo wa kujitangaza zaidi nje ya mipaka ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, natoa wito kwa sekta binafsi kutumia fursa hiyo kujitangaza, lakini pia kutengeneza vipindi bora vitakavyorushwa na vituo bora vya Television, vile vile nitoe wito kwa Watanzania kuendelea kuiangalia *channel* hiyo, ambayo imesajiliwa kuonyeshwa kwa umma bila malipo yoyote (*a must-carry channel*).

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie sekta ya afya na hasa upatikanaji wa *X-ray* za kisasa kwa mikoa 11. Uimarishaji wa sekta ya afya hususan upatikanaji wa huduma bora za afya kwa watu wote ni moja kati ya vipatumbele vya Serikali ya Awamu ya Tano. Katika kutekeleza jukumu

hilo Serikali imenunua na kufunga mashine 11 za X-raykwenye Hospitali za Amana, Bukoba, Chato, Katavi, Magu, Morogoro, Njombe, Nzega, Simiyu, Singida na Hospitali iliyoko Songea Mkoani Ruvuma. Vifaa hivyo vinatarajiwa kuimarisha upatikanaji wa huduma za uchunguzi kwenye hospitali hizo.

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya ujenzi na ukarabati wa hospitali nchini. Serikali imeendelea pia kuimarisha upatikanaji wa huduma za afya katika ngazi za mikoa na halmashauri. Hivi sasa ujenzi wa hospitali 67 katika halmashauri na hospitali nne za rufaa kwenye mikoa ambayo haikuwa na hospitali za rufaa unaendelea. Hadi kufikia tarehe 31 Januari, 2019 tayari jumla ya shilingi bilioni 100.5 sawa na shilingi bilioni 1.5 kwa kila hospitali ya Halmashauri zimekwishatolewa na kazi za ujenzi zinaendelea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vile vile shilingi bilioni 6.5 zimetolewa kwa ajili ya ujenzi wa hospitali mpya za rufaa za Mikoa ya Geita, Njombe, Katavi, Simuyu na Songwe. Ujenzi wa hospitali hizo uko kwenye hatua mbalimbali za utekelezaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba Mheshimiwa Rais alielekeza kuwa fedha zilizopangwa kutumika kwenye sherehe za Uhuru mwaka 2018 zitumike kujenga hospitali mpya Mkoani Dodoma. Napenda kilitaarifa Bunge lako Tukufu kwamba taratibu za ujenzi wa Hospitali hiyo ambayo Mheshimiwa Rais ameipa jina la Uhuru zimeanza kufanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imeendelea na ukarabati wa hospitali katika mikoa mbalimbali nchini. Hadi kufikia tarehe 31 Januari, 2019 shilingi bilioni saba zilikuwa zimeshatumika kwa ajili ya ukarabati wa Hospitali za Rufaa za Sekou toure Mkoani Mwanza, Babati- Manyara, Mount Meru pale Arusha, Mawenzi Mkoani Kilimanjaro, Bombo Mkoani Tanga na Hospitali za Mikoa ya Dodoma, Singida, Shinyanga na Mara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ukarabati huo unahusisha *ward* za wazazi na watoto, *ward* za kulaza wagonjwa, vyumba vya upasauji na wagonjwa wa nje ninaelekeza kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, kuendelea kusimamia kwa ukarabati wa ukaribu wa ujenzi wa hospitali hizo mpya, pamoja na ukarabati wa hospitali za rufaa kwenye mikao nilioitaja.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Elimu, hasa uandikishaji wa wanafunzi wa kidato cha kwanza 2019. Matokeo ya Mtihani wa Taifa kwa mwaka 2018 yanaonesha kuwa wanafunzi 733,101 walifaulu mitihani yao. Hata hivyo ni wanafunzi 599,356 sawa na asilimia 81.76 ya waliofaulu ndio pekee walipata nafasi ya kuanza kidato cha kwanza mwaka 2019. Wanafunzi 133,747 wallobaki sawa na asilimia 18.24 ya waliofaulu walikosa nafasi kutokana na uhaba wa vyumba vya madarasa.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wenye sifa za kujunga na kidato cha kwanza wanapata nafasi, Wakuu wote wa Mikoa na Wilaya wameelekezwa kuhakikisha wanasmamia ujenzi wa vyumba vya madarasa na kwamba ifikapo tarehe 28 Februari, 2019 vyumba hivyo viwe vimekamilika na wanafunzi hao wawe wamekaa darasani. Nasisitiza kuwa kazi hiyo iendelee na *TAMISEMI* ifuatilie kwa ukaribu zaidi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi hizo za ujenzi zinazofanywa na mamlaka ya Serikali za Mitaa, mwezi Januari, 2019 Serikali imepeleka shilingi bilioni 54 kuititia programme ya lipa kwa maendeleo P4R kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya Shule za Msingi na Sekondari. Sehemu ya fedha hizo zitatumika pia kuongeza vyumba vya madarasa ambavyo vitasaidia uandikishwaji wa wanafunzi wa kidato cha kwanza pamoja na ujenzi wa mabweni na mambwalo kwa sekondari ili kuwanusuru wanafunzi wa kike.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa matokeo ya kidato cha nne kwa mwaka 2018 ufaulu umeongezeka na

kufikia asilimia 79.27. Taarifa ya motokeo hayo pia inaonesha kwamba ubora wa ufaulu kwa kuangalia madaraja walioyapata wanafunzi umeongezeka kwa asilimia 1.6 ikilinganishwa na mwaka 2017. Napenda kutumia fursa hii kutoa pongezi nyingi kwa Walimu, shule na wanafunzi waliofanya vizuri katika mtihani wa kidato cha nne, wote tunawapongeza sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nizungumzie hali ya amani na usalama hapa nchini. Hali ya usalama imeendelea kuwa shwari, aidha wananchi nao wanaendelea kutekeleza shughuli zao mbalimbali za kiuchumi kwa utulivu na bila bugudha yoyote. Hata hivyo licha ya hali ya usalama kuendelea kuwa shwari katika siku za hivi karibuni huko Mkoani Njombe, Wilayani Njombe kumezuka kikundi cha wahuni wachache kinachoteka na kuua watoto wadogo kwa imani za kishirikiana. Katika kauli ya Serikali iliyosomwa Bungeni na Mheshimiwa Alphaxard Kangi Lugola, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, alieleza kuwa hadi sasa watoto saba wamesharipotiwa kuuawa na mmoja kujeruhiwa. Aidha, tayari watuhumiwa wasiopungua 29 wamekamatwa kwa ajili ya uchunguzi wa kusaidia upelelezi.

Mheshimiwa Spika, Serikali inalaani vitendo hivyo na matukio hayo ya kinyama dhidi ya watoto wetu na pia inaonya wale wote wenye kujaribu kutumia matukio hayo kuzua tataruki kwa jamii, nitumie fursa hii kusisitiza kwamba Serikali haitavifumbia macho kabisa, vitendo vya ukatili dhidi ya watoto wetu.

Mheshimiwa Spika, tayari Serikali imevielekeza vyombo vyake vya ulinzi na usalama kuhakikisha kwamba vinawatafuta kwa mbinu zozote wale wote wanaohusika na uhalifu huo na kuwafikisha kwenye vyombo vya sheria. Niwasihii Waheshimiwa Wabunge wenzangu na Watanzania wote kwa ujumla kutoa ushirikiano wa kutosha kwa vyombo vya dola ili kudhibiti hali hiyo.

Mheshimiwa Spika, jambo la msingi katika kipindi hiki ni kila mmoja adumishe hali ya ulinzi na usalama katika eneo

pale alipo, aidha tuendelee kumwomba Mwenyezi Mungu awape nguvu na miyo ya subira wazazi, ndugu na jamaa na marafiki wote wa watoto waliopoteza maisha na Mwenyezi Mungu aziweke roho zao mahali pema.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie kidogo eneo la Ugaidi. Tarehe 15 Januari, 2019, jirani zetu Wakenya walikumbwa na shambulio la Kigaidi katika hoteli ya kifahari ya DusitD2 Jijini Nairobi ambako liligharimu maisha ya watu na mali. Naomba nitumie fursa hii kuungana na Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Watanzania wenzangu kuwapa pole majirani zetu Kenya kufuatia tukio bayaa ambalo linapaswa kulaaniwa na kupingwa na kila mpenda amani hapa duniani.

Mheshimiwa Spika, Tanzania itaendelea kushirikiana na nchi wanachama wa Jumuia ya Afrika Mashariki pamoja na Jumuia za Kimataifa katika mapambano dhidi ya ugaidi. Vyombo vyta Ulinzi na Usalama vimekuwa vikichukua tahadhari kubwa dhidi ya vitisho vyta matukio ya kigaidi ikiwa ni pamoja na kuongeza umakini katika kuwachuja wageni wanaoingia nchini, ili kuhakikisha kwamba wanakidhi vigezo vyote vyta kiusalama vilivyowekwa.

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine zilizochukuliwa ni kutoa elimu kwa umma, utayari wa vyombo vyta ulinzi na usalama na kuimarisha ushirikiano na nchi ya jirani kikanda na kimataifa na tumeendelea kubadilishana uzoefu wa nchi rafiki pamoja na taarifa za kiintelijensia kuhusu ugaidi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba nizungumzie kidogo mazungumzo yaliyofanywa kati ya Mheshimiwa Rais na Viongozi wa dini. Napenda kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwa ujumla ya kuwa moja ya sifa yetu sisi Watanzania tulioachiwa na waasisi wa Taifa hili ambayo inatufanya tuwe kimbilio la wale waliovurugikiwa na amani katika nchi zao ni kuvumiliana na kustahimiliana. Siku zote tumekuwa tukimaliza tofauti zetu sisi wenye kwa mazungumzo.

Mheshimiwa Spika, ukweli wa jambo hili umedhihirishwa pia na kitendo ambacho hakina budi kuigwa cha Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, cha kukutana na viongozi wa madhehebu mbalimbali ya dini pale Ikulu na kufanya nao mazungumzo ya papo kwa papo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kufanya kazi maoni, ushauri na mapendekezo yote yaliyotolewa na viongozi wa dini, naelekeza viongozi na watendaji wote wa Serikali kuanzia ngazi za Wizara, Mkoa na Wilaya kwamba wahakikishe wanaweka utaratibu wa kukutana na kuzungumza na viongozi wa madhehebu ya dini na makundi mengine maalum, mahususi katika maendeleo yetu na hasa kushughulikia kwa haraka changamoto zinazokabili maeneo walimo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuzungumzia uchaguzi Mkuu wa Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Itakumbukwa tarehe 30 Disemba, 2018 wananchi wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) walipiga kura kuchagua Rais, Wabunge wa Taifa na Magavana wa Majimbo. Aidha, tarehe 24 Januari, 2019, Mheshimiwa Felix Tshisekedi mshindi wa uchaguzi huo Mkuu aliapishwa rasmi kuwa Rais wa Awamu ya Tano wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo tangu kupata uhuru wake mwaka 1960.

Mheshimiwa Spika, napenda kuungana tena na Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kitendo cha kumpongeza Mheshimiwa Tshisekedi na wananchi wote wa DRC kufanya uchaguzi wa amani na utulivu na pia kubadilishana madaraka kwa njia ya amani kutoka awamu moja ya uongozi kwenda awamu nyingine. Tanzania inamuahidi Mheshimiwa Tshisekedi, Rais wa DRC kuendeleza uhusiano mzuri uliopo baina ya nchi hizi mbili.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie sekta ya michezo; tarehe 1 – 9 Disemba, 2018, Timu yetu ya Bunge ilishiriki kwenye Michezo ya Tisa ya Mabunge ya Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyofayika Jijini Bujumbura nchini Burundi.

Katika mashindano hayo timu yetu ya Bunge ilinyakua jumla ya medali 16. Nami niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuipongeza sana timu yetu kwa kutuwakilisha vizuri na kulipatia sifa Bunge letu Tukufu la Tanzania na Taifa kwa ujumla, hongereni sana wanamichezo wote wa timu ya Bunge na tunaamini mashindano ya mwaka huu watakuja na medali zaidi ya hizi walizokuja nazo.

Mheshimiwa Spika, mwaka huu nchi yetu imepewa heshima ya kuandaa mashindano ya mpira wa miguu wa vijana wenye umri chini ya miaka 17 Barani Afrika, (*AFCON under 2017*). Wito wangu kwa Watanzania wote kuthamini heshima hii kwa kuunga mkono timu na kutumia vizuri fursa zitakazopatikana kutoptana na ujio wa wageni wengi watakuja kushiriki mashindano haya. Ni nafasi nzuri kwa Taifa letu kwa timu yetu ya vijana kushiriki kwenye mashindano haya makubwa na ni matumaini yetu kwamba timu yetu itafanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, hitimisho; wakati nikielekea kuhitimisha hotuba yangu, napenda nikushukuru wewe Mheshimiwa Spika na Naibu Spika, kwa katuongoza vyema ndani ya Bunge lako Tukufu. Kadhalika niwashukuru wenye Viti wa Bunge, kwa umahiri mkubwa mmekuwa mkiendesha Vikao vya Bunge hapa kwenye Bunge hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niwashukuru pia Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa michango yenu muhimu yanye mwelekeo wa kuboresha maisha ya wananchi wetu, nimshukuru Katibu wa Bunge na Wasaidizi wake kwa huduma nzuri ambayo wamekuwa wakitupatia kwa kipindi chote tulichokuwa hapa Bungeni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa niwashukuru Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa umahiri na weledi mkubwa katika kuandaa Miswada, watendaji wa Serikali na Taasisi mbalimbali kwa kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa weledi mkubwa, umahiri mkubwa na ufanisi mkubwa na hivyo kufanikisha shughuli zilizopangwa na Bunge lako Tukufu, bila kuwasahau Wanahabari amba o nawaona wako

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

mbele yetu kwa uchambuzi wa hoja na mwendendo mzima wa Bunge na kufikisha habari hizo kwa wananchi wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, niendelee kuvishukuru sana Vyombo vya Ulinzi na Usalama kwa huduma ambazo wamekuwa wakizitoa kwa ushiriki wa Bunge hili na kuendelea kuwa salama hadi tunafikia hatua hii. Aidha, nitakuwa mchoyo wa fadhila endapo kama sitawashukuru madereva wote waliotuhudumia wakati wa kuja hapa na tukiwa hapa. Niendelee kuwatakiwa heri na afya na umakini mkubwa na niwataki safari njema za kurejea nyumbani kwetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya yote, naomba sasa nitoe hoja kwamba Bunge lako Tukufu liahirishwe hadi siku ya Jumanne, tarehe 2 Aprili, 2019, saa tatu asubuhi katika ukumbi huu hapa Jijini Dodoma.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Hoja imeungwa mkono kweli kweli Mheshimiwa Waziri Mkuu. Waheshimiwa Wabunge, nawashukuruni sana. Ahsante sana kwa hotuba yako Mheshimiwa Waziri Mkuu imegusa maeneo mengi na imetoa ufahamu mkubwa sana sio kwetu tu Wabunge lakini pia Watanzania kwa ujumla, tunakushukuru sana kwa hotuba nzuri. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, sasa imetolewa hoja na Waziri Mkuu ya kuahirisha Bunge, naomba niwahoji wale wanaoafiki kwamba tuahirishe Bunge hadi tarehe 2 Aprili.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja ilihamuliwa na Kuafikiwa)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa hatua hii naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza na kuwashukuruni sana kwanza kwa kazi ya leo, maana kila mmoja akiangalia saa yake atakubaliana kwamba leo inabidi Katibu wa Bunge arekebishe mambo yakae vizuri. Maana Bunge linafanya kazi na ni mfano kwa kweli kwa wapigakura wetu na ni majibu tosha kwa wanaofikiri sisi ni dhaifu, haiwezekani dhaifu akafanya kazi kwa masaa mengi kiasi hiki. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo nawashukuru sana kwa kweli kwa *perseverance* ya leo na muda wote na Kamati zetu kama mlivyokuwa mnasema wakati ule kwamba zimekuwa zinafanya kazi mpaka saa sita/saa saba usiku, kwa kweli Wabunge kwa ujumla wake wa Bunge hili la Tanzania ni wachapakazi sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, wakati wote tunapofanya hizo kazi watumishi wa Bunge chini ya Katibu pamoja na yeye mwenyewe huwa tuko nao muda wote, kwa hiyo ningependa kuwapongeza pia watumishi wetu wa Ofisi ya Bunge, ambao kwa wakati wote ambao tupo kazini wao huwa wanajua muda wa kuingia kazini lakini saa ya kuondoka ni majaaliwa. Tunawashukuru sana na tungewashauri muendelee na utaratibu huo wa kufanya kazi kwa bidii zaidi. (*Makofi*)

Leo tumeshughulikia Azimio la kupandisha hadhi zile Hifadhi tano kuwa National Parks ni jambo jema sana, lakini pia tumeshauri kwa Wizara ya Fedha wakae na TANAPA waangalie ule mzigo wa kodi walionao kwa kweli zipo nyingine ambazo inabidi tuwapunguzie mzigo kidogo ili wakafanye kazi nzuri ya kuzipandisha hadhi kweli kweli zile Hifadhi na nyingine hizi kumi na moja ambazo na zenyewe kimapato huwa zinasuasua, lakini mambo fulani fulani yakirekebishwa zinaweza na zenyewe zikaanza kujitegemea kimapato.

Pia tumeshughulikia ule Muswada wa Sheria Mbalimbali ulioletwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na tumerekebisha Sheria za Madini, Sheria za Kodi upande wa madini, upande

wa majengo, upande wa zabibu na maeneo mengine jambo ambalo ni zuri sana. Tunaishukuru sana Serikali na zoezi hilo la marekebisho ya kodi za maeneo mbalimbali kwa kuwa tunaelekea kwenye Bunge ijalo la Bajeti basi zoezi hilo liendelee pia, kwa sababu yapo maeneo kadhaa kwenye *fields* mbalimbali kwa kweli yanahitaji kuangaliwa vizuri ili kuwapunguzia watu mzigo lakini kuiongezea Serikali mapato pia. Kuna mahali unapunguza kiwango cha kodi lakini mwisho wa siku unakuwa umechagiza kodi kulipwa zaidi na kwa hiyo unaishia kuwa na mapato mengi. Tunaishukuru sana Serikali.

Naomba niwashukuru sana wasaidizi wangu ambao tumesaidiana hapa Mezani, Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Andrew Chenge, Mheshimiwa Mussa Zungu na Mheshimiwa Najma Giga kwa kazi nzuri sana ambayo tumefanya kwa kushirikiana, bila usaidizi huo nadhani isingekuwa rahisi tukafika hapa tulipofika.

Niwataarifu tu Waheshimiwa Wabunge kwamba Kamati ya Maadili imemaliza kazi zile ambazo tulikuwa tumewapa, lakini muda hauruhusu kufanyia kazi ushauri wao, tutaufanya kazi wakati tutakaporudi tena hapa.

Niweise tu ushauri wa jumla, tusifanye *fashion* hasa sisi Wabunge kulishambulia Bunge kuwa ndio *fashion* ya kutaka kuonekana huko kwa wananchi, tusifanye hivyo. Huo ndio ushauri wangu wa jumla na anayejitoa kwa maana ya mapambano ya kulishambulia Bunge aingie tu kwenye 18. (*Makofii*)

Hatusemi Bunge lisikosolewe, lakini hatutakubali udhalilishwaji wa watu wazima ambao wana heshima zao wako humu ndani, wameaminiwa na wananchi, wanahehimiwa sana katika jamii, halafu mtu mmoja ananyanyuka anawadharau tu. Hapana sio vizuri. Tushauriane, tusaidiane lakini tusidharauliane. Hilo haliendi hivyo. (*Makofii*)

Naomba Tume tukimaliza hapa saa 11.00 jioni tuonane kwa kikao pale Ukumbi wa Spika, Jengo la Utawala.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mwisho nawatakia safari njema Waheshimiwa Wabunge, kokote mtakapokuwa mnaenda mwende salama na mjue katikati tu ya mwezi ujazo tunarudi tena na safari ijayo Kamati nyingi zitakuwa na safari lakini pia tutakuwa tunapitia makabrasha ya mapendekezo ya bajeti na kazi za Wizara zilizofanyika kwa mwaka mzima uliopita.

Kwa hatua hiyo sasa, naomba tusimame Waheshimiwa Wabunge ili tuweze kupata wimbo wa Taifa kutoka kwa *Brass Band* yetu.

WIMBO WA TAIFA

(Hapa Wimbo wa Taifa Uliimbwa)

SPIKA: Ahsanteni sana *brass band*, mmeshinda na sisi kutwa nzima ya leo, tunawashukuruni sana Maafande.

Waheshimiwa Wabunge kwa hatua hii sasa naomba nahirishe shughuli za Bunge hadi tarehe 2 Aprili, 2019. Ahsanteni sana.

*(Saa 9.07 Alasiri Bunge lilahirishwa hadi Siku ya Jumanne,
Tarehe 2 Aprilli, 2019, Saa Tatu Asubuhi)*